

**USASA KATIKA USHAIRI WA KITHAKA WA MBERIA: UCHANGANUZI
WA MAUDHUI NA MTINDO**

NA

SAMSON ONTIRI ONGARORA

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA MAHITAJI YA
SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA IDARA YA KISWAHILI,
CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

NOVEMBA, 2020

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu kingine chochote kwa mahitaji ya shahada ya uzamifu.

Samson Ontiri Ongarora

Sahihi.....

Tarehe.....

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamifu kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Profesa Kineene wa Mutiso

Sahihi.....

Tarehe.....

Profesa Rayya Timammy

Sahihi.....

Tarehe.....

Daktari James Nyachae Michira

Sahihi.....

Tarehe.....

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia mke wangu Irene Moraa na wanangu Amos Ontiri, Lameck Ontiri na Aiden Ontiri.

SHUKRANI

Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kufika umbali huu. Pili, kazi hii haingekamilika bila msaada wa hali, ushauri na himizo kutoka kwa watu mbalimbali. Kwa hivyo, kwa njia ya kipekee nawashukuru sana wasimamizi wangu: Profesa Kineene wa Mutiso, Profesa Rayya Timammy na Daktari James Nyachae Michira kwa mwongozo na ushauri mwafaka mlionipa kutoka hatua ya pendekezo la utafiti hadi kukamilika kwa tasnifu hii.

Mbali na hao, shukrani jazila ziwaendee wahadhiri wafuatao: Profesa Iribe Mwangi, Profesa Kithaka wa Mberia, Profesa Kyallo Wamitila, Profesa John Habwe, Profesa Evans Mbuthia, Daktari Zaja Omboga, Daktari Amir Swaleh, Daktari Ayub Mukhwana, Daktari Theresia Kazungu na Daktari Basilio Mungania. Mumenishajiisha na kunihimiza katika kuukwea mlima huu wa usomi. Ushauri wenu na kunitia moyo kumenifaa pakubwa katika kukamilisha kazi hii.

Siwezi kuwasahau wasomi wenzangu waliokuwa mwega mkubwa nilipoelekea kukata tamaa. Enoch Matundura na Nafwa Barasa, Mungu awajaalie baraka katika shughuli na usomi wenu pia. Fauka ya hayo, shukrani za dhati ziwaendee wazazi wangu Peter Ongarora na Keziah Moraa. Kupitia malezi yenu mema na kunisomesha, nimefika kileleta hiki.

Kwa mke wangu Irene Moraa na wanangu Amos Ontiri, Lameck Ontiri na Aiden Ontiri nawashukuru sana kwa kunionyesha upendo na uvumilivu mwingi mbali na kuniombea nifaulu katika utafiti wangu. Isitoshe, shukrani za kipekee ziwaendee kaka zangu Joash, Haron, Isaiah, Benson na dada Annah, Stella na Everline. Ahsanteni kwa mchango wenu wa hali na mali. Hatimaye, namshukuru Rachel Maina kwa kunifanyia kazi bora ya kuipiga chapa tasnifu hii. Kwenu nyote, Mungu awabariki.

IKISIRI

Maudhui na mtindo ni masuala mawili katika kazi ya fasihi ambayo hayawezi kutenganishwa. Katika utafiti huu tumeangazia usasa wa kimaudhui kama unavyoweza na mtindo wa kipekee katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Malengo ya kufanya utafiti huu ni: kuchunguza ruwaza mbalimbali za kimaudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia, kufafanua mbinu za kimtindo alizotumia mshairi, kutathmini upekee wa maumbo ya kishairi na kudadisi namna mshairi amesawiri athari na matokeo ya ukoloni. Utafiti wa maudhui na mtindo umejikita katika diwani tano za ushairi wa Kithaka wa Mberia ambazo ni: *Mchezo wa Karata* (1997), *Bara Jingine* (2001), *Redio na Mwezi* (2005), *Msimu wa Tisa* (2007) na *Rangi ya Anga* (2014). Nadharia mbili zimetumika katika uchanganuzi huu. Nadharia ya baadaukoloni imetumika kuchanganua usasa wa kimaudhui, ilhali nadharia ya elimumitindo mkabala wa uhakiki mpya imetumika kuchanganua mbinu za kimtindo alizotumia mshairi. Utafiti huu ni wa kimaktaba na matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa njia ya kinathari. Tumbainisha kuwa mashairi yenye maudhui mbalimbali yanadhihirisha ruwaza za kimaudhui. Kuna maudhui juu ya siasa, utawala na mamlaka katika mataifa ya Afrika. Aidha, kunayo maudhui yanayogusia juu ya uharibifu na uhifadhi wa mazingira. Fauka ya hayo, kuna maudhui juu ya utamaduni mahuluti na mengine yanahusu dhuluma na ukombozi wa wanawake. Baadhi ya vipengele vya kimtindo vilivyotawala ushairi wake katika diwani zake zote ni kama vile matumizi ya kipekee ya tashibihi, sitiari, tashihisi, takriri, maswali ya balagha, tasifida, chuku, msamiati teule, uchimuzi, nyimbo, ndoto na usimulizi. Mbinu zingine za kimtindo anazotumia kwa uchache kama kiungo cha kuwasilisha maudhui kwa msomaji ni kejeli, mazungumzo, oksimora, uzungumzi nafsia, majazi, tanakali za sauti, sauti, sajili ya gazeti na mgao wa kitamthilia katika baadhi ya mashairi.

ABSTRACT

Themes and style are two inseparable aspects in a literary work. This research mainly focuses on modernity of themes as enabled by the unique style in Kithaka wa Mberia's poetry. The objectives of this study are: to investigate different thematic patterns in Kithaka wa Mberia's poetry, to elaborate stylistic techniques employed by the poet, evaluate unique poetry forms in Kithaka wa Mberia's poetry and to interrogate how the poet portrays the effects and consequences of colonialism. This study on themes and style covers Kithaka wa Mberia's five poetic anthologies namely: *Mchezo wa Karata* (1997) (*A Game of Cards*), *Bara Jingine* (2001) (*Another Continent*), *Redio na Mwezi* (2005) (*Radio and the Moon*), *Msimu wa Tisa* (2007) (*The Ninth Season*) and *Rangi ya Anga* (2014) (*Colour of the Sky*). We have applied two theories in this analysis. Postcolonial theory has been used in analyzing modernity of themes whereas the theory of stylistics a new criticism approach has been useful in analyzing stylistic techniques the poet uses in addressing various thematic issues. This research is library based and the research findings have been presented in prose form. We have demonstrated that different poems covering various themes exhibit thematic patterns. There are themes on politics, governance and authority in African nations. There are also themes that focus on destruction and conservation of the environment. Besides that, there are themes concerning cultural hybridity whereas other themes focus on oppression and liberation of women. Some of the stylistic devices dominant in all the five poetic anthologies include special use of similes, metaphors, personification, repetition, rhetorical questions, euphemism, hyperbole, unique vocabulary, foregrounding, songs, dreams and narration. Other stylistic devices used in presenting themes to the reader include sarcasm, dialogue, oxymoron, soliloquy, nicknaming, onomatopoeia, voices, newspaper register and play structure in some poems.

FASILI ZA ISTILAHU MUHIMU ZILIZOTUMIKA

Baadaukoloni: Uchunguzi wa athari za ukoloni kwenye tamaduni na jamii. Uchunguzi wa baadaukoloni unahusu namna mataifa ya Ulaya yalivyotawala na kudhibiti tamaduni za ulimwengu wa tatu na namna makundi hayo yameitikia na kupinga nyanyaso hizo.

Elimu ya kigeni: Utaratibu ambao dola la kikoloni linasilimisha ama wenyeji au kundi kubwa la watu kwa misingi yake ya kifikiria na mwonoulimwengu.

Lugha: Katika muktadha wa ukoloni na baadaukoloni, lugha imekuwa chanzo cha ukoloni na pingamizi. Katika hali mahususi, urejeaji kwa matumizi ya lugha za kiasili umetetewa kwa vile lugha za kiasili zilikandamizwa na nguvu za kikoloni. Matumizi ya lugha za kigeni ni suala linalojadiliwa miongoni mwa waandishi wa baadaukoloni.

Mamlaka na utawala: Uwezo wa mtu au kundi la watu kuwa na nguvu za kudhibiti na kutoa maamuzi yanayoathiri maisha ya watawaliwa.

Masefule: Matabaka ya chini au yaliyotawaliwa ambayo yana uwezo mdogo wa kueleza juu ya hali zao na hivyo yanategemea lugha na mbinu za tabaka tawala ili kujieleza yasikike.

Mbari: Ugawaji na uainishaji wa wanadamu kwa misingi ya sifa za mwonekano na bayolojia.

Shairi-picha: Aina ya shairi linaloundwa kwa maneno ili kuunda umbo fulani la kipekee linalosaidia kueleza ujumbe na dhamira ya mshairi kwa njia wazi.

Uigaji: Mbinu ambazo watu au kundi linalotawaliwa linachukua utamaduni (lugha, elimu, mavazi na kadhalika) wa mtawala.

Ujitambuzi: Namna mtu binafsi au kundi fulani linajieleza au kujielewa.

Ukoloni: Upanuzi wa kibeberu (kiuchumi, kisiasa na kitamaduni) wa nchi ya Ulaya kwa sehemu zote za ulimwengu katika kipindi cha miaka mia nne iliyopita ambapo

ilikuwa na udhibiti na ushawishi kwa maeneo na makoloni yake yote. Mfumo huu ulikuwa na ubaguzi wa mbari na hali ya kujiona bora kuliko watu wengine wasio Wazungu.

Ukoo: Mchanganyiko wa sifa za thamani, imani, kaida, tabia, vionjo, tajriba zinazohusu kundi fulani. Sifa hizi zinasaidia katika ujitambuzi wa mtu.

Umahuluti: Mchanganyiko wa tamaduni, usilimishaji na marekebisho ya mitindo ya kitamaduni ya watu weusi au watawaliwa kutoka kwa Wazungu. Umahuluti unaweza kuwa wa kijamii, kisiasa, kiisimu, kidini na kadhalika. Utamaduni mahuluti si lazima uwe shwari. Unaweza kuwa tata na wa kuvuruga mambo.

Usasa: Dhana ya usasa imetumiwa kuelezea au kuzitambulisha sifa mpya za dhamira, tanzu, dhana na mitindo ya kifasihi inayohusishwa na miongo ya kwanza ya karne ya ishirini. Katika mielekeo ya ushairi huru, usasa katika ushairi unapimwa kwa mizani ya kuepuka mitindo ya wanamapokeo katika vipengele vya mada, maumbo, dhana na mitindo. Washairi wa kisasa hujaribu ubunifu wao katika nyanja mbalimbali za mitindo mipya na maumbo mapya, matumizi ya lugha na maneno, mielekeo mipya katika kujiwasilisha hasa ujenzi wa taswira halisi. Washairi wa kisasa pia wamebuni mbinu changamano za kuelezea na kuwasilisha maudhui na maana ya maudhui yao.

Wingine: Njia za kijamii au kisaikolojia ambapo kundi moja linajitenga na kundi jingine. Kundi au watu wanaojiona bora kuliko wengine wanatilia mkazo kwenye yale mambo yanayowafanya kuwa tofauti na hao watu wengine. Hujitokeza namna wanavyowasilisha watu wengine kupitia jazanda zinazodunisha.

VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA TASNIFU

Khj	-	kama hapo juu/keshatajwa
Kur	-	kurasa
Mhr	-	mhariri
n.w	-	na wengine
Uk	-	ukurasa
Wahr	-	wahariri

YALIYOMO

UNGAMO.....	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI	v
FASILI ZA ISTILAHU MUHIMU ZILIZOTUMIKA.....	vii
VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA TASNIFU.....	ix
SURA YA KWANZA	1
1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Tatizo la Utafiti	4
1.3 Maswali ya Utafiti.....	5
1.4 Malengo ya Utafiti	5
1.5 Sababu za Kuchagua Mada.....	5
1.6 Upeo na Mipaka.....	6
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada.....	7
1.8 Msingi wa Kinadharia.....	16
1.8.1 Nadharia ya Baadaukoloni	16
1.8.2 Nadharia ya Elimumitindo	20
1.9 Mbinu za Utafiti	24
1.9.1 Uteuzi wa Sampuli	24
1.9.2 Ukusanyaji na Uchanganuzi wa Data.....	24
1.9.3 Uwasilishaji wa Data.....	25
1.10 Hitimisho.....	25
SURA YA PILI: MIKTADHA YA MAWASILIANO NA USEMI KATIKA	
USHAIRI WA KITHAKA WA MBERIA	26
2.1 Utangulizi.....	26
2.2 Mukstadha wa Kisiasa.....	26
2.3 Mukstadha wa Kiuchumi.....	33
2.3.1 Shughuli za Kilimo na Viwanda	34
2.3.2 Utabaka na Biashara ya Ukahaba.....	37
2.3.3 Shughuli za Kiuchumi Zinazoharibu Mazingira	39
2.4 Mukstadha wa Kimazingira.....	41
2.4.1 Msamiati wa Kimazingira	41
2.4.2 Uharibifu wa Mazingira	45

2.4.3 Uhifadhi wa Mazingira.....	46
2.5 Mukadha wa Kitamaduni.....	49
2.5.1 Ubakaji na Ukahaba	49
2.5.2 Unafiki wa Kidini.....	50
2.5.3 Matumizi ya Vileo na Dawa za Kulevya	52
2.5.4 Ubaguzi wa Rangi na Hadhi.....	54
2.5.5 Mila Zilizopitwa na Wakati.....	55
2.6 Mukadha wa Kihistoria.....	58
2.7 Hitimisho.....	59
SURA YA TATU: SIASA, UTAWALA NA MAMLAKA KATIKA MATAIFA	
YA AFRIKA	62
3.1 Utangulizi.....	62
3.2 Maudhui	62
3.2.1 Unafiki na Tamaa Katika Siasa.....	62
3.2.2 Uongozi wa Kidikteta	66
3.2.3 Ukoloni Mkongwe na Ukoloni Mamboleo	70
3.2.4 Changamoto za Mataifa ya Afrika	75
3.2.5 Ujenzi wa Jamii Mpya.....	78
3.3 Mtindo Katika Siasa, Utawala na Mamlaka Katika Mataifa ya Afrika	80
3.3.1 Sitiari	80
3.3.2 Tashibihhi.....	84
3.3.3 Tashihisi	87
3.3.4 Chuku	91
3.3.5 Maswali ya Balagha	93
3.3.6 Mbinu Nyingine za Kisanaa.....	96
3.4 Hitimisho.....	112
SURA YA NNE:UHARIBIFU NA UHIFADHI WA MAZINGIRA	114
4.1 Utangulizi.....	114
4.2 Maudhui	114
4.2.1 Uharibifu wa Mazingira	114
4.2.2 Uhifadhi wa Mazingira.....	122
4.3 Mtindo Katika Uharibifu na Uhifadhi wa Mazingira	124
4.3.1 Tashibihhi.....	124
4.3.2 Tashihisi	128

4.3.3 Chuku	133
4.3.4 Ritifaa	134
4.3.5 Maswali ya Balagha	136
4.3.6 Mbinu Nyingine za Kisanaa	138
4.4 Hitimisho.....	148
SURA YA TANO: UTAMADUNI MAHULUTI	149
5.1 Utangulizi.....	149
5.2 Maudhui	149
5.2.1 Ubepari na Unyonyaji	150
5.2.2 Ukahaba, Uasherati na Usenge.....	154
5.2.3 Vileo na Mihadarati.....	160
5.2.4 Ubaguzi	163
5.2.5 Unafiki wa Kidini.....	165
5.2.6 Elimu ya Kigeni	167
5.3 Mtindo Katika Utamaduni Mahuluti.....	169
5.3.1 Tashihisi	169
5.3.2 Sitiari	173
5.3.3 Tashibihi.....	176
5.3.4 Tasifida.....	179
5.3.5 Maswali ya Balagha	181
5.3.6 Kinaya	183
5.3.7 Chuku	185
5.3.8 Ritifaa.....	186
5.3.9 Mbinu Nyingine za Kisanaa.....	186
5.4 Hitimisho.....	195
SURA YA SITA: DHULUMA NA UKOMBOZI WA WANAWAKE	197
6.1 Utangulizi.....	197
6.2 Maudhui	197
6.2.1 Dhuluma za Kimapenzi Dhidi ya Wasichana na Wanawake	197
6.2.2 Mila na Tamaduni Potofu Zinazowakandamiza Wasichana na Wanawake	206
6.2.3 Ukombozi wa Wanawake na Usawa wa Kijinsia.....	213
6.3 Mtindo Katika Dhuluma na Ukombozi wa Wanawake	214
6.3.1 Tashibihi.....	214
6.3.2 Sitiari	222

6.3.3 Tashihisi	223
6.3.4 Tasifida.....	226
6.3.5 Kinaya	228
6.3.6 Maswali ya Balagha	229
6.3.7 Chuku	232
6.3.8 Mbinu Nyingine za Kisanaa.....	232
6.4 Hitimisho.....	246
SURA YA SABA: MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	248
7.1 Utangulizi.....	248
7.2 Muhtasari wa Matokeo	248
7.3 Hitimisho.....	251
7.4 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi	252
MAREJELEO	253
VIAMBATISHO	257
Kiambatisho I: Boga (<i>Mchezo wa Karata</i>)	257
Kiambatisho II: Nyumba (<i>Mchezo wa Karata</i>)	258
Kiambatisho III: Dau Haliendi! (<i>Mchezo wa Karata</i>)	259
Kiambatisho IV: Mruko wa Nyuki (<i>Bara Jingine</i>).....	260
Kiambatisho V: Mwashahi Mahiri (<i>Bara Jingine</i>).....	263

SURA YA KWANZA

1.1 Utangulizi

Utafiti wowote wa ushairi wa Kiswahili ni nyongeza kwa eneo ambalo tayari limetafitiwa, lenye mawazo na misimamo inayotofautiana. Kwa hivyo, utafiti wowote utakaofanywa haijalishi utachukua mwelekeo gani, lazima ushughulikie masuala mengi na yanayotofautiana. Kwa mfano, kubainisha vigezo vya utafiti kwa sababu uchunguzi wa ujumbe katika ushairi wowote mahususi katika kipindi au mshairi fulani lazima uhusishe uelewa usiobishaniwa wa tafiti zilizokwisha kufanywa. Ili kuelewa dhana ya usasa katika ushairi wa Kithaka wa Mberia, utafiti kama huo lazima usaili na kuelewa mwingiliano baina ya vipengele fulani vya ushairi, kama vile vya kimtindo na kimuundo, ambavyo vimetumika.

Isitoshe, utafiti wa usasa wa kimaudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia lazima uonyeshe na usaili namna mawazo na mwelekeo wake unavyochochewa na utamaduni, historia na usasa kwa sababu uzingatiaji kama huo utawezesha kuweka wazi maudhui ya mshairi na namna maudhui hayo yanajitokeza kupitia uteuzi wa vipengele vya kimuundo, kimtindo na kimsamiati, utendakazi wao na jinsi vinavyoakisi kwa ujumla uandishi wa historia wa Kithaka wa Mberia. Kwa hivyo, katika utafiti huu tunadai kuwa suala la usasa wa kimaudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia una nguzo yake katika usasa wa kihistoria, kwa sababu historia hujenga mitazamo na mielekeo mbalimbali.

Ili kutaka kufahamu vyema uchangamano na mwingiliano wa masuala haya, ni muhimu kuelewa muktadha wa ushairi wa Kithaka wa Mberia, katika historia ya ubadilikaji wa ushairi wa Kiswahili. Ushairi wa Kithaka wa Mberia umo katika kitanzu cha ushairi huru. Ushairi huru ni utunzi wa mashairi bila ya kujifunga kwenye arudhi za vina, mizani, beti, vipande na kibwagizo. Hata hivyo, matumizi ya neno 'huru' yanaweza kumpotosha msomaji kuamini kuwa mashairi ya aina hii hayana sifa maalumu zinazoyatambulisha. Kwa mfano, mtunzi wa mashairi huru bado huzingatia kaida ya mishororo kwa hali fulani. Bradford (1997) anadai kuwa ushairi huru unaweza kuwekwa katika kategoria tatu muhimu: ushairi ambao unazingatia arudhi za ushairi mapokeo kwa kiwango cha chini; mashairi ambayo mshororo unaakisi mazungumzo ya kawaida na mashairi ambayo mshororo usiokuwa na mizani unakiuka mpangilio wa sintaksia.

Mashairi huru si jambo geni katika ushairi wa Kiswahili tu kwa vile yalishuhudiwa katika ushairi wa nchi zingine pia. Baadhi ya wahakiki wa ushairi wa Kiswahili wanadai kuwa ushairi huru uliingizwa katika ushairi wa Kiswahili kutokana na athari za Kimagharibi. Kwa mfano, Mwai (1988) anasema kuwa ushairi huru ulianzishwa kupitia upataji wa maarifa mapya. Washairi walikuwa wamepata maarifa mapya ya jinsi ya kutunga mashairi huru kwa kusoma ushairi wa kimagharibi. Kwa hivyo, walianza kutumia mbinu hizo mpya kutunga mashairi huru ya Kiswahili. Maoni sawa na hayo yanatolewa na Arege (1998) kuwa uchipukaji wa ushairi huru katika Kiswahili ulichochea na usomaji wa kazi za ushairi za kimagharibi miongoni mwa washairi wa Kiswahili.

Kuna mitazamo miwili kuhusu asili na uibukaji wa mashairi huru katika fasihi ya Kiswahili. Baadhi ya wasomi wanadai kuwa ushairi huru wa Kiswahili unahusishwa na juhudi za kuanzia miaka ya 1960 za kuutoa ushairi wa Kiswahili kwenye kanuni za vina na mizani. Wamitila (2002) ana maoni kuwa mapinduzi ya kutunga mashairi huru yaliongozwa na washairi kama Mulokozi na Kahigi (1973), Kezilahabi (1974) na Mazrui (1988) miongoni mwa wengine wengi. Hata hivyo, kuna mtazamo mwingine unaokanusha dai hilo kwa kusema kuwa ushairi huru katika fasihi ya Kiswahili haukuibuka kutokana na athari za kimagharibi, bali ni urejelezi wa umbo la zamani la ushairi uliohusu utunzi wa nyimbo bila vina na mizani miongoni mwa Waswahili:

Chanzo na asili ya ushairi wa Kiswahili ni nyimbo zilizoimbwa katika magoma ya harusi, pungwa, sherehe za jando na unyago, kufanya kazi na kadhalika; hasa pale kazi ilipohitaji ushirikiano. Awali nyimbo hizi hazikuwa na vina wala mizani bali zilifuata mdundo wa ufanyakazi au muktadha mpana wa uimbaji (Njogu na Chimerah, 1999:110)

Uibukaji wa ushairi huru haukupokelewa vyema na wahafidhina wa ushairi mapokeo. Kulingana na Njogu na Chimerah (1999), kundi la wahafidhina linawakilishwa na washairi kama vile Amri Abedi, Abdilatif Abdalla, Shihabuddin Chiraghdin, Hassan Mwalimu Mbega, Ibrahim Noor Shariff, Saadan Kandoro, Mayoka na Ahmad Sheikh Nabhany. Kundi hili lilishikilia kuwa mtunzi wa shairi lolote la Kiswahili lazima azingatie kanuni za ushairi zilizowekwa kama vile vina, mizani, mishororo, beti, vipande na kibwagizo. Kwa kutimiza kanuni hizo kungelipatia shairi la Kiswahili umbo na muundo mahususi. Kwa upande mwingine, waasisi na waliounga mkono ushairi huru walikariri kuwa si lazima kuwa na umbo au muundo maalumu ambao

unatumiwa na mshairi katika utunzi wake. Mawazo ya wanamabadiliko ni kuwa mshairi hastahili kufungwa na sheria ambazo zitakwaza uwazaji na mtiririko wa mawazo yake wakati wa kutunga. Si lazima atunge shairi lenye vina, mizani, mishororo au uwezo wa kuimbika ili liitwe shairi la Kiswahili. Kundi la wanamabadiliko linawakilishwa na washairi kama Jared Angira, Euphrase Kezilahabi, Ebrahim Hussein, Crispin Haule, Mugyabuso Mulokozi na Kulikoyela Kahigi.

Wahafidhina wa ushairi mapokeo wa Kiswahili walihisi na bado wanahisi kwamba ushairi huru utauua ushairi wa Kiswahili polepole kwa kupuuza kanuni za kutunga mashairi. Hata hivyo, wanaotetea ushairi huru wanashikilia kuwa ushairi huru hautaudhalilisha usanii wa washairi wa Kiswahili bali utaupanua, kuueneza na kuuimarisha ushairi huo. Badiliko la mtindo, muundo na umbo la shairi la Kiswahili ni jambo lisiloepukika.

Washairi kadha wa Kiswahili ambao wametunga mashairi huru ni kama vile: Kezilahabi ambaye ametunga *Kichomi* (1974), *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008); Mulokozi na Kahigi: *Mashairi ya Kisasa* (1973), *Malenga wa Bara* (1976) na *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (1979); Mvungi, *Chungu Tamu* (1985); Wa Mutiso, *Mizani Yangu* (1986); Mazrui, *Chembe cha Moyo* (1988); Mohamed, *Jicho la Ndani* (2002); Wa Mberia: *Mchezo wa Karata* (1997), *Bara Jingine* (2001), *Redio na Mwezi* (2005), *Msimu wa Tisa* (2007) na *Rangi ya Anga* (2014).

Kati ya washairi huru hawa wote, ushairi wa Kithaka wa Mberia umejitokeza kuwa wa kipekee, kwa sababu ya miktadha ya kimaudhui, kusemi na mielekeo anayoitumia kutoa usasa wa maudhui katika diwani zake za ushairi. Licha ya hayo, mshairi huyu anateua msamiati wake kutoka kwa mazingira halisi ya mimea na wanyama, ili kuunda sitiari na jazanda za vitu kama wadudu, matunda mbalimbali, miti ya kiasili, ruwaza za hali ya hewa, taratibu za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Jazanda katika ushairi wa Kithaka wa Mberia, usimulizi wake wa kishairi, usemezano na maumbo ya ushairi wake, yajulikanayo kama mashairi-picha, ni ishara za sifa zake za kimtindo kwa jumla ambazo zimetumika ili kuonyesha uhusiano kati ya sifa hizi na maudhui anayoangazia katika ushairi wake.

1.2 Tatizo la Utafiti

Kithaka wa Mberia ni miongoni mwa wanamabadiliko ambao wanatunga mashairi huru badala ya mashairi mapokeo. Watunzi wa mashairi mapokeo hutunga mashairi yao kwa kuzingatia kanuni na arudhi kama vile mizani, vina, beti, mishororo, vipande na kibwagizo. Mashairi huru anayotunga mashairi huyu ni ya kisasa kwa sababu amekiuka kanuni na arudhi zilizofuatwa au zinazofuatwa na wanamapokeo na hivyo kuibua mtindo mpya katika ushairi wake. Katika mielekeo ya ushairi huru, usasa katika ushairi unapimwa kwa namna mashairi anaepuka mitindo ya wanamapokeo katika vipengele vya dhamira, mada, maumbo, dhana na mtindo. Washairi wa kisasa hujaribu ubunifu wao katika nyanja mbalimbali za mitindo mipya na maumbo mapya, matumizi ya lugha na maneno, mielekeo mipya katika kujiwasilisha hasa ujenzi wa taswira. Washairi wa kisasa pia wamebuni mbinu changamano za kuelezea na kuwasilisha maudhui na maana ya maudhui yao.

Usasa wa kimaudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia unabainika wazi katika ruwaza za kiusemi anazozishughulikia. Aidha, miktadha ya kimawasiliano ya mashairi huyu kuhusu siasa na utawala, tofauti za matabaka, maisha ya mijini, mazingira, kilimo, mifumo ya vijiji na masuala ya kitamaduni yanafanya ushairi wake kuwa na maudhui ya kisasa. Isitoshe, usasa unahusiana na namna anavyotumia lugha. Kithaka wa Mberia anatumia sitiari, jazanda, tashihisi na misamiati teule iliyochotwa kutoka katika mazingira halisi ya Kiafrika na vilevile ya kijamii na kisiasa. Hali hii inawezesha uwepo wa kiungo kati ya maudhui anayoyashughulikia na hali za kisasa za kazi zake. Katika kufanya hivyo, mashairi huyu anatumia semi kama vile kinaya, dhihaka na kejeli kwa nia ya kuhamasisha hadhira iangalie upya masuala anayoyaangazia. Masuala haya ndiyo yanafanya ushairi wa Kithaka wa Mberia kuwa na upekee kimaudhui, kimtindo na kimuundo.

Namna Kithaka wa Mberia anavyoshughulikia maudhui ya kisasa na mtindo wake wa kimajaribio, ambao wakati mwingine unajulikana kama wa kimapinduzi umenasa makini ya wasomi mbalimbali. Tafiti zilizofanywa kuhusu ushairi wa Kithaka wa Mberia zinaelekea kuchunguza masuala ya maudhui anayoshughulikia ilhali wengine wamechunguza nafasi na msimamo wake kuhusiana na mabishano kati ya ushairi mapokeo na ushairi huru katika fasihi ya Kiswahili. Wakati ambapo tafiti hizi zote zimetoa mchango ili kuelewa ushairi wa Kithaka wa Mberia; suala la ni vipi maudhui

ya tungo zake yanaonyesha usasa halijatafitiwa. Kwa hali hiyo, suala la kiungo baina ya usasa wa kimaudhui na mtindo wa kimajaribio halijachunguzwa. Hili ndilo suala ambalo tumekusudia kulichunguza katika utafiti wetu.

1.3 Maswali ya Utafiti

Maswali ya utafiti ambayo yananuiwa kujibiwa katika utafiti huu ni:

- a) Je, ushairi wa Kithaka wa Mberia una ruwaza gani za kimaudhui?
- b) Ni mbinu gani za kimtindo ambazo mshairi anatumia kuonyesha usasa wa kimaudhui?
- c) Je, kuna mashairi yenye maumbo maalumu katika ushairi wa Kithaka wa Mberia?
- d) Je, Kithaka wa Mberia anasawiri athari na matokeo ya ukoloni kwa njia gani?

1.4 Malengo ya Utafiti

Katika utafiti huu tumeongozwa na malengo yafuatayo:

- a) Kuchunguza ruwaza mbalimbali za kimaudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.
- b) Kufafanua mawanda ya mbinu za kimtindo zilizotumiwa na mshairi na umuhimu wake.
- c) Kutathmini upekee wa maumbo ya kishairi katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.
- d) Kudadisi ikiwa Kithaka wa Mberia anatathmini athari na matokeo ya ukoloni.

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Kama ilivyotajwa awali, tafiti zilizowahi kufanywa katika ushairi wa Kithaka wa Mberia zimekuwa zikiegemea kwenye masuala ya kijumla kuhusu maudhui bila kuonyesha kiungo kati ya usasa wa kimaudhui na mtindo wa kimajaribio wa mshairi huyu. Utafiti wowote muhimu juu ya ushairi wa Kithaka wa Mberia hauna budi kuonyesha namna historia inavyoimba na kushughulikia masuala yanayokumba watu moja kwa moja, katika wakati wa sasa. Miktadha tofauti ya diskosi ya mawasiliano, washiriki wa usemi na shughuli tofauti za kibinadamu zinazopatikana katika ushairi wa Kithaka wa Mberia zinastahili kutafitiwa ili kuonyesha jinsi maudhui hayo yalivyo ya kisasa. Utafiti huu utawafaidi wanafunzi wa fasihi na wasomi wengine ambao wangetaka kuelewa zaidi juu ya usasa katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

Wasomi na wahakiki wa kifasihi huwa na maoni, falsafa na misimamo tofauti juu ya masuala fulani katika jamii. Katika juhudi za kutaka kuelewa usasa wa kimaudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia, tunataka kugundua vichocheo vinavyomsukuma mshairi kuangazia masuala anuwai anayoyashughulikia katika diwani zake. Katika utafiti huu tunanua kugundua chemichemi ya msukumo wake, namna anavyochukulia masuala hayo na nia ya kuweka masuala hayo wazi kwa hadhira. Tafiti za awali katika ushairi wa Kithaka wa Mberia hazijaonyesha kinachomsukuma mshairi huyu kutunga mashairi yake. Kwa hivyo, katika utafiti huu tunatoa mchango wa maarifa mapya juu ya mjadala na tafiti zilizopo kuhusu ushairi wa Kithaka wa Mberia.

Ni bayana kuwa mshairi huyu anatunga mashairi huru. Hata hivyo, mtindo wake wa uteuzi wa msamiati uliochotwa kutoka kwa mazingira, mpangilio wa kimuundo wa mashairi yake, mbinu za kisimulizi na zaidi ya yote uwasilishaji wa baadhi ya mashairi kwa maumbo maalumu ya picha unafanya ushairi wake kuwa wa kisasa kuliko washairi wengine wanaotunga mashairi huru ya Kiswahili. Ubunifu huu umelazimu utafiti ufanywe kugundua namna mbinu hizi za kimtindo zinamsaidia mshairi kuyafanya maudhui kuwa ya kisasa na hivyo kuwa tofauti na washairi wengine wa wakati wake. Usanii na ubunifu huu ni mambo muhimu yanayostahili kutafitiwa.

Maudhui na mtindo hubadilika katika kazi za kifasihi baada ya muda fulani. Jambo hili hutokana na hali zinavyobadilika na masuala mapya kuchipuka katika jamii na vilevile nia ya mtunzi kujaribu mbinu mpya za kifasihi au athari kutoka kwa wasanii wengine. Wakati ambapo maudhui mengine yamerudiwa katika diwani mpya za mwandishi huyu, kuna pia maudhui mengine mapya yamewasilishwa kulingana na hali na masuala yaliyopo katika jamii ya leo ambayo hayapaswi kupuuzwa. Vilevile, jinsi mshairi anavyoibua masuala tata mapya ndivyo anatumia mbinu za kipekee kimtindo kuangazia masuala hayo. Kwa hivyo, utafiti huu unachukulia kuwa hili ni jambo muhimu kutafitiwa ili kufuatilia mabadiliko ya kimaendeleo, kimaudhui na kimtindo katika ushairi wake.

1.6 Upeo na Mipaka

Katika kuchanganua kwa kina usasa wa kimaudhui na mtindo katika ushairi wa Kithaka wa Mberia, tumetumia diwani zifuatazo, kama vyanzo vya msingi katika

ukusanyaji wa data, uchanganuzi, ufasiri wa data na uwasilishi wa matokeo ya utafiti: *Mchezo wa Karata* (1997), *Bara Jingine* (2001), *Redio na Mwezi* (2005) *Msimu wa Tisa* (2007) na *Rangi ya Anga* (2014).

Katika utafiti huu tunaangazia usasa wa maudhui kama unavyoweza na mtindo hususan katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Baadhi ya maudhui yanayochanganuliwa ni: unafiki miongoni mwa wanasiasa, udikteta, ukoloni, ukandamizaji wa wanyonge, ufitadi, ugaidi, uharibifu na uhifadhi wa mazingira, matumizi ya dawa za kulevya, ukahaba, ubaguzi wa rangi, unafiki wa kidini na dhuluma kwa wanawake miongoni mwa mengine mengi. Haya ni masuala yaliyopo katika jamii ya leo na kwa hivyo yanastahili kushughulikiwa. Utafiti huu unanua kuonyesha namna masuala haya yanaathiri maisha ya watu, jinsi watu wanavyoyachukulia na kuyashughulikia. Ili kuchanganua usasa wa kimaudhui kwa njia bayana, utafiti huu unaainisha maudhui hayo katika matapo yafuatayo: siasa, utawala na mamlaka katika mataifa ya Afrika, uharibifu na uhifadhi wa mazingira, utamaduni mahuluti na dhuluma na ukombozi wa wanawake katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

Fauka ya hayo, katika utafiti huu pia tunaangazia mtindo wa kibunifu, uteuzi wa msamiati na jinsi unavyomwezesha kuwasilisha maudhui katika kazi zake. Unagusia mambo kama tamathali za usemi, usimulizi, usemezano na maumbo ya kipicha na umuhimu wake katika kuwasilisha maudhui. Hata hivyo, utafiti huu haulinganishi usasa wa kimaudhui na mtindo wa Kithaka wa Mberia na washairi wengine wa wakati wake kwa sababu itakuwa ni kupanua upeo wa utafiti huu. Hakuna muda wa kutosha wa kufanya utafiti wa kina hicho. Isitoshe, ni muhimu kujikita tu kwenye malengo ya utafiti huu pekee.

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Watafiti ambao wamefanya utafiti katika ushairi wa Kithaka wa Mberia wamejishughulisha sana na aina za maudhui, namna maudhui hayo yamejitokeza katika ushairi huru na umuhimu wake katika jamii. Watafiti hao, labda kwa sababu ya mielekeo yao ya utafiti wameweka pembeni masuala mengine muhimu pia kama vile uhusiano kati ya usasa wa kimaudhui na mtindo wake wa kibunifu. Kwa hivyo, mapitio ya yaliyoandikwa katika sehemu hii yanaonyesha, kwa ujumla tafiti ambazo

zimekwishafanywa kuhusu maudhui, maumbo na mtindo katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

Katika mwelekeo huu wa mapitio, tuna nia ya kuchunguza iwapo kuna watafiti ambao wamejishughulisha kuelewa uhusiano kati ya maudhui na mtindo katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Kuna umuhimu pia kujaribu kuelewa ikiwa kuna watafiti ambao wamejaribu kuelewa usasa katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Jambo lingine lenye mshawasha katika mapitio haya ni kutaka kuchunguza kama kuna mambo muhimu katika ushairi wake ambayo hayajapewa kipaumbele katika mijadala ya ushairi mapokeo na ushairi huru.

Kithaka wa Mberia ni mwanamabadiliko na mtetezi wa utunzi wa mashairi huru, ambayo ni mashairi ya kisasa. Anaamini kuwa shairi la Kiswahili si lazima liwe na vina na mizani kama wanavyodai wanamapokeo. Wa Mberia (1990) akitetea nia yake ya kutunga mashairi huru anasema kuwa ushairi wa mtiririko badala ya kuuangusha ushairi wa Kiswahili, utaupanua, kuusambaza na kuuimarisha. Anadai kuwa wazungumzaji wa Kiswahili ambao wangependa kuwasilisha fikira zao kwa ushairi lakini wakawa ama wanatishika na umbo la kulazimishwa la mashairi ya Kiswahili au kupuuzwa vina na mizani kwa kusema kwamba ni utamaduni wa Waswahili, sasa wataweza kuchangia ukuzaji na maendeleo ya ushairi wa Kiswahili.

Kwa maoni ya Wa Mberia (khj), kutakuwa na watunzi sio tu kutoka Pate, Lamu, Mombasa na Tanga, bali pia kutoka Lodwar, Nyahururu, Gulu na Mwanza. Hayo yatakuwa sio tu maendeleo ya ushairi wa Kiswahili, bali pia ukuzaji na utukuzaji wa lugha ya Kiswahili kwa jumla. Msimamo wake kuhusu mjadala wa umbo la mashairi ni kuwa badala ya ushairi wa mtiririko kuangusha ushairi wa Kiswahili, pingamizi na vikwazo vya kukuza na kuendeleza Kiswahili ndivyo vitakavyoanguka.

Tafiti zilizofanywa kuhusu mtindo katika ushairi wa Kithaka wa Mberia zinaonyesha kuwa mashairi hutunga mashairi ya kipekee kimaumbo na kimuundo. Kwa mfano, Ndung'o na Mwai (1991) wanasema kuwa hakuna ushahidi wowote kuwa mashairi-picha yalikuwepo katika ushairi huru wa Kiswahili hadi wakati yanapoanza kujitokeza katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Mashairi-picha kama vile "Boga" (uk. 2), "Nyumba" (uk. 17) na "Dau Haliendi!" (uk. 32) katika diwani ya *Mchezo wa*

Karata na “Mruko wa Nyuki” (uk. 20) na “Mwashi Mahiri” (uk. 45) katika diwani ya *Bara Jingine* ni mashairi yenye upekee kimaumbo na kimuundo na hivyo yanaonyesha utunzi wa kisasa katika ushairi wa Kithaka wa Mberia na ushairi wa Kiswahili kwa jumla.

Utafiti mwingine kuhusu ushairi wa Kithaka wa Mberia ni wa Ngari (1998). Ngari ameibua mjadala kuhusu namna Kithaka wa Mberia anatetea haki za wafanyakazi, watawaliwa, wakulima na maskini katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Amechanganua jinsi wanyonge hunyanyaswa kiuchumi, kisiasa na kitabaka. Alitumia nadharia ya Umaksi kuchanganua shida za wanyonge. Nadharia ya Umaksi inaonyesha mvutano wa kitabaka unaoendelea kati ya mabwanyenye na wafanyakazi. Katika kuangazia suala la utetezi wa wanyonge, Ngari amechanganua baadhi ya vipengele vya kimtindo alivyotumia mshairi kuzungumzia juu ya dhuluma kwa wanyonge. Amechambua vipengele kama vile tashibihii, maswali ya balagha, urudiaji na mashairi-picha.

Ingawa uhakiki wa Ngari ni muhimu katika kufafanua maudhui machache ya kisasa ya mshairi, alikusanya na kuchanganua data yake kutoka diwani moja pekee, kulingana na malengo ya utafiti wake. Isitoshe, vipengele vya kimtindo alivyoangazia ni vichache, kuliko vile vimechanganuliwa katika utafiti huu. Fauka ya hayo, mjadala huu hauonyeshi wazi uwiano wa usasa wa maudhui na jinsi mtindo wa kiubunifu unawezesha kuzungumzia masuala hayo kwa ufasaha. Tofauti na Ngari ambaye ametumia data kutoka diwani moja ya mshairi, katika utafiti huu tumekusanya na kuchanganua usasa wa maudhui na mtindo kutoka diwani zingine nne zaidi (*Bara Jingine, Redio na Mwezi, Msimu wa Tisa na Rangi ya Anga*) za Kithaka wa Mberia. Malengo ni kuchanganua ruwaza za kimaudhui zinazojitokeza, kuchunguza ufaafu wa mashairi-picha, mbali na kudadisi vile mshairi anatathmini historia na athari za ukoloni katika ushairi wake. Fauka ya hayo, wakati Ngari alitumia nadharia moja ya Umaksi kuzungumzia suala la wanyonge, sisi tumetumia nadharia mbili: nadharia ya baadaukoloni kuangazia usasa wa maudhui na nadharia ya elimumitindo mkabala wa uhakiki mpya kuchanganua mtindo katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

Tahakiki juu ya sitiari za kimchoro katika ushairi wa Kithaka wa Mberia imefanywa na Wamitila (2002). Wamitila anasema kuwa kuna matumizi ya sitiari za kimchoro

katika diwani za Mberia za *Mchezo wa Karata na Bara Jingine*. Mashairi yenye sitiari za kimchoro katika diwani ya *Mchezo wa Karata* ni “Boga” (uk. 2), “Nyumba” (uk. 17) na “Dau Haliendi!” (uk. 32). Katika diwani ya *Bara Jingine*, kuna mashairi kama “Mruko wa Nyuki” (uk. 20) na “Mwashi Mahiri” (uk. 45). Wamitila anaendelea kusema kuwa sitiari hizi ni mbinu za uchimuzi; zinaweka bayana dhamira za tungo zinazohusika. Sitiari za aina hii zinatumiwa katika ushairi wa aina hii ambao hujulikana kama ‘ushairi-ruwaza’. Katika utunzi wa mashairi huru, uchimuzi unaweza kutokea kwa njia ya mpangilio wa utungo. Tunapoliangalia shairi kwa macho, tunaona limechukua muundo fulani. Tahakiki hii imetufaa tunapochanganua mashairi-picha na kuonyesha umuhimu wake katika uchanganuzi wetu.

Mwingiliano kati ya fani na maudhui ni utafiti mwingine ambao umeshughulikiwa katika ushairi wa Kithaka wa Mberia na Nzuki (2003). Nzuki amechanganua maudhui ya siasa, mazingira, utamaduni na dhuluma za kimapenzi kwa kutumia nadharia ya sosholojia. Aidha, amechanganua namna mshairi anatumia tashibihi, sitiari, kinaya na uhuishaji kuwasilisha maudhui yake kwa hadhira kwa kuegemea nadharia ya umuundo. Zaidi ya hayo, ametathmini ufaafu wa mashairi-picha katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Utafiti wa Nzuki umetuwekea msingi thabiti wa kuendeleza mjadala zaidi kuhusu usasa wa kimaudhui na mtindo katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

Hata hivyo, utafiti wa Nzuki (khj) unatofautiana na utafiti wetu kwa njia kadha. Kwanza, Nzuki hajaonyesha ruwaza zozote za kimaudhui zinazojitokeza katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Jambo hili linajitokeza katika utafiti wetu. Pili, hakuchanganua kwa kina maudhui yanayojitokeza katika diwani mbili alizozihakiki. Aidha, hajaonyesha namna mshairi anatathmini historia katika ushairi wake. Isitoshe, kuhusu mtindo alioutumia mshairi kuwasilisha maudhui, Nzuki hajachanganua kikamilifu juu ya uteuzi wa msamiati unaohusu wadudu, miti, matunda, usimulizi, mgao wa kitamthilia na mbinu nyingine nyingi.

Wakati ambapo Nzuki (khj) alikusanya data yake juu ya mwingiliano kati ya fani na maudhui kutoka diwani ya *Mchezo wa Karata na Bara Jingine*, katika utafiti wetu tumeongezea diwani zingine tatu (*Redio na Mwezi*, *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*), ili kuangazia maudhui zaidi mbali na kushughulikia mtindo wa kiubunifu

aliouzua kuangazia masualaibuka. Alitumia nadharia mbili: nadharia ya sosholojia, ambayo ilimsaidia kuchanganua maudhui mbalimbali na jinsi yanaathiri jamii ya mtunzi na nadharia ya umuundo, ambayo ilimsaidia kuangazia suala la lugha na maumbo maalumu aliyoyatumia mshairi, hasa mashairi-picha. Kwa upande wetu, tumetumia nadharia mbili tofauti ambazo ni nadharia ya baadaukoloni, inayotumika kuchambua usasa wa kimaudhui na nadharia ya elimumitindo mkabala wa uhakiki mpya inayotumika katika kuchanganua usasa wa mtindo, kwa mujibu wa malengo ya utafiti huu.

Suala la mabadiliko katika umbo la ushairi na athari zake katika ushairi wa Kiswahili limeshughulikiwa na Indede (2008). Indede amechunguza suala la kuepuka matumizi ya vina, mizani, beti na muwala katika ushairi mapokeo na kuingia kwa mtindo mpya wa utunzi wa mashairi huru. Ametathmini ubadilikaji wa umbo la shairi katika mashairi ya Alamin Mazrui (1988), Said Mohamed (2002) na Kithaka wa Mberia (*Mchezo wa Karata* 1997, *Bara Jingine* 2001). Indede anasema kuwa miundo hii mipya ni mabadiliko makubwa katika ushairi wa Kiswahili na hivyo itaandikisha historia mpya katika ushairi. Hata hivyo, maumbo hayo mapya ya Kithaka wa Mberia yanazua athari nyingine katika uhakiki na uchambuzi wa ushairi. Ikiwa maumbo haya yanadhihirisha uwazi wa ayasemayo mtunzi, basi mhakiki atafanya kazi gani ilhali mtunzi ashamdokezea kuhusu taswira ya maudhui yake? Ubora wa ushairi hutokana na uchangamano wa ufasiri wa maudhui yake yanayotokana na taswira anazoziumba mhakiki na kumwongoza katika kufikia ufasiri mwafaka.

Indede (khj) anatoa mfano anapolinganisha shairi “Boga” (Wa Mberia 1997:2-3) na shairi “Mnazi Vuta N’kuvute” (Abdalla 1973:17-22). Katika ngonjera, hii mhakiki anaumba taswira ya watu wawili ambapo Badi amekwea mnazi na kukatalia huko juu na Ali amenyimwa nafasi ya kuukwea huo mnazi. Ijapokuwa katika mashairi yote mawili picha tunayoipata inahusu kunyanyaswa kwa kunyimwa haki, umbo la boga ni wazi zaidi kuliko taswira ya mnazi ambapo mhakiki lazima atumie akili yake kufichua siri iliyopo. Hata shairi “Mruko wa Nyuki” (Mberia 2001:20-25) lina sifa hiyo. Kuna hatari katika kuonyesha uwazi katika fasihi kwa sababu ufiche ni kipengele muhimu katika fasihi na humpa mhakiki nafasi ya kudadisi yaliyomo kwa hekima yake. Tahakiki ya Indede kuhusu mabadiliko katika umbo la shairi na athari

zake katika ushairi wa Kiswahili ni muhimu katika utafiti wetu kwa kuwa tunachambua ufaafu wa mashairi-picha katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

Tahakiki nyingine ya Indede (2011) kuhusu utata wa mwanamke katika ushairi wa kisasa ni mjadala mwingine wa kiusomi unaogusia ushairi wa Kithaka wa Mberia. Anasema kuwa ushairi wa 'karne mpya' umejitokeza na taswira ya kuogofya ya mwanamke. Umbo tunalolipata katika ushairi wa karne hii si la mwanamke kuwa ua au pambo tena, bali mwanamke kuwa chombo cha madhila na unyanyasaji katika matukio ya aina tofauti kutokana na maisha ya ndoa, siasa, dini, vita na kazi. Kwa mfano, Kithaka wa Mberia (2007:28) katika shairi "Mkataba Tena" analalamikia aina mbalimbali za mikataba inayofanywa baina ya mataifa tofauti. Kwa Mberia, mikataba hii ni kinaya kitupu kwani mwishowe huishia katika kuchafua ardhi kwa risasi na mabomu. Mikataba hii huwanyang'anya wananchi haki yao. Aelezeavyo Kithaka wa Mberia ni kwamba askari wanaofanya mazoezi huja na magenge ya uhuni na ubakaji. Nia yao hasa huwa ni kuwatega wanawake na kuwaacha kwenye majonzi na huzuni akilini daima. Uchanganuzi huu wa Indede kuhusu taswira tata ya mwanamke katika ushairi wa kisasa ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu tunaangalia pia dhuluma na ukombozi wa wanawake katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

Utafiti mwingine kuhusu ushairi wa Kithaka wa Mberia umeendelezwa na Gicuku (2011). Gicuku amechunguza juu ya usawiri wa maudhui ya ndoa katika ushairi wa Euphrase Kezilahabi na Kithaka wa Mberia. Katika kuendeleza utafiti huu, mtafiti ameteua ushairi wa Euphrase Kezilahabi; *Kichomi* (1974) na wa Kithaka wa Mberia *Bara Jingine* (2001) na *Msimu wa Tisa* (2007). Kulingana na Gicuku (khj), ndoa ni asasi muhimu na ya kimsingi katika maisha ya binadamu. Ndoa ni mojawapo ya asasi zinazohakikisha kuendelea kwa jamii. Utafiti huu umechochewa na imani kwamba ndoa ina manufaa na ndio msingi wa familia na pia hujenga jamii. Utafiti huu umetufaa kwa vile tumeangalia namna mwanamke ananyanyaswa katika ndoa kupitia dhuluma za kinyumbani.

Utafiti wa Gicuku umeongozwa na nadharia ya umuundo-tekelezi. Katika nadharia hii, jamii ni mfumo unaochangiwa na vipengele vyake vyote ili kuleta mshikamano na utangamano. Nadharia ya umuundo-tekelezi inasisitiza juu ya utekelezaji wa majukumu ya wanajamii ili waendeleo kuwa vipengele muhimu vya jamii. Gicuku

amebainisha namna Kezilahabi alivyosawiri changamoto katika asasi ya ndoa pamoja na hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kukabiliana na changamoto hizo. Aidha, ameonyesha changamoto katika asasi ya ndoa kama zinavyojitokeza katika ushairi wa Kithaka wa Mberia na namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

Utafiti wa Gicuku unatufaa katika uchanganuzi wetu kwa sababu tunazungumzia suala la mapenzi nje ya ndoa kama unafiki wa wanandoa unaochangia maambukizi ya virusi vya ukimwi mbali na kutokea kwa talaka miongoni mwa wanandoa. Hata hivyo, utafiti wa Gicuku ni tofauti na wetu kwa sababu ameangazia suala la ndoa kwa kujikita katika diwani mbili za watunzi wawili tofauti. Fauka ya hayo, ametumia nadharia moja kuchanganua mada yake ilhali sisi tunatumia nadharia mbili: baadaukoloni na elimumitindo mkabala wa uhakiki mpya ili kuchanganua maudhui na mtindo, mtawalia, katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

Uchanganuzi wa mashairi-picha kama sitiari katika baadhi ya mashairi ya Kithaka wa Mberia ni utafiti mwingine wa kiusomi ulioshughulikiwa na Sangili (2012). Kama lengo kuu, utafiti huu umelenga kuchanganua ushairi-picha kama sitiari katika mashairi teule ya Kithaka wa Mberia. Sampuli ya utafiti wa Sangili ni mashairi saba katika jumla ya mashairi 137 katika diwani ya *Mchezo wa Karata* (1997), *Bara Jingine* (2001) na *Redio na Mwezi* (2005). Ili kutimiza lengo hili, amezingatia madhumuni kama vile: kutambua na kujadili ngazi mbili za ubunifu katika mashairi teule; kuchanganua maumbo ya mashairi-picha kama sitiari katika mashairi teule na kujadili umuhimu wa taipografia katika kuchanganua ushairi-picha katika mashairi teule.

Utafiti wa Sangili umeongozwa na nadharia mbili: kiunzi cha kinadharia cha taswira na nadharia ya ushuhunuzinafsi kifasihi. Wananadharia wa nadharia ya taswira hudai kwamba taswira au picha ichanganuliwe katika ngazi zake mbili, yaani ngazi ya maneno na ngazi ya picha ilhali wananadharia ya kisasa ya sitiari hudai kwamba sitiari iweze kuchanganuliwa kwa kuhusisha elementi nyinginezo zinazoumba sitiari maalumu. Wananadharia wa ushuhunuzinafsi kifasihi hudai kuwa elementi nyinginezo zinazomwathiri msanii zichanganuliwe ipasavyo.

Utafiti wa Sangili ni muhimu katika utafiti wetu, kwa vile tunachunguza matumizi na ufaafu wa mashairi-picha, kama kipengele kimojawapo cha kimtindo alichotumia mshairi kuwasilisha maudhui mbalimbali kwa wasomaji. Hata hivyo, kuna vipengele vingine kama vile uteuzi wa msamiati, usimulizi, mgao wa kitamthilia na ndoto, ambavyo havijitokezi katika utafiti wake lakini tumeviangazia katika utafiti wetu. Data ya Sangili imetoka katika diwani tatu za mshairi, lakini katika utafiti huu, tunatumia diwani tano za Kithaka wa Mberia. Aidha, katika utafiti wa Sangili na wetu tumetumia nadharia mbili lakini zinazotofautiana kulingana na malengo ya utafiti husika.

Suala la matumizi ya kinaya katika ushairi wa Kithaka wa Mberia limeshughulikiwa na Nyambura (2014). Madhumuni ya mtafiti huyu ni pamoja na kubainisha sababu kuu ya kinaya cha dhihaka katika ushairi wa Kithaka wa Mberia, kubainisha namna kinaya kimetumika katika ushairi wa Kithaka wa Mberia na kuchanganua uamilifu wa kinaya cha dhihaka kama mbinu ya kisanaa katika utunzi wa mashairi. Katika utafiti huu ametumia mihimili ya nadharia ya elimumitindo iliyoasisiwa na Leech (1969). Mwananadharia huyu anadai kuwa lugha ni chombo muhimu katika kuelewa ujumbe katika mashairi. Aidha, mtafiti huyu ameteua mashairi mbalimbali yaliyotumia kinaya kutoka diwani nne za Kithaka wa Mberia ambazo ni: *Mchezo wa Karata* (1997), *Bara Jingine* (2001), *Redio na Mwezi* (2005) na *Msimu wa Tisa* (2007). Utafiti wa Nyambura umeonyesha vile mshairi ametumia kinaya katika masuala ya kisiasa, kiuchumi na ya kijamii.

Utafiti wa Nyambura umetufaa kwa kuwa ameangazia matumizi ya tamathali ya kinaya katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Wakati ameangazia tamathali moja, utafiti wetu umeangazia tamathali zaidi zinazojitokeza katika ushairi wa Kithaka wa Mberia kama vile tashibihi, sitiari, tasifida, chuku, ritifaa, maswali ya balagha, takriri na tashihisi. Aidha, tumeangazia mbinu nyingine za kisanaa kama vile nyimbo, ndoto, usimulizi na nidaa miongoni mwa nyingine nyingi. Fauka ya hayo, utafiti wa Nyambura kuhusu matumizi ya kinaya umeongozwa na nadharia moja ya elimumitindo ilhali katika utafiti huu tumeongozwa na nadharia ya baadaukoloni kuangazia usasa wa kimaudhui na nadharia ya elimumitindo mkabala wa uhakiki mpya kuchanganua vipengele anuwai vya mtindo wa mshairi.

Ukiushi ni suala jingine ambalo lajitokeza katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Njuguna (2015) ameshughulikia ukiushi katika mashairi teule ya Amri Abedi na ya Kithaka wa Mberia. Mtafiti amejikita katika diwani mbili za mashairi: *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1954) na *Mchezo wa Karata* (1997). Uteuzi wa diwani hizo umefanywa kwa kuwa zimedhihirisha matumizi ya ukiushi. Katika utafiti wake, Njuguna amezingatia matumizi ya ukiushi wa msamiati, ukiushi wa sarufi, ukiushi wa maumbo na ukiushi wa awamu ya kihistoria katika mashairi husika.

Katika utafiti huu, ameongozwa na nadharia changamano: nadharia ya kimtindo na nadharia ya kihemenitiki. Mihimili ya nadharia ya kimtindo kwa mujibu wa Leech (khj) imetumika kubainisha aina za ukiushi zilizotumika katika utunzi wa mashairi husika. Mihimili ya nadharia ya kihemenitiki imemwongoza mtafiti katika ufasiri wa ujumbe wa mashairi. Mtafiti ameshughulikia ukiushi wa msamiati katika mashairi huru na ya arudhi. Aidha, ameshughulikia ukiushi wa sarufi na maumbo katika mashairi huru. Vilevile, amezingatia ukiushi wa awamu ya kihistoria katika mashairi ya arudhi.

Katika utafiti wake, Njuguna amebaini kuwa ukiushi wa msamiati umetumiwa katika mashairi ya Abedi na Kithaka wa Mberia lakini uteuzi wao wa msamiati ni tofauti. Hata hivyo, umetumiwa kuchimuza ujumbe wao. Ukiushi wa sarufi umebainika katika mashairi huru teule. Ukiushi huu, umetumiwa kusesitiza ujumbe pamoja na kuyapa mashairi mahadhi. Ukiushi wa maumbo umedhihirika katika mashairi huru kupitia sitari za kimchoro. Ukiushi huu umetumiwa kuchimuza na kusesitiza ujumbe. Ukiushi wa awamu ya kihistoria umepatikana katika mashairi ya arudhi kupitia maneno ya kilahaja na yale yenye asili ya Kiarabu katika ushairi wa Abedi. Matumizi ya ukiushi huu yanafanikisha urari wa vina na mizani.

Utafiti wa Njuguna ni muhimu katika utafiti wetu. Suala la ukiushi wa maumbo na msamiati katika ushairi wa Kithaka wa Mberia ni suala ambalo tumelichunguza pia. Hata hivyo, Njuguna hajachanganua maudhui, ilhali tumeangazia maudhui katika diwani tano za ushairi wa Kithaka wa Mberia. Matumizi ya nadharia ya elimumitindo katika kuangazia ukiushi kama mtindo walioutumia Amri Abedi na Kithaka wa Mberia ni sawa na ile tumetumia kuangazia mtindo, ijapokuwa sisi tumetumia mkabala wa uhakiki mpya. Kwa upande mwingine, wakati Njuguna ametumia

nadharia ya kihemenitiki kufasiri ujumbe wa mashairi, tumetumia nadharia ya baadaukoloni kuchanganua maudhui mbalimbali katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

1.8 Msingi wa Kinadharia

Katika utafiti huu, tumeangazia masuala mawili tofauti lakini yenye uhusiano wa karibu; usasa wa kimaudhui kama unavyoweza na mtindo katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Nadharia moja haingeweza kushughulikia masuala yote mawili kikamilifu. Kwa hivyo, tungetumia nadharia mbili kuchanganua masuala yote mawili. Nadharia ya baadaukoloni imetumika kuchanganua usasa wa maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia kutoka kipindi cha ukoloni na baada ya ukoloni. Kwa upande mwingine, nadharia ya elimumitindo mkabala wa uhakiki mpya imekuwa mwafaka katika kuchanganua matumizi ya mbinu za kimtindo na mbinu nyingine za kisanaa anazotumia mshairi kuwasilisha maudhui katika diwani zake.

1.8.1 Nadharia ya Baadaukoloni

Nadharia ya baadaukoloni ilizuka miaka ya themanini na tisini. Waasisi wakuu wa nadharia ya baadaukoloni kwa mujibu wa Baldick (2001) ni Said, Spivak na Bhabha. Nadharia ya baadaukoloni ni dhana pana ambayo inazidi kubadilika ili kujumuisha dhana kama vile uhakiki wa kifeministi na uhakiki wa kimaksi. Wananadharia wengi wa baadaukoloni, wahakiki wa baadaukoloni na wanaharakati wametumia mawazo ya Umaksi ili kuunga kujitokeza tena ujitambulishaji wa kitaifa, ujitambulishaji wa kijamii na ujitambulishaji wa kitamaduni katika enzi ya baadaukoloni. Mavuguvugu mengi ya kitaifa katika karne ya ishirini yaliyosaidia kuleta uhuru kwa mataifa yaliyotawaliwa na wakoloni, yalishawishiwa na kuchochewa na Umaksi. Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa wahakiki waliofuatia baadaye kuanzia Fanon (1967), ambaye alipigania uundaji wa fasihi ya kitaifa kama njia muhimu ya ujitambulishaji wa baadaukoloni, hadi kwa Bhabha (1990), ambaye amechunguza uhusiano kati ya utaiifa na uvyazaji wa kitamaduni kutoka kwa mikabala anuwai.

Vilevile, wanawake katika nchi nyingi zilizotawaliwa na wakoloni wameangalia hali yao tofauti na wanaume, hasa katika zile tamaduni ambapo shinikizo za kikoloni zikiunganishwa pamoja na misimamo asili ya kiume imewakandamiza maradufu. Wahakiki wa kifeministi katika ulimwengu wa tatu kama vile Spivak (1988) wametumia nadharia ya baadaukoloni kuweka wazi masuala yao.

Wananadharia hawa huangazia masuala ya kisiasa, utamaduni na ujitambulishaji wa kitaifa, “uwingine” yaani utofauti wa kijinsia, rangi, na uwezo wa kiuchumi. Isitoshe, wao huangazia suala la mbari, ubeberu na suala la lugha wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Barry (2002) anasema kuwa nadharia ya baadaukoloni imepata umaarufu kupitia vitabu kama vile: *In Other Worlds: Essays in Cultural Politics* (Spivak 1987), *The Empire Writes Back* (Ashcroft 1989), *Nation and Narration* (Bhabha 1990) and *Culture and Imperialism* (Said 1993).

Shughuli moja muhimu inayokabili nadharia na uhakiki wa baadaukoloni ni kueleza tofauti za tajiriba za mataifa na watu waliojinasua kutokana na ukoloni. Kwa mfano, Padley (2006) anasema kuwa uhakiki wa baadaukoloni umejaribu kufahamu kuwa tambuzi na miitiko ya watu waliotawaliwa kule India au Afrika, ambapo Wazungu walilazimisha thamani zao za kijamii, kitamaduni na kisiasa kwa wenyeji zinaweza kuwa tofauti na tajiriba za watu wa Marekani ya Kati na Kusini walioteseka wakiwa uhamishoni na hivyo wakapoteza ujitambuzinafsi wao.

Nadharia ya baadaukoloni huangazia vitendo na mambo muhimu ya kitamaduni yanayoonyesha tajiriba anuwai za kikoloni. Mwelekeo wa uhakiki wa kazi za baadaukoloni unajikita kuwili: kwanza, unachunguza kazi zilizoandikwa na waandishi kutoka mataifa ya kibeberu kuhusu vipengele fulani vya utamaduni uliotawaliwa; na pili ni kuchunguza kazi zilizoandikwa na wakaazi wa tamaduni zenyewe kuhusu tajiriba za ukoloni na matokeo yake. Kwa hivyo, uchunguzi wa usasa wa maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia unaangazia athari za tajiriba za ukoloni na matokeo yake baada ya ukoloni.

Jambo moja kuhusu kazi zilizoandikwa na waandishi wa kikoloni ambalo wahakiki wa baadaukoloni hunuia kufichua ni jinsi kazi hizo zinavyochora utamaduni na wakaazi waliotawaliwa kuwa duni wakilinganishwa na wenzao wa nchi za Magharibi na Ulaya. Said, ambaye ndiye mwasisi mkuu wa nadharia ya baadaukoloni, katika maandishi yake muhimu kama vile *Orientalism* (1978) na *Culture and Imperialism* (1993), ameonyesha namna maandishi ya kikoloni yanavyohibitisha na kuendeleza siasa na utamaduni wa mbeberu na kuwachora waliotawaliwa kama watu duni na tofauti nao. Kwa hivyo, lugha ilitumika kumnyanyasa na kumkandamiza mtawaliwa na kumchora kwa njia hasi. Hii ndiyo ilikuwa awamu ya kwanza ya uhakiki wa baadaukoloni.

Katika sehemu ya pili ya karne ya ishirini, wakaazi wa nchi zilizotawaliwa walianza kujiunga tena na historia na desturi zao zilizowekwa pembeni kwa mapendeleo ya thamani za wabeberu. Padley (2006) anadai kuwa katika fasihi, hali hii ilijitokeza kulipozuka maandishi mengi ya baadaukoloni. Hii ndiyo ilikuwa awamu ya pili ya uhakiki wa baadaukoloni. Waandishi hawa walinuia kujichunguza kwa nia ya kujielewa na kujitambua pamoja na jamii zao. Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007) mfano wa maandishi hao ni kama Ngugi wa Thiong'o, Chinua Achebe, Ben Okri, Salman Rushdie, Alamin Mazrui na Said Mohamed.

Kanuni mojawapo ya nadharia ya baadaukoloni ni ufahamu wa jinsi watu wasio Wazungu wanavyosawiriwa kama watu waovu na tofauti. Mbari na koo zimetumiwa kwa njia zinazoweza na kukandamiza. Hall (2001) anasisitiza kuwa uchanganuzi wa baadaukoloni unaanza kwa kutambua kuwa uwezo wa kijamii unaopachikwa kwa makundi ya mbari na koo umeibua dhuluma nyingi. Ubaguzi wa mbari na koo ni kero kwa karibu kila jamii na eneo la ulimwengu kwa vile tofauti za rangi, lugha na desturi zimetumika kuonyesha kuwa kundi moja ni bora kuliko jingine. Kuna wenye nguvu kiuchumi, kisiasa na kiteknolojia kuliko wengine. Hii ni dhana ya uwingine katika nadharia ya baadaukoloni. Hali hii inafaa kushughulikiwa kwa vile matokeo yake yanashuhudiwa kupitia vita baina ya mataifa yenye ushawishi mkubwa ulimwenguni, mashambulizi ya kigaidi na uhalifu mwingine mwingi mijini. Ushairi wa Kithaka wa Mberia unaangazia masuala yanayoonyesha vile mataifa yaliyostawi na yenye uwezo mkubwa yanatumia nafasi zao kukandamiza mataifa machanga. Kwa sababu hiyo, visa vya ulipizaji kisasi kwa njia ya mashambulizi ya kigaidi vinashuhudiwa katika nchi nyingi ambapo watu wasio na hatia wanapoteza maisha yao ilhali wengine wanaachwa na makovu kwenye miili yao.

Kanuni ya pili ya nadharia ya baadaukoloni ni kuwa nguvu za upanuzi na ulafi wa kiuchumi zinaakisiwa katika historia ndefu ya ubeberu na ukoloni. Utumwa, uporaji wa mali na unyanyasaji ni baadhi ya vitendo vya maamuzi yasiyo ya haki. Katika kipindi cha karne ya kumi na nane na kumi na tisa, mataifa ya Ulaya yaling'ang'ania kudhibiti maeneo mengine ya ulimwengu huku yakipora mali na kunyanyasa wakaazi wa maeneo hayo. Tamaduni zilizokuwa na maadili mema na ustaarabu wa kiasili ziliharibiwa, pale dini, lugha na maadili za Wazungu zilianzishwa miongoni mwa wakaazi hao. Kwa kujikita katika kanuni hii, mshairi anaangazia vile wafanyakazi,

hasa wakulima wanatia bidii katika mashamba yao kukuza mazao yanayoishia kwenye masoko ya ughaibuni lakini wanalipwa fedha kidogo sana kwa mazao yao. Huu ni mfano mzuri wa unyanyasaji wa kiuchumi. Isitoshe, wafanyakazi wengine wanafanya kazi shuleni, viwandani na kwenye kampuni kwa muda mrefu katika mazingira duni na wanalipwa malipo duni. Masefule au wanyonge hawana haki wala mtu wa kuwatetea na kusikiliza shida zao. Mataifa ya Kiafrika hutia sahihi mikataba ya kibiashara na mataifa yaliyostawi yakiwa na matumaini kuwa mikataba hiyo itawanufaisha wote lakini mataifa haya yenye uwezo, nguvu na ushawishi mkubwa hufaidika zaidi. Licha ya hayo, Waafrika waliacha mila na tamaduni zao nzuri wakapapia Ukristo na utamaduni mwingine wa kigeni wenye maovu mengi. Hivyo ndivyo historia imejikita kwa njia ya usasa katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

Uchunguzi wa urithi wa matumizi ya nguvu za kikatili na athari za utawala wa Ulaya kwa wakaazi wa bara la Afrika, Asia na Kaskazini, Kati na Kusini mwa Amerika ni kanuni ya tatu ya nadharia ya baadaukoloni. Nadharia ya baadaukoloni inanua kuchunguza matokeo ya kisiasa na kitamaduni ya ukoloni na vilevile kutathmini mabadiliko makubwa yaliyoletwa kwa watawaliwa. Kithaka wa Mberia anaangazia dhana za mamlaka na utawala kama zinavyojitokeza katika nchi huru baada ya ukoloni. Anaonyesha wazi namna nchi hizo hasa nchi za Kiafrika zinaendeleza uongozi wa kidikteta, zinatumia sera na kasumba za kikoloni katika utawala. Huu ni ukoloni mamboleo. Nchi za Kiafrika zingali zikitegemea nchi zilizostawi au nchi zilizozitawala kwa misaada na hali nyingine nyingi. Jambo hili linazua maswali kuhusu uhuru wa kisiasa na kujitawala wakati huu. Kwa hivyo, kuna ulazima wa kuanza kufuta mawazo ya kikoloni yaliyodumisha mambo ya kale.

Msisitizo katika utamaduni mahuluti ni kanuni nyingine ya nadharia ya baadaukoloni. Utamaduni mahuluti ni dhana inayorejelea ile hali ya kuchota baadhi ya vipengele vya utamaduni na maisha ya kabla ya ukoloni, sehemu ndogo ya urithi wa kikoloni pamoja na tamaduni zitokanazo na kuupinga ukoloni (Wamitila 2002). Ushairi wa Kithaka wa Mberia unaonyesha kuwa usilimishaji na marekebisho ya mienendo ya kitamaduni yanaweza kuwa na manufaa na kukandamiza pia.

Kanuni nyingine ya nadharia ya baadaukoloni ni kuwa uchanganuzi wa matini kuhusu mbari, koo na ubaadaukoloni unaweza kuwa mwanzo mzuri wa mageuzi ya kijamii katika siku za usoni. Maadam tafiti kuhusu mbari, koo na baadaukoloni zinachunguza

mambo ya siku za nyuma ili kupata ithibati za kihistoria, kuna imani kwamba kwa kuchanganua masuala ya ukandamizaji, wahakiki wa kifasihi na kitamaduni wanaweza kuunda jamii mpya siku za usoni. Maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia yanadhihirisha namna historia imekuwa nguzo kuu katika kujenga mitazamo na mielekeo katika nyakati za sasa hasa katika nchi ya Kenya na Afrika kwa jumla. Kwa kuangazia namna historia inavyokandamiza watu, mshairi huyu huwa mpiganiaji wa mageuzi ya kijamii kwa kuhamasisha watu wachunguze upya historia zao ili kujenga jamii mpya yenye usawa kiuchumi na kisiasa. Kwa kutafiti na kuchanganua namna nguvu za kitamaduni zimeyatenganisha na kuainisha makundi ya watu, wahakiki wa kifasihi na kitamaduni hujaribu kuangazia matatizo mengi ya kijamii yanayokumba ulimwengu leo hii.

1.8.2 Nadharia ya Elimumitindo

Kabla ya kueleza kuhusu nadharia ya elimumitindo ni muhimu kueleza dhana ya mtindo ili kuweka msingi mzuri katika kuelewa umuhimu wa elimumitindo katika kuchanganua mtindo katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

1.8.2.1 Mtindo

Wahakiki watumia mtindo katika fasihi hurejelea matumizi ya lugha. Dhana hii ni muhimu kwa sababu inahusu tofauti zilizopo baina ya fasihi na maandishi ya kawaida. Ongarora (2007) amesema kuwa lugha ya fasihi ni ya kihisia na inabeba kiimbo na mkabala wa mwandishi. Mbali na kuwasilisha ujumbe fulani, lugha ya fasihi humshawishi msomaji ili kujaribu kuuathiri na pengine kuubadilisha msimamo wake. Ili kumwathiri msomaji kihisia na kimawazo, msanii huifinyanga lugha yake kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuteua tamathali za usemi, wizani na hata ukiushi wa kaida za kisarufi.

Katika uandishi wa kifasihi, mtindo pia ni tabia ya uandishi katika kikundi fulani cha maandishi katika kipindi fulani. Kwa mfano, twaweza kuzungumzia mtindo wa urasimu, urasimu mpya na uhalisia au tunaweza kuzungumzia mtindo wa ushairi wa Kiswahili wa karne ya 18 au 19 na mtindo wa ushairi wa kisasa. Kauli hii inatokana na sababu kwamba kikundi fulani kinachoandika kwa mbinu za aina moja na katika kipindi fulani cha wakati huelekea kufanana kwa kiasi fulani katika uandishi wao. Inawezekana pia maandishi wanaotoka sehemu moja wakafanana kimtindo.

Wakati mwingine, mtindo huangaliwa kama tabia ya mtu binafsi au mazoea ya mwandishi fulani ambayo hujionyesha katika kutumia lugha. Mazoea hayo ya mwandishi ya kuandika, kuteua msamiati, tamathali za usemi, taswira, uakifishi na mengine mengi humpambanua mwandishi huyo na wenzake. Waandishi hutofautiana katika mitindo kwa kuzingatia utofauti wa dhamira, nafsi ya msanii na kipindi alichandikia kazi yake ya sanaa (Ongarora khj). Ingawa waandishi wa Kiswahili hutumia lugha ya Kiswahili, kila mwandishi ana mtindo wake wa kuyaelezea mambo yake.

Mtindo pia huangaliwa kama ukiushi. Neno ukiushi latokana na kitenzi ‘kiuka’ chenye maana ya kwenda kinyume au kufanya jambo jinsi lisivyostahili kufanywa. Ukiushi ni dhana ambayo hutumiwa kuelezea sifa za kimtindo ambazo sio za kawaida na zinaelekea kwenda kinyume na matarajio au sifa za kimatumizi ya lugha zilizopo katika jamii fulani wakati fulani maalumu. Mwandishi anaweza kufanya ukiushi unaojitokeza katika viwango kadha. Kuna ukiushi wa kifonolojia, kimsamiati, kisintaksia, kisémantiki au wa kihistoria.

Kwa upande wa mwandishi, mtindo unatawaliwa na mambo kadha. Kwanza, ni nia na lengo la mwandishi. Pili, ni mtazamo na msimamo wake. Mtazamo wa mwandishi unahusu maono yake juu ya suala zima au masuala anayoyaangalia katika kazi yake. Wakati mwingine mtindo unaweza kutokana na mazingira ya elimu ya mwandishi. Kiwango cha elimu na tajiriba yake inaweza kuongeza ufanisi wa kazi yake. Mwandishi anapotumia stadi alizojifunza katika elimu yake anaweza kuandika kazi nzuri. Kwa misingi hiyo, maoni yetu ni kwamba Kithaka wa Mberia anatumia mtindo wa kipekee katika ushairi wake ili kuwasilisha dhamira na maudhui.

1.8.2.2 Elimumitindo

Nadharia ambayo tumetumia kuchanganua mtindo kama unavyosaidia kuwasilisha maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia ni ya elimumitindo. Elimumitindo ni dhana ambayo ni changamano kuifasili kwa sababu ni pana na hujumuisha mikabala tofauti katika kuchanganua matini. Hata hivyo, Leech na Short (1981) wamefasili elimumitindo kuwa ni uchunguzi wa mtindo. Aidha, wanafafanua mtindo kuwa ni namna lugha inavyotumiwa katika muktadha na mtu fulani kwa lengo fulani. Wanasisitiza kuwa katika upana wake, neno mtindo hutumika kwa usemi wa

kimdomo na maandishi katika masuala ya kifasihi lakini mara nyingi mtindo huhusishwa na matini.

Kwa upande mwingine, Wales (2001) amefasili elimumitindo kama taaluma inayoshughulikia na kueleza sifa za matini na uamilifu wa sifa hizo katika kuifasiri matini. Mwandishi anatumia sifa fulani za lugha kama vile tamathali za usemi, msamiati na mbinu nyingine za kisanaa kuwasilisha kazi yake. Sifa hizi ndizo zinasaidia kuifasiri maana. Wamitila (2003a) anasema kuwa elimumitindo ni dhana inayotumiwa kurejelea taaluma inayohusu uchunguzi na uchanganuzi wa jinsi mbalimbali za kuelezea matukio katika kazi ya kifasihi. Elimumitindo huhusisha uchunguzi wa sifa za kimtindo zinazojitokeza katika kazi fulani na zinazomtambulisha mwandishi anayehusika.

Ingawa uchanganuzi wa mtindo ulianza kama njia ya kutumia mbinu za kiisimu kuchanganua matini za kifasihi, mbinu hizo zinaweza kutumika katika uchanganuzi wa matini yoyote. Kwa hivyo, aina za matini ambazo elimumitindo hutumika kuchanganua zimepanuliwa kutoka zile za kifasihi ili kuhusisha matini yoyote. Katika jaribio la kutaka kuelewa elimumitindo huhusu nini, Thornborrow na Wareing (1998) wanatambua vipengele vitatu vikuu vya elimumitindo: kwanza ni utumizi wa isimu kuchanganua matini; pili ni mjadala kuhusu matini kwa malengo fulani wazi na tatu, ni msisitizo kwenye sifa za kiujumi za lugha.

Azma ya elimumitindo ni kuchanganua sifa za lugha kwa nia ya kutambua kutoka mkusanyiko wa sifa za kiisimu, zile sifa zinazohusishwa na muktadha fulani; kueleza ikiwezekana pahali sifa hizo zimetumiwa na kuainisha sifa hizo katika kategoria kulingana na utendakazi wao katika muktadha huo. Kwa hivyo, wanaelimumitindo huchunguza kile kinachosemwa na namna kinavyosemwa. Hiyo ndiyo sababu utafiti huu unachunguza usasa wa maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia na namna mtindo kupitia uteuzi wake wa lugha na ubunifu, unasaidia kuwasiliana na wasomaji.

Dhana ya kisasa ya elimumitindo ina mizizi yake katika taaluma tatu tofauti, lakini zinazohusiana kwa namna fulani. Taaluma hizo ni: balagha, uhakiki wa fasihi na isimu. Baadaye, uchunguzi wa kiisimu wa lugha uligawanywa katika maeneo matatu makuu: urasimi, umuundo na uamilifu. Maeneo haya matatu yalikuwa mikabala mitatu ya kuchunguza matumizi ya lugha na ufaafu wake katika matini.

Wanaelimumitindo wana maoni na misimamo tofauti kuhusu matumizi ya lugha katika matini.

Kwa ajili ya utafiti huu na hasa utanzu unaohusika, yaani utanzu wa ushairi, tumetumia taaluma ya uhakiki wa fasihi katika elimumitindo kwa kuegemea mkabala wa uhakiki mpya ambao unapigania njia mpya ya kuchanganua fasihi. Waasisi wa mkabala wa uhakiki mpya ni Brooks na Warren (1938). Waasisi hawa wanadai kuwa kazi ya kisanaa inastahili kuchukuliwa kama usemi huru bila kuzingatia unuiaji wa mwandishi. Kwa misingi hiyo, tunachukulia kuwa ushairi wa Kithaka wa Mberia ni usemi huru. Wanamtindo wenye mkabala wa uhakiki mpya katika elimumitindo hushughulika na uelezaji wa matini za kifasihi, hasa ushairi. Kwa hivyo, nadharia hii inafaa katika uchanganuzi wa mtindo katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Uhakiki mpya unahusu usomaji wa makini, ambapo mhakiki anatoa dai kuhusu maudhui au athari ya matini na kisha kunukuu neno au kifungu kulipatia uzito dai lake. Hivyo ndivyo tumefanya katika sehemu ya mtindo, ili kuoanisha maudhui na mtindo wa mshairi.

Kanuni moja ya mkabala wa uhakiki mpya ni kwamba shairi huchukuliwa kama usemi huru unaojitosheleza. Hii inamaanisha kuwa hakuna masuala mengine ambayo hayahusiani na matini yanayozingatiwa. Urejelezi wowote wa wasifu wa mwandishi huchukuliwa kama kizuizi cha uchanganuzi wa matini. Katika kuchanganua usasa wa maudhui na mtindo katika ushairi wa Kithaka wa Mberia, msisitizo umewekwa kwenye diskosi na miktadha ya mawasiliano, maumbo na semi anazotumia kusaidia wasomaji kusimbua ujumbe wake.

Kanuni nyingine ya uhakiki mpya ni kuwa fasihi ni njia maalumu ya kutumia lugha na taratibu za kuchanganua maana na mahusiano ya maneno, maumbo, usemi, na ishara kwa vile zinachangia ufasiri wa kazi. Kanuni hii imesaidia katika utafiti huu ili kutathmini namna Kithaka wa Mberia anachagua msamiati, kwa nini anachagua maneno mahususi kupitisha maudhui na maana mahususi kwa wasomaji. Fauka ya hayo, kanuni hii imesaidia utafiti huu kuchunguza uwasilishaji wa kiishara kupitia sitiari na mashairi-picha katika baadhi ya mashairi na umuhimu wao katika kuchimuza maudhui.

Kanuni ya tatu ya uhakiki mpya ni usomaji wa makini kama uchanganuzi wa kina wa mahusiano changamano na utata wa vipengele vya tamathali za usemi katika kazi ya kifasihi. Kanuni hii ina maana kuwa mhakiki hana budi kufanya uchanganuzi wa kina wa matini inayohusika ili kuelewa hali changamano ya kazi husika. Katika juhudi za kuelewa usasa wa maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia na vile unawezeshwa na mtindo wa uwasilishaji, utafiti huu lazima uchunguze kila habari katika mashairi ya mwandishi ili kuelewa jinsi uchangamano na utata wa maudhui na mtindo unamwezesha mshairi kuunda kazi kamilifu kisanaa na kimaana.

1.9 Mbinu za Utafiti

Kimsingi, utafiti huu umekuwa wa maktabani kwa sababu ni utafiti wa sifa wala si utafiti wa kiidadi.

1.9.1 Uteuzi wa Sampuli

Kuna diwani tano ambazo mtafiti aliteua kuwa msingi wa kukusanya na kuchanganua data katika utafiti huu kuhusu usasa wa maudhui na mtindo katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Diwani hizo ni: *Mchezo wa Karata* (1997), *Bara Jingine* (2001), *Redio na Mwezi* (2005), *Msimu wa Tisa* (2007) na *Rangi ya Anga* (2014). Uteuzi wa diwani hizi ulifanywa ili kusiwe na upendeleo wa diwani fulani kuliko nyingine mbali na kupata ruwaza za kimaudhui na sifa za kimtindo zinazojitokeza katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

1.9.2 Ukusanyaji na Uchanganuzi wa Data

Mtafiti amesoma mashairi yote katika diwani hizo tano kwa nia ya kutambua maudhui yanayojitokeza na sifa za mtindo alizotumia mshairi kumwezesha kuwasilisha maudhui hayo. Baada ya kutambua maudhui yote yajitokezayo, mtafiti ameyagawa na kuyaainisha katika kategoria kutegemea namna maudhui hayo yanavyojitokeza katika diwani zote tano. Mashairi yenye maudhui yanayohusiana yameainishwa na kujadiliwa katika ruwaza au kategoria moja. Kila kategoria imeunda sura moja. Kila sura ina sehemu mbili; katika sehemu ya kwanza tumejikita kwenye uchanganuzi wa maudhui yanayojitokeza katika mashairi mbalimbali na kuonyesha usasa wake ilhali sehemu ya pili imeangazia sifa za kimtindo zilizotumiwa na mshairi katika maudhui yaliyojadiliwa sehemu ya kwanza. Baadhi ya sifa hizo za kimtindo katika sura ya tatu zimerudiwa au kujitokeza katika sura ya nne, sura ya tano na sura ya sita katika

uchanganuzi wetu ili kubaini mtindo wa mshairi. Kwa hivyo, si urudiaji wa sifa za kimtindo bila sababu maalumu. Kila sifa ya mtindo iliyotambuliwa imeelezwa, mifano imetolewa kutoka kwa mashairi ambapo imetumika na kuonyesha ufaafu wake katika kuwezesha maudhui kujitokeza wazi.

Mbali na kusoma matini za kimsingi za kukusanya na kuchanganua data, mtafiti amesoma vitabu vya fasihi ili kupata uelewa mzuri wa dhana na istilahi za kifasihi zilizojitokeza wakati wa uchanganuzi wa data. Fauka ya hayo, mtafiti amesoma vitabu anuwai kuhusu nadharia za baadaukoloni na elimumitindo, ili kufahamu vyema kanuni za msingi na kuzitumia inavyostahili katika utafiti huu.

Katika kuchanganua na kufasiri data iliyokusanywa, mtafiti alihitaji mchango wa wahakiki na wasomi wengine wa kifasihi hasa pale vipengele vya maudhui na mtindo havikuwa vimechanganuliwa na kufasiriwa vyema. Kwa hivyo, maoni yao yamekuwa ya manufaa katika utafiti huu.

1.9.3 Uwasilishaji wa Data

Uchanganuzi na ufasiri wa data yote katika diwani zote tano kuhusu usasa wa maudhui na mtindo katika ushairi wa Kithaka wa Mberia pamoja na matokeo yamewasilishwa kwa njia ya kimaielezo na kwa mtindo wa nathari.

1.10 Hitimisho

Katika sura hii, tumezungumzia juu ya usuli wa mada, kueleza tatizo la utafiti, kutaja maswali ya utafiti na kuonyesha malengo ya utafiti. Mbali na hayo, tumeeleza sababu za kuchagua mada, kuweka upeo na mipaka ya utafiti na kujadili kuhusu yaliyoandikwa kuhusiana na mada. Isitoshe, tumefafanua nadharia zinazoongoza utafiti huu na namna zinatumiwa mbali na kueleza mbinu za utafiti zilizotumiwa kuchanganua, kufasiri na kuwasilisha data ya utafiti huu.

SURA YA PILI

MIKTADHA YA MAWASILIANO NA USEMI KATIKA USHAIRI WA KITHAKA WA MBERIA

2.1 Utangulizi

Hakuna msanii ambaye hutunga kazi yake katika ombwe tupu. Kila msanii huchota masuala anayoyaangazia kutoka katika mazingira na hali mbalimbali za kijamii, ambapo hujitokeza. Mazingira na hali mbalimbali ndizo zinazojenga miktadha ya mawasiliano na usemi katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Fauka ya hayo, mshairi hubuni wahusika kama vile watu, miti, wadudu, matunda na wanyama ambao wanasaidia kuendeleza maudhui mbalimbali katika ushairi wake. Wahusika hao ama wanatoa kauli kwa niaba ya umma au Kithaka wa Mberia binafsi anatoa sauti yake kuhamasisha, kupongeza, kushambulia na kukejeli mambo fulani yanayotendeka katika jamii ya leo. Kwa hivyo, katika sura hii tumeangazia miktadha kama vile ya kisiasa, kiuchumi, kihistoria, kimazingira na kitamaduni kwa nia ya kuonyesha jinsi inavyochangia kuibua maudhui ya mshairi katika diwani zake. Uchanganuzi wa kina wa maudhui na mtindo wa mshairi umeendelezwa katika sura ya tatu, nne, tano na sita.

2.2 Mukstadha wa Kisiasa

Siasa ni dhana telezi. Kwa hivyo, ni muhimu kutoa kijejezi kifupi kuhusu “siasa” kama itakavyoeleweka katika kazi hii. Eagles (2008) anaeleza siasa kama uundaji na utekelezaji wa maamuzi yanayostahili kufuatwa na watu katika jamii na mahusiano kati ya wanaounda au kutekeleza maamuzi hayo na wale watu wanaoathiriwa na maamuzi yenyewe. Katika siasa kuna uongozi, uundaji na utekelezaji wa maamuzi na watawaliwa ambao wanaathiriwa na sera na maamuzi hayo. Mshairi ametunga mashairi kadha juu ya siasa na utawala kutokana na mukstadha wa siasa.

Namna nchi zinavyoendesha siasa na kujitawala ni jambo muhimu katika maisha ya kila siku. Serikali na wanasiasa wanabuni katiba na manifesto za vyama vya kisiasa kama mikakati ya kutoa uongozi au kupata uongozi. Lakini mara nyingi katiba haifuatwi na manifesto za vyama hazitekelezwi na wanasiasa, pindi wanapochaguliwa na wananchi. Jambo hili ndilo humchochea mshairi kuhamasisha wananchi kuwa macho dhidi ya viongozi wanafiki, wasio waadilifu na wasiojali maslahi ya wananchi waliowachagua. Kwa hivyo, mshairi anatoa sauti yake kukemea na kukejeli uongozi

mbaya. Vilevile, humsaidia msomaji kuona namna jamii ilivyo ili achukue hatua fulani kisiasa kwa vile siasa nzuri huimarisha maisha ilhali siasa duni huchangia maisha mabaya.

Katika diwani ya *Mchezo wa Karata*, kuna mashairi ambayo yamejikita katika muktadha wa siasa. Mashairi hayo ni “Mchezo wa Karata” (uk. 18), “Dau Haliendi!” (uk.32), “Swali kwa Konokono” (uk. 33), “Karamu ya Nzige” (uk. 35), “Viwavi na Nzige” (uk. 36), “Swali kwa Yangeyange” (uk. 41), “Papa” (uk. 45) na “Mlipuko wa Furaha” (uk. 56). Kwa mfano, katika shairi “Mchezo wa Karata” mshairi anazungumzia namna wanasiasa hutumia hila kuongoza wananchi. Karata ni kadi ambazo hutumiwa katika mchezo wa kubahatisha. Katika siasa, wanasiasa hutumia maneno matamu, ahadi za uwongo na hata pesa kusudi wapate nafasi za uongozi kutoka kwa wananchi. Pindi tu wanapopewa nyadhifa za uongozi, hutelekeza wananchi na kuanza kufanya mambo yanayojali maslahi yao tu. Kwa mfano, hujinunulia magari mazuri, hujijengea nyumba nzuri, kuanzisha biashara na miradi ya kuwapatia mapato na kusahau ahadi za kuanzisha miradi ya maendeleo. Viongozi hawa hawatengenezi barabara, hospitali, shule, hawavutii watu maji na stima vijijini kama walivyoahidi wakati wakitafuta kura kutoka kwa wananchi. Kwa hivyo, wanasiasa huwatupia wananchi kadi za uongo, ilhali wananchi nao huwapigia kura wakiamini kuwa maisha yao yatabadilika endapo viongozi watatekeleza yale yote waliyoahidi. Katika mchezo huu wa karata, wanasiasa ndio wanashinda wala si wananchi.

Shairi “Dau Haliendi!” (uk. 32) ni mfano mwingine wa namna siasa mbaya haiwezi kuendeleza nchi kwa vyovyote vile. Dau ni sitiari inayomaanisha nchi. Nchi huwa inabeba mamilioni ya watu wanaoongozwa na serikali. Katika shairi hili, dau linaenda mwendo duara yaani mwendo wa mzunguko. Mwendo wa mzunguko unaonyesha kuwa rais wa nchi, mawaziri na wabunge hawana maono ya kusaidia nchi kusonga mbele kimaendeleo. Hakuna maendeleo katika sekta ya elimu, afya, uchumi, kilimo, uchukuzi na teknolojia miongoni mwa sekta zingine nyingi. Maisha ya wananchi ambao ndio mamilioni ya wasafiri katika dau yanakuwa duni. Wananchi wana makaazi duni, magonjwa yanawasumbua, wanakosa elimu bora, kuna tatizo la uchukuzi mbali na njaa ya mara kwa mara. Kwa hivyo, viwango vya umaskini vinaongezeka katika nchi husika. Mambo kama haya yanadhihirika katika nchi nyingi

zilizojipatia uhuru miaka mingi iliyopita. Kwa sababu hiyo, nadharia ya baadaukoloni inakuwa muhimu kuangazia mambo hayo ili kuona ni wapi nchi nyingi zilipo kimaendeleo miongo kadha baada ya uhuru.

Katika shairi “Swali kwa Konokono” (uk. 33), mshairi anadokeza namna kiongozi hasa rais wa nchi anatawala nchi kwa maslahi yake akisaidiwa na mawaziri wake na kukataa kung’atuka uongozini hadi atishwe kwa mapinduzi au umwagikaji wa damu. Huu ni mfano wa uongozi mbaya wa kidikteta. Mshairi anauliza:

Nambie ewe konokono
Ungeligeuka mtu mithili sisi
Ukapaa hadi kiti-adimu
Ungelichukua tabia ya nzige
Ukala na watu wako
Bila kujali umati
Upigayo miayo chini ya ngazi? (uk. 33)

Katika dondoo hili, konokono ni mtu au kiongozi yeyote ambaye anapanda cheo na kuwa rais wa nchi (kiti-adimu). Kiongozi huyo akishakalia kiti cha urais anakuwa na tabia ya ulafi kama nzige wanaokula majani ya miti. Anafuja rasilimali ya nchi akisaidiwa na mawaziri na wabunge bila kujali wanyonge wanaoteseka chini yake. Mshairi anauliza uhalali wa viongozi kuwa na tamaa na kukosa utu wa kuhudumia wananchi waliosaidia kuwaweka mamlakani.

Kwengineko, katika shairi “Karamu ya Nzige” (uk. 35) Kithaka wa Mberia anafafanua vile wanasiasa (nzige) wanafanya sherehe ya kutumia vibaya pesa na rasilimali nyingine za taifa kwa maslahi yao tu. Wanasiasa wananyakua ardhi za serikali, kuiba pesa za serikali zilizotengewa miradi ya ujenzi na upanuzi wa barabara, hospitali, shule, kilimo, maji na stima miongoni mwa huduma zingine muhimu. Fauka ya hayo, wanasiasa wanaendeleza ukabila na uufisadi katika nafasi za ajira. Mambo haya yote yanaonyesha “karamu ya wanasiasa” wakati wangali uongozini. Viongozi kama hawa hawana sera na maono ya kusaidia wananchi na nchi kupata maendeleo. Maamuzi yao yanaathiri maisha ya watawaliwa.

Uongozi na utawala wa kidikteta unaonekana katika shairi “Papa” (uk. 45) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Papa ni aina ya samaki mkubwa na mkali anayeishi baharini. Kuna methali isemayo kuwa “avumaye baharini papa kumbe wengine wapo” (Wamitila 2001). Mbali na papa, kuna samaki wengine wadogo baharini.

Katika shairi hili, papa ambaye ni kiongozi mwenye nguvu na mamlaka anahangaisha samaki yaani watu wa chini au watawaliwa. Bahari ni nchi au eneo la utawala. Mshairi anaonyesha kuwa katika siasa na utawala, kuna viongozi dhalimu wanaojigamba na kuwanyanyasa wanyonge katika jamii bila sababu. Hata hivyo, dhuluma zinapozidi, wanyonge huungana pamoja na kumshambulia kiongozi dhalimu mpaka wamtoe mamlakani. Mwandishi anaonyesha kuwa kiongozi mwovu hawezi kukaa uongozini daima. Aidha, wema utashinda uovu siku moja. Ujumbe sawa na huu unapatikana katika shairi “Mlipuko wa Furaha” (uk. 56) ambapo nguvu zisizozuilika zinamkabili simba (kiongozi) na kumng’oa meno na kucha kiasi kwamba mbuga (nchi) inalipuka kwa furaha ya uhuru.

Katika diwani ya *Bara Jingine* shairi la “Machozi ya Damu” (uk. 1) linagusia majuto na vilio vya wananchi kutokana na makosa wanayoyafanya kwa kuchagua viongozi wanaowadhulumu na kuwanyanyasa. Mshairi anasema:

Tulipochezea kinamo
Katika karakana ya siasa
Hatukujua kwamba vinyago
Vingejibadilisha maumbile
Na kujigeuza miungu-wajeuri
Watulize machozi ya damu
Kwa kutuzamisha kucha
Hadi mafundo ya neva! (uk. 1)

Katika shairi hili, “kinamo” ni kura wanazopiga wananchi ilhali “vinyago” ni wanasiasa. Wananchi wanapochagua viongozi, viongozi hao wanabadilisha mienendo yao na kujiongezea kiburi na ujeuri kwa kuanza kutowajali wapigakura tena. Wananchi wanachagua viongozi wasio waadilifu ambao wanaanza kutumia mamlaka visivyo na kufanya maisha yao kuwa magumu. Kwa hivyo, mshairi anaonyesha vile wananchi wanafanya makosa wakati wa uchaguzi bila kujua kuwa watajuta baadaye.

Kwa upande mwingine, mwandishi anapongeza na kusifu siasa na uongozi wa aliyekuwa rais wa Nigeria, Olusegun Obasanjo katika shairi “Obasanjo” (uk. 17). Mshairi anasema kuwa Olusegun Obasanjo alitawala vizuri nchi ya Nigeria na kuondoka mamlakani bila vitisho licha kwamba alikuwa na nguvu, majeshi na silaha kali za kuweza kupigana hata na nchi ya Israeli. Mwandishi anashtumu uongozi wa kidikteta kwa kusema:

Badala ya kushikilia kifyatulio
Kama onyo kali kwa wananchi
Uliinua mkono wa kwaheri
Na kwa hiari
Ukateremka bila ujanja
Kutoka kiti cha enzi (uk. 17)

Katika dondoo hili, mtunzi anatumia mhusika wa kweli kutoa mfano wa uongozi bora. Obasanjo hakushika bunduki ili kutisha na kunyamazisha wananchi kusudi aendelee kutawala. Alitoka kwenye kiti cha urais kwa hiari. Mshairi analenga marais wengi wa bara la Afrika ambao wanafika kileleni lakini wanakataa kung'atuka uongozini. Wanatumia hila na nguvu kusalia mamlakani hata wakati wananchi wanataka viongozi wapya. Ikiwa wananchi waliochoka na uongozi wao hawawataki, harakati za kuwaondoa mamlakani zinaanza kwa maandamano na mapinduzi ambayo yanaishia katika umwagikaji wa damu. Hali kama hii iliwahi kuonekana katika nchi ya Misri, Libya, Burundi, Zimbabwe na Sudan. Mwandishi anaonelea kuwa marais wengine hasa wa mataifa ya Afrika wanastahili kuiga uongozi na utawala wa busara wa Obasanjo ili kuepokana na uongozi wa kidikteta ambao kwa namna fulani ni mwangwi wa ukoloni mamboleo.

Diwani ya *Msimu wa Tisa* ina mashairi kadha pia ambayo yanadhihirisha muktadha wa siasa. Kwa mfano, shairi "Nahodha na Jahazi" (uk. 5) linazungumzia juu ya nahodha ambaye ni rais wa nchi na wasaidizi wake yaani mawaziri na wabunge wanavyokosa kuwajibika katika uongozi. Kulingana na mshairi kabla ya shangwe za wananchi waliomsaidia nahodha kuingia kwenye urais kupungua, mkataba uliomwinua hadi kwenye kilele unakiukwa na wasaidizi wenye ulafi. Kwa hivyo, mawaziri na wabunge wanakuwa na ujeuri kwa sababu ya mamlaka. Hali hii inazaa misukumano na mitingishano isiyokoma. Uongozi huu unapeleka nchi kwenye mikondo ya ukabila na kukosa mwelekeo. Mshairi anasema:

Nahodha angelimakinika kwenye usukani
Wasaidizi wake wangelidhibiti matanga
Jahazi halingedumu kwenye mlango wa bahari
Likisukwasukwa na mawimbi yanayozozana (uk. 5)

Dondoo hili lina maana kuwa rais (nahodha) akiwa makini kwenye uongozi wake na wasaidizi wake washikilie wizara, idara na taasisi mbalimbali vizuri, nchi (jahazi) haiwezi kuwa na shida. Mawimbi ni shida zinazosumbua nchi kama vile ufisadi,

ukabila, njaa, magonjwa na ukosefu wa miundo msingi. Kwa hivyo, kiongozi asiyemakinika akiwa na wasaidizi wasiowajibika nchi itabaki kwenye shida daima.

Katika shairi “Tope la Mizozo” (uk. 6), mtunzi amejikita katika muktadha wa siasa. Serikali iliyoingia mamlakani ikiwa na ahadi nyingi za kuinua maisha ya wananchi ina mizozo mingi; jambo ambalo linarudisha nchi nyuma kimaendeleo. Viongozi waliochaguliwa wanaanza kugongana na kurushiana cheche za matusi. Isitoshe, viongozi hao wana tamaa na hutumia mamlaka kujitwalia mashamba, biashara, mishahara minono, magari na marupurupu mengi huku wakiachia wananchi makombo. Ufisadi unashamiri miongoni mwa viongozi walioungana pamoja ili ‘kumaliza ufisadi’. Mizozo kama hii miongoni mwa viongozi waliochaguliwa na kupewa wajibu wa kuongoza nchi itazamisha taifa.

Katika shairi “Werevu” (uk. 8) mshairi anakejeli namna rais anashauriwa na viongozi wajanja na wanafiki wanaomzunguka. Rais hathamini maneno ya wimbo wa taifa “haki iwe ngao na mlinzi” na kanuni za katiba. Kiongozi ambaye hustahili kujali maslahi ya watu wote hugawa rasilimali ya nchi kwa watu wachache bila kujali usawa. Jambo hili huchangia ukosefu wa usawa kimaendeleo na kimaeneo, ukabila na unyanyasaji. Mshairi anasema:

Badala ya kuongozwa na ndoto ya taifa angavu
Mgavi alizingatia sauti laini za genge la walafi
Akawapakulia thuluthi mbili za sinia la ngawira
Na kuwapunja simba waliopigana kwa meno na kucha (uk. 8)

Kiongozi mzuri ni yule hutenda haki kwa watu wote badala ya kuzingatia maslahi ya viongozi wachache wanaomzunguka. Anastahili kujua kuwa uaminifu kwa wananchi ni akiba inayozaa matunda. Anastahili kugawa mapato kwa ratili sawa na aheshimu matakwa ya wananchi wazalendo (simba) wanaojitolea kila kuchao kujenga nchi. Wakati wananchi wanahisi kuwa wananyanyaswa, wanangojea tena wakati wa uchaguzi na kuwaondoa viongozi wote wasiowajibika katika kazi zao. “Werevu” wao unaisha wanapokosa kuchaguliwa. Uongozi duni unachangia siasa kuchukua mkondo mbaya kama anavyosema mshairi:

Gari la siasa likaacha barabara ya lami
Na kujitosa kwenye ujia wenye udongo chepechepe
Mwendo wa kasi tuliotarajia utufikishe kwenye ufanisi
Ukawa safari ya kusukuma na kuvuta matopeni... (uk. 8)

Kwengineko, katika shairi “Msimu wa Tisa” (uk. 9) kwa maana ya bunge la tisa katika nchi ya Kenya, mwandishi anamulika ulafi, uzembe na kiburi cha wabunge. Wabunge waliochaguliwa na kula kiapo cha kuwatumikia wananchi na serikali kwa uaminifu wanajali maslahi yao tu. Nyoyo zao zimejaa ubinafsi ambapo wanavamia ghala la taifa kwa tamaa. Mawaziri wanapeperusha bendera kwenye mabenzi ya bei ghali vijijini kwa watu waliovaa matambara na kuwashangaza watu kwa mabenzi na mapajero mapya. Bila kujali wananchi maskini, wanajitwalia marupurupu ya kugharimia usafiri. Wanashindwa kutimiza jukumu la kuondoa watu kutoka minyororo ya shida.

Vikao vya majadiliano bungeni vinavunjwa kwa kukosa idadi inayohitajika kwa sababu wabunge hawafiki bungeni. Pale wanapokuja bungeni, huwa wameshiba na wengine wanalala bungeni na hivyo mambo muhimu yanawapita. Muda wa maswali unapowadia bungeni, baadhi yao wamo hotelini wakijipumbaza kwa vinywaji ilhali waziri anayestahili kujibu maswali anacheza mchezo wa gofu. Mambo haya na mengine yanaonyesha ubinafsi, ulafi na kutojali kwa wabunge. Huu ni usaliti mkubwa kwa wananchi wanaoendelea kuteseka katika umaskini.

Katika shairi “Msimu Mwingine wa Wasaliti” (uk. 12) mwandishi analinganisha wanasiasa na wasaliti. Wanasiasa wanaahidi wananchi mambo mazuri wakati wa kampeni. Wanasema watajengea wananchi barabara, shule, hospitali, masoko, kuwavutia maji na stima vijijini miongoni mwa miradi mingine mingi. Wanasiasa hao wakishapata nyadhifa hizo, wanaanza kushughulikia maslahi yao na kupuuza au kusahau ahadi walizotoa. Hivyo ndivyo wanasaliti wananchi. Hata hivyo, baada ya muda waliopewa kuhudumia wananchi kuisha, wanasiasa hao wanarudi tena kwa wananchi kuwarai wawachague tena. Wanawapatia wapigakura pesa, pombe, maneno matamu na ahadi za maendeleo ya kuimarisha maisha ya wananchi. Wananchi nao kwa sababu ya kusahau, kupokea mlungula na kukubali kudanganywa, wanapanga milolongo mirefu katika mvua na matope kuwapigia kura viongozi hao hao. Hawapigi msasa au kufikiria ni kiongozi yupi aliyewasaidia ili wamchague na kumwondoa aliyezembea kazini. Kwa kufanya hivyo, wanakaribisha msimu mwingine wa wanasiasa wanafiki na wadanganyifu. Ndio maana katika siasa kuna kauli kuwa nyani ni walewale tu, ni msitu wanabadilisha. Wananchi wanaendelea kulia na kulalamika

kuwa viongozi waliowachagua wamewatelekeza ilhali wao wenyewe walichangia kuwachagua viongozi hao.

Mwandishi anakejeli tabia ya kubuni tume nyingi zinazochunguza masuala yasiyo na manufaa yoyote kwa nchi katika shairi “Tume za Rais” (uk. 31). Rais wa nchi anateua tume za kuchunguza masuala anuwai ili kutatua shida zilizoko. Lakini tume hizo hazina maana. Tume inaundwa kuchunguza kama njaa inaweza kuua, kuchunguza jina la Rais wa Jamhuri, kumtangazia rais jina, kuchunguza kama rais ni rais bila tume za rais na tume ya kumshauri rais namna ya kuficha taarifa za tume za rais. Wanatume hufaidika kutokana na ununuzi wa magari ya bei ghali na kujijengea nyumba za kifahari kutokana na marupurupu ya vikao vyao. Kuna ubadhirifu wa pesa mwandishi anaposema kuwa, “Napendekeza tuunde tume ya rais, tuitengee nusu ya akiba ya Banki Kuu” (uk. 31). Si haki kutengea tume nusu ya pesa kutoka benki kuu. Isitoshe, si halali kuunda tume ya rais na “kuilipa kwa mkopo kutoka vitanzi vya Bretton Woods” (uk. 31). Inashangaza kuwa serikali ina nia ya kulipa tume mkopo kutoka nchi ya kigeni ili baada ya miaka mitano ya kujivinjari na kunywa mvinyo imshauri rais namna ya kuficha taarifa za tume za rais. Mshairi anatomia tashtiti kuwasuta viongozi au marais katika shairi hili.

Diwani za *Redio na Mwezi* na *Rangi ya Anga* hazina mashairi yanayojikita katika muktadha wa kisiasa moja kwa moja. Kwa mfano, diwani ya *Redio na Mwezi* ina mashairi yanayoangazia mazingira, ugonjwa wa ukimwi, unafiki wa kidini, uasherati, elimu na dawa za kulevya. Kwa upande mwingine, diwani ya *Rangi ya Anga* inaangazia masuala ya tamaduni zilizopitwa na wakati kama vile wasichana kutorithi mali, ukeketaji wa wasichana, dhuluma za kinyumbani dhidi ya mwanamke, uozwaji wa wasichana kwa wazee matajiri, ubakwaji wa wasichana na wanawake katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1). Aidha, kuna mashairi yanayoangazia uharibifu wa mazingira katika shairi “Wanda” (uk. 27) ilhali kuna ukoloni na ukoloni mamboleo katika shairi “Zimwi la Theluji” (uk. 48).

2.3 Mukadha wa Kiuchumi

Uchumi ni dhana inayorejelea mfumo wa mapato na matumizi katika nchi. Tofauti katika uzalishaji wa mali zinachangia uwepo wa matabaka katika jamii. Kuna tabaka la watu matajiri na watu maskini. Tabaka lenye uwezo hutaka kuzalisha mali zaidi na liendelee kubaki kwenye mstari wa mbele ilhali tabaka la kati linang’ang’ana pia

lipande daraja kiuchumi. Kwa upande mwingine, tabaka la watu maskini linalazimika kufanya kazi kwenye idara na taasisi za serikali, kampuni za kibinafsi au kwenye biashara na nyumba za matajiri. Katika pilikapilika za kutafuta riziki, kunatokea dhuluma, unyanyasaji na migongano ya kiuchumi kati ya tabaka lenye uwezo na wanyonge au kati ya mataifa yaliyostawi na mataifa yanayoendelea. Mivutano kama hii ndiyo inakuwa muktadha muhimu unaoangaziwa na Kithaka wa Mberia katika ushairi wake.

Muktadha wa kiuchumi katika ushairi wa Kithaka wa Mberia umegawika katika sehemu tatu ambazo ni shughuli za kilimo na viwanda, biashara ya ukahaba na utabaka pamoja na shughuli za kiuchumi zinazoharibu mazingira.

2.3.1 Shughuli za Kilimo na Viwanda

Katika diwani ya *Mchezo wa Karata* kuna shairi “Wimbo wa Mkulima” (uk. 9). Wakulima ni watu muhimu wanaochangia katika ukuaji wa uchumi. Wanafuga mifugo wanaotoa maziwa, nyama, mayai, ngozi, samadi na manyoya. Fauka ya hayo, wanakuza mimea anuwai kama vile miwa, mahindi, ngano, mchele, kahawa, majani-chai, maharagwe, matunda, mboga na kadhalika. Wakulima wanauza mazao yao ili kupata pesa za kujikimu. Hata hivyo, katika harakati za kutafuta soko na kusafirisha mazao sokoni, kuna mabepari na matajiri wajanja ambao wananunua bidhaa za wakulima kwa bei ya chini. Wanahifadhi bidhaa hizo kwa muda fulani hadi bei inapanda kisha wanauza na kupata faida nyingi kuliko wakulima wenyewe. Wanawapunja wakulima na huo ni unyanyasaji wa kiuchumi. Katika shairi hili “Wimbo wa Mkulima” mshairi anatoa sauti na kilio kwa niaba ya wakulima kuonyesha jinsi watu wasio wakulima wanafaidika kuliko wakulima halali. Mshairi anasema:

Inakera sana moyo
Hii anga ambayo
Inawapa
 Maziwa ya ng’ombe
 Na mayai ya kuku
 Wasiofuga
 Ng’ombe
 Na kuku
Na kuwatemea mate
Wafugaji! (uk. 9)

“Wimbo wa Mkulima” ni kilio cha nyanyaso kwa mkulima. Watu wasiofuga wanapata maziwa na mayai kwa bei ya chini na kuuza kwa bei ya juu. Wanafaidika ilhali wafugaji hawapati faida yoyote.

Vilevile, katika shairi “Nyuki, Ndege na Nyegere” (uk. 10) na “Kero” (uk. 28) mshairi anaonyesha vile wafanyakazi wenye bidii wananyanyaswa kiuchumi na mabwanyenye. Kwa mfano, katika shairi “Nyuki, Ndege na Nyegere”, nyuki wanafanya juhudi za kutafuta mbelewele kutengeneza asali. Ndege wajanja wanakuja kwa maneno matamu na kurai nyuki kuwa wawasaidie kutafuta mbelewele kwenye minga na mikakaya. Nyuki wanakubali lakini baadaye wanalipa ndege kwa huduma adhimu. Kadiri nyuki wanavyotengeneza asali, ziara za nyegere zinaongezeka mzingani na asali inatoweka. Kumbe kulikuwa na hila baina ya ndege na nyegere kulaghai nyuki asali yao. Katika muktadha huu, nyuki ni wafanyakazi wanaofanya kazi mashambani, viwandani, kwenye kampuni na biashara mbalimbali. Ndege na nyegere ni mabwanyenye wanaotumia ujanja kunyonya jasho la wafanyakazi kwa kununua bidhaa zao kwa bei ya chini au kuwalipa mishahara duni ambayo hailingani na kazi wanazofanya. Huu ni mfano mwingine wa unyanyasaji wa kiuchumi dhidi ya tabaka la makabwela.

Katika shairi “Kero” (uk. 28), mwandishi analalamika pia vile watokao mashambani na wanaogonga nyundo wakipasua mawe mchana kutwa wanadharauliwa ilhali watu wazembe wanaostarehe bila kufanya kazi ndio wanaopewa chakula. Ni kinaya kwamba watu wazembe wanafaidika kuliko wafanyakazi wanaotia bidii katika kujenga uchumi wa nchi. Mshairi analalamika:

Inakera moyo
Hii anga ambayo
Huwasonya njiani
Watokao mashambani
Na kusalimu kwa bashasha
Wanaoshinda kivulini
Chini ya mwembe
Wa umma (uk. 28)

Katika dondoo hili, bidii za wakulima na wafanyakazi wengine hazitambuliwi. Kutotambuliwa huku kunatokana na serikali na mabwanyenye kutolipa wakulima bei nzuri za bidhaa zao kulingana na gharama ya pembejeo wanazotumia shambani pamoja na muda na nguvu wanazotumia katika kukuza kilimo. Aidha, wafanyakazi

hawalipwi ujira unaotoshana na nguvu wanazotumia mbali na muda wanaotumia kufanya kazi.

Kithaka wa Mberia anazidi kupigania haki na kupinga unyanyasaji wanaotendewa wafanyakazi katika shairi “Jembe, Surupwenye na Kalamu” (uk. 26) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Jembe ni taashira ya wakulima, surupwenye ni taashira ya watu wanaofanya kazi viwandani ilhali kalamu inasimamia walimu. Makundi haya yote yanafanya kazi ngumu lakini hayafaidi jasho lao. Mshairi anasema:

Jembe limelalamika
Napanda mpunga
Napalilia migomba
Napura mawele
bali
Nasononeka
-Kwa ombwe tumboni
Surupwenye imenung'unika
Nafua chuma
Naunda mitambo
Nabeba makasha
bali
Nagofuka
-Kwa ukata maishani! (uk. 26)

Mkulima analalamika kuwa anafanya kazi ya kupanda, kupalilia, kunyunyizia dawa mimea na kuvuna lakini mwishowe anasumbuka kwa sababu hana kitu cha kujivunia. Kwa upande mwingine, kuna watu wanaofua vyuma, kuunda mitambo na kubeba makasha bali pia wanaishi maisha ya umaskini. Mambo haya yanaonyesha kuwa maslahi ya masefule yaani watu maskini na wanyonge ambao ndio wengi katika jamii hayazingatiwi. Ujira wanaopata haulingani na kazi wanazofanya. Spivak (1988) msomi na mwananadharia wa fasihi nchini India aliandika makala yanayoitwa “Masefule wanaweza kuzungumza?” (tafsiri yetu) ili kupigania haki za wanyonge wanaodhulumiwa katika nchi zinazoendelea. Anasema kuwa ni vigumu kwa masefule kuzungumza juu ya dhuluma wanazotendewa kwa sababu wamegawanyika katika misingi ya jinsia, tabaka, dini, eneo na mambo mengine. Katika muktadha huu, wakulima na wafanyakazi wengine waliopo katika tabaka la chini hawawezi kuzungumzia shida zao wakaeleweka na ndio maana wanalalamikia hali zao duni ila hakuna wa kuwasikiliza au kuwasaidia.

Katika diwani ya *Redio na Mwezi*, shairi “Kiwanda” (uk. 6) linazungumzia namna moshi wa hudhurungi unafuka kutoka kiwanda kinachotengeneza karatasi cha Webuye. Moshi huo una chembe nyeupe ambazo zina sumu inayoshuka na kuharibu mimea mashambani, kuhasi udongo, maji na hewa. Sumu kali ya kemikali inaharibu mapaa ya nyumba kwa kutoboa vitundu. Wakati mvua inaponyesha maji yanajaa ndani ya nyumba. Watu wanaokaa karibu na kiwanda hiki wana shida ya macho, ngozi na koo kwa sababu ya kemikali kutoka kiwanda cha kutengenezea karatasi cha Webuye. Mazingira ya eneo la Webuye hayafurahishi tena kwa sababu ya athari mbaya za kiwanda hiki cha kutengeneza karatasi.

2.3.2 Utabaka na Biashara ya Ukahaba

Mshairi pia anaangazia mwanya uliopo kati ya matajiri na maskini kwa kuonyesha ukosefu wa usawa kati ya matajiri na maskini. Anazungumzia namna maisha yanavyowanyookea matajiri na kuporomokea maskini kila kuchao. Hali hiyo inabainika wazi katika shairi “Kiwambo cha Televisheni” (uk. 37) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Maskini anawakilishwa kwa sauti ya 1 ilhali tajiri anawakilishwa kwa sauti 2. Maskini analalamika kuwa rasilimali za nchi zinamjenga tajiri pekee ilhali yeye maskini anaumwa na njaa. Tajiri anamjibu kwa kiburi. Lakini maskini anamwambia kuwa mali ya nchi (mama) ni haki yao wote na hivyo wagawane kwa usawa baina yao. Mnyonge anataka usawa na haki katika ugavi wa rasilimali ili kuondoa mpaka uliopo kati ya matajiri na maskini. Mshairi anasema:

SAUTI 1: Kwa nini
 Titi la Mama
 Likujenge misuli pekee
 Wakati mwangu tumboni
 Natafunwa na njaa?

SAUTI 2: Ni-ni-no!
 Ni-ni-no!

SAUTI 1: Kugeuzwa yonda
 Nimekataa, katakata!

 Mali ya Mama
 Ni haki yangu
 Ni haki yako
 Basi ya kugawa
 Baina yetu (uk. 39)

Watu wa tabaka la chini wanaposhindwa kumudu maisha yao kwa kukosa mahitaji ya kimsingi, wanatumia njia za mkato kukimu matakwa yao. Hali kama hii inabainika miongoni mwa wanawake na wasichana ambao wanaanza kushiriki biashara ya ukahaba kama njia ya kujipatia pato. Katika biashara hiyo, wanapitia shida na changamoto nyingi kama vile kutolipwa pesa, kupigwa na baridi usiku wakisubiri wateja, kushikwa na kutiwa seli na hatari ya kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa. Ukahaba ni njia ya mkato ya wanawake na wasichana kujitafutia riziki kutoka kwa wanaume wenye pesa. Mshairi, mbali na kuonyesha jinsi tofauti za kiuchumi zinachangia uovu kama huu, anaonyesha kuwa wote wanaoshiriki katika ukahaba, wanawake na wanaume wanadhihirisha ukosefu wa maadili katika jamii.

Katika diwani ya *Bara Jingine*, Kithaka wa Mberia ametunga mashairi yanayogusia ukahaba na athari zake kama vile “Mimi, Monika” (uk. 37) na “Wanabiashara Barabarani” (uk. 43). Kwa mfano, katika shairi “Mimi, Monika”, mwanamke huyu anaelezea vile amekutana na wanaume wengi kutoka maeneo mbalimbali. Katika biashara hiyo, amejikuta katika nyumba za mawe, vyumba vya hoteli na sakafu za polisi. Haya ni maisha ya dhiki na mauti. Fauka ya hayo, wanawake wenzake walio Shiriki katika biashara hii wamekufa kwa sababu ya ugonjwa wa ukimwi.

Aidha, katika shairi “Wanabiashara Barabarani”, mshairi anasema kuwa wanawake wanasimama pembeni katika barabara za miji huku wakiwa wamevaa mavazi mafupi na kuzungumza kwa lugha ya ufasaha na macho ya kuwashawishi wateja. Mwandishi ana maoni kuwa baadhi ya wanawake wanashiriki ukahaba kwa sababu ya uvivu na matarajio ya kutumia njia ya mkato katika maisha. Baadhi ya hawa ni wajinga ambao hawakutia bidii darasani na maktabani. Hata hivyo, kuna wale walioachwa mayatima na wengine wakabakwa na wakazaa watoto. Wanatafuta njia ya kukimu wana wao. Baadhi yao walivunjika moyo baada ya kujikakamua wakitafuta namna ya kujinusu kutokana na mahitaji maishani. Wakakosa matumaini ndiposa wakaamua kushiriki biashara hii haramu.

Maudhui ya biashara ya ukahaba yameangaziwa tena katika diwani ya *Radio na Mwezi* ambapo kunajitokeza vitendo vya ufuska. Kuna mashairi kama “Msimu wa Kaburi!” (uk. 3), “Mgeni Katili” (uk. 4), “Biringanya na Matikiti” (uk. 28), “Matunda Haramu” (uk. 39), “Vituko Mjini” (uk. 40) na “Matumizi Mengine” (uk. 41). Katika

shairi “Msimu wa Kaburi” wanaume na wanawake wanaoshiriki ngono kiholela wameambukizwa ugonjwa wa ukimwi. Matokeo ya maambukizi hayo ni vifo vya watu wengi ndio maana ya kichwa “msimu wa kaburi”. Watu wasiojihadhari wanajipata wameambukizwa ukimwi na hatima yao ni kifo. Ujumbe huu wa madhara ya ugonjwa wa ukimwi ndio unaojitokeza tena katika shairi “Mgeni Katili”. Ugonjwa wa ukimwi ndio mgeni asiye na huruma kwa wanawake na wanaume wasiojichunga.

Katika shairi “Biringanya na Matikiti” (uk. 28), mwandishi anaonya wanawake na wanaume wanaoshiriki mapenzi kiholela kuwa kuna hatari ya kuambukizwa ukimwi ambapo hatima yake ni mauti. Analinganisha viungo vya siri vya wanaume na “biringanya” ilhali “matikiti” ni viungo vya siri vya wanawake. Wanawake wasitamani biringanya kwa sababu mumo humo kuna sumu ya mauti. Aidha, wanaume wasitangatange wakila vipande vya matikiti kwa sababu wataangamia kutokana na ugonjwa wa ukimwi.

Shairi “Matunda Haramu” (uk. 39) laangazia wanandoa wenye jicho la nje kinyume na viapo walivyokula hadharani. Wanandoa wanachuma raha haramu na kuondoka faraghani huku wakiwa na kumbukumbu ya karamu marufuku. Wanaume na wanawake wanapofika nyumbani wanaonyesha nyuso za uaminifu na furaha ili kuficha vitendo vya mapenzi haramu walivyoshiriki faraghani. Vitendo hivi vinasababisha ndoa kuvunjika, mapigano ya kinyumbani na maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi na magonjwa ya zinaa.

Mwandishi anadokeza vile watu wanashiriki ngono kiholela pahali pasipostahili katika shairi “Vituko Mjini” (uk. 40). Wanawake kwa wanaume wanashiriki mapenzi kwenye mazulia ofisini wakati wa jioni baada ya watu kwenda nyumbani. Fauka ya hayo, wengine wanashiriki uovu huo ndani ya magari yaliyoegeshwa kando ya barabara wakati wa usiku. Huu ni ukosefu wa maadili. Ujumbe huu unajitokeza vilevile katika shairi “Matumizi Mengine” (uk. 41). Mwandishi anaeleza kuwa watu wamebadilisha mazulia ya ofisi, matakia ya ofisi na viti vya magari kuwa pahali pazuri pa kufanyia vitendo vya ufuska bila kujali.

2.3.3 Shughuli za Kiuchumi Zinazoharibu Mazingira

Kwengineko, mwandishi anaonyesha vile shughuli za kiuchumi zinachangia uharibifu wa mazingira. Kuna mashairi kadha katika diwani ya *Bara Jingine* yanayoonyesha

vile shughuli za kiuchumi zinachangia kuharibiwa kwa mazingira. Mashairi hayo ni kama “Jinamizi” (uk. 55), “Ngao” (uk. 59), “Thagicu” (uk. 61), “Mimi, Mto Nairobi” (uk. 63), “Okidi, Piga Ukelele” (uk. 64), “Mikoma” (uk. 66) na “Bwawa la Ithanje” (uk. 69).

Shairi “Jinamizi” (uk. 55) linamulika watu wanaokata miti kwa mashoka, mapanga na misumeno kwa tamaa ya kupata mbao za kujengea nyumba na kuunda samani, mbali na kupata mashamba ya kuendeleza shughuli za kilimo. Ukataji miti unachangia mmomonyoko wa udongo. Katika shairi “Ngao” (uk. 59) mshairi anazungumzia juu ya uharibifu wa utandu wa ozoni. Utandu wa ozoni ni ngao inayomkinga mwanadamu dhidi ya miale mikali ya jua ili watu wasipate magonjwa ya ngozi kama vile saratani ya ngozi. Lakini shughuli za kiuchumi zinachangia kutolewa kwa kemikali ambazo zinaharibu utandu huo na hivyo kuhatarisha maisha ya binadamu.

Katika shairi “Thagicu” (uk. 61) mshairi anaeleza vile eneo hili linalopatikana nchini Kenya limeharibiwa kwa vile limejaa mchanga mweupe na mawe ilhali mwanzoni lilikuwa pahali pazuri pa kuvutia macho. Limeharibiwa kutokana na shughuli za kilimo. Kwa upande mwingine, shairi “Mimi, Mto Nairobi” (uk. 63) linazungumzia vile shughuli za wakaazi wa Nairobi zinachangia kuchafua maji ya mto Nairobi. Wakaazi wa Nairobi wakiendeleza shughuli zao mbalimbali wanachafua maji kwa mafuta machafu, makopo, tairi, talimbo na takataka nyinginezo.

Shairi “Mikoma” (uk. 66) linaangazia namna wagemaji, wasonga-mizinga, na wakulima wa Igaironi, Irarani, Kirukuma na Kaguma wanakata mikoma ili kutimiza mahitaji yao mbalimbali bila kujali. Ukataji huu wa miti ya mikoma unatishia kuangamiza miti hii ya kiasili, lakini wenyeji hawajali. Kwengineko, katika shairi “Bwawa la Ithanje” (uk. 69), wakulima wanyunyiziao maji mashamba wanakamulia sumu katika maji ya bwawa la Ithanje. Vilevile, viwanda vya Limuru vinaelekeza majitaka hadi bwawa la Ithanje na hivyo kuhatarisha maisha ya binadamu wanaotumia maji ya bwawa hilo na viumbe wengine wanaoishi humo.

Katika diwani ya *Rangi ya Anga*, Kithaka wa Mberia anaangazia pia shughuli za kiuchumi zinazochangia kuharibu mazingira. Shughuli hizo zinapatikana katika shairi “Wanda” (uk. 27). Wakulima wanakata mikoma na miangati ili kupata mashamba ya kilimo. Wafugaji wa kuhamahama wanahujumu ardhi na kugofua rutuba. Mifugo

wanakula nyasi, majani na kuharibu udongo kwa kwato zao. Jambo hili linachangia mmomonyoko wa udongo wakati mvua inaponyesha. Kwa hivyo, muktadha wa kiuchumi ni kichocheo muhimu cha utungaji wa mashairi katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

2.4 Muktadha wa Kimazingira

Mazingira ni dhana pana ambayo inahusisha vitu vingi. Kuna maji, hewa, ardhi, miti na wanyama. Mshairi ameangazia maudhui yanayohusu uharibifu wa mazingira kama vile ukataji wa miti, uchimbaji wa madini, mbinu duni za kilimo, ufugaji wa kuhamahama, shughuli za viwanda miongoni mwa mengine. Fauka ya hayo, mwandishi ameonyesha umuhimu wa kutunza na kuhifadhi mazingira kupitia upanzi wa miti katika maeneo yaliyokatwa miti au kuchimbwa madini, mabonde na kuendeleza kilimo-mseto. Mwandishi anaonyesha jinsi mwanadamu anachangia kuharibu mazingira katika shughuli zake za kiuchumi ama kwa kutojali kwa sababu ya tamaa, ubinafsi au kwa kutojua.

2.4.1 Msamiati wa Kimazingira

Msamiati ni jumla ya maneno katika lugha fulani. Ingawa mshairi ametumia maneno ya Kiswahili katika ushairi wake, amefanya uteuzi wa msamiati kwa makini kulingana na ni nini anasema, vipi anakisema ili kuleta athari na hisia fulani kwa msomaji. Msamiati ambao ametumia unaweza kugawika katika makundi saba kama vile: wadudu, wanyama, miti, matunda, vifaa, sayari, tabia-nchi na majina ya nchi na mahali mahususi.

2.4.1.1 Msamiati wa Wadudu

Katika diwani ya *Mchezo wa Karata*, mwandishi ametumia majina ya wadudu kama vile nyuki katika shairi “Nyuki, Ndege na Nyegere” (uk. 10), sisimizi katika shairi “Sisimizi Nijulisheni” (uk. 27), utandabui katika “Utandabui Muuaji” (uk. 31), nzige katika mashairi “Karamu na Nzige” (uk. 35) na “Viwavi na Nzige” (uk. 36), mdudu katika “Maswali kwa Mdudu (uk. 51) na mende katika shairi “Kifo cha Mende” (uk. 52). Katika diwani ya *Bara Jingine* ametumia tena neno nyuki katika “Mruko wa Nyuki” (uk. 20) na mbu katika “Hatima ya Mbu” (uk. 19). Mshairi anatumia majina haya kimakusudi ili yaafiki ujumbe anaouzungumzia na kumsaidia msomaji kuelewa ujumbe kwa njia rahisi.

2.4.1.2 Msamiati wa Ndege na Wanyama

Mshairi ametumia pia msamiati wa ndege na wanyama. Kwa mfano, ametumia msamiati wa ndege katika shairi “Nyuki, Ndege na Nyegere” (uk. 10) na “Swali kwa Yangeyange” (uk. 41) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Aidha, ametumia kwarara katika shairi “Kwarara” (uk. 12) katika diwani ya *Redio na Mwezi*. Kwengineko, ametumia neno “ubalozi wa mwewe” katika shairi “Mkasa” (uk. 13) katika diwani ya *Msimu wa Tisa*.

Aidha, Kithaka wa Mberia ametumia msamiati wa wanyama kama vile nyegere katika shairi “Nyuki, Ndege na Nyegere” (uk. 10), panya katika shairi “Vitani na Panya” (uk. 12), papa katika shairi “Papa” (uk. 45), mbwa katika shairi “Mzoga wa Mbwa” (uk. 55) na simba katika shairi “Mlipuko wa Furaha” (uk. 56) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Isitoshe, ametumia neno mamba katika mashairi “Hatutaaga Ndoto” (uk. 4) na “Bara Jingere” (uk. 10) katika diwani ya *Bara Jingere*. Fauka ya hayo, ametumia neno samaki katika shairi “Samaki Nje ya Maji!” (uk. 16) katika diwani ya *Redio na Mwezi*. Msamiati huu unamsaidia mshairi kuchimuza kile anakidokeza kwa msomaji mbali na kuonyesha kuwa anaelewa mazingira yake vizuri.

2.4.1.3 Msamiati wa Miti

Mwandishi ametumia miti mbalimbali anapogusia maudhui ya ukoloni na uharibifu na utunzaji wa mazingira. Kwa mfano, neno mgunga katika shairi “Mgunga Shambani” (uk. 20), mti au miti katika “Miti ya Matunda” (uk. 50) na “Mti Ukingoni mwa Mto” (uk. 54) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Katika diwani ya *Bara Jingere* mshairi ametumia neno mikoma katika shairi “Mikoma” (uk. 66), mkalitusi katika shairi “Mkalitusi” (uk. 67), mibuyu katika shairi “Mombasa Mibuyuni” (uk. 72) na mjakaranda katika shairi “Mjakaranda” (uk. 75). Aidha, ametumia mivinje katika shairi “Mivinje Saba” (uk. 5) katika diwani ya *Redio na Mwezi*. Isitoshe, kuna matumizi ya mti aina ya mnga katika shairi “Ndoto Chini ya Mnga” (uk. 47) katika diwani ya *Msimu wa Tisa*.

2.4.1.4 Msamiati wa Matunda

Kithaka wa Mberia anatumia neno matunda kama sitiari anapogusia vitendo vya ufuska miongoni mwa wanaume na wanawake, matunda kama chakula na ugavi wa rasilimali. Kwa mfano, anatumia neno boga katika shairi “Boga” (uk. 2) katika diwani

ya *Mchezo wa Karata* kuhimiza umuhimu wa ugavi sawa wa rasilimali ya nchi miongoni mwa ndugu wawili. Katika diwani ya *Redio na Mwezi*, anatumia neno matikiti katika shairi “Biringanya na Matikiti”(uk. 28) kuonya wanaume dhidi ya kifo kutokana na ugonjwa wa ukimwi. Fauka ya hayo, anatumia neno matunda katika shairi “Matunda Haramu” (uk. 39) kuonyesha jinsi wanandoa wanashiriki uasherati nje ya ndoa. Kwengineko, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, mwandishi anataja vile anga ya Ekweta inatupatia matunda anuwai kama vile parachichi, chungwa, papai, karakara, ndizi, embe, tufaha, pera na plamu katika shairi “Ukarimu wa Ekweta”(uk. 78). Isitoshe, katika diwani ya *Rangi ya Anga* mshairi ametumia majina ya matunda kama vile maembe, matomoko, machungwa na malimau katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya pili.

2.4.1.5 Msamiati wa Vyombo na Vifaa

Kuna msamiati wa vifaa na vyombo maalumu ambao mwandishi anatumia kama taashira mbali na kuchimuza maudhui anayoyaangazia. Kwa mfano, katika diwani ya *Mchezo wa Karata* mshairi ametumia msamiati jembe, surupwenye na kalamu katika shairi “Jembe, Surupwenye na Kalamu” (uk. 26) ili kuzungumzia shida za wakulima, wafanyakazi viwandani na kwenye sekta ya juakali na walimu. Aidha, anatumia neno nyumba katika shairi “Nyumba” (uk. 17) kuonyesha watu wanaostahili kufurahia kukaa katika nyumba (nchi) yaani watu wanyonge ambao wametumia nguvu na misuli yao kujenga nyumba. Mwandishi pia anatumia neno dau katika shairi “Dau Haliendi!” (uk. 32) kueleza vile nchi haiendelei kwa sababu ya siasa na uongozi duni. Mwandishi anatumia neno televisheni katika shairi “Kiwambo cha Televisheni” (uk. 37) kuonyesha tofauti kati ya maskini na matajiri inayochangiwa na ukosefu wa ugavi wa rasilimali sawasawa. Aidha, anatumia neno taa katika shairi “Taa Sebuleni” (uk. 58) kuzungumzia umuhimu wa makabila mbalimbali katika nchi kukaa pamoja kwa udugu na amani bila uchochezi kutoka kwa viongozi.

Katika diwani ya *Bara Jingine*, mwandishi ametumia maneno kamba na jabali katika shairi “Kamba na Jabali” (uk. 3) kuzungumzia hatua ya wanyonge kukataa dhuluma za viongozi wanaotumia jabali yaani pingamizi kuziba njia ya binadamu. Kuna matumizi ya neno redio katika shairi “Redio na Mwezi” (uk. 26) katika diwani ya *Redio na Mwezi*. Aidha, mshairi anatumia neno jahazi katika shairi “Nahodha na

Jahazi” (uk.5) katika diwani ya *Msimu wa Tisa* kuzungumzia namna kiongozi wa nchi, mawaziri na wabunge wanashindwa kuiongoza nchi vizuri.

2.4.1.6 Msamiati wa Tabia-nchi na Sayari

Kithaka wa Mberia ametumia msamiati unaoambatana na tabia-nchi. Kwa mfano, ametumia neno mazigazi katika shairi “Msimu wa Mazigazi” (uk. 23) na tufani katika shairi “Tufani” (uk. 48) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Katika diwani ya *Bara Jingine* ametumia neno giza katika shairi “Giza Mbele” (uk. 26). Aidha, ametumia neno mvua kuisifia mvua katika shairi “Matone ya Mvua” (uk. 73). Kwengineko, katika diwani ya *Redio na Mwezi* ametumia maneno msimu katika shairi “Msimu wa Kaburi” (uk. 3), kimbunga katika shairi “Kimbunga” (uk. 25), mwezi katika mashairi “Redio na Mwezi” (uk. 26) na “Bahari na Mwezi” (uk. 27). Fauka ya hayo, ametumia pia neno jangwa katika shairi “Janga Jangwani”(uk. 75) na ekweta katika shairi “Ukarimu wa Ekweta” (uk. 78) katika diwani ya *Msimu wa Tisa*.

2.4.1.7 Msamiati wa Majina ya Nchi na Sehemu Mahususi za Kijiografia

Mwandishi ametumia majina ya nchi kadha anapogusia vita au mapigano, udikteta, uharibifu na uhifadhi wa mazingira miongoni mwa masuala mengine. Kwa mfano, katika diwani ya *Bara Jingine*, anataja Addis Ababa katika shairi “Kikaoni Addis Ababa” (uk. 2). Katika diwani ya *Msimu wa Tisa* anataja nchi ya Sudan Kusini kuhusu mapigano na vita katika shairi “Darfur” (uk. 26) na “Petali za Amani?” (uk. 29). Vilevile anataja nchi ya Kongo katika shairi “Wendawazimu Kongo” (uk. 19), “Lopinding I” (uk. 44), “Lopinding II” (uk. 45) na “Kakuma” (uk. 66). Aidha, anazungumzia vita na mauaji ya aliyekuwa rais wa Msumbiji, Samora Machel katika shairi “Msumbiji” (uk. 71). Isitoshe, ametaja milima ya Nuba, jangwa la Sahara, bahari ya Mediteraneani na milima ya theluji ya Alps katika shairi “Johari Angani” (uk. 34).

Kithaka wa Mberia ametaja sehemu halisi za mazingira yaliyoharibiwa. Kwa mfano, katika diwani ya *Bara Jingine* kuna Thagicu katika shairi “Thagicu” (uk. 61) na Ithanje katika shairi “Bwawa la Ithanje” (uk. 69). Katika diwani ya *Rangi ya Anga* katika shairi “Wanda” (uk. 27) mwandishi anataja sehemu tofautitofauti zilizoharibiwa na shughuli za wakulima. Sehemu hizo ni kama vile: Kereka, Gitugu, Kamwathu, Kaguma, Kamanyaki, Gaciongo, Gakauni, Kamaindi, Mutino, Nkarini,

Ntoroni, Kamajagi na Ntumira (kur. 41-42). Aidha, kuna sehemu kama Karimi, Karauki, M'kamwara na Muriungi katika eneo la Meru (kur. 43-44).

Mbali na msamiati wa mahali palipoharibiwa, mwandishi anataja maeneo yanayohusu uhifadhi wa mazingira na mandhari yanayopendeza. Kwa mfano, katika diwani ya *Bara Jingine* kuna majina kama “Nyeri” (uk. 70), “Mombasa Mibuyuni” (uk. 72) na “Kambi Malindi” (uk. 79). Katika diwani ya *Redio na Mwezi kuna Shairi* “Johari Bamburi” (uk. 8). Kwengineko, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* kuna maeneo kama “OlKaria” (uk. 64), “Mwea” (uk. 70) na “Ntharene” (uk. 75).

2.4.2 Uharibifu wa Mazingira

Kithaka wa Mberia amepata ilhamu ya kutunga mashairi kuonyesha jinsi mwanadamu anavyochangia kuharibu mazingira yake. Mazingira yanayochafuliwa ni pamoja na maji, hewa, mimea, miti na ardhi. Katika diwani ya *Bara Jingine* mshairi ametunga mashairi kadha juu ya uharibifu wa mazingira. Kwa mfano, shairi “Jinamizi” (uk. 55) linazungumzia juu ya halaiki ya watu wanaokata miti mingi kwa kutumia mapanga, mashoka na misumeno ili kupata mbao na mashamba ya kuendeleza shughuli za kilimo. Ukataji huo wa miti unaleta madhara ya mmomonyoko wa udongo mvua inaponyesha, mifugo kukosa nyasi, vifo vya mifugo, watu, njaa, na kutokea kwa jangwa.

Katika shairi “Ngao” (uk. 59), mwandishi anazungumzia juu ya uharibifu wa utandu wa ozoni. Utandu wa ozoni unasaidia kukinga mwanadamu dhidi ya miale hatari ya jua inayoweza kumsababishia mwanadamu saratani ya ngozi. Licha ya umuhimu huu wa ozoni, binadamu wanaharibu utandu huu kwa kemikali zinazotokana na maendeleo ya teknolojia. Hivyo basi, uharibifu wa utandu wa ozoni unatishia maisha ya mwanadamu kote ulimwenguni.

Katika shairi “Thagicu” (uk. 61), mwandishi anaeleza vile ardhi ya eneo hili imeharibiwa na watu. Mabonde ya Thagicu yamejaa mchanga mweupe. Aidha, kuna mawe yaliyojitokeza ambayo hayana manufaa kwa wakaazi kama hapo mwanzo kabla ya uharibifu. Aidha, katika shairi “Mimi, Mto Nairobi” (uk. 63), sauti ya mshairi inaeleza vile wakaazi wa Nairobi wanachafua maji ya mto huo kwa uchafu wa mafuta ya magari, tairi, makopo, talimbo na takataka nyingine nyingi.

Shairi “Mikoma” (uk. 66) linazungumzia vile wagama, wasonga-mizinga na wakulima katika sehemu za Igaironi, Irarani, Kirukuma na Kaguma wanakata mikoma. Wakaazi wa Gituma wanakata mikoma michanga ili kupata miyaa ya kufuma miteka na vikapu. Ukataji huu wa mikoma unatishia kuangamiza mikoma katika maeneo haya. Kwengineko, katika shairi “Bwawa la Ithanje” (uk. 69), mshairi anaeleza vile wakulima wanyunyiziao maji wanatia sumu ndani ya maji ya bwawa la Ithanje na hivyo kuhatarisha afya ya mifugo, watu na wanyama wanaoishi karibu na bwawa hilo. Aidha, taka za viwanda vya Limuru zinaelekezwa katika bwawa hili na kuchafua maji zaidi.

Katika diwani ya *Redio na Mwezi*, shairi “Kiwanda”(uk. 6) linazungumzia madhara ya gesi ya sumu kutoka kiwanda cha Webuye cha kutengeneza karatasi. Gesi kutoka kiwanda hiki inaduru mimea shambani, inatoboa vitundu kwenye mabati ya nyumba za wakaazi kiasi kwamba maji yanajaa ndani ya nyumba wakati wa msimu wa mvua. Aidha, gesi hiyo mbaya inasababishia watu magonjwa ya macho na ngozi mbali na watoto kupumua kwa shida.

Katika diwani ya *Rangi ya Anga*, sehemu nyingi katika shairi “Wanda” (uk. 27) zinaonyesha uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli na vitendo vya binadamu. Kwa mfano, katika sehemu ya tatu, mwandishi anaeleza vile wakulima wamekata miangati, wagama wamekata mikoma, wasonga-mizinga wamekata mianjate. Ukataji huu wa miti unapatia dhoruba kali nafasi ya kuharibu udongo. Katika sehemu ya nne, ukataji wa miti unachangia kiangazi na joto kali kusumbua kuku, mbuzi, ng’ombe mbali na udongo kukauka. Katika sehemu ya tano, udongo unasombwa na maji hadi kwenye mito. Kwengineko, katika sehemu ya sita, ukataji wa miti kwenye kingo za mito na vijito, miinuko ya vilima na miteremko ya mabonde unachangia mmomonyoko wa udongo. Aidha, kwato za mifugo zinaharibu nyasi zinazokinga udongo na kujeruhi udongo na hivyo kuwa rahisi kusombwa na maji.

2.4.3 Uhifadhi wa Mazingira

Kithaka wa Mberia licha ya kuangazia namna mazingira yamechafuliwa au yanachafuliwa, anazungumzia pia umuhimu na juhudi za kuhifadhi mazingira ili yamfaidi binadamu sasa na vizazi vijavyo. Anapongeza hatua zilizochukuliwa kuhifadhi mazingira yaliyoharibiwa na vilevile kusifu mandhari yanayopendeza ili kutia motisha watu wahifadhi na kutunza mazingira. Katika diwani ya *Bara Jingine*,

kuna mashairi yanayoangazia uhifadhi wa mazingira na mandhari yanayovutia macho. Katika shairi “Nyeri” (uk. 70) mshairi anaeleza vile wakulima wameendeleza kilimo-mseto kwa kupanda majani-chai, kahawa, mahindi na ngómbe wa gredi. Hali hiyo imefanya mandhari ya kijani kuridhisha macho. Aidha, kuna tangazo la kupanda miti kwenye milango ya nyumba katika maeneo ya Othaya, Tetu, Mathira na Mukurweini. Huu ni utunzaji mzuri wa mazingira wa wakaazi wa Nyeri.

Katika shairi “Mombasa Mibuyuni” (uk. 72), mwandishi anaeleza mandhari ya eneo la Mama Ngina katika mji wa Mombasa linalovutia macho kwa sababu ya mibuyu ambayo imesimama imara. Watu wanaenda kuyeyusha machovu yao chini ya mibuyu huku kwenye tanzu zake ndege wanasifia maumbile na rangi nzuri za kupendeza. Kwengineko, katika shairi “Mjakaranda” (uk. 75) mshairi anasifu uzuri wa rangi ya urujuani ya mjakaranda inayopamba mazingira katika bustani ya Jevanje. Aidha, mwandishi anaeleza juu ya ukarimu na mandhari ya kuvutia katika eneo la Malindi katika shairi “Kambi Malindi” (uk. 79).

Katika diwani ya *Redio na Mwezi* shairi “Johari Bamburi” (uk. 8) linaeleza juu ya ardhi iliyochimbwa na matrekta kwa sababu ya kutafuta malighafi ya kutengeneza saruji katika eneo la Bamburi. Katika uchimbaji huo wa kutafuta johari, ardhi iliharibiwa na mandhari yakawa hayavutii macho tena. Lakini baada ya kupanda miche ya miti mbalimbali na mvua kunyesha mandhari yamekuwa ya kuvutia. Mivinje, mibambakofi, mikilifi, mivuli na mikoko imestawi. Wadudu, ndege wa kila aina wanapamba mazingira. Wenyeji wanavutiwa na mazingira ya kupendeza na yamekuwa pia hazina kwa kampuni ya saruji. Watalii wanakuja kuona wanyama mbalimbali kama swara, kiboko, mamba na twiga na kuletea nchi pato la kigeni. Huu ni mfano mzuri wa utunzaji wa mazingira yaliyoharibiwa ambao umeleta faida tele.

Kwengineko, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, mwandishi ametunga mashairi kadha akisifia mazingira mazuri yanayopendeza. Kwa mfano, katika shairi “Johari Angani” (uk. 34) mshairi anaeleza mandhari tofauti ya kupendeza aliposafiri kwa ndege. Aliruka juu ya milima ya Nuba, akavuka jangwa la Sahara, akatazama bahari ya Mediteraneani na milima ya theluji ya Alps kabla ya ndege kutua. Maumbile haya ya asilia yanafurahisha macho ya msafiri yeyote akiwa juu angani.

Katika shairi “Ol Karia” (uk. 64) mwandishi anazungumzia juu ya nishati inayotoka chini ya udongo katika eneo la Ol Karia, nchini Kenya. Nishati hii inatoa umeme ambao unasaidia nchi kupata mwanangaza. Isitoshe, inatumika kuendesha mitambo viwandani, maseremala kuunda samani za mbao kwa kutumia umeme na wakulima wa mboga na matunda pia wanahifadhi mazao yao ndani ya majokofu. Watengenezaji milango na madirisha wanaunga viungo kwa moto. Faida hizi zote za nguvu kutoka Ol Karia zinasaidia kupunguza watu kwenda mijini kutafuta kazi. Nchi inanawiri kwa uwezo wa kiuchumi na kupunguza ufukara.

Shairi “Mwea” (uk. 69) linaangazia eneo tambarare la Mwea, nchini Kenya ambalo ni eneo moja maarufu ambapo wakulima wanapamba mandhari kwa kukuza mpunga. Mwandishi anaonyesha vile rangi ya eneo hili inabadilika. Mara kijani-kibichi, mara rangi ya dhahabu. Haya ni mandhari ya kufurahisha macho. Baadaye, wakulima wanavuna mchele na mandhari kubadilika hadi rangi ya kijivu. Ng’ombe wanatembea wakila mabaki ya mavuno ya mchele mashambani. Maelezo haya yanadhihirisha umuhimu wa mazingira ya Mwea kwa wakulima na taifa la Kenya.

Katika shairi “Ntharene” (uk. 74), mshairi anazungumzia juu ya kituo cha Ntharene katika maeneo ya Meru, Kenya kunakokuzwa bidhaa mbalimbali mashambani. Juhudi za wakulima zikiungwa mkono na udongo mwekundu, mawingu na miali ya jua la Ekweta zinakuza bidhaa zinazouzwa katika kituo cha Ntharene. Wanakijiji wanapanga kandokando mwa barabara bidhaa kama wanga, mapapai, nyanya, ndizi, parachichi, viazi vikuu na viazi vitamu. Malori yanachukua shehena za vyakula hadi mji mkuu kulisha watu wanaofanya kazi ofisini na viwandani na kudumisha urafiki baina ya mashamba na miji. Mambo haya yanaonyesha utunzaji na manufaa ya mazingira kupitia kilimo-biashara.

Kwengineko, katika shairi “Ukarimu wa Ekweta” (uk. 78) mwandishi anasifu hali nzuri ya anga kama vile jua, mvua, udongo na hewa. Hali hii nzuri ya anga ambayo ndio ukarimu wa Ekweta inawasaidia wakulima wanaoishi eneo la Ekweta kukuza parachichi, machungwa, mapapai, karakara, ndizi, maembe, matufaha, plamu na matunda mengine mengi. Matunda haya yanauzwa kwenye masoko ili kupata pesa na vilevile yanaliwa ili kuimarisha afya ya wananchi.

2.5 Muktradha wa Kitamaduni

Mshairi ametumia muktradha wa kitamaduni kuangazia masuala mengi. Utamaduni ni dhana inayojumuisha mila, imani, tabia, mavazi na vyakula vya jamii au kundi fulani la watu. Utamaduni unaweza kuwa mzuri au mbaya kutokana na mkabala wa kuuangalia utamaduni wenyewe. Baadhi ya masuala ya kuangazia chini ya muktradha wa kitamaduni ni mila zilizopitwa na wakati, unafiki wa kidini, ukahaba, ubakaji, matumizi ya vileo na dawa za kulevya na ubaguzi wa rangi.

2.5.1 Ubakaji na Ukahaba

Visa vya ubakaji, ukahaba, uasherati na usenge vimezidi katika jamii ya leo. Licha ya sheria na maadili ya dini kuwepo ili kudhibiti uovu huu, hakuna dalili kuwa visa hivi vitapungua. Kwa mfano, mshairi anaangazia visa vya ubakaji wa wanawake na wasichana wa shule. Matokeo ya ubakaji ni wasichana na wanawake kupata mimba zisizotakikana, wasichana wanakatiziwa masomo yao na uambukizwaji wa ugonjwa wa ukimwi. Siku hizi hata watoto wachanga wanabakwa na baba zao, wavulana waliobaleghe, walimu, wanaume wa umri wa makamo na wazee. Visa vya ubakaji wa wasichana na wanawake vinajitokeza katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) katika diwani ya *Rangi ya Anga*.

Mashairi “Giza Mbele” (uk. 26) “Pamela” (uk. 29) na “Flora na Wenzake” (uk. 33) katika diwani ya *Bara Jingine* yanagusia namna wasichana wanaosoma shuleni wanadhulumiwa kimapenzi na wavulana, wanaume na walimu kiasi cha kukatiziwa masomo yao baada ya kupata mimba za mapema. Wasichana hawa wanalazimika kuacha shule ili kulea mimba zao kwa sababu hawaruhusiwi kuendelea kusoma. Katika shairi “Giza Mbele” na “Flora na Wenzake” wasichana wanapata mimba wakiwa darasa la nane na kuachia masomo yao hapo. Hawaendelei tena kwenda shule ya upili. Kisa cha msichana wa shule kuacha shule baada ya kupachikwa mimba na mvulana mwenzake kinajitokeza pia katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya kumi katika diwani ya *Rangi ya Anga*. Wasichana hawa hawapati elimu ya maana itakayowasaidia katika maisha yao ya siku za usoni.

Kwengineko, mwandishi anagusia tabia ya ukahaba miongoni mwa wanawake katika mashairi “Mimi, Monika” (uk. 37) na “Wanabiashara Barabarani” (uk. 43). Wanawake wanafanya biashara ya ukahaba ili kupata pesa za kutimizia mahitaji yao ya chakula, nguo, kulipia kodi ya nyumba na mengine mengi. Jambo hili linabainika

pia katika shairi “Kisa Chuoni” (uk. 45) katika diwani ya *Redio na Mwezi*. Mwanamke fulani anafanya ukahaba chuoni kwa nia ya kupata pesa za kutimizia mahitaji ya mtoto wake. Vilevile, shairi “Nakumbuka Ulivyokuwa”(uk. 76) katika diwani ya *Bara Jingine* linazungumzia juu ya majeraha na maumivu anayouguza hospitalini mwanamke aliyeshiriki mapenzi na mume wa mtu. Mwanamke huyo alifumaniwa na mke wa mwanamume huyo na akaumizwa mwili kutokana na kichapo alichopata.

Katika diwani ya *Redio na Mwezi*, mwandishi anaeleza matokeo ya ukahaba na uasherati. Ugonjwa wa ukimwi ambao unaangamiza wanawake na wanaume unaangaziwa katika mashairi “Msimu wa Kaburi!” (uk. 3) na “Mgeni Katili” (uk. 4). Baada ya wazazi na walezi kufa, wanaacha msururu wa watoto mayatima. Watoto hao wanakosa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, mavazi, elimu, afya, ulinzi na mapenzi. Aidha, mashairi anaangazia visa vya uzinzi katika mashairi “Biringanya na Matikiti” (uk. 28), “Matunda Haramu” (uk. 39), “Vituko Mjini” (uk. 40) na “Matumizi Mengine” (uk. 41). Vitendo vya uzinzi vinatokea miongoni mwa wanawake na wanaume kila siku na kuonekana ni mambo ya kawaida tu lakini ni ishara ya uozo wa kimaadili uliopo katika jamii ya leo. Kwa mfano, katika shairi “Vituko Mjini” mwandishi anaeleza vile wanawake na wanaume wanashiriki mapenzi kwenye mazulia ndani ya maofisi punde tu wafanyakazi wenzao wanapoenda nyumbani baada ya kumaliza kazi za siku.

2.5.2 Unafiki wa Kidini

Dini ni mfumo fulani wa imani kwa njia ya kuabudu, kusali na kumtii Muumba. Kabla ya kuja kwa dini ya Kikristo, Waafrika walikuwa na imani na miungu wao waliowaabudu. Hata hivyo, wamishenari wa Kikristo walipokuja Afrika kuhubiri na kueneza injili, waliwashawishi Waafrika waache imani zao kwa madai kuwa zilikuwa potovu. Waafrika wengi waliacha imani na mila zao wakafuata dini ya Kikristo kama dini inayofundisha maadili mema. Lakini licha ya hayo, viongozi wa dini na waumini wenyewe wanaonyesha unafiki wa kidini. Unafiki ni hali ya kutokuwa mkweli. Kithaka wa Mberia anaonyesha vile wachungaji na waumini hawaishi maisha yanayodhihirisha maadili na mafundisho ya dini. Baadhi ya waumini wanakwenda kinyume na maagizo ya dini ilhali pia baadhi ya wachungaji wanatumia dini kujinufaisha hasa katika tamaa za kimwili.

Katika diwani ya *Redio na Mwezi* shairi “Muumini” (uk. 29) linaonyesha wazi unafiki wa muumini wa kike kanisani. Baada ya misa ya tatu kuisha, wanawake kwa wanaume, wazazi kwa watoto wanatoka nje ya lango la kanisa. Lakini mwanamke mmoja mwenye umri wa makamo anabaki nyuma akiomba kwa unyenyekevu. Anatubu dhambi zake kwa sababu ya vitendo viovu alivyofanya siku iliyotangulia ili kujenga njia ya kuingia mbinguni. Mwandishi anasema:

Au jana, Jumamosi, baada ya kikao cha pombe,
Baada ya akili kulemaa, mwili ulimhadaa
Bila tahadhari, kiholela, akapanda angani
Na kukata rumba ukumbini mwa upinde-wa-mvua
Na sasa, akitapatapa katika bwawa la hofu
Anaomba Mola amwepushe na tanzi la virusi (uk. 29)

Katika dondoo hili, mwanamke huyu anabaki nyuma kuomba Mungu amwepushie hatari ya kupata virusi vya ugonjwa wa ukimwi. Siku iliyotangulia, alienda kwenye klabu akanywa pombe. Akili yake ililemaa akajisahau na mwili ukamdanganya. Alishiriki mapenzi kiholela na mwanamume. Baada ya kuleuka na kupata ufahamu, dhamiri yake inamsumbua na ndipo anakuja kanisani siku ya Jumapili kutubu baada ya waumini wengine kuondoka. Mwanamke huyu hashiki maagizo ya dini kama muumini wa kweli. Huu ni mfano wa unafiki wa kidini.

Kwengineko, katika shairi “Mchungaji na Muumini” (uk. 31) kuna unafiki wa kidini pia. Mchungaji na muumini wa kike wanakutana kwenye usiku wa manane kwa nia ya kushiriki mapenzi. Mshairi anasema:

Wanasimama kwenye lindi la usiku, wakitabasamu
Mchungaji, hanui kusoma injili, hatachambua Torati...
Aliacha joho la utakatifu nyumbani, kwenye kiango
Akafuata rangi ya dunia ...
Naye muumini, johari ya maumbile, waridi kanisani
Hafuati mlo wa kiroho, ananyemelea asali ya moyo
Wanazama katika upinde-wa-mvua wa anga la hisia...(uk.31)

Mchungaji na muumini wanaonyesha unafiki wa kidini. Hawana maadili ya dini ndani yao. Wanaongozwa na tamaa za mwili. Mchungaji anatumia ushawishi wake wa kidini kuzini na muumini wake wa kike.

Katika shairi “Mhubiri na Mjinga” (uk. 42) mwandishi anaonyesha vile mhubiri anatumia dini kujinufaisha. Mhubiri anamtembelea muumini wa kike nyumbani kwake kila mara kumpa lishe ya roho. Mume hamshuku mhubiri wala mke wake.

Lakini siku moja mume anapanga kwenda safari. Kwa sadfa, safari inavunjika na mume anarejea nyumbani wakati wa usiku. Anawakuta mhubiri na mke wake wakipigana mabusu chumbani. Mume, kwa hasira anapigana na mhubiri kiasi cha kumuua. Jamaa na marafiki za mhubiri wanahuzunika. Kunakuwa na vikao mahakamani na mshangao kanisani. Visa vya wahubiri kushiriki mapenzi na waumini wao vinaripotiwa kwenye redio, runinga na magazeti kila kuchao. Unafiki wa kidini unajitokeza katika diwani ya *Redio na Mwezi* kuliko diwani hizo nyingine.

2.5.3 Matumizi ya Vileo na Dawa za Kulevya

Katika jamii ya Kiafrika, historia inaonyesha kuwa vileo vilitumiwa na wazee katika sherehe maalumu na vikao vya wazee kama njia ya kujiburudisha. Kulikuwa na utaratibu wa kutumia vileo hivyo. Aidha, wanawake hawakuruhusiwa kutumia vileo. Lakini siku hizi, mambo yamebadilika. Unywaji wa pombe kiholela umekuwa jambo la kawaida na unachangia mizozo na hata vifo katika familia nyingi. Isitoshe, wanafunzi wa shule, wavulana kwa wasichana wanashiriki ulevi na kutumia dawa zingine za kulevya, jambo ambalo lilikuwa mwiko katika jamii za Kiafrika tangu jadi. Licha ya kuwepo kwa sheria zinazodhibiti matumizi ya vileo na dawa zingine za kulevya, vijana wengi wamejiingiza katika matumizi na ulanguzi wa dawa za kulevya. Kwa mfano, Kithaka wa Mberia anaonyesha matumizi ya sigara, vileo na dawa za kulevya miongoni mwa watoto katika shairi “Ni Sumu kwa Watoto” (uk. 49) katika diwani ya *Bara Jingine*. Wazazi wanawapatia watoto pesa nyingi ambazo wanatumia katika ulevi na dawa za kulevya. Mwandishi anasema:

Ni sumu, sumu jeruhi
Unajeruhi watoto
Kwa mapenzi yako hatari
Ya kuliwaza watoto kwa pesa,
Pesa chungu nzima ambazo
Zinawafikisha kwenye sigara na ulevi
Na kisha kwenye dawa za kulevya (uk. 50)

Suala la matumizi ya vileo na dawa za kulevya linagusiwa tena na mshairi katika diwani ya *Redio na Mwezi* kwenye shairi “Evergreen Ltd” (uk. 49). Katika klabu hii, wananchi kutoka karibu na mbali wanakutana kikaoni kuvuta na kutafuna dawa mbalimbali za kulevya mbali na kunywa vileo vya kila aina. Baada ya kulewa, wanaume kwa wanawake wanashiriki mapenzi bila tahadhari. Mwandishi anaeleza:

Sokomoko ya harufu
Pombe, mairungi, pumzi
Mioshi mbalimbali
Na siri za kimaumbile
Inapiga pua kumbo (uk. 49)

Vilevile, shairi “Tembo” (uk. 56) linagusia namna pombe ilivyomharibia maisha mvulana aliyesoma mpaka chuo kikuu lakini anakosa kazi. Anaomba marafiki nauli na mahali pa kulala. Mvulana huyu hana kazi, makazi na familia. Mwandishi anaeleza:

Lakini tembo lilimtaka urafiki, akakubali
Taratibu, bila nia mbaya kudhihiri
Tembo lilimdanganya, lilimzuga akili... (uk. 56)

Katika shairi “Rafiki Katili” (uk. 57) mwandishi anamulika madhara ya pombe kwa wanaume na wanawake. Waliolewa wanapigana nyumbani, watu wanachomana visu na risasi zinapigwa vifuani. Madereva wanasababisha ajali kwa sababu ya ulevi na wasio na tahadhari wanapata ugonjwa wa ukimwi kwa sababu ya kunywa na kushiriki mapenzi kiholela. Mshairi anasema:

Tembo, unasababisha mieleka nyumbani
Unachoma amani kwa moto wa ugomvi
Visu vinapasua mapafu na figo
Panga zinashtua mifupa na mishipa
Risasi zinapiga mbizi vifuani
Badala ya ndoa, kunabaki jivu (uk. 59)

Mwandishi anazidi kudhihirisha matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana katika diwani ya *Msimu wa Tisa* katika shairi “Macho Mekundu” (uk.59). Macho ya vijana yamekuwa mekundu kwa sababu ya kutumia dawa za kulevya. Vijana hao wanafanya vitendo vya ukatili kama kupiga wazazi na majirani na kubaka ndugu na binamu wa kike. Isitoshe, vijana hao wanatumika kubebea watu mizigo na wananyang’anya wakaazi ng’ombe na mbuzi. Haya ni madhara ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana. Mwandishi anasema:

Macho yao, tofauti na ya watoto wengine
Hayashangilii rangi za upinde-wa-mvua
Wala kuvutiwa na wadudu warembo,
La! Yamezoea wekundu wa damu
Yana dhiki, ni mekundu kama hoho
Ni mateka, wamefungwa minyororo
Yamekamatwa na dawa za kulevya (uk. 59)

2.5.4 Ubaguzi wa Rangi na Hadhi

Ubaguzi ni mfumo wa kijamii wa kutoa huduma kwa upendeleo kwa misingi ya rangi, jinsia, kabila miongoni mwa vigezo vingine. Ubaguzi wa rangi ni hali ambapo mtu fulani anahudumiwa au kukosa kuhudumiwa kwa sababu ya rangi ya ngozi yake. Jambo hili linaonyesha kuwa kuna watu walio “bora” kuliko wengine. Huu ni mfano wa “uwingine” katika nadharia ya baadaukoloni. Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi “Muuaji Mwenye Furaha” (uk. 22) linazungumzia juu ya ubaguzi wa rangi. Mwanajeshi wa kigeni mwenye ngozi nyeupe alimuua mwanamke Mwafrika usiku wa manane, karibu na bahari kwa ncha kali ya chupa. Kutokana na kosa la mauaji, uchunguzi ulifanywa na hatimaye analetwa mahakamani akiwa na pingu mkononi ili kukabiliana na sheria. Halaiki ya watu iliyofika mahakamani ina matarajio kuwa mshukiwa atapewa adhabu kali kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo, jaji anatoa hukumu ya kumwachilia huru mwanajeshi huyo aende kwao ambapo watu wao wanampokea kwa furaha. Mwandishi anasema:

Alitetwa mahakamani akiwa na pingu mikononi
Ngozi yake, tofauti na zetu, sawa na jaji na mshtaki...
Jaji alipofungua kinywa, alipotangaza hukumu kwa muuaji
Muuaji aliambiwa aende zake nyumbani!

Kumbe! Sheria za taifa zina macho yasiyohitaji miwani
Zinaona na kutambua vyema ngozi za washtakiwa
Kwa nini mahakama ichanganywe weupe na weusi!! (uk. 22)

Katika dondoo hili, muuaji anakuwa mwenye furaha kwa sababu anaachiliwa huru badala ya kufungwa. Hatozwi hata faini. Anaachiliwa kwa sababu yeye ana ngozi nyepesi ilhali jaji na mshtaki wana ngozi nyeusi. Hakuna haki kwa familia ya mwanamke aliyeuawa. Mwandishi anakejeli na kulaani hukumu ya namna hii. Hukumu hii inaonyesha dhuluma na unyanyasaji kwa misingi ya ubaguzi wa rangi. Tabia hii ya kuwaona watu wengine kuwa bora kuliko wengine kwa sababu ya rangi ni hali bado ingalipo katika jamii ya leo.

Shairi “Wahalifu Huru” (uk. 30) linaonyesha ubaguzi wa hadhi. Watu wenye nyadhifa kuu serikalini hawatiwi mbaroni wanapofanya makosa. Lakini watu wa chini wanapokosea, wanashikwa haraka na kushtakiwa. Huu ni ubaguzi wa wenye uwezo dhidi ya wanyonge. Huu ni mfano mwingine wa dhana ya “uwingine” katika nadharia ya baadaukoloni. Katika shairi hili, wanasiasa wanachochea mashambulizi dhidi ya

“wageni” katika eneo fulani. Mali ya watu wasio wenyeji inaharibiwa. Nyumba zinachomwa ambapo samani, nguo na vyeti vinachomeka. Maghala ya vyakula yanachomwa pia. Watu wa kabila moja wanawachoma mishale mbali na kuikata kwa mapanga miili ya wakaazi wa makabila mengine. Vituo vya biashara vinachomwa. Mashamba yaliyohimili familia kwa mimea na mifugo yanavamiwa na kwekwe. Kukawa na wajane na mayatima.

Kutokana na mashambulizi na chuki za kikabila, wasichana wanaanza kufanya ukahaba ilhali wavulana wanaanza kutumia dawa za kulevya na kisha kutumbukia katika visa vya wizi na unyang’anyi. Kinaya ni kuwa licha ya haya yote kutokea waasisi wa mashambulizi haya wako huru kwa sababu wao ni wakubwa serikalini. Mwandishi anasema:

Badala ya wahandisi wa jakamoyo kutetemeka mahakamani
Badala ya wenye damu viganjani kutupwa korokoroni
Wanaendesha mashagingi yenye bendera za mamlaka
Wanalipwa mishahara minono wakiitwa “viongozi wa taifa” (uk. 30)

2.5.5 Mila Zilizopitwa na Wakati

Mila ni mambo yanayofanywa na jamii fulani ambayo yanalingana na asili, mazingira na nyendo za jamii hiyo. Kila jamii ina mila ambazo inazingatia ili kuendeleza maisha yake ya kila siku. Hata hivyo, baadhi ya mila zimepitwa na wakati kwa sababu ya maendeleo na usasa uliopo hivi leo. Katika ushairi wa Kithaka wa Mberia mila zilizopitwa na wakati zinajitokeza vizuri katika diwani ya *Rangi ya Anga* kuliko hizo diwani zingine. Mshairi anashtumu hali na mila zilizopitwa na wakati zinazokandamiza wasichana na wanawake kwa jumla. Katika diwani ya *Rangi ya Anga* katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1), mshairi ameangazia kwa mapana jinsi mwanamke ananyanyaswa na mila kama vile kunyimwa haki ya kurithi mali, ukeketaji wa wasichana, uozaji wa wasichana wachanga kwa wanaume matajiri, dharau ya mwanamke asiyezaa watoto wa kiume na ukatili wanaotendewa wanawake katika mizozo ya kinyumbani. Mambo haya yanaonekana kuwa ya kawaida lakini yanamnyima mtoto wa kike na wanawake wote haki zao na uhuru wa kujieleza.

Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya pili, mwandishi anasema kuwa mwanamume anamiliki mali kwa kushika upanga mkononi. Mwanamke anapoishiwa na uvumilivu na kuingia katika mapambano ya kutaka usawa katika urithi wa mali,

mwanamume anashika upanga na kumkatakata hadi damu ikatiririka. Kwa mujibu wa mila, mwanamume ndiye ana haki ya kurithi mali: ardhi, mikahawa, migomba, miparachichi, miembe, viazi-vikuu, mifugo na kadhalika. Mwandishi anauliza:

Kwa kanuni za mababu
Ni nani atakayerithi shamba
Ambamo mnukio adhimu
Wa maembe na matomoko
Na machungwa na malimau
Umepamba chembe za hewa
Kama moshi-manukato
Wa ubani au ambari? (kur. 3-4)

Kumnyima mwanamke haki ya kurithi shamba, mimea ya kila aina na mifugo ni kumnyanyasa na kumbagua. Anastahili kurithishwa mali ili ayatumie kwa namna atakavyo. Hali hii ndio imechangia wanawake kubuni makundi ya kutetea haki zao dhidi ya mila na mifumo ya ubabedume inayowachukulia kuwa watu wa jinsia duni.

Mbali na suala la urithi, jambo jingine ambalo linakandamiza na kukiuka haki za wasichana ni ukeketaji. Jamii nyingi zilishikilia na bado zinashikilia kuwa ili msichana avuke kutoka rika la utoto hadi utu uzima, sharti apashwe tohara. Msichana akipenda au asipende sharti apashwe tohara kwa sababu ni mila. Akikataa basi atakuwa amekiuka mila za jamii. Wasichana wanaokataa kukeketwa wanatengwa na jamii kuwa ni watu waasi na wanatungiwa nyimbo za kuwakashfu. Mshairi anasema katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya nne:

Wasanii waliofungwa pingu za mila
Wametungia nyimbo sumbufu kama mpupu
Wakilalamika kwamba kijana wa kike
Kukataa kukeketwa kunakokeketwa
Ni kinyume na utamaduni wa kabila
Ni kitendo kinachonuka vumba ya aibu! (uk. 6)

Mara tu msichana anapopashwa tohara, anachukuliwa kuwa mtu mzima ambaye anaweza kuolewa haijalishi kama anasoma. Wazazi wanampangia aolewe bila ridhaa yake kwa mwanamume mzee mwenye mali kusudi wapate mahari ya kuwaondolea umaskini. Kuna jamii zinaamini kwa sababu ya mila kuwa hakuna manufaa ya kumsomesha msichana kama mvulana. Kumsomesha msichana ni kuharibu mali na muda kwa sababu ataolewa na ataenda kusaidia familia alikoolewa. Jamii kama hizi zinaonelea msichana aozwe mapema katika ndoa ya kupangiwa. Katika shairi “Rangi

ya Anga” (uk. 1) sehemu ya sita kupitia sauti ya mshairi anasema kuhusu ndoa za mapema kwa msichana:

Wewe sasa ni mtu mzima
Mshale wa mizani ya miaka
Unaonyesha miaka kumi na minne
Mbona usiolewe na Mzee Malimali
Kusudi mahari ya ng’ombe na mbuzi
Ituzimie moto wa umaskini? (uk. 8)

Katika dondoo hili, msichana wa miaka kumi na minne amefikia umri wa kuolewa. Wazazi wenye tamaa ya kupata mahari wanapanga aolewe kwa mtu ambaye ni mzee, hamjui wala hampendi. Badala ya kuozwa kwa mvulana wa umri wake anaozwa kwa mzee mwenye mali. Hii ni dhuluma kwa msichana ambaye bado kwa umri wake anahitaji mapenzi, ulinzi, elimu, mavazi na ushauri wa mwongozo maishani kutoka kwa wazazi.

Kwengineko, mshairi anaeleza juu ya mateso anayopitia mwanamke anayejifungua watoto wasichana pekee. Jamii nyingi hasa za Kiafrika zinamthamini mtoto wa kiume sana katika ndoa. Ndoa huonekana kamilifu na ya kufaulu ikiwa wanandoa wamejaaliwa mtoto wa kiume. Lakini pale ambapo mke anajifungua watoto wa kike tu, anabezwa na jamii kwa sababu ya mila na taasubi ya jinsia. Mwandishi anasema kuwa mwanamke kama huyo anabezwa anaposema, anatwezwa anapotenda, anadharauliwa sokoni na nyumbani, anakemewa mezani na kuonywa vikali chumbani. Mshairi anasema katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya nne:

Upepo wa masuto wa daima
Na fedheha na vitisho vizito
Ukimviringisha kwenye vumbi
Kwa “kosa lisilostahimilika”
La kuleta duniani watoto wa kike
Badala ya “watoto wastahiki” (uk. 6)

Katika jamii zingine, wanaume huamini kuwa kumpiga mwanamke katika ndoa ni haki na jambo la kawaida. Mume humpiga mke anapokosea na kuumumiza mwili. Humpiga makofi, ngumi na kumtoa damu puani na meno kinywani. Sababu ya mume kumwadhibu mkewe ni kuwa wanawake ni kama watoto ambao wanastahili kurekebishwa. Isitoshe, mume ana haki na anaruhusiwa kumpiga mke wake kwa sababu alimlipia mahari. Mila za namna hii zinamkandamiza mwanamke. Mbali na

hayo, wanaume husahau kuwa wanawake ni watu wenye hisia na haki sawa na wanaume. Mwandishi katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya tano anasema:

Mume amemwadhibu mkewe
Wanawake, ni kama watoto
Usipowarudi, hupoteza njia!

Mume ana haki thabiti
Anaruhusiwa kumwadhibu mkewe-
Si alilipa mahari! (uk. 7)

Dondoo hili linaonyesha wazi misimamo hasi ya wanaume dhidi ya wanawake. Ingawa mila kama hizi zilikuwepo na zilishikiliwa na jamii nyingi za Kiafrika, hazina nafasi tena katika jamii ya kisasa.

2.6 Mukadha wa Kihistoria

Historia ni muhimu katika ukuaji wa nchi kwa kuwa inazungumzia mambo yaliyopita au hali ya mambo ilivyokuwa na kisha kuwa kiunzi cha mambo yanayoendelea sasa na pengine yatakayokuja. Kwa hivyo, historia inaonyesha nchi ilikotoka, iliko na pengine itakakoelekea. Ikiwa kuna mambo mazuri yaliyofanyika yanapongezwa na yale mabaya yanakashifiwa. Kithaka wa Mberia anatumia mukadha wa kihistoria ili kumulika ilikokuwa nchi ya Kenya na bara la Afrika wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Anagusia uhusiano kati ya wakoloni na watawaliwa na juhudi zilizofanywa ili kujipatia uhuru. Isitoshe, anaangazia tabia na mienendo ya viongozi walioingia mamlakani kuendeleza ukoloni mamboleo katika nchi zao huru kupitia uongozi wa kidikteta. Fauka ya hayo, mwandishi anamulika namna mataifa ya Afrika hayajapiga hatua kimaendeleo miaka mingi baada ya kupata uhuru kwa sababu ya siasa na demokrasia duni. Kwa mfano, katika diwani ya *Mchezo wa Karata*, shairi “Mgunga Shambani” (uk. 20) limekitwa katika historia kwa sababu mshairi anazungumzia juu ya ukoloni na ukoloni mamboleo.

Kuhusu ukoloni, mwandishi anaeleza kuwa katika miaka mingi iliyopita kulistawi gongo la mgunga kwenye shamba la mawe. Gongo la mgunga linaashiria mkoloni alivyoingia nchini Kenya yaani shamba la mawe. Baada ya kuingia nchini Kenya, mkoloni alianza kuchoma wenyeji kwa michomo mikali kwa maana ya kuwadhulumu na kuwatesa wananchi kupitia utumwa na sheria zilizokandamiza uhuru wao. Wananchi walipochoka kukandamizwa na mkoloni, walianza harakati za kujikomboa

kutoka kwa minyororo ya wabeberu. Walipigana na mkoloni hadi wakafanikiwa kumwondoa. Wakasherehekea kwa shangwe kuwa wamepata uhuru.

Hata hivyo, baada ya kupata uhuru, miaka mingi ilipita. Wananchi wakagundua kuwa pale walipong'oa mgunga yaani kumuondoa mkoloni na utawala wake dhalimu, palistawi mti mwingine. Mti mwingine hapa unamaanisha viongozi walioingia mamlakani baada ya kupata uhuru. Viongozi hao walitawala kwa kufuata mienendo ya mkoloni na kuanza kunyanyasa wananchi kama katika enzi ya ukoloni. Kwa hivyo, walibadilisha ngozi tu lakini wanatumia mizungu ya mkoloni kutawala. Viongozi hao wapya wanaiga tabia na mienendo ya wakoloni. Huu ni ukoloni mamboleo.

Diwani ya *Rangi ya Anga* pia inagusia historia ya bara la Afrika. Shairi “Zimwi la Theluji” (uk. 48) linazungumzia juu ya ung'ang'aniaji na ugawaji wa bara la Afrika na wakoloni kama vile Waingereza, Wafaransa, Wabelgiji na Wajerumani. Mshairi anaonyesha kwamba dini ya Kikristo ilitangulia kisha ikafuatwa na ukoloni. Wakoloni waligawanya bara la Afrika, wakachukua mashamba ya Waafrika na wakajijengea nyumba nzuri. Fauka ya hayo, walikuza mimea kama majani-chai, kahawa, pareto, pamba, mkonge miongoni mwa mingine na kupeleka mazao katika nchi zao. Wanaume wenye misuli walichukuliwa kuwa watumwa katika nchi za ng'ambo. Haya pamoja na mengine ni madhila waliyotendewa Waafrika miaka mingi iliyopita. Baadhi ya athari za ukoloni huo zimefumbatwa katika ukoloni mamboleo. Historia hii imebainika katika ushairi wa Kithaka wa Mberia kama kumbukumbu muhimu.

2.7 Hitimisho

Katika sura hii, tumechanganua miktadha ya mawasiliano na usemi ambayo imekuwa vichocheo na vyanzo vya maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Miktadha ambayo imeangaziwa ni pamoja na muktadha wa kisiasa, muktadha wa kiuchumi, wa kimazingira, muktadha wa kitamaduni na muktadha wa kihistoria. Katika muktadha wa kisiasa, tumeangazia namna viongozi na wanasiasa ni wajanja na wanafiki. Wana tamaa na ulafi kiasi kwamba hawazingatii maslahi ya wananchi. Aidha, viongozi wengine hasa marais wanapopata vyeo hivyo wanatumia mamlaka yao kunyanyasa watawaliwa kwa kuonyesha udikteta na mwishowe wanakataa kuondoka uongozini ili kuachia wengine nafasi ya kutawala.

Katika muktadha wa kiuchumi, kuna matabaka ya matajiri na maskini. Aidha, kuna waajiri na wafanyakazi. Matajiri wanamiliki na kudhibiti nyenzo za uzalishaji mali kama vile mashamba, mtaji, nguvukazi na kadhalika. Wafanyakazi wanalazimika kuwafanyia kazi matajiri ambao wanawafanyisha kazi ngumu na katika mazingira duni kisha wanawalipa ujira mdogo. Juhudi za wakulima, wafanyakazi wa jua kali, walimu na watu wengineo hazitambuliwi. Wafanyakazi na watu maskini wanapodai haki ya kulipwa vizuri, wanatishwa au kufungwa kupitia sheria zisizozingatia haki na usawa.

Muktadha wa kimazingira umeonyesha jinsi binadamu wanaharibu mazingira yao kama vile ardhi, misitu, maji na hewa. Mazingira yanapoharibiwa, maisha ya binadamu na wanyama yanakuwa hatarini kwa sababu ya magonjwa na njaa. Aidha, uharibifu wa mazingira unachangia mmomonyoko wa udongo, ongezeko la joto na utokeaji wa jangwa. Licha ya uharibifu huu, mwandishi anaonyesha umuhimu wa kuhifadhi na kutunza mazingira kupitia upanzi wa miti na mimea mbalimbali kwa nia ya kudhibiti mazingira na kurembesha mandhari yawe mahali pazuri pa kuishi na kwa vizazi vya baadaye.

Kuhusu muktadha wa kitamaduni, mshairi ameangazia mila na kaida ambazo zinanyanyasa watoto wa kike na wanawake kwa jumla. Mila zinazohusu urithi wa mali, ukeketaji wa wasichana, ndoa za mapema, kudharau mwanamke anayezaa watoto wa kike pamoja na kumpiga mke eti kwa sababu alilipiwa mahari zinadhulumu wanawake. Aidha, anaonyesha vitendo na tabia zisizofaa ambazo zinachukuliwa kama mambo ya kawaida kwa sababu ya utamaduni mahuluti lakini zinaonyesha ukosefu wa maadili. Tabia na vitendo hivyo ni pamoja na uasherati, ukahaba, ushoga, ubakaji, utumizi wa vileo na dawa za kulevya na ubaguzi wa rangi. Mambo haya yanaonyesha mifumo iliyooza na utovu wa maadili katika jamii ya leo.

Muktadha wa kihistoria nao unadhihirisha vile hali na mambo ya miaka ya nyuma yana athari katika maisha ya sasa na hata ya baadaye. Mataifa ya Afrika yalipopigana na wakoloni, yalikuwa na nia ya kuondoa ukoloni ili yawe huru kujitawala na kuendesha shughuli zao yenyewe. Hata hivyo, kwa mujibu wa mwandishi, historia inaonyesha kuwa hata baada ya kujipatia uhuru; bado kuna chembechembe za ukoloni mamboleo katika mataifa ya Afrika, hasa katika serikali, uongozi, mahakama na mashirika ya kimataifa. Fauka ya hayo, maazimio yaliyokusudiwa kushughulikiwa na

mataifa ya Afrika baada ya uhuru hayajatekelezwa. Maazimio hayo ni kama vile kumaliza shida ya magonjwa, kutojua kusoma na kuandika na umaskini. Chagamoto hizi zingali zinakabili bara la Afrika.

SURA YA TATU

SIASA, UTAWALA NA MAMLAKA KATIKA MATAIFA YA AFRIKA

3.1 Utangulizi

Masuala ya siasa, utawala na mamlaka yameangaziwa kwa mapana na marefu katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Masuala haya yanagusia namna wanasiasa na serikali za mataifa ya Afrika zinaendesha mambo yao baada ya ukoloni. Mambo haya ndiyo yanayochangia kutumia nadharia ya baadaukoloni ili kuchanganua na kuweka wazi namna nchi za Afrika zinavyojitawala. Mshairi ametunga mashairi kadha yanayoonyesha namna utawala unavyoendeshwa nchini Kenya na mataifa mengine ya Kiafrika kwa jumla. Kwa mfano, anaangazia siasa ya unafiki miongoni mwa wanasiasa, ufisadi na ulafi pasi na kuzingatia katiba na haki. Matokeo ya siasa za mkondo huu ni kuwa wananchi wanaishi maisha ya umaskini na kunyanyaswa.

Wananchi wasiporidhika na uongozi, wanaanza harakati za kujikomboa dhidi ya utawala wa siasa dhalimu. Ili kudumisha hali ya mambo, serikali inatumia taasisi na vyombo kandamizi vya dola kuzima jaribio la mapinduzi. Fauka ya hayo, mtunzi anamulika namna viongozi na matabaka yenye uwezo katika nchi zilizostawi wanatumia mamlaka kudhibiti makundi mengine ya watu au nchi zinazoendelea. Kwa hivyo, katika sura hii tumechanganua maudhui yote yanayohusu siasa, utawala na mamlaka katika mataifa huru ya bara la Afrika kwa kutumia mihimili ya nadharia ya baadaukoloni. Isitoshe, mtindo uliotumiwa na mwandishi kuwasilisha maudhui hayo pia umeangaziwa kwa misingi ya nadharia ya elimumitindo.

3.2 Maudhui

Maudhui ni jumla ya mawazo yanayozungumziwa na mwandishi katika kazi ya kifasihi iwe ni riwaya, tamthilia, hadithi fupi au shairi. Kithaka wa Mberia ameshughulikia maudhui kadha yanayogusia siasa, utawala na mamlaka. Baadhi ya maudhui ambayo tumechanganua katika sura hii ni pamoja na unafiki na tamaa katika siasa, uongozi wa kidikteta, ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo, changamoto za mataifa ya Afrika na ujenzi wa jamii mpya miongoni mwa mengine.

3.2.1 Unafiki na Tamaa Katika Siasa

Unafiki ni hali ya kujifanya kuwa rafiki na kutokuwa mkweli (TUKI 2013). Mshairi ameangazia masuala ya unafiki na tamaa ya viongozi na wanasiasa katika diwani zake

kadha. Kwa mfano, katika diwani ya *Mchezo wa Karata* baadhi ya mashairi yanayogusia unafiki na tamaa ya viongozi na wanasiasa ni kama vile: “Mchezo wa Karata” (uk. 18), “Msimu wa Mazigazi” (uk. 23), “Dau Haliendi!” (uk. 32) na “Karamu ya Nzige” (uk. 35) miongoni mwa mengine. Katika diwani ya *Bara Jingine* shairi lenye maudhui ya kisiasa ni “Machozi ya Damu” (uk. 1). Fauka ya hayo, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, mashairi “Nahodha na Jahazi” (uk. 5), “Tope la Mizozo” (uk. 6), “Werevu” (uk. 8), “Msimu wa Tisa” (uk. 9), “Msimu Mwingine wa Wasaliti” (uk. 12), “Kitini” (uk. 18), “Tume za Rais” (uk. 31) na “Magenge Matatu” (uk. 32) yanaangazia uongozi mbaya, utawala duni na unafiki wa kisiasa.

Dhana ya siasa inahusu mambo mawili. Kuna watu au viongozi wanaounda au kutekeleza maamuzi fulani na pia kuna watu wanaoathiriwa na maamuzi hayo. Kwa misingi hiyo, Kithaka wa Mberia anaonyesha kuwa watu wanaotamani uongozi huenda kwa wananchi kwa unyenyekevu na kuwapa maneno matamu na ahadi za kuwaletea maendeleo pindi wakipewa nguvu na mamlaka ya kutawala. Wakati mwingine wanatoa mlungula na kuwapumbaza wananchi akili kuwa ni watu wanaowajali ili wawapigie kura. Lakini baada ya uchaguzi, viongozi hao wanawasahau wananchi waliowapigia kura, wanakosa kutekeleza ahadi walizozitoa wakati wa kampeni, wanafuja pesa kupitia kashfa, miradi na kandarasi bandia pamoja na kujitwalia mali huku wananchi wakiteseka. Matokeo ya uongozi na siasa za aina hii ni ukosefu wa maendeleo, dhuluma na unyonge, ongezeko la umaskini na jaribio la wananchi kusitisha kero na dhuluma.

Katika diwani ya *Mchezo wa Karata*, shairi “Mchezo wa Karata” (uk. 18) linaonyesha wazi ujanja na unafiki wa viongozi wanaotawala. Mazimwi ambao ndio watawala wanatumia hila, uonevu na nguvu kutawala wananchi. Zimwi ni kiumbe mwenye uwezo wa kujibadilisha katika hali mbalimbali ambaye anaweza kudhuru. Mwandishi anaita viongozi mazimwi kwa sababu ni vigeugeu na wanadhulumu wananchi. Mshairi anasema:

Tuliketi, tukiangaliana
kwenye ukumbi wa maisha
Tulikuwa vikundi viwili
Kimoja chetu
Kingine cha mazimwi
Tukicheza karata (uk. 18)

Ujumbe katika shairi hili unaonyesha namna tabaka tawala linavyotumia hila kuendesha siasa kwa maslahi yake tu. Hata pale wananchi wanataka mabadiliko ya kisiasa, mazimwi, yaani tabaka tawala linabadili vipengele fulani vya katiba kusudi wabaki uongozini ili kuendeleza siasa za ubinafsi na kuwakandamiza wanyonge.

Kwengineko, katika shairi “*Dau Haliendi!*” (uk. 32), mwandishi anaeleza vile ubinafsi, tamaa, siasa duni ya ukosefu wa maono kutoka kwa viongozi inazuia nchi kupiga hatua za maendeleo. Dau ambalo ni sitiari inayorejelea nchi yenye mamilioni ya watu, linaenda mwendo wa mzunguko. Ukosefu wa sera imara katika sekta za afya, kilimo, elimu, uchumi, siasa na utamaduni unachangia nchi kutoendelea mbele.

Ujumbe wa unafiki na tamaa katika siasa unabainika pia katika shairi “*Karamu ya Nzige*”(uk. 35) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Mwandishi anaangazia namna viongozi au wanasiasa wanafuja hazina ya taifa kwa sababu ya ubinafsi na tamaa. Katika shairi hili, “shamba la mawele” ni rasilimali za taifa, “nzige” ni wanasiasa na “sherehe” ni kitendo cha ufujaji wa hazina na rasilimali za taifa. Nzige ni wadudu waharibifu wanaokula majani ya mimea na kuacha mimea ikiwa imekauka. Kwa hivyo, viongozi wenye ubinafsi na tamaa wakivamia rasilimali za taifa, hakuna maendeleo yatakayopatikana katika nchi. Mwandishi anasema:

Kwa mvumo unaorindima
Mithili yowe la katadole
Katika shamba la mawele,
Sherehe ya nzige yaterema
Katika bonde la kijani ridhishi... (uk. 35)

Mshairi ameangazia suala la unafiki na tamaa katika siasa katika diwani ya *Bara Jingere*. Shairi “*Machozi ya Damu*” (uk.1) linafafanua namna wapigakura wanajuta kwa sababu ya kunyanyaswa na kukandamizwa na wanasiasa waliowachagua.

Wananchi wanajuta kwa kutumia vibaya haki yao ya kidemokrasia kuchagua viongozi ambao wanajigeuza miungu-wajeuri kwa maana ya kuwa na kiburi na kuwatesa. Kama Loomba (1998) anavyosema, wananchi hawa wanaodhulumiwa hawana mtu wa kuwatetea. Kwa hivyo, dhana ya masefule katika nadharia ya baadaukoloni yaani watu wachochole wasio na usemi wowote inajitokeza katika shairi hili la “*Machozi ya Damu*”. Wananchi wanadhulumiwa na viongozi waliowachagua. Maoni ya Loomba

(khj) yanawiana na Gandhi (1998) kwamba watu wa kawaida na maskini wanadhulumiwa na tabaka tawala.

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, mshairi anazidi kufafanua jinsi uongozi mbaya unazua misukosuko na ukabila. Mfano mzuri ni shairi “Nahodha na Jahazi” (uk. 5). Mwandishi anaonyesha vile viongozi wasiokuwa na maono na sera nzuri wanaongoza wananchi bila mwelekeo. Nahodha ni rais au kiongozi wa nchi anayeshikilia nafasi muhimu kuongoza taifa. Wasaidizi wa nahodha ni mawaziri wanaomsaidia kuongoza wizara mbalimbali na wabunge wanaounda sheria na kuidhinisha bajeti na miradi mbalimbali ya serikali. Jahazi ni nchi ambayo imebeba wananchi wanaoongozwa na rais. Kwa mujibu wa mwandishi, ikiwa rais atakuwa makini anapoongoza na asaidiwe na mawaziri na wabunge sawasawa basi nchi itakuwa imara bila misukosuko wala mizozo. Nchi ikiwa imara kutakuwa na maendeleo na maisha ya wananchi yatakuwa bora. Hata hivyo, katika shairi hili, kiongozi wa nchi na wasaidizi wake hawamakiniki na hivyo nchi inaangamia kwa sababu ya uongozi duni.

Unafiki na tamaa miongoni mwa wanasiasa inaonekana bayana katika shairi “Msimu wa Tisa” (uk. 9). Katika shairi hili, mwandishi anasema kuwa baada ya wabunge kula kiapo cha uaminifu kwa nchi wanavamia hazina ya taifa kwa tamaa bila kujali wananchi wenye njaa. Wanatimiza majukumu waliyopewa na wapigakura kwa mwendo wa polepole. Mshairi anasema:

Leo, Ukumbi wa ulumbi umejaa vumbi jeuri
Kimbunga cha ubinafsi, uzembe na kiburi
Kinavuma kama bahari inayoteta na tufani

Punde walipokula kiapo cha uaminifu kwa nchi
Bila kujali vinywa vinavyopiga miayo ya njaa
Walivamia ghala la taifa kwa tamaa inayovuma (uk. 9)

Katika dondoo hili, ukumbi wa ulumbi ni bunge ambapo wabunge wanakutana kujadili masuala muhimu ya kitaifa, kubuni sera na sheria za kuendesha nchi. Lakini badala watekeleze majukumu muhimu waliyopewa na wananchi, wabunge wanageuka kuwa wazembe, wenye kiburi, tamaa, majivuno na uwongo. Wanadai kutetea maslahi ya wanyonge lakini vitendo vyao vinaonyesha kinyume cha mambo. Wabunge hao wanapigania waongezwe marupurupu ya nyumba, ya kusafiri nchi za ughaibuni na mikopo ya kutimizia matakwa yao binafsi.

Maudhui ya unafiki wa kisiasa yanajitokeza pia katika shairi “Msimu Mwingine wa Wasaliti” (uk. 12). Katika shairi hili, wanasisia waliochaguliwa kuwakilisha na kutetea maslahi ya wananchi wanajifunisha kwa vyeo, ulinzi, mishahara na faida nyinginezo zinazoambatana na nyadhifa za waheshimiwa. Muda wao wa kuhudumu unapokaribia kuisha, wanarudi tena kwa wananchi waliowapigia kura kwa maneno matamu na ahadi za maendeleo zaidi hata baada ya kuwasaliti kwa kutotekeleza ahadi walizotoa mwanzo. Wananchi nao wakiongozwa na ubinafsi wanachagua viongozi wengine wasaliti. Mshairi anasema:

Vitimbakwiri watarudi karibuni kutoka karamu haramu
Utazona barakoa za tabasamu kwenye nyuzo zao
Watakuja kutugawia peremende zenye sumu ya akili
Watalewesha watu kwa pombe kutoka vibuyu vya maneno
Wataahidi kesho yenye mapipa ya maziwa na mitungi ya asali
Nasi, tukiongozwa na ramani ya tumbo na dira ya ubinafsi
Tutapanga milolongo katika mvua na matope ya Disemba
Kukaribisha, labda, msimu mwingine wa wasaliti (uk. 12)

Katika dondoo hili, “vitimbakwiri” ni wanasisia waliochaguliwa na wananchi. Peremende zenye sumu ya akili ni pesa au vitu vingine ambavyo wanasisia wanahonga wananchi kwavyo kama ishara ya kuwasaidia ili kuwapumbaza wawapigie kura tena. Aidha, wanatumia maneno matamu ya ushawishi na kuwaahidi maendeleo na maisha mazuri pindi wakiwachagua tena. Lakini kwa sababu wapigakura washapokea pesa, wanapanga milolongo kuchagua viongozi wengine watakaowasaliti kwa kutowaletea maendeleo yoyote kama viongozi wa awali. Kwa mujibu wa shairi hili, kusaliti wapigakura ni kutotekeleza ahadi walizotoa viongozi walipokuwa wanatafuta kura kutoka kwa wananchi.

3.2.2 Uongozi wa Kidikteta

Maudhui ya uongozi wa kidikteta yanajitokeza wazi katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Kwa mujibu wa TUKI (2013), dikteta ni mtu anayetawala nchi kwa amri yake peke yake bila ya kushauriwa. Aidha, ni mtu mwenye tabia ya kutaka lifanywe lile analosema bila ya kupingwa. Dhana ya nguvu na mamlaka katika nadharia ya baadaukoloni inabainika katika uongozi wa kidikteta. Viongozi wanaoshika hatamu za kuongoza nchi wanakuwa na nguvu na mamlaka ya kuongoza watakavyo. Atakalosema kiongozi lifanyike ndilo litakalofanyika. Wananchi wakipinga au kulalamika juu ya udikteta wanapigwa, kufungwa au hata kuangamizwa kupitia mipango madhubuti ya kisiri. Hali kama hii iliwahi kushuhudiwa Kenya katika enzi

za utawala wa chama kimoja. Fauka ya hayo, uongozi wa udikteta ulishuhudiwa au unashuhudiwa katika nchi ya Uganda, Zaire, Misri, Libya, Msumbiji, Zimbabwe, Burundi na Sudan Kusini.

Licha ya kuongoza kwa kutumia nguvu na mamlaka kupita kiasi, marais wengi hasa katika nchi za Afrika wanakataa kung'atuka mamlakani zamu zao zinapokwisha hata kama wananchi wanataka mabadiliko ya uongozi. Matokeo ya kukatalia uongozini ni machafuko, mauaji na mapinduzi ya serikali. Mambo kama haya ndiyo yanaonyesha usasa katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

Kuna mashairi kadha yanayoangazia maudhui ya uongozi wa kidikteta na dhuluma za kihistoria. Kwa mfano, katika diwani ya *Mchezo wa Karata* kuna mashairi kama: “Sisimizi Nijulisheni” (uk. 27), “Swali kwa Konokono” (uk. 33), “Swali kwa Yangeyange” (uk. 41), “Papa” (uk. 45) na “Mlipuko wa Furaha” (uk. 56). Aidha, katika diwani ya *Bara Jingine* kuna mashairi kama “Kikaoni Addis Ababa” (uk. 2), “Jumapili ya Damu” (uk. 6) na “Obasanjo” (uk. 17). Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, mashairi yanayogusia uongozi wa kidikteta ni “Mnara Mwangavu” (uk. 36) na “Msumbiji” (uk. 72).

Katika shairi “Sisimizi Nijulisheni” (uk. 27), mwandishi anadokeza kuwa kuna viongozi wanaoingia uongozini kisha wanaanza kuwa na njama mbovu, ulaghai, unafiki, ubaguzi, kiburi na vitisho. Anaongeza kuwa viongozi wanakuwa na uchoyo na ulafi. Mambo haya yanaonyesha matumizi mabaya ya nguvu na mamlaka na hivyo kudhihirisha sifa ya uongozi wa kidikteta. Mshairi anauliza:

Katika nasaba yenu
Wapo wapaa vileleni
Wakaloa
 Njama na ulaghai
 Unafiki na ubaguzi
 na
 Kiburi na vitisho
Au, maisha yenu
Si ya uchoyo unaonuka
Na ulafi usiokauka
Miongoni mwa viongozi? (uk. 27)

Mwandishi anashtumu tabia ya baadhi ya marais, ambao wakionja mamlaka na faida zitokanazo na wadhifa huo hawataki kung'atuka uongozini. Wanataka wakae mamlakani licha ya umri mpevu au katiba kutowaruhusu bila kuachia watu wengine

fursa ya kuongoza. Kwa mfano, katika shairi “Swali kwa Konokono” (uk. 33) katika diwani ya *Mchezo wa Karata* mshairi anauliza:

Konokono, ungliiga saruji
Na kugandama mamlakani
Bila kujali malalamiko,
Au ungeliongozwa na akili
Badala ya umio na tumbo
Na kushuka bila hasira
Na vitisho vikali
Vya gharika la damu? (uk. 33)

Katika shairi hili, mwandishi anauliza uhalali wa kiongozi kukwama kwenye uongozi hata kama anaowaongoza hawaridhiki na uongozi wake. Anashauri kuwa kiongozi mwadilifu anastahili kutumia akili na kuondoka uongozini bila kusababisha hasira na vitisho vikali vya umwagikaji wa damu kupitia mapinduzi.

Ujumbe wa utawala wa udikteta na madhara yake unapatikana katika shairi “Papa” (uk. 45) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Papa ni aina ya samaki mkubwa baharini anayeogopewa na samaki wadogo. Katika muktadha wa shairi hili, “papa” ni kiongozi yeyote anayetawala kwa nguvu na mamlaka. Kiongozi wa aina hii anahangaisha wananchi kupitia matumizi mabaya ya nguvu kupita kiasi. Mwandishi anasema:

Papa, mkali kama mauti
Anahangaisha samaki
Kwa ndaro na maringo
Daima akijigamba
Kwamba baharini
Haupo uwezo unaomtisha
Wala tisho linalomweza (uk. 45)

Mwandishi anaeleza kuwa watawaliwa wanapochoka na uongozi wa udikteta, wanajumuika pamoja na kuanza harakati za kuung’oa uongozi wa udikteta. Wananchi wanaanza mashambulizi makali dhidi ya kiongozi dhalimu mpaka wanamng’oa mamlakani. Ujumbe sawa na huu unaangaziwa na mwandishi katika shairi “Mlipuko wa Furaha” (uk. 56). Mwandishi anaonyesha namna simba anayeogopewa na wanyama wengine mbugani anatawala kwa kiburi na maringo. Kutokana na mpito wa wakati, wanyama wanapanga njama ya kumng’oa simba mamlakani. Mtunzi anasema:

Kutoka anga ‘tulivu’
Mawingu yalitanda
Kimya kikayeyuka
Mbingu zikatetemeka
Nguvu zisizozuilika
Zikamkabili simba
Na kumng’oa meno
Na kucha
Mbuga ikalipuka
Kwa furaha
Ya uhuru (uk. 57)

Ujumbe katika shairi hili unaonyesha kuwa kiongozi wa kidikteta hawezi kuendelea kukaa mamlakani. Siku moja watawaliwa wanapochoka kukandamizwa wanaungana pamoja na kumwondoa mamlakani kiongozi anayewadhulumu. Haya ni mapinduzi ya kutaka haki na uhuru.

Kwengineko, katika shairi “Jumapili ya Damu” (uk. 6), mwandishi anaonyesha jaribio la mapinduzi ya serikali ili kumng’oa mamlakani kiongozi dhalimu. Jaribio hilo halifaulu kwa sababu kiongozi huyo anatumia wanajeshi wenye bunduki, magari ya rangirangi, vifaru na mizinga hatari kudhibiti hali, kusudi abaki uongozini. Matokeo ya jaribio hili ni uharibifu wa mali na mauaji ya wananchi wasio na hatia. Mwandishi anasema:

Kwa tabasamu
Nakumbuka Obasanjo
Na uamuzi wake angavu
Bali pia
Kwa huzuni
Nakumbuka Bokassa na Amin,
Na Mobutu na Doe,
Na damu na mafuvu
Matita ya mafuvu (uk. 8)

Licha ya kukemea udikteta, mwandishi anaonyesha mfano mwema wa aliyekuwa rais wa Nigeria, Olusegun Obasanjo; namna kiongozi mwadilifu anafaa kuongoza na kung’atuka mamlakani punde tu hatamu yake inapoisha bila kungojea mapinduzi. Anashauri kuwa marais wengine wanastahili kuiga mfano wa kiongozi huyu. Katika diwani ya *Bara Jingine* katika shairi “Obasanjo” (uk. 17) mshairi anamsifu hivi:

Badala ya kushikilia kifyatulio
Kama onyo kali kwa wananchi
Uliinua mkono wa kwaheri

Na kwa hiari
Ukateremka bila ujanja
Kutoka kiti cha enzi (uk. 17)

Kwa mujibu wa mwandishi, Olusegun Obasanjo alikuwa rais wa Nigeria mwenye nguvu na mamlaka. Alikuwa na silaha hatari. Lakini licha ya hayo yote, wakati wake wa kuondoka uongozini ulipofika, hakuendelea kubaki mamlakani bali aliondoka kwa hiari. Kitendo chake kilikuwa mfano mzuri wa kuigwa kwani marais wengine barani Afrika wanapoingia uongozini hawaondoki kwa hiari mpaka wauawe au kufanyike mapinduzi na umwagikaji wa damu.

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa* katika shairi “Mnara Mwangavu” (uk. 36), mwandishi anaangazia namna Nelson Mandela alifungwa katika jela kuu ya Pretoria, akateseka kwa miaka ishirini na saba. Alipotoka jela, Nelson Mandela alipewa nafasi ya kuiongoza nchi ya Afrika Kusini. Aliongoza kwa miaka mitano bila ubaguzi wala kulipiza kisasi. Tofauti na marais wengine katika ikulu za Afrika, Mandela hakujawa na kiburi cha mamlaka. Mwandishi anamsifu:

Kinyume na majambazi wa ikulu
Badala ya kuwa shujaa wa ujanja
Na kugandama kwenye usukani
Uliinuka kitini kwa unyenyekevu
Kutoa nafasi kwa nahodha mpya (uk. 38)

Msisitizo wa mwandishi katika shairi hili ni kuwa rais mzuri huongoza na kuondoka uongozini kwa hiari na kutoa nafasi kwa kiongozi mwingine. Si vyema kukatalia uongozini kwa ujanja wala nguvu. Kiongozi mwovu hukatalia uongozini ili kuendeleza udikteta na dhuluma kwa watawaliwa.

3.2.3 Ukoloni Mkongwe na Ukoloni Mamboleo

Ukoloni mkongwe ni dhana inayorejelea namna mataifa ya Ulaya hasa Ujerumani, Ufaransa Ubelgiji, Ureno na Uingereza yaliingia katika bara la Afrika na kutawala mataifa ya Afrika. Rodney (2012) anafafanua namna mataifa haya yalichangia kudhulumu bara la Afrika hadi likadidimia kimaendeleo. Mataifa haya yaligawa bara la Afrika katika makoloni tofauti na kutumia lugha zao kuendeleza ukoloni katika nchi husika. Mataifa haya yalichukua mashamba ya Waafrika, yakadhibiti njia za uchumi, yakaharibu utamaduni na umoja wa Waafrika mbali na kuwafanya watumwa katika bara lao. Ung’ang’aniaji na ugawanyaji wa bara la Afrika ulionyesha wazi

namna mataifa hayo yalitumia nguvu na mamlaka yao kama kanuni mojawapo katika nadharia ya baadaukoloni kukandamiza na kuumbua Waafrika. Kwa mfano, nchi ya Kenya ilitawaliwa na Uingereza. Waingereza walipoingia nchini Kenya, walitwaa mashamba mazuri ya wenyeji, walitawala kwa sheria za kimabavu mbali na kudhibiti uchumi wa nchi. Aidha, walianzisha elimu ya kikoloni.

Utawala wa mkoloni Mwingereza ulikuwa na dhuluma nyingi. Kwa hivyo, Wakenya na Waafrika walipochoka na utawala dhalimu wa wabeberu, walianza harakati za kupigania uhuru na haki zao. Kulitokea mavuguvugu mengi yaliyopigania uhuru wa Wakenya na Waafrika kutoka kwa minyororo ya ubeberu. Kwa mfano, nchini Kenya, kulikuwa na vuguvugu la “Mzungu Aende Ulaya, Mwafrika Apate Uhuru” (MAUMAU). Baada ya kumwaga damu, nchi nyingi zilijipatia uhuru. Katika diwani ya *Mchezo wa Karata*, sehemu ya kwanza ya shairi “Mgunga Shambani” (uk. 20) inaangazia maudhui ya ukoloni mkongwe. Mshairi anasema:

I

Huko zama za nyuma
Kwenye shamba letu la mawele
Kulistawi gongo la mgunga
Ambalo kwa miiba yake myeupe
Lilituchoma michomo mikali

Tuliamua kulingo’ a
Kusudi kuyeyusha dhiki
Ambayo ilikifunika kijiji
Kama blanketi ya mipupu... (uk. 20)

Katika shairi hili, “mgunga” ni sitiari ya mkoloni ilhali “shamba la mawele” ni nchi iliyotawaliwa. “Miiba” ni dhuluma walizotendewa watawaliwa. Mshairi anaeleza vile Wazungu waliingia nchini Kenya “wakatawala kwa hila, nguvu na unyanyasaji mwingi”. Baada ya mateso mengi, Wakenya waliamua kumwondoa mkoloni kwa “kutingisha mgunga shambani” ili wajitawale wenyewe. Hatimaye, walifaulu kumtimua mkoloni na wakasherehekea uhuru walioupata. Mwandishi anasema, “Hatimaye, tuliusikia mshindo tukadhani mwisho wa mashaka ulikuwa umefika shambani. Tukasherehekea kwa shangwe...” (uk. 20). Lakini uhuru waliodhani wameupata ulikuwa wa bendera tu.

Kwengineko, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, mshairi anafafanua tena maudhui ya ukoloni mkongwe. Kithaka wa Mberia anaeleza vile Waarabu, Wakristo na hatimaye

Wazungu walivyokuja katika eneo la Afrika Mashariki katika shairi “Zimwi la Theluji” (uk. 48). Mwandishi anasema katika sehemu ya pili ya shairi hili:

Kwa kunyemelea
Lilikuja zimwi jeupe
Kwanza kwenye upwa
Ambapo upepo
Hupuliza manukato ya chumvi...(uk. 49)

Mshairi anatumia sitiari “zimwi jeupe” kurejelea Waarabu waliokuja pwani ya Afrika Mashariki kuanzia karne ya kumi. Kuna wale waliokuja kutalii na wengine walikuja kwa ajili ya kufanya biashara ya pembe za ndovu na kutafuta watumwa waliopeleka nchi za ng’ambo kama vile Ulaya na Amerika kufanya kazi za sulubu. Biashara iliposhamiri, utawala wa Waarabu uliingia bara ya Afrika Mashariki polepole hadi nchi ya Kongo kule Afrika ya Kati.

Wageni waliofuata Waarabu ni wamishenari waliokuja kwa nia ya kueneza dini ya Kikristo. Katika sehemu ya nne ya shairi “Zimwi la Theluji” (uk. 48) mshairi anaeleza:

Lilikuja zimwi la theluji
Likibeba simulizi
Mkururo wa vituko vya ajabu...
Katika kitabu maalumu
Lilijidai kuwa tarishi
Wa muumba wa yote
Likakunjua hadithi
Ya Baba na Mwana... (kur. 51-52)

Katika shairi hili, mwandishi anaeleza shughuli zote walizotekeleza wamishenari. Walihubiria watu waache dhambi na waokoke. Kwa mujibu wa mshairi, wamishenari kwa ujanja “Waliapa kuwahamisha wenyeji kutoka kichocho kichafu cha giza waingie kwenye bustani” (uk. 53). Baada ya miaka mingi ya kueneza Ukristo, mkoloni alipata nafasi ya kuingia bara la Afrika. Mwandishi anaeleza:

Zimwi la theluji
Lilipokaza fundo
Kwa mikono imara
Lilichukua mitungi
Likavamia kiwele
Na kwa tamaa iliyokithiri
Kuanza kukamua maziwa
Na akiwa amechangamka

Kuyapakia katika vyombo
Kuyasafirisha
Hadi ng'ambo (uk. 55)

Katika dondoo hili, mwandishi anaangazia maudhui ya ukoloni mkongwe. Mkoloni ambaye ndiye “zimwi la theluji” alidhibiti rasilimali na njia kuu za uchumi wa nchi za Afrika. Huko ndiko “kuchukua mitungi na kuvamia kiwele na kuanza kukamua maziwa”. Kwa hivyo, mkoloni alichukua malighafi na bidhaa nyingine na kuzipakia katika ndege na meli na kuzisafirisha hadi nchi zao. Kwa mujibu wa Rodney (2012), hivi ndivyo mkoloni alichangia Afrika kubaki nyuma kimaendeleo.

Mbali na kuangazia suala la ukoloni mkongwe, Kithaka wa Mberia anashughulikia suala la ukoloni mamboleo. Ukoloni mamboleo ni hali ambapo nchi zilizotawaliwa na wakoloni zingali zinatawaliwa kwa mlango wa nyuma kupitia mashirika ya kimataifa, mikataba ya biashara na kasumba za ukoloni. Fauka ya hayo, mataifa huru yanatumia sera, katiba na mawazo ya kigeni kuendesha serikali zao. Katika ukoloni mamboleo, sifa za ukoloni mkongwe kama vile ukandamizwaji, udikteta na ukosefu wa haki hudhahirika. Kanuni moja ya nadharia ya baadaukoloni ni kuchunguza urithi wa matumizi ya nguvu za kikatili na athari za utawala wa Ulaya kwa wakaazi wa bara la Afrika. Kwa hivyo, katika ukoloni mamboleo, viongozi walioshika hatamu katika mataifa yao huwa wamegeuza tu rangi ya watawala bali hao viongozi huwa wamerithi tabia za wakoloni.

Kithaka wa Mberia anaangazia ukoloni mamboleo katika diwani ya *Mchezo wa Karata* katika sehemu ya tatu ya shairi “Mgunga Shambani” (uk. 20). Anasema:

III
Pale tulipong'oa mgunga
Palistawi mti mwingine
Michomo ikatuliza machozi
Mithili zama za nyuma

Watu wakashangaa:
Imekuwaje mti mzuri
Ambao umesimama pahali pa mgunga
Kurithi yake michomo!

Ndipo sauti za washairi
Zilipoibuka na kuimba
Mara nyingine, migunga

Huigiza kuanguka
Bali hubaki imara
Ikistawi shambani
Kwa sura tofauti (uk. 21)

Dondoo hili linabainisha wazi ukoloni mamboleo. Viongozi walioshika hatamu za uongozi baada ya mkoloni kuondoka walianza kuiga na kuongoza kwa kutumia njia, katiba na mawazo sawa na mkoloni mwenyewe. Kwa hivyo, watawaliwa wanaona kuwa hakuna tofauti na utawala wa ukoloni mkongwe kwa sababu wanadhulumiwa kwa njia nyingi. Viongozi hao wapya walirithi ile “michomo” ya mkoloni. Wanakuwa madikteta wanaotumia nguvu na mamlaka kutwaa mali na kunyanyasa watawaliwa sawa na wakoloni walivyofanya miaka ya nyuma walipokuwa wanatawala Afrika. Huu ndio ukoloni mamboleo ambao unaonekana katika mataifa yanayoendelea hasa ya Kiafrika yenye misukosuko ya kisiasa. Masuala haya ndiyo yanaonyesha vile historia inamchochea mshairi kutunga mashairi yake na kuyaoanisha na wakati wa sasa. Hali hizi zinaonyesha usasa unaopatikana katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

Kuna dhana ya ujitambuzinafsi katika nadharia ya baadaukoloni. Viongozi walioshika nyadhifa za uongozi baada ya ukoloni wanastahili kujisaka na kurejesha utu ulioubuliwa na mkoloni. Warejeshe imani kwa watawaliwa kuwa Mwafrika ana utu na utamaduni wake na kwamba anaweza kujiamulia mambo yake chini ya utawala mpya. Hata hivyo, kwa sababu ya kuendeleza ukoloni mamboleo, ni wazi kuwa viongozi hawa hawajajikomboa kimawazo na kasumba za ukoloni mkongwe. Nchi za Kiafrika zingali zinategemea nchi zilizostawi au nchi zilizozitawala kwa misaada na mikopo. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* katika shairi “Mlima wa Dhahabu” (uk. 23) mwandishi anasema:

Tulishindwa kujipamba kutoka maduka
Kuvaa mitumba kukawa mtindo kuu wa taifa
Nchi ikageuka kapu la kutupa mavazi makuukuu
Tukawa warithi wa jasho la nchi nyingine (uk. 24)

Katika shairi hili, mwandishi anaonyesha wazi kuwa watu wa taifa husika wanashindwa kujinunulia nguo zilizotengenezwa katika viwanda vyao na kuuzwa katika maduka yao. Badala yake, wanavaa nguo za mitumba ambazo zimeshawaliwa na watu wa nchi zingine. Kitendo hicho kinaonyesha vile taifa huru husika bado linategemea mavazi ya bei ya chini ambayo yashatumika kutoka mataifa yaliyostawi.

Baada ya kupata uhuru, Waafrika walianza kuunda jamii mpya. Walifanya juhudi kuondoa fikira, dhana na uharibifu uliofanywa na wakoloni. Waliingia mashambani kuimarisha kilimo. Lakini ujanja wa kutawaliwa na wakoloni kisiri kwa mlango wa nyuma unaonekana. Malighafi na bidhaa nyingine muhimu zinasafirishwa kwa ndege za mizigo hadi ng'ambo kwa misingi ya biashara nafuu kwa manufaa ya Wazungu. Huu ni mfano mzuri wa ukoloni mamboleo uliopo sasa. Mshairi anasema katika shairi “Zimwi la Theluji” (uk. 48) sehemu ya tisa hivi:

Katika uwanja wa lami
Karibu na ndege ya mizigo
Naona mitungi ya maziwa
Ikingojea kupakiwa chomboni
Na kubebwa hadi ng'ambo
Kulisha jamaa za zimwi la theluji
Na kuacha wanakijiji wafugaji
Kwenye mabindo ya chatu wa njaa (uk. 60)

3.2.4 Changamoto za Mataifa ya Afrika

Kithaka wa Mberia anachanganua masuala mengi yanayojitokeza katika mataifa mengi ya Kiafrika yanapoendelea kujitawala baada ya kupata uhuru. Mataifa mengi yalikuwa na matumaini ya kujiongoza vizuri kuliko utawala wa wakoloni. Lakini matumaini na matarajio hayo yamegeuka kuwa mazigazi baada ya miongo kadha ya kujitawala baada ya ukoloni mkongwe. Masuala haya ndiyo ambayo Kithaka wa Mberia anashughulikia pia katika diwani zake.

Katika baadhi ya mashairi, Kithaka na Mberia amefafanua maudhui ya mapigano, vita vya kikabila na mizozo katika mataifa ya Afrika kama vile Sudan Kusini, Somalia, Kongo, Angola, Zimbabwe, Rwanda, Burundi na Msumbiji. Kwa mfano, mashairi “Darfur” (uk. 26), “Petali za Amani?” (uk. 29) na “Mafuta yenye Damu” (uk. 49) katika diwani ya *Msimu wa Tisa* yanamulika mizozo na misukosuko ya kisiasa katika nchi ya Sudan Kusini. Mapigano yanayoshuhudiwa yanatokana na siasa za mirengo tofauti, makundi yenye itikadi kali na ung'ang'aniaji wa rasilimali kama vile mafuta. Matokeo ya mapigano haya ni vifo vya halaiki ya watu, ubakaji wa kina mama na wasichana, watoto kuachwa mayatima, ukosefu wa amani, uharibifu wa mali na watu kuwa wakimbizi katika nchi jirani.

Wakimbizi ambao wanatafuta hifadhi wanakuwa mzigo mkubwa kwa mashirika kama Umoja wa Mataifa yanapotoa misaada kwa wakimbizi hao. Mashairi “Mkimbizi” (uk.

58) na “Kakuma” (uk. 66) katika diwani ya *Msimu wa Tisa* yanabainisha shida za wakimbizi kama vile wasiwasi wa waliko jamaa na marafiki, mazingira duni ya afya katika kambi, baridi wakati wa usiku, joto kali wakati wa mchana, ubakaji wa wanawake, ukosefu wa elimu bora kwa watoto na ukahaba kambini unaochangia kusambaa kwa magonjwa ya zinaa miongoni mwa wakimbizi.

Licha ya hayo, mataifa ya Afrika yanakumbwa na shida ya njaa kama mshairi anavyodokeza katika shairi “Minyororo ya Njaa” (uk. 1) katika diwani ya *Msimu wa Tisa*. Ingawa Kenya na mataifa mengine ya Kiafrika yana ardhi nzuri yenye rutuba ya kustawisha kilimo, serikali hazijaweka mikakati mwafaka ya kutumia teknolojia ya kilimo kupitia unyunyuziaji maji mashamba ili kuongeza mazao na kupunguza njaa. Jambo hili ndilo linalomfanya mshairi kusema kuwa mataifa haya ni kama yako usingizini katika shairi “Usingizini” (uk. 3) katika diwani ya *Msimu wa Tisa*. Kwa hivyo, mataifa haya yanakumbwa daima na visa vya njaa na kuomba misaada ya chakula kutoka mataifa yaliyostawi. Watoto na wakongwe wanakufa kwa sababu ya njaa. Katika diwani ya *Msimu wa Tisa* katika shairi “Minyororo ya Njaa” (uk. 1) mwandishi anasema:

Kurasa za magazeti na viwambo vya runinga
Vinaonyesha tena picha zinazoshtua hisia:
Watoto waliomumunywa na kinywa cha njaa
Wakabakia na macho yanayodondoka dhiki
Na vipande vya mianzi mikavu badala ya miguu (uk.1)

Mtunzi anasawiri picha ya watoto walioathiriwa na njaa. Kwa hivyo, tatizo la njaa lipo na ni suala linastahili kushughulikiwa na serikali za mataifa ya Afrika.

Isitoshe, bara la Afrika linakabiliwa na shida ya magonjwa mbalimbali. Ingawa magonjwa hayapo Afrika tu, ukweli ni kwamba shida ya umaskini mwingi barani Afrika huchangia kuwepo kwa magonjwa ya kila aina. Miongoni mwa magonjwa yanayosumbua bara la Afrika ni ugonjwa wa ukimwi. Wazazi au walezi wa watoto wanapokufa kwa sababu ya ukimwi, wanaacha watoto mayatima ambao hawaendi shule na wanalea watoto wadogo waliochwa na wazazi au walezi. Kifo cha wazazi huwa pigo kwa taifa kwa sababu hakuna nguvukazi ya kuchangia maendeleo ya taifa. Aidha, watu walioambukizwa ukimwi wanahitaji msaada wa dawa za kupunguza makali ya ukimwi pamoja na vyakula vya kuimarisha kinga ya mwili.

Mataifa haya yanategemea ufadhili wa pesa na dawa kutoka nchi zilizostawi. Hili ni tatizo kubwa. Mashairi “Msimu wa Kaburi” (uk. 3) na “Mgeni Katili” (uk. 4) katika diwani ya *Redio na Mwezi* yanaangazia ugonjwa wa ukimwi. Kwa upande mwingine, shairi “Miche Pweke I” (uk. 54) na “Miche Pweke II” (uk. 55) katika diwani ya *Msimu wa Tisa* yanazungumzia shida za watoto mayatima walioachwa na wazazi baada ya kufa kutokana na ukimwi. Watoto hao wanakosa elimu, mapenzi ya wazazi, malezi mazuri na wanafanya kazi ngumu ili kujikimu kimaisha ilhali wasichana wanajiingiza katika ukahaba.

Kithaka wa Mberia anamulika vilevile suala la elimu na ukosefu wa elimu katika mataifa ya Afrika. Baadhi ya maazimio serikali ya Kenya ilinulia kuangazia punde tu baada ya kupata uhuru ni kupigana na magonjwa, umaskini na kutojua kusoma na kuandika. Hata hivyo, Kenya na mataifa mengine ya Kiafrika hayajatoa elimu ya msingi kwa watu wote kwa sababu ya umaskini. Kwa hivyo, tatizo la kutojua kusoma na kuandika miongoni mwa watu wengi lingalipo. Kwa mfano, katika shairi “Pamela” (uk. 29) na “Flora na Wenzake” (uk. 33) wasichana wa shule wanapata mimba kutoka kwa wavulana wanaosoma pamoja nao au hata walimu kisha wanaacha shule ili kulea watoto. Jambo hili linachangia kutojua kusoma na kuandika. Isitoshe, katika diwani ya *Rangi ya Anga* katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) mwandishi anaonyesha tamaduni zilizopitwa na wakati ambazo zinachangia wasichana wa shule kutopata elimu sawa na wavulana. Tamaduni zenyewe ni pamoja na wasichana kuozwa mapema kwa wazee matajiri na ukeketaji wa wasichana. Mambo haya huwanyima haki yao ya kusoma ili kupunguza idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika.

Changamoto nyingine inayokumba mataifa ya Afrika ni uharibifu wa mazingira. Mazingira ni sehemu muhimu ya maisha ya mwanadamu kwa vile husaidia kuzalisha chakula, husaidia kutoa hewa safi, kupunguza visa vya magonjwa mbali na kuwa mandhari ya kuvutia. Watu wanakata miti na kuchangia mmomonyoko wa udongo na kiangazi. Isitoshe, wanachafua maji ya mito, mabwawa na maziwa. Maji yakichafuliwa yanachangia magonjwa ya tumbo kama vile homa ya matumbo na ugonjwa wa ngozi. Aidha, hewa inapochafuliwa, watu wanapata magonjwa ya kupumua. Baadhi ya mashairi yanayogusia uharibifu wa mazingira katika diwani ya *Bara Jingine* ni “Jinamizi” (uk. 55), “Ngao” (uk. 59), “Mimi, Mto Nairobi” (uk. 63), “Mikoma” na “Bwawa la Ithanje” (uk. 69). Katika diwani ya *Redio na Mwezi* kuna

shairi “Kiwanda” (uk. 6). Katika diwani ya *Rangi ya Anga* katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) kuna uharibifu wa mazingira kupitia ukataji miti na mbinu mbaya za kilimo.

Changamoto na shida zote zilizoangaziwa hapo juu zinaonekana bayana katika mataifa ya Afrika baada ya ukoloni. Kwa hivyo, nadharia ya baadukoloni imekuwa kurunzi mwafaka inayosaidia kumulika na kuchanganua matatizo yanayokumba mataifa ya Afrika baada ya kujipatia uhuru. Tumechanganua na kuonyesha namna yanaoana kiwakati na hivyo kuafiki usasa katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

3.2.5 Ujenzi wa Jamii Mpya

Mataifa mengi ya Afrika yalikuwa na ndoto, matumaini na matarajio mengi baada ya kujipatia uhuru. Lakini mizozo ya uongozi, udikteta, ufiisadi, mapigano, umaskini, magonjwa na njaa miongoni mwa matatizo mengine yanazidi kuandama mataifa haya. Hata hivyo, mshairi ana matumaini kwamba licha ya changamoto hizi, kuna uwezekano na matumaini ya kuunda jamii mpya ambapo wananchi watafurahia maisha mazuri siku za usoni.

Katika shairi “Hatutaaga Ndoto” (uk. 4) katika diwani ya *Bara Jingine*, mwandishi anazungumzia juu ya shida ya umaskini, viongozi wanaokataa kung’atuka mamlakani, ufiisadi na kutojua kusoma na kuandika kama baadhi ya masuala yanayokumba bara la Afrika. Hata hivyo, licha ya changamoto hizi mtunzi anaonyesha matumaini kuwa siku moja shida hizi hazitakuwepo. Mwandishi anasema:

Bali
Sisi, watoto wa Afrika
Tumekataa kuaga ndoto
Ewe ndoto ya dhahabu
Ndoto ya kesho
Kesho ambapo
Mamba wanaoota jua
Juu ya mazulia mekundu
Watakuwa hadithi...
Kesho ambapo
Watoto watatembea vijijini
Bila kutafunwa njiani
Na ukambi au kifaduro
Kesho ambapo
Watoto watakweza akili

Bila kuvutwa chini na ufukara
Kesho ambapo
Teknolojia ya kilimo
Itabusu mashamba
Yazae kiazzi – kikuu
Kikubwa kuliko Afrika... (kur. 4-5)

Katika dondoo hili, mwandishi ana matumaini yaani kutoaga ndoto kuwa kuna siku za usoni ambapo viongozi wanaodhulumu wananchi na kukatalia uongozini hawatakuwepo. Aidha, anaamini kuwa watoto hawatasumbuliwa na magonjwa kama ukambi au kifaduro. Watoto watasoma hadi viwango vya juu bila shida ya umaskini. Isitoshe, kuna nyakati teknolojia ya kilimo itasaidia kukuza chakula ili nchi za Afrika zikome kuomba misaada ya chakula kutoka mataifa yaliyostawi.

Ujumbe wa ujenzi wa jamii mpya unapatikana pia katika shairi “Bara Jingere” (uk. 10). Shairi hili linazungumzia juu ya matumaini ya kuunda bara jipya. Mwandishi anasema kuwa bara jipya litakuwa huru kutokana na mambo mengi. Katika bara jipya, bunge halitakuwa na wabunge walafi wala polisi na jeshi kulinda marais na viongozi wengine wakuu serikalini pekee. Anazidi kuona bara ambapo vizuizi na jela hazitakuwa za kuumbua utu wala za kusababisha vifo; bara jipya ambapo ulafi na ufisadi hautakuwepo. Afrika mpya ambayo mataifa kwa mataifa hayatazozana, utafiti wa teknolojia utakuwa wa juu na watu kufurahia ngozi nyeusi ya Uafrika.

Kwengineko, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, mwandishi anaangazia ujenzi wa Sudan Kusini mpya katika shairi “Majira ya Ujenzi” (uk.49). Baada ya miongo mingi ya mapigano yaliyosababisha umwagikaji wa damu na uharibifu wa mali, ni wakati wa kuijenga upya nchi hiyo. Wakaazi na viongozi watumie rasilimali ya mafuta nchini humo ili kustawisha kilimo, afya, elimu, viwanda na sekta ya uchukuzi. Ikiwa viongozi hawataendeleza ufisadi na ukabila basi nchi hii itazalisha shibe ya kutosha. Mwandishi anasema:

Haya ni majira ya kuokota vigae
Ambavyo vimetapakaa ardhini
Na katika nyoyo na akili za wakaazi,
Huu ni wakati wa kuongea na chuma na mawe
Na kushirikiana na kokoto na saruji
Katika kukarabati nyufa za ndoto
Na kujenga kuta imara za maisha (uk. 49)

Msimamo wa mshairi ni kuwa umefika wakati wa serikali na wananchi wa Sudan Kusini kuanza kujenga nchi yao baada ya mapigano ya miaka mingi.

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, Kithaka wa Mberia ana matumaini ya Afrika mpya anapoonyesha namna mataifa ya Afrika yameungana pamoja kwa nia ya kupata maendeleo na kusuluhisha changamoto za Afrika. Ujumbe huu unapatikana katika shairi “Muungano wa Afrika” (uk. 90). Mwandishi anasema:

Tumezaa,
tukate kiunga mwana kwa makini
Tumlee,
tumtunze kwa mikono mikunjufu
Tumlishe... (uk. 90)

Katika dondoo hili, mtunzi anarejelea muungano wa Afrika kuwa ndiye mwana aliyezaliwa. Muungano huu wa nchi za Afrika unastahili kulelewa vizuri, kulindwa na kujengwa ili usaidie kutatua shida na unyonge wa bara la Afrika. Mataifa ya Afrika yakiwa yameungana yatashughulikia masuala ya umaskini, njaa, elimu, afya, utamaduni wa Mwafrika miongoni mwa masuala mengine mengi.

3.3 Mtindo Katika Siasa, Utawala na Mamlaka Katika Mataifa ya Afrika

Katika sehemu hii tumechunguza mtindo kama kiungo muhimu kinachomwezesha mshairi kuzungumzia maudhui juu ya siasa, utawala na mamlaka katika diwani zake. Katika kuchanganua mtindo alioutumia mwandishi, nadharia ya elimu mtindo mkabala wa uhakiki mpya imetuongoza katika kuchanganua na kuhakiki ufaafu wa vipengele anuwai vya kimtindo alivyovitumia. Baadhi ya vipengele vya mtindo tumeangazia hapa ni: sitiari, tashibihi, tashihisi, maswali ya balagha, matumizi ya wimbo, usimulizi, na msamiati teule.

3.3.1 Sitiari

Sitiari ni tamathali ya usemi ya ulinganishi usiotumia vilinganishi ‘kama’, ‘mithili’, ‘mfano wa’ miongoni mwa vingine (Wamitila 2008). Katika sitiari, kuna dhana tatu kuu: kilinganishi, kilinganishwa na msingi. Kilinganishi ni kile kinachotumiwa kama kiini cha kufananisha ilhali kilinganishwa ni kile kinachofananishwa. Kwa upande mwingine, msingi ni ile sifa yenyewe ya ulinganishi. Kuna sitiari za aina nyingi kama vile sitiari sahili, sitiari changamano, sitiari ambatani, sitiari fiche, sitiari kuu, sitiari

ya kikaida na sitiari pana. Sitiari inapotumika inaleta uhamisho wa maana pamoja na kujenga picha fulani katika akili ya msikilizaji au msomaji.

Mshairi ametumia sitiari nyingi katika ushairi wake ambazo zinarejelea wanasiasa na siasa potofu. Kwa mfano, akizungumzia juu ya unafiki na tamaa katika siasa, mwandishi anatumia sitiari “**mazimwi**” katika shairi “Mchezo wa Karata” (uk. 18) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Maana ya kawaida ya “zimwi” ni kiumbe kinachodhaniwa kuwa kinaishi, chenye uwezo wa kujibadilisha katika hali mbalimbali, kinachoogopesha na kinaishi katika misitu mikubwa. Kuna hadithi nyingi zinazohusu mazimwi katika fasihi simulizi za jamii za Kiafrika. Mwandishi analinganisha wanasiasa au viongozi na mazimwi. Wanasiasa au viongozi ni mazimwi kwa sababu wanatumia hila na ujanja wanapoongoza wananchi. Ujanja huo ambao unawanufaisha unasababisha wananchi kuumia kiuchumi, kisiasa na kimaendeleo. Wakati wa kampeni, wanasiasa wanatumia maneno matamu kushawishi wapigakura kuwa watakuwa waadilifu, wanaojali maslahi ya wanyonge na kuhudumia watu wote kwa hali na mali ili kuwe na maendeleo. Lakini pindi wanapochaguliwa na kula kiapo cha kutumikia wananchi, wanasahau ahadi walizotoa kwa wapigakura. Kwa hivyo, wanakuwa wamebadilisha sura zao za awali kabla ya uchaguzi na kuanza kuhepa wananchi. Wanaonyesha ubinafsi kwa kusahau wanyonge. Huku ni kudhuru maisha ya watu wa kawaida waliowapigia kura.

Vilevile, mshairi ametumia neno “**nzige**” kisitiari kuonyesha ulafi wa wanasiasa kwenye shairi “Karamu ya Nzige” (uk. 35) katika *Mchezo wa Karata*. Kawaida, nzige ni wadudu wanaokaa katika makundi makubwa. Wanapenda kula majani ya mimea bila kubakisha hata jani moja kwenye miti. Kithaka wa Mberia analinganisha wanasiasa hasa wabunge na nzige kwa maana kuwa wana tamaa ya ulafi. Wanafuja pesa kwa kujiongezea mishahara na marupurupu mengine mbali na kutumia pesa za maeneo bunge isivyostahili. Hiyo ndiyo maana ya “karamu ya nzige” kwa mujibu wa mshairi. Hawafikirii umma unaoteseka kwa sababu ya umaskini na njaa. Wanavamia hazina ya taifa na kufuja pesa kwa faida zao, familia na jamaa zao wa karibu. Wanasiasa hawa wanapoharibu pesa zilizotengewa maendeleo basi hakuna maendeleo yoyote yanayotarajiwa katika jamii au nchi kwa jumla. Kwa hivyo, sitiari ya nzige inaonyesha picha ya ulafi wa wanasiasa mithili ya nzige wanaovamia mimea na miti wasibakishe chochote.

Mwandishi ametumia sitiari katika shairi “Nahodha na Jahazi” (uk. 5) katika diwani ya *Msimu wa Tisa*. Mshairi, akizungumzia juu ya uongozi mbaya analinganisha rais wa nchi na **nahodha** anayeendesha jahazi baharini. **Jahazi** ni nchi inayobeba wananchi anaowaongoza kama kiongozi wa nchi. Mtunzi anafafanua kuwa kiongozi au rais wa nchi asipomakinika akisaidiwa na mawaziri na wabunge, siasa inachukua mkondo usioridhisha na hivyo nchi inayumbayumba kisiasa na kiuchumi. Ujumbe wa **nahodha** na **jahazi** unapatikana pia katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) ya Ebrahim Hussein.

Kwengineko, mshairi anatumia sitiari ya “**dau**” kuonyesha namna nchi haipigi hatua zozote za kimaendeleo kutokana na uongozi na utawala mbaya katika shairi “Dau Haliendi!” (uk. 32) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Dau ni chombo cha kusafiria baharini au kwenye ziwa. Mwandishi analinganisha nchi na dau ambalo linasafirisha watu na mizigo. Nchi inabeba wananchi sawa na dau linavyobeba abiria na mizigo. Nchi inapokuwa na viongozi waadilifu na wenye maono inapiga hatua kubwa kimaendeleo. Vinginevyo, nchi inabaki katika mzunguko tu licha ya miaka mingi ya kuchagua viongozi msimu baada ya msimu. Ili kuchimuza maudhui yake vizuri, Kithaka wa Mberia ameliumba shairi “Dau Haliendi!” kwa maneno likachukua umbo la dau lenyewe ili iwe rahisi kuunda taswira ya nchi iliyo sawa na dau. Mtindo huu wa shairi-picha ndio unaupa ushairi wa Kithaka wa Mberia upekee na usasa wa msanii huyu. Isitoshe, picha hii inaonyesha bayana uhusiano wa mtindo na maudhui anayozungumzia. Fauka ya hayo, mtindo huu wa kutumia mashairi picha unaonyesha kuwa mtindo ni ukiushi wa kaida za utunzi wa mashairi.

Mshairi anapogusia maudhui ya ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo, anatumia sitiari ya “**mgunga**” na “**shamba**” katika shairi “Mgunga Shambani” (uk. 20) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Mgunga ni mti wa kiasili unaostawi katika sehemu kame na zile zenye rutuba na una miiba myeupe. Haukauki kwa urahisi. Kwa upande mwingine, shamba ni sitiari ya nchi iliyotawaliwa na mkoloni. Mwandishi analinganisha mkoloni na “mgunga” na “shamba” kwa maana ya nchi iliyotawaliwa na mkoloni. Wakoloni walipoingia nchini Kenya, walitawala kwa miaka kadha. Walitawala kwa mabavu na wakanyanyasa wananchi kwa kunyakua mashamba yao mazuri yenye rutuba, wakawafanyisha kazi ngumu mashambani na viwandani,

wakaishi kwenye ufukara, wakadhibiti uhuru wao wa kutembea na wakapeleka wanaume wengine wenye nguvu kuwa watumwa katika nchi za ng'ambo. Udhalimu huo waliotendewa na wakoloni ndiyo michomo iliyoliza wananchi.

Baada ya kupigania uhuru, Kenya ilijikomboa na wananchi wakasherehekea uhuru kwa kumng'oa mkoloni. Viongozi wapya Waafrika wakashika hatamu za uongozi. Baada ya muda, wananchi walishindwa kuona tofauti kati ya uongozi wa mkoloni na uongozi mpya kwa sababu njama, dhuluma na hila za ukoloni mkongwe bado zinajitokeza katika uongozi mpya. Viongozi Waafrika wana sura za kibeberu katika kuongoza nchi zao ambazo ndizo mashamba. Unyanyasaji, ufidadi, ulafi na dhuluma nyingine zinaonekana katika uongozi wa sasa na hivyo basi kuibua dhana ya ukoloni mamboleo. Kwa hivyo, viongozi Waafrika bado ni sitiari ya “**mgunga**” na nchi yenyewe ni sitiari ya “**shamba**” kunakoendelezwa ukoloni mamboleo.

Kithaka wa Mberia anatumia sitiari ya “**mgeni**” katika shairi “Mgeni Katili” (uk. 4) katika *Radio na Mwezi* kueleza juu ya ugonjwa wa ukimwi. Aidha, mwandishi anatumia sitiari ya “**miche**” katika shairi “Miche Pweke I” (uk. 54) na “Miche Pweke II” (uk. 55) katika diwani ya *Msimu wa Tisa* kwa maana ya watoto mayatima walioachwa na wazazi na walezi waliokufa kutokana na ugonjwa wa ukimwi. Mshairi anauona ugonjwa wa ukimwi kuwa “**ugonjwa mgeni**” ulioingia Kenya na kwingineko Afrika. Ni ugonjwa mgeni unaosambaa kwa haraka hasa kupitia watu kushiriki mapenzi kiholela bila kinga. Ugonjwa wa ukimwi unaua watu wengi kila mwaka na kuacha watoto wengi (miche) wakiwa mayatima.

Watoto mayatima wanalinganishwa na miche kwa sababu ni wachanga ambao bado wanahitaji kulindwa na kutunzwa kiasia, kielimu na kupewa mapenzi na ulinzi ili wawe watu wazima wa kujitegemea. Mataifa mengi ya Kiafrika Kenya ikiwemo yameathirika sana kutokana na uwezo wao wa kiuchumi wa kutojimudu kudhibiti usambaaaji na athari za ugonjwa huu. Kenya na mataifa mengine yanategemea ufadhili kutoka nchi za ng'ambo kupunguza maambukizi mapya kwa kuhamasisha watu na kutoa dawa za kupunguza makali kwa walioambukizwa.

Mwandishi anatumia pia sitiari kadha anapoangazia maudhui kuhusu uongozi wa kidikteta. Kwa mfano, katika shairi “Papa” (uk. 45) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*, mshairi anatumia neno “**papa**” kurejelea kiongozi yeyote anayetawala

kimabavu. Kawaida, papa ni aina ya samaki mkubwa anayeishi baharini na huogopwa na samaki wadogo. Fauka ya hayo, katika shairi “Mlipuko wa Furaha” (uk. 56) katika diwani hii ya *Mchezo wa Karata*, mwandishi anatumia sitiari ya “**simba**” kurejelea kiongozi mwenye mamlaka anayewadhulumu watu kwa muda. Vilevile, neno “**mbuga**” ni sitiari ya nchi inayotawaliwa na simba. Utawala wa simba unapowaudhi wanyama (wananchi) wengine mbugani, wanyama hao wanakuwa na nguvu za kumkabili simba (kiongozi) na kumng’oa meno na kucha yaani uwezo na nguvu na kupata ushindi.

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa* katika shairi “Mnara Mwangavu” (uk. 36) mwandishi anaeleza juu ya uongozi wa aliyekuwa rais wa Afrika Kusini, Nelson Mandela. “**Mnara Mwangavu**” ni sitiari inayomaanisha Nelson Mandela. Anaeleza vile alivyoongoza nchi ya Afrika Kusini kwa miaka mitano. Hatamu yake ilipokamilika, “aliinuka kutoka kitini” na kutoa nafasi kwa “**nahodha**” mpya. Neno nahodha ni sitiari ya rais au kiongozi mpya aliyechukua nafasi ya Nelson Mandela. Aidha, mtunzi anasema kuwa “kinyume na majambazi wa ikulu”, Nelson Mandela hakukataa kuondoka uongozini. Maneno “**majambazi wa ikulu**” ni sitiari inayorejelea wale marais wengine wanaokaa ikulu wakitawala nchi zao.

3.3.2 Tashibih

Harding (2017) anafafanua tashibih kuwa ni tamathali ya usemi inayolinganisha kitu kimoja na kingine kwa kutumia maneno “kama” ili kuunda picha fulani katika akili ya msikilizaji au msomaji na kusaidia uelewekaji wa ujumbe sawasawa. Maneno mengine ambayo yanaweza kutumika kuunda tashibih ni pamoja na “mithili ya”, “sawa na”, “ja” na “kama vile”. Tashibih husaidia wasanii kutia ladha kazi zao za kifasih. Kithaka wa Mberia anatumia tashibih kadha wa kadha anapofafanua maudhui mbalimbali katika ushairi wake. Kwa mfano, anapozungumzia juu ya unafiki wa tamaa katika siasa, anatumia tashibih katika shairi “Karamu ya Nzige” (uk. 35) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Mshairi anagusia namna viongozi wanafuja hazina ya taifa ambayo ndiyo karamu kwa sababu ya ubinafsi na tamaa nyingi. Anasema, “kwa **mvumo unaorindima mithili yowe la katadole katika shamba la mawe**le, sherehe ya nzige yaterema...” (uk. 35). Analinganisha mvumo wa viongozi wanapofuja hazina ya taifa na yowe la katadole katika shamba la mawele. Picha hii

inasaidia kueleza maudhui ya ubadhirifu wa rasilimali miongoni mwa viongozi waliopewa jukumu la kuongoza na kuleta maendeleo katika nchi.

Mwandishi pia amezungumzia juu ya maudhui ya ubinafsi, uzembe na kiburi miongoni mwa wabunge katika bunge la taifa. Katika shairi “Msimu wa Tisa” (uk. 9) katika diwani ya *Msimu wa Tisa* mshairi anatumia tashibihi anaposema, **“Kimbunga cha ubinafsi, uzembe na kiburi kinavuma kama bahari inayoteta na tufani”** (uk. 9). Amelinganisha ubinafsi, uzembe na kiburi cha wabunge na upepo unaozunguka kwa nguvu kutoka baharini kuelekea nchi kavu. Viongozi hawa wanafanya mambo bila kujali waliowapigia kura wanapokuwa bungeni.

Kithaka wa Mberia amezungumzia juu ya utawala wa kidikteta katika shairi “Papa” (uk. 45) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Papa ni kiongozi yeyote ambaye anatumia nguvu na mamlaka yake kudhulumu watawaliwa. Mwandishi anatumia tashibihi kulinganisha ukali wa papa na mauti anaposema, **“Papa mkali kama mauti anahangaisha samaki”** (uk. 45). Kawaida papa ni samaki mkubwa baharini anayeogopwa na samaki wadogo kwa sababu ya nguvu zake mbali na mazoea ya kuwala samaki wadogo. Mshairi anatumia tashibihi hii kurejelea kiongozi mkali anayehangaisha watu (samaki) wa ngazi za chini. Huo ni uongozi dhalimu ambao haufai kukubaliwa na yeyote.

Kwengineko, katika diwani ya *Mchezo wa Karata* katika shairi “Mgunga Shambani” (uk. 20), mshairi anafafanua maudhui ya ukoloni. Anaeleza vile wakoloni waliingia Kenya na nchi zingine za Afrika wakatawala wenyeji kwa dhuluma nyingi zikiwemo kuwanyang’anya mashamba yenye rutuba, kuwafanya watumwa, kudhibiti uhuru wao wa kutembea na maovu mengine. Maovu hayo kwa wenyeji yalikuwa sawa na michomo mikali ya miiba ya mgunga. Mateso yalipozidi, wenyeji waliamua kuungana kumng’oa mkoloni ili kujiondolea dhiki. Mshairi anasema, **“Tuliamua kuling’oa gongo la mgunga kusudi kuyeyusha dhiki ambayo ilikifunika kijiji kama blanketi ya mipupu”** (uk. 20). Mwandishi analinganisha dhiki iliyoletwa na mkoloni sawa na blanketi ya mipupu. Mpupu ni mmea ambao una majani yanayofanana na mharagwe na wenye upupu ambao ukigusana na ngozi unawasha sana. Kwa hivyo, mshairi analinganisha mateso ya mkoloni kwa wataliwa na blanketi ya miti inayowasha ngozi punde inapoguswa. Tashibihi hii inaonyesha picha ya mateso yaliyokumba wenyeji wakati wa utawala wa mkoloni.

Kithaka wa Mberia ameeleza tatizo la njaa kama shida mojawapo inayokumba mataifa ya Afrika katika diwani ya *Msimu wa Tisa* katika shairi “Minyororo ya Njaa” (uk. 1). Mwandishi anaonyesha vile watoto na wazee wanateseka kwa sababu ya njaa. Mshairi ametumia tashibihi anapoeleza picha ya mzee aliyekalia gogo kuwa “**Mbavu zake zimechomoza kama fito zilizopinda**” (uk. 2). Mbavu zimelinganishwa na fito za kujengea nyumba zilizopinda kuonyesha picha ya mzee aliyedhoofika kwa sababu ya ukosefu wa chakula. Aidha, katika shairi hili, mwandishi anatumia tashibihi anaposema kuwa, “**Jamaa na majirani waliovaa huzuni kama veli**” wanaaga udongo wa fusi la kaburi ya tano (uk.1). Mshairi amelinganisha huzuni iliyogubika jamaa na majirani wanapomzika mtoto wa tano aliyekufa kwa sababu ya njaa na veli linavyomfunika bibi harusi siku ya sherehe ya harusi.

Suala la wakimbizi ni changamoto pia inayokumba mataifa ya Afrika. Kuna mataifa yanayopigana kiasi kwamba raia wa nchi hizo wanatorokea kwengine kwa sababu ya kutafuta amani na usalama. Vilevile, kuna mizozo ya kikabila na kisiasa ndani ya nchi ambayo wakati mwingine huzua vita vya kikabila. Hali kama hiyo huchangia kuwa na wakimbizi wa ndani katika nchi husika. Anapozungumzia juu ya suala la wakimbizi katika shairi “Mkimbizi” (uk. 58) katika diwani ya *Msimu wa Tisa* mwandishi anatumia tashibihi ifuatavyo:

Nilikuwa na **bahati kama mtende**
Mbio za usiku wa kelele gizani
Zilinitema kutoka kinywa cha mauti
Kama mbarika kutoka ganda la mbono... (uk. 58)

Katika dondoo hili, mshairi ametumia tashibihi kueleza vile mhusika alibahatika kutoroka ili asiawe. Mtende ni mti mrefu wenye shina na magamba, unaostawi kwenye maeneo ya joto hasa Uarabuni na huzaa tende. Mbono ni mmea unaozaa mbarika yaani mbegu zinazotokana na mmea huo. Mbarika hufyatuka kwa kasi zinapotoka kwenye ganda la mbono. Kwa hivyo, mhusika alikuwa na bahati kama mtende ambao haukauki kwa urahisi katika maeneo ya joto alipotoroka mapigano. Mbio zake zilimsaidia kutoroka kwa kasi kama vile mbarika zinavyotoka kwa kasi kutoka ganda la mbono.

3.3.3 Tashihisi

Tashihisi ni tamathali ya usemi ambapo vitu visivyokuwa na uhai vinawasilishwa kwa namna iliyo sawa na binadamu ya kuweza kufikiri na kuhisi (Wamitila 2003a). Tashihisi ina uwezo mkubwa wa kugusa hisia za msikilizaji au msomaji. Paxson (1994) anasema kuwa wasomi wa fasihi wanatumia tashihisi kuathiri hisia za hadhira ili kuona uzito wa kile kinazungumziwa na msanii. Mshairi anatumia tashihisi kadha wa kadha anapogusia maudhui yanayohusu udikteta, changamoto za mataifa ya Afrika na ujenzi wa jamii mpya. Kwa mfano, katika shairi “Jumapili ya Damu” (uk. 6) katika diwani ya *Bara Jingine*, mshairi anaeleza kuhusu jaribio la wanamgambo kumng’oa mamlakani kiongozi dhalimu. Risasi zinatumiwa na watu wengi wanauawa. Vikosi vya jeshi vya kiongozi huyo dhalimu vinatumia vifaru, bunduki na mizinga kuzima jaribio la mapinduzi. Mwandishi anatumia tashihisi kueleza vile risasi zinapiga kuta, milingoti ya stima, magari ya rangirangi na watu. Anasema, **“Risasi zinaanza kupiga miluzi”** (uk. 7). Mluzi ni sauti inayotolewa na mtu anapobana midomo na kupuliza hewa nje kwa nguvu. Risasi zinapewa sifa ya kupiga miluzi kama mtu. Hata hivyo, mtunzi anamaanisha zile sauti kali za kutisha zinazotokana na milio ya risasi.

Kwengineko, kuna matumizi ya tashihisi katika diwani ya *Msimu wa Tisa* katika mashairi “Minyororo ya Njaa” (uk. 1), “Usingizini” (uk. 30), “Mkimbizi” (uk. 57) na “Kakuma” (uk. 65). Mashairi haya yanajikita katika matatizo yanayokumba mataifa mengi ya Afrika. Kwa mfano, shairi “Minyororo ya Njaa” linahusu tatizo la njaa miongoni mwa mataifa ya Afrika licha kwamba kuna mvua na ardhi nzuri ya kilimo. Njaa inaathiri afya ya watoto na wazee na hata kusababisha kifo. Akionyesha namna watoto wameathiriwa na njaa, mwandishi anasema, **“Watoto waliomumunywa na kinywa cha njaa wakabakia na macho yanayodondoka dhiki”** (uk. 1). Katika mfano huu, njaa inapewa sifa ya kuwa na kinywa cha kutafuna kama mwanadamu. Tashihisi hii inasaidia kuleta picha ya watoto waliodhoofika sana kwa sababu ya makali ya njaa.

Mara nyingi visa vya kusikitisha vya makali ya njaa katika mataifa mengi ya Afrika huandikwa kwenye magazeti, kutangazwa kwenye idhaa za redio mbali na kuonyeshwa kwenye runinga. Aidha, katika shairi hili, mwandishi anaonyesha vile watoto wanakufa kwa kutumia tashihisi anaposema, “Wametoa kwaheri zenye moto

wa uchungu kwa **mtoto aliyeshikwa mkono na njaa akaambiwa njoo nikupeleke kuzimu!**” (uk.1). Kauli hii ni tashihisi kwa sababu njaa haina mikono ya kushika mtoto wala uwezo wa kumwambia mtoto kuwa inampeleka kuzimu.

Katika shairi “Usingizini” (uk. 3), mshairi ameeleza vile watu wanazembea kwa kutolima ardhi yenye rutuba na kutumia vyema maji ya mvua ili kuimarisha kilimo na kupunguza visa vya njaa. Kwa hivyo, watu wamelala badala ya kutumia rasilimali muhimu kujiendeleza katika bara la Afrika. Akionyesha namna ardhi imelala bila kutumiwa, mwandishi anasema, “**Ardhi yenye siha na uchangamfu wa rutuba imelala usingizi katika kitanda cha maumbile**”(uk. 3). Katika dondoo hili, ardhi imepewa sifa ya afya, uchangamfu na kulala usingizi katika kitanda kumaanisha kuwa haitumiki kwa shughuli muhimu za kuzalisha chakula. Kwa hivyo, watu pamoja na ardhi kwa jumla wamelala. Watu hawagutuki wakatumia akili zao kukuza kilimo ilhali ardhi haitumiki kamwe.

Aidha, katika shairi “Mkimbizi” (uk. 57) mshairi ameeleza juu ya shida za wakimbizi. Katika mataifa ya Afrika, watu wanapigana kwa sababu ya siasa, utawala dhalimu, ukabila, wizi wa mifugo, mipaka ya utawala na mashamba. Hali kama hizi zinafanya watu kuuana, mali kuharibiwa na watu kutorokea sehemu au nchi zingine kutafuta usalama. Watoto, wazee na kina mama wajawazito wanateseka sana. Katika shairi hili, mwandishi anaeleza jinsi hali tulivu inavyogeuka na kusababisha watu kutoroka makwao. Anasema:

**Masikio ya kumbukumbu bado yanasikia
Yanasikia miluzi na hasira za risasi hewani
Zikisaka roho za watu bila hatia wala silaha (uk. 57)**

Mwandishi ametumia tashihisi anaposema kuwa masikio yanasikia miluzi na hasira za risasi hewani. Risasi zinapewa sifa ya kutoa miluzi kwa maana ya ile milio mikali ya risasi. Aidha, risasi zinapewa sifa ya hasira na kusaka. Tamathali hii inatumiwa na mwandishi kuleta picha na taharuki kwa msomaji ili kuona namna hali hiyo inachangia watu kuuana na wengine kutorokea usalama kwengine.

Kwengineko, katika shairi “Kakuma” (uk. 65) kuna matumizi ya tashihisi. Kakuma ni kambi moja maarufu nchini Kenya inayohifadhi wakimbizi wanaotoroka misukosuko ya siasa na vita nchini Sudan Kusini, Somalia, Uganda na Ethiopia. Mwandishi anaonyesha vile wakimbizi wanateseka wakiwa kambini kwa sababu ya jua kali,

vumbi, wadudu hatari kama vile siafu wakati wa usiku, kukosa usingizi, ubakaji wa wasichana na kina mama wakienda kutafuta kuni, ukahaba na shida ya elimu bora kwa watoto kambini. Kwa mfano, mwandishi anasema:

Vibanda vya plastiki mbugani
Mchana, jua lenye ghadhabu kali
Linatawala kwa sheria za kiimla (uk. 65)

Mshairi ametumia tashihisi anaposema kuwa “jua lenye ghadhabu kali linatawala kwa sheria za kiimla”. Jua limepewa sifa ya kuwa na hasira na kutawala kwa sheria za kimabavu. Tashihisi hii inamaanisha kuwa jua linawaka sana mchana na hivyo kunakuwa na joto kali linalosumbua wakimbizi kambini. Isitoshe, mshairi anatumia tashihisi pale anaposema, “**Baada ya jua kuokota miale na kuaga kambi na wakaazi**” (uk. 65). Jua limepewa sifa ya kuwa na mikono ya kuokota miale yake na vilevile kuaga kambi na watu wanaokaa humo. Anachomaanisha mwandishi ni kuwa wakati wa jioni jua linapotua na usiku kuingia viumbe hatari kama tandu, jongoo, ng’e, buibui, nyenze na nyoka wanaanza kuingia kambini na hivyo wanahatarisha maisha ya wakimbizi.

Uharibifu wa mazingira kwa kukata miti kiholela ni shida nyingine inayokabili mataifa ya Afrika. Watu hukata miti ili kupata mbao za kujengea nyumba, kutengeneza samani, kuchoma makaa na mashamba ya kuishi na kuendeleza shughuli za kilimo. Madhara ya ukataji miti kama anavyosema mwandishi katika shairi “Jinamizi” (uk. 55) kwenye diwani ya *Bara Jingine* ni pamoja na mmomonyoko wa udongo, ukosefu wa malisho kwa mifugo na mifugo na binadamu kufa kwa sababu ya ukame na njaa. Akionyesha namna mvua inasababisha madhara baada ya miti kukatwa mwandishi anasema:

Mvua ilikuja kwa hasira,
Kwa kucha zake ndefu
Ilihujumu ardhi... (uk. 56)

Katika dondoo hili, mshairi anaonyesha kuwa mvua ina sifa ya hasira na kucha ndefu kama vile mtu au mnyama mkali kama simba au chui. Tashihisi hii inasaidia mwandishi kueleza vile mvua ilinyesha kwa kasi na matone yake yenye nguvu kusomba mchanga na vumbi lililokuwepo baada ya miti kukatwa na watu wenye tamaa ya kupata mbao za kujengea na mashamba ya kilimo.

Licha ya hayo, Kithaka wa Mberia ametumia tashihisi katika mashairi “Hatutaaga Ndoto” (uk. 4) na “Bara Jingine” (uk. 10) katika diwani ya *Bara Jingine* anapoangazia maudhui ya ujenzi wa jamii mpya. Kwa miaka mingi, mataifa ya Afrika yamekuwa yaking’ang’ana kupunguza umaskini, kutojua kusoma na kuandika, ufisadi, magonjwa na njaa. Ingawa hayajafanikiwa sana kumaliza matatizo hayo, mwandishi ana matumaini kuwa ndoto ya kuwa na Afrika nzuri itatimia. Anatumia tashihisi anaposema kuwa, “**Teknolojia ya kilimo itabusu mashamba yazae kiazikikuu**” (uk. 5). Mshairi anaipa teknolojia sifa na uwezo wa kubusu mashamba kana kwamba ina midomo ya kufanya hivyo. Kimsingi anachomaanisha mwandishi hapa ni kuwa kuna wakati utafika kuwe na matumizi mema ya teknolojia mpya ya kilimo kama vile unyunyiziaji maji mashamba na ukuzaji wa mazao. Jambo hilo litafanya Afrika ijitegemee kwa upande wa chakula na kuacha kuombaomba misaada ya chakula wakati wa njaa kutoka mataifa yaliyostawi.

Aidha, maudhui ya ujenzi wa jamii mpya yanapatikana katika shairi “Bara Jingine” (uk. 10). Mwandishi ana matumaini kuwa upo wakati ambapo barani Afrika usalama utakuwa kwa watu wote bali si kwa viongozi wakuu serikalini, viziwi na jela hazitakuwa za kudhulumu watu na hakutakuwa na ulafi wala ufisadi. Kuna wakati ambapo utafiti utasaidia kupunguza magonjwa Afrika na kuimarisha ukuzaji wa chakula. Katika kuonyesha namna vyakula vitakua shambani, anatumia tashihisi anaposema:

Mbaazi
Zinazokua bila kinyongo,
Mboga na matunda
Yanayozomea adui shambani (uk. 13)

Katika dondoo hili, mwandishi amezipatia mbaazi sifa ya kukua bila chuki kana kwamba zina uwezo huo wa kibinadamu wa kuwa na kinyongo. Aidha, mboga na matunda yanapewa pia sifa ya kuzomea au kutolea adui maneno makali shambani kana kwamba yana kinywa cha kuzungumza. Mwandishi ametumia tashihisi hizo kueleza vile mbaazi, mboga na matunda yatanawiri shambani na kuimarisha kilimo biashara.

3.3.4 Chuku

Chuku ni tamathali ya usemi ambapo sifa fulani hukuzwa kupita kiasi (Wamitila 2003b). Kukuzwa huko kunaweza kuwa kwa udogo au ukubwa. Lengo la kutumia chuku ni kulifanya jambo fulani litokeze kwa uwazi, kuikuza sifa fulani mbali na kumfikirisha msomaji kwa kuuona uzito uliopo. Mshairi ametumia chuku katika kueleza maudhui yanayohusu njaa na siasa katika diwani ya *Msimu wa Tisa* na ujenzi wa jamii mpya katika diwani ya *Bara Jingine*. Kwa mfano, katika shairi “Minyororo ya Njaa” (uk. 1) katika *Msimu wa Tisa*, mwandishi anatumia chuku anapoeleza sura ya watoto walioathiriwa na njaa. Macho ya watoto yanaonyesha shida ya njaa na miguu yao imekonda na kuwa mianzi mikavu. Anasema:

Watoto waliomumunywa na kinywa cha njaa
Wakabakia na macho yanayodondoka dhiki
Na vipande vya mianzi mikavu badala ya miguu (uk. 1)

Mwanzi ni mti unaofanana na muwa wenye uwazi ndani kama mrija unaotumika kama fito za kujengea nyumba za miti. Mwandishi amepiga chuku anaposema kuwa watoto wana vipande vya mianzi mikavu badala ya miguu. Usemi huu unaibua hisia za kutisha na huruma kwa msomaji ili kuona athari za makali ya njaa kwa watoto hao wachanga.

Kwengineko, katika shairi “Msimu wa Tisa” (uk. 9), mwandishi amegusia maudhui ya uzembe, ubinafsi na tamaa ya wabunge katika shughuli zao za kuwakilisha wananchi waliowachagua. Wanashambulia hazina ya taifa kwa maslahi yao tu bila kujali wananchi wengi wanaoteseka. Mshairi anasema:

Punde walipokula kiapo cha uaminifu kwa nchi
Bila kujali vinywa vinavyopiga miayo ya njaa
Walivamia ghala la taifa kwa tamaa inayovuma (uk. 9)

Katika dondoo hili, wabunge wamesawiriwa kuwa watu wanaosahau haraka kiapo cha utii kwa serikali na wananchi na kuvamia ghala la taifa bila kujali watu maskini wanaoteseka kwa sababu ya njaa na kutotimiziwa ahadi za maendeleo. Mwandishi anapiga chuku anaposema kuwa “walivamia ghala la taifa kwa tamaa inayovuma”. Katika hali halisi, tamaa haiwezi kuvuma kama upepo ufanyavyo. Mwandishi anakuza tamaa ya wabunge ili kuonyesha namna ilivyozidi hali ya kawaida.

Kuna matumizi ya chuku katika shairi “Hatutaaga Ndoto” (uk. 4) katika diwani ya *Bara Jingine*. Mwandishi anaeleza kuwa watu wa Afrika hawataaga ndoto ya kuwa na Afrika mpya tofauti na ilivyo sasa. Katika Afrika mpya, viongozi dhalimu hawatakuwepo, magonjwa yanayosumbua watoto kama ukambi na kifaduro hayatakuwepo, umaskini utapungua ili watoto wasome bila tatizo na teknolojia ya kilimo itasaidia kukuza chakula cha kutosha ili serikali ikome kuomba misaada kutoka mataifa mengine duniani. Mwandishi anapiga chuku kwa kusema:

Teknolojia ya kilimo
Itabusu mashamba
Yazae kiazzi-kikuu
Kikubwa kuliko Afrika... (uk. 5)

Katika dondoo hili, kiazzi-kikuu ni mmea mdogo ambao hutoa kiazzi kikubwa kisichokuwa na utamu. Afrika ni bara kubwa lenye mataifa mbalimbali. Kwa hivyo, haiwezekani mashamba kuzaa kiazzi-kikuu ambacho ni kikubwa kuliko bara la Afrika. Hiyo ni chuku. Kupitia chuku hii, mwandishi anamaanisha kuwa bara la Afrika linaweza kuzalisha chakula kingi ili kupunguza visa vya njaa ya mara kwa mara.

Tamathali ya chuku imejitokeza tena katika shairi “Bara Jingine” (uk. 10) katika diwani hii ya *Bara Jingine*. Mwandishi ana matumaini ya kuona bara jipya ambapo bunge halitakuwa ukumbi wa ulafi, hakutakuwa na ufiadini, hakutakuwa na marais madikteta katika ikulu, kutakuwa na chakula cha kutosha na umeme wa kuendesha mitambo ili kuleta maendeleo. Akizungumzia kuhusu bara la Afrika kujitosheleza kwa upande wa chakula, mshairi anasema:

Washairi
Watakariri mashairi
Kusifia kwa ukunjufu
Siyo majani-chai na kakao
Siyo kahawa na tumbako
Bali viazi
Vikubwa kuliko njaa... (uk. 13)

Maneno “viazi vikubwa kuliko njaa” ni chuku. Viazi vinaweza kuwa vikubwa lakini haviwezi kuwa vikubwa kuliko njaa. Isitoshe, njaa haiwezi kupimwa kwa kifaa maalumu lakini matokeo na athari yake ndiyo yataonyesha kiwango cha njaa iliyopo.

3.3.5 Maswali ya Balagha

Swali la balagha ni tamathali ya usemi inayouliza swali ili kutoa hoja fulani kuliko kutaka jibu. Hii ni tamathali ya kuuliza maswali ambayo hayahitaji majibu kwa sababu majibu yake yako wazi. Swali la balagha huulizwa wakati anayeuliza anajua jibu tayari au jibu lenyewe halihitaji kutolewa. Swali la balagha ni mbinu moja ya kuisitiza usemi katika kazi ya fasihi. Aidha, swali la balagha linahitaji msomaji au msikilizaji aone ukweli fulani katika jambo ili achukue hatua fulani.

Kithaka wa Mberia ametumia maswali ya balagha katika maudhui yanayoangazia udikteta katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Kwa mfano, katika shairi “Sisimizi Nijulisheni” (uk. 27) mshairi anauliza:

Sisimizi mvukao njia
Nijulisheni, nibaini
Katika nasaba yenu
Wapo wapao vileleni
Wakaloa
Njama na ulaghai
Unafiki na ubaguzi
Kiburi na vitisho
Au, maisha yenu
Si ya uchoyo unaonuka
Na ulafi usiokauka
Miongoni mwa viongozi? (uk. 27)

Katika shairi hili, mshairi anauliza sisimizi swali la balagha. Sisimizi ni mdudu mdogo wa kahawia au mweusi aliye na umbo kama siafu. Mshairi hatarajii jibu kutoka kwa sisimizi bali anauliza ukweli fulani kuhusu viongozi ambao wanapokuwa mamlakani wanakuwa na ulaghai, unafiki, ubaguzi, kiburi na vitisho.

Aidha, mwandishi ametumia swali la balagha katika shairi “Swali kwa Konokono” (uk. 33). Mshairi anauliza uhalali wa rais wa nchi kutumia mamlaka yake kunufaisha jamaa na watu wa karibu bila kujali watu wote walio chini yake ambao wanateseka. Isitoshe, anauliza uhalali wa kiongozi kukatalia mamlakani bila kujali malalamiko kutoka kwa wananchi ilhali anastahili kung’atuka uongozini bila vitisho au umwagikaji wa damu. Mwandishi anauliza:

Konokono, ungeliga saruji
Na kugandama mamlakani
Bila kujali malalamiko,
Au ungeliongozwa na akili

Badala ya umio na tumbo
Na kushuka bila hasira
Na vitisho vikali
Vya gharika la damu? (uk. 33)

Katika shairi “Swali kwa Yangeyange” (uk. 41) katika diwani hii ya *Mchezo wa Karata*, mshairi anauliza yangeyange swali la balagha. Yangeyange ni ndege mweupe wa mwili, mwenye kishungi, miguu mieusi anayepatikana kwenye maziwa yenye matope. Mwandishi anamtumia ndege huyu kuulizia uhalali wa viongozi wanaofikia vyeo vya juu kupitia demokrasia au kutumia nguvu kuvunja vichwa vya wapinzani wao. Aidha, anauliza ni kwa nini viongozi wengine wanafikia ngazi za juu kwa kutumia mitutu ya bunduki na wakishafika huko kileleni wanaanza kunyanyasa watawaliwa. Anauliza:

Yangeyange
Ungelifikia hicho kidato
Ungelimea pembe kama kifaru
Ukanyanyasa kwa kutonga
Au ungelibaini
Kwamba ameaye pembe
Na kwa kiburi kingi kutonga
Hatimaye haki humpiga kumbo
Akalipuka mithili baruti...
Akaishia katika jalala
La historia? (kur. 41-42)

Katika dondoo hili, mwandishi au msomaji hahitaji jibu la swali. Kuna ukweli kuwa kiongozi anayetumia nguvu na kiburi kunyanyasa watu siku moja atatoka uongozini kwa utaratibu au kuondolewa kwa nguvu za mapinduzi na akasahaulika au kubaki katika kumbukumbu za historia za watawaliwa.

Mwandishi anapoangazia maudhui kuhusu changamoto zinazokumba mataifa ya Afrika, ametumia maswali ya balagha katika baadhi ya mashairi. Kwa mfano, katika shairi “Si Maskani Mapya!” (uk. 25) katika diwani ya *Bara Jingine*, mtunzi anazungumzia juu ya maisha ya kunyanyaswa na kukandamizwa kwa wanyonge katika nchi huru. Kwa hivyo, nchi kama hiyo si maskani mapya ya kuishi. Si mazingira mazuri kwa wananchi kamwe. Mwandishi anauliza:

Haya si maskani mapya
Maskani mapya gani, ambapo
Tunapokonywa ndoto daima
Na nguchiro vizimbani

**Na mende majikoni
Na panya maghalani? (uk. 25)**

Mwandishi anaonyesha kuwa nchi ambamo wananchi wanakosa matumaini ya maisha mazuri si makaazi mazuri ya kuishi. Mwandishi anatumia sitiari ya “nguchiro”, “mende” na “panya” kurejelea viongozi wanaotumia uwezo wao kunyonya jasho la wanyonge na kufanya maisha yao kuwa magumu.

Kwengineko, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* mshairi ametumia maswali ya balagha anapoangazia uongozi usio wa maono katika shairi “Usingizini” (uk. 3). Anaonyesha vile ardhi yenye rutuba haitumiki, maji ya mvua yanapotelea kwenye mito, bahari na maziwa huku njaa inaua watu. Isitoshe, hakuna reli na barabara za lami na stima vijijini. Kutokana na mambo haya, mwandishi anauliza:

**Ni nani anayejua siku adhimu au mwezi azizi
Ambamo wanaokoroma kwenye makochi ya uongozi
Wataamka kutoka usingizi wa siasa bila ramani
Wafikiche macho kwa viganja vya uona-mbali
Waongoze taifa kutoka hili bonde la aibu? (uk. 4)**

Katika shairi “Darfur” (uk. 26), mwandishi anaeleza maovu yanayotendeka katika nchi ya Sudan Kusini. Wenyeji wenye ngozi nyeusi wanawekewa vikwazo ili wasifikie hazina ya taifa, kunyimwa kauli kuhusu uendeshaji wa serikali na kutendewa maonevu na dhuluma. Mambo haya yanachochea vita nchini humo wenyeji wakidai haki, heshima na shibe. Kundi la *Janjaweed* linaanza mashambulizi. Kundi hili linashambulia nyumba hadi zinabaki magofu, mimea shambani inanyongwa na kwekwe mbali na wanawake na wasichana vijijini kubakwa. Kwa sababu ya maovu haya, mwandishi anauliza:

**Kwa nini waliojitwika jukumu la polisi wa dunia
Wamesimama kimya wakiangalia upande wa pili
Maisha ya watu milioni mbili yakiungua katika mwako? (uk. 27)**

Kwengineko, katika shairi “Petali za Amani?” (uk. 29) anazungumzia iwapo amani ya kudumu itapatikana katika nchi ya Sudan Kusini. Anahisi kwamba ni wakati mwafaka kuvumiliana na kuaminiana baina ya watu wenye rangi tofauti na amani kudumu Sudan Kusini ili kusiwe na umwagikaji mwingine wa damu. Mwandishi anauliza:

**Enyi miche michanga ya mmea wa uvumiliano
Ambao mmeatikwa udongoni uliozoea chuki**

**Mtashamiri kwenye ardhi inayonuka damu
Msambae kwenye makaburi ya maiti milioni mbili
Mtwae vijiji vilivyonyimwa usingizi na jinamizi
Kijasiri, mzamishe mizizi yenu ijikite kwa kani
Upepo wa shaka ukose nafasi ya kuleta mashaka? (uk. 29)**

3.3.6 Mbinu Nyingine za Kisanaa

Mbinu nyingine za kisanaa ni jumla ya vipengele ambavyo haviwezi kuorodheshwa kama tamathali za usemi lakini mshairi amevitumia anapoeleza juu ya maudhui yanayohusu siasa za unafiki, udikteta, ukoloni, changamoto za mataifa ya Afrika na ujenzi wa jamii mpya. Kwa hivyo, mbinu hizi zimechanganuliwa chini ya mtindo kwa kutumia nadharia ya elimumitindo mkabala wa uhakiki mpya.

3.3.6.1 Taswira

Taswira ni dhana inayoelezea neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji (Wamitila 2003a). Taswira zinaweza kuwa za kimaelezo ambapo maelezo fulani yanaunda picha. Taswira zinaweza kuwa za ki-ishara yaani zinazounda picha inayoashiria jambo fulani. Fauka ya hayo, taswira inaweza kuundwa kupitia tashibihi na sitiari.

Katika shairi “Mchezo wa Karata” (uk. 18) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*, kuna taswira inayojitokeza kutokana na vile mazimwi yaani wanasiasa wanavyocheza mchezo wa karata na wananchi. Mwandishi anatumia taswira kuonyesha vile wanasiasa wanatumia hila katika uwanja wa siasa. Mshairi anasema:

Ulipoanza mchezo
Tulitupa karata
Wakatupa karata
Tukatupa karata
Wakatupa karata
Na kwa ujanja
Wakashinda hiyo duru (uk. 18)

Maelezo haya yanaonyesha picha dhahiri namna mchezo wa kutupa karata unavyoendelea baina ya wanasiasa na wananchi. Mwishowe, wanasiasa wanashinda kwa sababu wana njama, ujanja na hila nyingi katika ulingo wa siasa.

Kuna taswira inayojitokeza katika shairi “Jumapili ya Damu” (uk. 6) katika diwani ya *Bara Jingine*. Mwandishi anaeleza vile wananchi waliochoshwa na utawala dhalimu wa kiongozi fulani wanapanga njama ya kupindua serikali Jumapili fulani. Jaribio hili

la mapinduzi linachangia watu kuvamia maduka na kuiba mali. Risasi zinaanza kupigwa kiholela kotekote wakati wa makabiliano makali kati ya waasi na majeshi. Hata hivyo, majeshi yanatumia silaha zao kudhibiti hali ili kiongozi dhalimu aendelee kubaki uongozini. Katika kuonyesha namna majeshi yanadhibiti jaribio la mapinduzi, mwandishi anatuchorea taswira hivi:

Magari ya rangirangi
Vifaru vya madoadoa
Vinatiririka kama mto
Bunduki zinalenga kushoto
Kulia, nyuma na mbele
Nayo mizinga hatari
Inatega mbingu;
Huu mtiririko
Ni safari ya marejeo
Anarejea mungu-wa-kinamo
Kwenye ulingo (uk. 8)

Katika dondoo hili, mwandishi anaeleza namna kuna makabiliano makali baina ya waasi wanaotaka kumng'oa mamlakani kiongozi dhalimu na majeshi ya kiongozi huyo. Matokeo ya mashambulizi haya ni umwagikaji wa damu. Majeshi yanafaulu kumrejsha mamlakani tena kiongozi (mungu-wa-kinamo) aendelee kutawala.

Suala la njaa ni changamoto inayokumba mataifa mengi ya Afrika. Njaa inachangia kuzorota kwa afya ya watu, watoto kwa watu wazima kudhoofika mbali na vifo kutokea. Mwandishi anapoangazia maafa ya njaa katika shairi “Minyororo ya Njaa” (uk. 1) katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, anachora picha ya watoto na mzee aliyeathiriwa na makali ya njaa:

Kurasa za magazeti na viwambo vya runinga
Vinaonyesha tena picha zinazoshtua hisia:
Watoto waliomumunywa na kinywa cha njaa
Wakabakia na macho yanayodondoka dhiki
Na vipande vya mianzi mikavu badala ya miguu

Mzee aneyekemewa na tumbo inayolalamika
Amekalia gogo huku ukungu wa kukata tamaa
Umezidisha idadi ya miaka usoni mwake
Mbavu zake zimechomoza kama fito zilizopinda (uk. 1)

Mapigano makali ya mara kwa mara katika nchi ya Sudan Kusini yanachangia watu wengi kuuawa na wengine kuachwa na majereha mabaya kwenye miili yao. Wanaonusurika mapigano hayo wanakimbilia usalama katika nchi za Kenya na

Ethiopia. Mwandishi anagusia suala la matokeo ya mapigano huko Sudan ya Kusini katika shairi “Lopinding I” (uk. 44) na “Lopinding II” (uk. 45). Majeruhi wa mapigano hayo wanapelekwa katika hospitali ya Lopinding inayopatikana katika kaunti ya Turkana nchini Kenya ili kupokea matibabu. Kwa mfano, katika “Lopinding I” (uk. 44) mshairi anachora taswira namna risasi zimelipua miguu na macho ya watoto kiasi cha kuibua hisia za huruma:

Katika wadi ya watoto
Macho yanayotetemeka
Yanauliza kimyakimya:
Risasi katili za kaskazini
Hazifi nyoyo ganzi
Zinapotafuna miguu
Na kulipua mboni machoni
Katika vichwa vya wakembe? (uk. 44).

Katika dondoo hili, tunaonyeshwa picha ya majeraha ya risasi waliyoyapata watoto wachanga kwenye miguu na mboni za macho yao. Taswira hii inaibua uchungu wanaohisi watoto hao wasio na hatia kwa sababu ya mapigano huko Sudan Kusini. Kwa hivyo, wanaletwa kwa magari hadi hospitali ya Lopinding huko Turkana ili kutibiwa. Mbali na watoto, watu wengine walioumia wanaingizwa katika wadi ya kuvuta viungo ili vinyooshwe visikakamae.

Taswira nyingine inaonekana katika shairi “Mafuta yenye Damu” (uk. 48) katika diwani ya *Msimu wa Tisa*. Mabwanyenye wenye tamaa ya kupata pesa wanaona mafuta safi ya bei nafuu kutoka Khartoum, Kusini mwa Sudan. Hawajali maiti za watu wengi waliouawa. Tamaa yao ni kupata petroli ya kuuza. Mwandishi anaonyesha taswira ya kutisha ya maiti zilizotapakaa kila mahali anaposema:

Naona majeruhi, damu na maiti
Maiti za wakulima mashambani
Maiti za wachungaji malishoni
Maiti za watoto shuleni
Maiti za vikongwe vijijini (uk. 48)

3.3.6.2 Takriri

Takriri ni mbinu ya lugha ambayo hutumiwa kuelezea urudiaji wa neno au maneno fulani katika matini au kazi fulani (Wamitila 2003a). Takriri ni muhimu sana katika ushairi. Mshairi anatumia takriri kusisitiza wazo, kuibua mdundo wa kukaririka kwa shairi au kuchezea maneno. Fauka ya hayo, takriri huibua ujumi na mnato wa kipekee

katika shairi. Kwa mfano, kuna takriri neno katika shairi “Mchezo wa Karata” (uk. 18) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Mshairi anapoeleza juu ya ujanja wa wanasiasa kwa wananchi, anarudia maneno “wakatupa karata” na “tukatupa karata” ili kuisitiza namna mchezo wa ujanja unavyoendelea baina ya wanasiasa na wananchi. Mshairi anatumia takriri kifungu hivi:

Ulipoanza mchezo
Tulitupa karata
Wakatupa karata
Tukatupa karata
Wakatupa karata....

Kwenye duru iliyofuata
Tulitupa karata
Wakatupa karata
Tukatupa karata
Wakatupa karata... (uk. 18)

Karata ni kadi yenye alama na tarakimu fulani inayotumiwa kuchezea. Wanasiasa ni watu wenye ujanja na hila nyingi. Katika mchezo huu, wanashinda duru ya kwanza, ya pili na hata zaidi. Wananchi wanabaki wakiumia kwa sababu hawashindi hila na ujanja wa wanasiasa na siasa zao za ubinafsi. Kwa hivyo, takriri anayoitumia mwandishi kama mbinu ya mtindo inasaidia kuisitiza uchezaji wa karata baina ya wanasiasa na wananchi, kujenga mdundo fulani mbali na kuongeza ladha katika shairi hili.

Kuna baadhi ya mashairi ambapo mtunzi amerudia maneno fulani kwa nia ya kuisitiza matumaini ya kujenga jamii mpya (Afrika) licha ya changamoto zilizopo. Kwa mfano, katika shairi “Hatutaaga Ndoto” (uk. 4) katika diwani ya *Bara Jingine*, mwandishi anarudia maneno “ndoto” na “kesho ambapo” ili kuisitiza kuwa kuna matumaini ya kujenga bara jipya siku za usoni ambapo umaskini, kutojua kusoma na kuandika, ufnadi, njaa na magonjwa hayatakuwepo. Urudiaji wa maneno “ndoto” na “kesho ambapo” yanaonyesha msimamo wa mshairi kuhusu hali hizo zinazokumba bara la Afrika na vilevile yanaleta ule mdundo wa shairi kukaririka vyema. Mshairi anasema:

Sisi, watoto wa Afrika
Tumekataa kuaga **ndoto**
Ewe **ndoto** ya dhahabu
Ndoto ya kesho

Kesho ambapo

Mamba wanaoota jua
Juu ya mazulia mekundu
Watakuwa hadithi

Kesho ambapo

Maktaba na maabara...

Kesho ambapo

Watoto watatembea vijijini ...

Kesho ambapo

Watoto watakweza akili...

Kesho ambapo

Teknolojia ya kilimo... (kur. 4-5)

Katika shairi hili, neno “ndoto” lina maana ya matumaini. Kwa hivyo, mshairi anaposema kuwa “hatutaaga ndoto” anamaanisha kuwa Waafrika hawatapoteza matumaini ya kuunda bara jipya siku za usoni ambapo maovu na changamoto zilizotajwa hazitakuwepo tena.

Maudhui ya ujenzi wa bara jipya yamerudiwa tena katika shairi “Bara Jingere” (uk. 10) katika diwani ya *Bara Jingere*. “Bara Jingere” ni kichwa cha shairi chenye maana ya bara tofauti au bara jipya ambapo maovu, mateso na shida barani Afrika zitakoma. Mwandishi anarudia maneno “ndoto” na “bara ambapo” kusisitiza ujumbe wake. Anasema:

Ndoto

Ndoto ya bara jipya

Bara ambapo

Bunge
Halitakuwa ukumbi
Wa genge la nzige...

Bara ambapo

“Usalama wa taifa”
Hautakuwa ngozi
Ya kulinda mamba wa ikulu...

Bara ambapo

Vizuizi
Na jela
Havitakuwa vinu
Vya kusagia utu...

Bara ambapo

Ulafi
Na ufigadi
Hazitanyesha kutoka juu... (kur. 10-11)

Katika dondoo hili, mwandishi ana matumaini kuwa kutakuwa na bara tofauti ambapo bunge halitakuwa ukumbi wa ulafi, usalama wa taifa hautalinda rais wa ikulu tu, vizuizi na jela havitakuwa mitambo ya kuumbua utu. Aidha, anatazamia bara jipya ambapo hakutakuwa na ulafi na ufisadi, utafiti utasaidia kupunguza visa vya magonjwa mbalimbali, hakutakuwepo na mapigano kati ya mataifa jirani miongoni mwa mambo mengine.

Mbinu ya takriri-neno inajitokeza katika shairi “Mgunga Shambani” (uk. 20) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Katika shairi hili, mshairi anaeleza juu ya juhudi walizofanya wenyeji kumfurusha mkoloni kutoka nchi yao. Neno “tingisha” limerudiwa mara kadha ili kusisitiza namna wenyeji walijitolea kupigania uhuru wao ili kujikomboa dhidi ya dhuluma za mkoloni. Mshairi anasema:

Tulilingisha kwa umoja
Huku jasho jembamba
Likutudondoka ndo!ndo!
Na damu yetu adimu
Kuvuja kutoka viganja

Tulilingisha
Na kutingisha
Na kutingisha (uk. 20)

Hata hivyo, baada ya kumng’oa mkoloni, mwandishi anaeleza kuwa baada ya muda mrefu, wale viongozi walioshika usukani walianza kuwadhulumu watawaliwa sawa na alivyowatesa mkoloni mwenyewe. Waliendeleza ukoloni mamboleo kupitia siasa na udikteta miongoni mwa maovu mengine. Kwa hivyo, ukoloni (mgunga) uliendelea kushamiri kwa sura tofauti (viongozi Waafrika). Mwandishi anatumia takriri-kifungu kuelezea mpito wa wakati kabla ya ukoloni mamboleo kujitokeza. Anasema:

II
Mafungia nyama yakawadia
Kisha jogoo wakawika
Mafungia nyama yakawadia
Kisha jogoo wakawika... (uk. 21)

Maneno “Mafungia nyama yakawadia” na “kisha jogoo wakawika” yanarudiwa ili kufupisha muda mrefu uliopita kabla ya sifa za ukoloni mamboleo kuanza kudhihirika miongoni mwa viongozi Waafrika waliounda serikali. Viongozi hao walianza kuwakandamiza watawaliwa tena kama ilivyokuwa enzi ya ukoloni mkongwe.

Kwengineko, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* kuna takriri katika shairi “ Mafuta yenye Damu” (uk. 48). Neno “maiti” linarudiwarudiwa ili kuisisitiza halaiki ya watu waliouawa katika nchi ya Sudan Kusini kwa sababu ya tamaa ya kupata mafuta. Watu walioponea mauti kutoka Antonov walitorokea Kenya na Ethiopia kwenye kambi za wakimbizi. Mwandishi anasema:

Naona majeruhi, damu na **maiti**
Maiti za wakulima mashambani
Maiti za wachungaji malishoni
Maiti za watoto shuleni
Maiti za vikongwe vijijini (uk. 48)

Kutokana na vifo hivi vya watu katika nchi ya Sudan Kusini, mwandishi anasema kuwa “usiniuzie petroli ya Kusini mwa Sudan, sitaendesha gari kwa damu ya watu” (uk. 48) kuonyesha ghadhabu yake juu ya watu waliouawa kwa sababu ya ubinafsi wa mabwanyenye wachache wanaotaka kupata mafuta kutoka kwenye mahame yanayonuka damu ya watu.

Katika shairi “Tume za Rais” (uk. 31) katika diwani hii ya *Msimu wa Tisa*, kuna takriri kifungu pia. Mwandishi anarudia maneno “napendekeza tuunde tume ya rais” kukejeli mazoea ya serikali kuunda tume za kuchunguza masuala mbalimbali lakini haitili maanani matokeo na mapendekezo yanayotolewa na tume hizo baada ya kukamilisha uchunguzi. Serikali inatumia pesa nyingi kuunda tume ambapo wanatume wanafaidika kwa kupewa magari na nyumba. Isitoshe, taarifa za tume za rais hazitekelezwi bali zinafichwa katika sefu za vyumba vya ndani vya mijengo ya rais. Mwandishi anasisitiza kwa kejeli anaposema:

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tumnunulie kila mwanatume *Hummer*

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tumjengee kila mwanatume kasri...

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tuitengee nusu ya akiba ya Banki Kuu...

Napendekeza tuunde tume ya rais... (uk. 31)

Mwandishi anatashtiti uundaji wa tume ya kuchunguza kama njaa inaweza kuua, tume ya rais kuhariri taarifa ya tume ya rais; tume ya kuchunguza jina la rais wa jamhuri na kisha tume ya kumtangazia rais jina. Tume hizi zinadhihirisha ufujaji wa pesa na

muda kwa sababu hazina manufaa kwa wananchi ilhali kuna masuala yanayostahili kupewa kipaumbele. Tume hizo zinakuwa na vikao vingi ambapo wanachama wanalipwa marupurupu mengi kutokana na ushuru anaotozwa mwananchi. Umma haujulishwi matokeo ya uchunguzi wa tume hizo.

3.3.6.3 Nyimbo

Nyimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka (Wamitila 2003b). Nyimbo huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi. Isitoshe, nyimbo zinapangwa kwa utaratibu wenye mapigo ya kimuziki. Kithaka wa Mberia anatumia nyimbo kueleza masuala ya siasa katika shairi “Magenge Matatu” (uk. 32) katika diwani ya *Msimu wa Tisa*. Genge ni kundi la watu wafanyao kazi pamoja. Mwandishi anazungumzia juu ya uongozi wa marais watatu na wasaidizi wao katika nchi ya Kenya yaani Jomo Kenyatta, Daniel Moi na Mwai Kibaki.

Mshairi anaeleza kuhusu utawala wa aliyekuwa rais wa kwanza wa Kenya, hayati Mzee Jomo Kenyatta na maazimio aliyotaka kutimizia Wakenya. Alitaka kupunguza shida ya kutojua kusoma na kuandika miongoni mwa wananchi, kupunguza maradhi kama vile malaria, kifaduro, ukambi na suala la umaskini. Ingawa alikusudia kutimiza hayo, utawala wake ulikumbwa na ulafi, ufisadi na ukabila. Kipindi cha utawala wa Jomo Kenyatta, mawaziri na wabunge ndicho genge la kwanza la mazimwi.

Genge la pili la mazimwi ni serikali na utawala wa Daniel Moi. Utawala wa Daniel Moi uliahidi Wakenya amani, upendo na umoja. Mshairi anasema kuwa, “**Watu walijjeruhi koo kwa kuimba “Juu! Juu! Juu sana!”** (uk. 32). Wakati huu pia watu waliimba nyimbo za kumsifu rais mstaafu Daniel Moi kama vile “**Tawala Kenya tawala, tawala Kenya tawala, Rais Moi tawala Kenya tawala!**”. Hata hivyo, katika miongo miwili ya utawala wake, viongozi waliifilisi nchi, ufisadi ukaongezeka, kukawa na mapigano ya kikabila na viwango vya umaskini vikazidi.

Utawala wa rais mstaafu Mwai Kibaki ndio uliokuwa genge la tatu. Mwai Kibaki aliahidi Wakenya katiba mpya na kumaliza ufisadi. Mshairi anasema, “**Tukaamini wimbo yote yawezekana bila mfalme wa nzige**” (uk. 32). Kwa hakika wananchi walifurahi Mwai Kibaki alipoingia uongozini mwaka wa 2002 baada ya kumrithi Daniel Moi. Waliimba kwa furaha na matumaini kuwa “**Yote yawezekana bila Moi!**”. Kenya ilipata katiba mpya mwaka wa 2010 wakati wa rais Mwai Kibaki. Hata

hivyo, ufiada uliendelea kushuhudiwa. Nyimbo hizi ni kumbukumbu ya historia ya siasa na utawala wa Daniel Moi na Mwai Kibaki.

3.3.6.4 Usimulizi

Usimulizi ni uelezeaji wa matukio katika hadithi. Kuna usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya pili na usimulizi wa nafsi ya tatu miongoni mwa aina nyingine nyingi. Wamitila (2008) anasema kuwa mtazamo unaochukuliwa katika usimulizi wa kisa chochote au matini yoyote huwa muhimu kwa sababu ni mbinu ya kimtindo ambayo inaathiri kwa kiasi kikubwa uelewekaji wa matini yenyewe. Vilevile, mkabala anaochukua unaweza kuonyesha msimamo wake, yaani ana maoni gani kuhusu hali fulani au anajitambulisha na nani.

Usimulizi unatumika sana katika utambaji wa hadithi katika fasihi simulizi, riwaya na hadithi fupi katika fasihi andishi. Ni nadra usimulizi kutumika katika ushairi. Hata hivyo, Kithaka wa Mberia ametumia mbinu ya usimulizi anapoangazia maudhui ya ukoloni, udikteta na ujenzi wa jamii mpya. Matumizi haya ya mbinu ya usimulizi ndiyo yanayoupa ushairi wake ubunifu mpya, usasa na upekee fulani. Kwa mfano, katika shairi “Mlipuko wa Furaha” (uk. 56) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*, mshairi anasimulia jinsi simba alivyong’olewa meno na kucha ndipo wanyama wengine wakapata uhuru mbugani. Simba anawakilisha kiongozi dhalimu, wanyama ni wananchi na mbuga ni nchi anayotawala kiongozi huyo. Mwandishi anasimulia:

**Siku zikapita
Simba akinguruma
Na kutabasamu**

**Siku zikapita...
Jogoo akawika...
Kutoka anga ‘tulivu’
Mawingu yalitanda
Kimya kikayeyuka
Mbingu zikatetemeka
Nguvu zisizozuilika
Zikamkabili Simba
Na kumn’goa meno
Na kucha
Mbuga ikalipuka
Kwa furaha
Ya uhuru (kur. 56-57)**

Katika dondoo hili, mshairi ametumia usimulizi mwakote kueleza namna kiongozi (Simba) alitawala kwa miaka na miongo akiwa na kiburi. Usimulizi mwakote ni mkabala wa usimulizi ambapo mwandishi anajua tabia za wahusika na hata fikira zao. Utawala wake ulikuwa wa dhuluma kwa watawaliwa. Wananchi walipochoshwa na uongozi wake, walimkabili na kumng'oa mamlakani na kujipatia uhuru. Maneno “siku zikapita Simba akinguruma na kutabasamu” na “siku zikapita jogoo akawika” yanaonyesha mpito wa wakati na mfuatano wa matukio na hali hadi kiongozi huyo alipong'olewa mamlakani.

Usimulizi vilevile umedhihirika katika shairi “Mgunga Shambani” (uk. 20) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Katika shairi hili, mshairi anazungumzia juu ya maudhui ya ukoloni na ukoloni mamboleo kwa mtindo wa usimulizi. Maudhui haya yanaonyesha historia ya nchi ya Kenya wakati wa ukoloni na baada ya uhuru. Mshairi anasimulia hivi:

I

Huko zama za nyuma

Kwenye shamba letu la mawele

Kulistawi gongo la mgunga

Ambalo kwa miiba myeupe

Lilituchoma michomo mikali

Tuliamua kuling'oa

Kusudi kuyeyusha dhiki...

II

Mafungia nyama yakawadia

Kisha jogoo wakawika

Mafungia nyama yakawadia

Kisha jogoo wakawika...

III

Pale **tulipong'oa** mgunga

Palistawi mti mwingine

Michomo ikatuliza machozi

Mithili zama za nyuma (kur. 20-21)

Mwandishi anaanza kusimulia kwa maneno “**huko zama za nyuma**” ambayo ni sawa na fomula ya “hapo zamani za kale” katika utambaji wa hadithi za fasihi simulizi. Aidha, anatumia usimulizi wa nafsi ya kwanza hali ya wingi “tu” katika maneno “**tuliamua**”, “**tulitingisha**”, “**tulusikia mshindo**” na “**pale tulipong'oa mgunga**” kuonyesha juhudi za wananchi kumwondoa mkoloni ili wajitawale. Katika kusimulia

pia, amerudia maneno “**tulilingisha**”, “**mafungia nyama yakawadia**”, “**kisha jogoo wakawika**”. Urudiaji ni sifa moja ya utambaji wa hadithi katika fasihi simulizi (Wamitila 2003a). Urudiaji huu unasisitiza mpito wa wakati na mfuatano wa matukio wakati wa harakati za kutafuta uhuru.

Kwengineko, katika diwani ya *Rangi ya Anga* kuna usimulizi mwakote katika shairi “Zimwi la Theluji” (uk. 48). Mohamed (1995) anasema kuwa usimulizi mwakote ni sauti inayojua yote, ya ndani na ya nje; sauti inayoangazia mahali, matukio, hisia, maumbile na tabia za wahusika na saikolojia zao. Msimulizi huingia apendavyo na atakavyo kwa uhuru na kisha kutoa habari atakavyo. Kwa hivyo, katika usimulizi mwakote msimulizi anajua na anaeleza yote. Katika shairi “Zimwi la Theluji.” (uk. 48), mwandishi anaeleza yote kuhusu wageni waliokuja eneo la Afrika Mashariki. Wageni hao ambao ndio “zimwi la theluji” ni Waarabu, wamishenari na wakoloni. Anaeleza kuhusu ujanja na madhila ya wageni hao kwa wenyeji wakati wa ung’ang’aniaji na ugavi wa bara la Afrika. Ametumia usimulizi mwakote kueleza walivyokuja Waarabu kisha Wakristo ifuatavyo:

Kwa kunyemelea
Lilikuja zimwi jeupe
Kwanza kwenye upwa
Ambapo upepo
Hupuliza manukato ya chumvi

Kama wimbi la maji
Zimwi lilisambaa
Na kufikia maeneo mapya...

Lilifuata mkondo wa wakati
Likavuka nyika na misitu... (kur. 49-50)

Katika dondoo hili, mwandishi amesimulia vile Waarabu walikuja kwenye upwa wa Afrika Mashariki na kukaa na wenyeji. Baadaye, walianza kuingia sehemu za bara katika shughuli za kufanya biashara ya kutafuta pembe za ndovu na watumwa (Chiraghdin na Mnyampala 1977).

Baada ya kuja kwa Waarabu, kundi jingine lililofuata lilikuwa la wamishenari wa Kikristo. Katika sehemu ya nne, mwandishi anasimulia hivi:

...lilikuja zimwi la theluji
Likibeba simulizi
Mkururo wa vituko vya ajabu...
Lilijidai kuwa tarishi
Wa Muumba wa yote
Likakunjua hadithi
Ya Baba na Mwana
Mwana wa pekee... (uk. 51)

Katika shairi hili “Zimwi la Theluji”, usimulizi huu unaonyesha kuja kwa Waarabu, wamishenari kisha wakoloni. Mshairi anadhihirisha hila walizotumia makundi yote haya kuwatesa na kuwadhulumu wenyeji. Akitumia usimulizi, anaonyesha walivyowafanya watumwa, kunyakua mashamba, kuvuruga imani na tamaduni zao kwa kuwafunza dini na elimu ngeni mbali na kudhibiti uhuru wao, kuwapiga na hata kuwaua wenyeji bila sababu yoyote.

3.3.6.5 Mazungumzo

Mazungumzo ni mbinu ya kupashana ujumbe kati ya wahusika katika fasihi. Mazungumzo aghalabu hutumika sana katika utanzu wa tamthilia ambapo wahusika wanaendeleza hadithi au kisa kwa njia ya dayalojia. Mazungumzo hayajitokezi sana katika ushairi isipokuwa katika bahari ya ngonjera ambapo wahusika zaidi ya mmoja wanajibizana. Kithaka wa Mberia ametumia mbinu ya mazungumzo katika mashairi yanayoangazia maudhui ya udikteta, ulafi na ubinafsi miongoni mwa viongozi na wanasiasa. Mshairi anaongea moja kwa moja na wahusika wake ambao wengi ni wadudu ili kuibua hisia na uzito fulani katika kile anachokisema.

Katika diwani ya *Mchezo wa Karata* kuna usemezano na baadhi ya wahusika kama vile katika mashairi “Sisimizi Nijulisheni” (uk. 27), “Swali kwa Konokono” (uk.33), “Swali kwa Yangeyange” (uk. 41) na “Maswali kwa Mdudu” (uk. 51). Kwa mfano, katika shairi “Sisimizi Nijulisheni” mshairi anasema, **“Sisimizi mvukao njia, nijulisheni nibaini”**. Katika shairi “Swali kwa Konokono” mshairi anazungumza na konokono anaposema, **“Nambie, ewe konokono, ungeligeuka mtu mithili sisi ukapaa hadi kiti-adimu ungelichukua tabia ya nzige...”** Mshairi anazungumza na konokono moja kwa moja kana kwamba konokono ana uwezo wa kumsikiliza.

Vilevile, katika shairi “Swali kwa Yangeyange” (uk. 41) mshairi anazungumza na yangeyange (aina ya ndege) anaposema, **“Ndugu yangeyange usiyedhuru kiumbe ila awe mfyonza damu...”**. Mshairi anamwita ndege huyu ndugu asiyedhuru kiumbe

isipokuwa kupe anayefyonza damu. Isitoshe, katika shairi “Maswali kwa Mdudu” mtunzi anaanza kwa kusema, “Ewe mdudu mla majani, uungapo nzige mkono...” Mtindo huu wa mazungumzo unamwezesha kuangazia maudhui ya udikteta, ulafi na ubinafsi kama tulivyochanganua katika sehemu ya maudhui. Mtindo huu ndio unaoonyesha usasa katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

3.3.6.6 Mgao wa Kitamthilia

Katika utunzi wa tamthilia, ni kaida ya kimuundo kupata kisa kimegawanywa katika maonyesho au sehemu. Kwa mfano, tamthilia ya *Hukumu* (1992) sehemu ya utangulizi ina onyesho la 1, onyesho la 2 hadi onyesho la 5. Hata hivyo, mshairi licha ya kutunga mashairi yake katika beti au vifungu, anaamua kugawa baadhi ya mashairi yake katika sehemu mahsusi kwa kutumia nambari. Huu ni mtindo wake pia kwa sababu ana uhuru wa kujieleza. Katika baadhi ya mashairi anagawa mashairi kwa kutumia nambari I, II na III ilhali kwingine anatumia nambari 1, 2, 3 na kadhalika.

Kithaka wa Mberia anatumia nambari I, II katika shairi “Mgunga Shambani” (uk. 20) katika *Mchezo wa Karata*. Shairi hili linaangazia maudhui ya ukoloni na ukoloni mamboleo. Katika sehemu ya kwanza mshairi anasema:

I
Huko zama za nyuma
Kwenye shamba letu la mawele
Kulistawi gongo la mgunga
Ambalo kwa miiba myeupe
Lilituchoma michomo mikali (uk. 20)

Dondoo hili linaonyesha namna wakoloni waliingia katika nchi ya Kenya na kutawala wenyeji. Wenyeji walianza harakati za kumwondoa mkoloni na hatimaye wakafaulu na kusherehekea kwa shangwe. Katika sehemu ya pili, mwandishi anaeleza vile muda ulisonga baada ya kupata uhuru. Anasema:

II
Mafungia nyama yakawadia
Kisha jogoo wakawika
Mafungia nyama yakawadia
Kisha jogoo wakawika... (uk. 21)

Baada ya muda mrefu kupita, wananchi walianza kuona kuwa utawala mpya hauna tofauti na utawala wa mkoloni. Ndiposa mshairi anasema katika sehemu ya tatu:

III

Pale tulipong'oa mgunga
Palistawi mti mwingine
Michomo ikatuliza machozi
Mithili zama za nyuma (uk. 21)

Kwengineko, katika shairi “Papa” (uk. 45) katika diwani hii pia, mwandishi anazungumzia kuhusu kiongozi dhalimu (papa). Uongozi wake unadhulumu watawaliwa katika sehemu ya kwanza. Katika sehemu ya pili, wananchi (samaki) wanavuta pamoja na kumshambulia papa. Katika sehemu ya tatu, wananchi wanaimba nyimbo za furaha kwa sababu ya kumshinda kiongozi dhalimu. Mwandishi anaeleza:

...Papa, mkali kama mauti
Anahangaisha samaki
Kwa ndaro na maringo
Daima akijigamba
Kwamba baharini
Haupo uwezo unaomtisha
Wala tisho linalomweza ... (uk. 45)

Katika sehemu ya pili, mshairi anaeleza kuhusu juhudi zinazochukuliwa na wananchi wanaodhulumwa ili kumng'oa mamlakani kiongozi huyo dhalimu. Anasema:

Kama kwa sumaku
Samaki wanavutwa pamoja
Na nyuma ya ngao ya umoja
Wanaenda mwendo wa mbele
Wakiimba nyimbo zenye cheche (uk. 45)

Katika sehemu ya tatu, mwandishi anaeleza furaha waliyo nayo watawaliwa baada ya kumshinda kiongozi anayewadhulumu. Anasema:

Sasa, baharini
Nyimbo za ufanisi
Zinapaa angani... (uk. 46)

Kwengineko, katika diwani ya *Bara Jingine*, kuna mashairi “Jumapili ya Damu” (uk. 6) na “Bara Jingine” (uk. 10) ambayo yamegawanywa katika sehemu ya I, II, III na IV. Shairi “Jumapili ya Damu” linazungumzia juu ya jaribio la kumbandua mamlakani kiongozi dhalimu pia. Jaribio hilo halifaulu kwa sababu majeshi ya kiongozi huyo yanadhibiti hali baada ya watu wengi kuuawa.

Shairi “Bara Jingine” limegawanywa katika sehemu ya I, II, III na IV. Shairi hili linazungumzia juu ya matumaini na ndoto ya kuwa na bara jipya. Bara ambapo

mabunge hayatakuwa kumbi za ulafi wa wabunge, hakutakuwa na ulafi, ufiadi, magonjwa, mapigano miongoni mwa nchi na njaa kati ya changamoto nyingine nyingi. Mwandishi pia amegawa shairi “Zimwi la Theluji” (uk. 48) katika diwani ya *Rangi ya Anga*. Ameligawa katika sehemu akitumia nambari ya 1 hadi 9. Mshairi anaeleza namna wageni walikuja barani Afrika wakati wa ung’ang’aniaji na ugavi wa bara la Afrika. Wageni hao ni Waarabu, wamishenari na wakoloni. Msanii anaonyesha athari za wageni hawa kwa wenyeji kama vile utumwa, unyakuzi wa rasilimali zao, dini, elimu ngeni na ukoloni mamboleo.

3.3.6.7 Shairi-picha

Shairi-picha ni shairi ambalo linachukua umbo la kitu fulani ambacho mshairi anaeleza juu yake. Shairi-picha ni mtindo mpya wa ushairi huru katika ushairi wa Kiswahili. Kithaka wa Mberia anatumia shairi-picha anapozungumzia juu ya maudhui ya uongozi mbaya katika shairi “Dau Haliendi!” (uk. 32) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*.

limo ingawa
 mbioni,
 hili
 dau,
 la
 kusafiria
 mamilioni,
 haliendi;
 huu
 ni
 mwendo
 duara-
 unaduru,
 ni
 mwendo
 mzunguko-
 unazunguka.
 mwendo
 mpeto-
 unaopeta,
 hauwi
 safari,
 bali,
 hupumbazika
 mamilioni,
 kwamba
 wanasafiri,
 katika
 bahari ya miaka

Shairi hili limechukua umbo la “dau” ambalo linaelea baharini likiwa na mamilioni ya wasafiri yaani wananchi. Dau ni sitiari ya nchi inayoongozwa na kiongozi (rais) na wasaidizi ambao hawamakiniki katika uongozi wao. Dau lenyewe haliendi kwa sababu ni “mwendo-duara unaduru, ni mwendo-mzunguko” ambapo mamilioni hupumbazika kwamba wanasafiri katika bahari ya miaka. Hii ina maana kuwa nchi haiwezi kupiga hatua zozote kimaendeleo kutokana na uongozi mbaya. Kwa hivyo, kimtindo, shairi hili linachangia maudhui kueleweka kwa sababu linajenga picha ambayo inamsaidia msomaji kuelewa kuhusu uongozi mbaya.

3.3.6.8 Msamiati Teule

Msamiati ni jumla ya maneno yanayotumiwa katika lugha fulani. Ingawa Kithaka wa Mberia anatumia maneno ya Kiswahili kujieleza, inaonekana kuwa anafanya uteuzi

wa msamiati kwa makini na kimakusudi ili apitishwe ujumbe kwa njia inayomgusa, kumnasa na kumwathiri msomaji. Anatumia uteuzi huu pia kutia ladha kazi yake. Katika nadharia ya elimumitindo, kuna dhana kuwa mtindo ni uteuzi. Kauli hii ina maana kuwa msanii hawezi kutumia rasilimali ya lugha yote iliyoko. Lazima atee maneno machache kutoka ujumla lugha yatakayomsaidia kupitisha ujumbe wake kwa hadhira kwa njia ya mnato.

Mshairi anachota msamiati wake kutoka kwa mazingira anayoandikia hasa kuhusiana na wanyama, wadudu na mimea. Kwa mfano, mwandishi anapoangazia maudhui ya udikteta katika baadhi ya viongozi wa mataifa ya Afrika, anatumia msamiati kama “sisimizi” (uk. 27), “konokono” (uk. 33), “yangeyange” (uk. 41), “papa” (uk. 45) na “simba” (uk. 56) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Maneno “sisimizi”, “konokono” na “yangeyange” yanarejelea wanyonge au wananchi wa kawaida wasio na uwezo. Kwa upande mwingine, maneno “papa” na “simba” yanarejelea viongozi dhalimu wanaotumia uwezo na mamlaka yao kukandamiza wanyonge. Kwa hivyo, maneno haya japo ni ya kawaida yanamfikirisha msomaji ili kupata ukweli fulani kuhusu kile anachosema mshairi.

Fauka ya hayo, akigusia maudhui ya ulafi na unafiki wa wanasiasa, mshairi anatumia maneno kama “ndoto” (uk. 1), “karata” (uk. 18), “mazimwi” (uk. 18), “mazigazi” (uk. 23) na “karamu ya nzige” (uk. 35). Neno “ndoto” linatumika kuonyesha ama matumaini au ukosefu wa matumaini. Akionyesha uwepo wa matumaini, anaeleza kuwa ipo siku uovu utashindwa na wema kutamalaki. Mazimwi ni neno linaloashiria tamaa na ulafi wa wabunge au wanasiasa sawa na nzige ambao wanakula majani ya mimea na miti bila kubakisha kitu. Isitoshe, mshairi anapozungumzia ukoloni na ukoloni mamboleo anatumia neno “mgunga” (uk. 20) ambao ni mti wa kiasili wenye miiba inayochoma sana. Aidha, kuna matumizi ya neno “vitimbakwiri” (uk. 12) katika *Msimu wa Tisa* akizungumzia juu ya wanasiasa kumaanisha watu ambao wanatumia vyeo vyao kujipatia faida fulani binafsi bila ya kufuata kanuni za nchi.

3.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumechanganua maudhui ya siasa, utawala na mamlaka kwa kina kwa kutumia nadharia ya baadaukoloni. Maudhui yaliyochanganuliwa ni pamoja na unafiki na tamaa katika siasa, udikteta, ukoloni mkongwe, ukoloni mamboleo, changamoto zinazokabili mataifa ya Afrika pamoja na ujenzi wa jamii mpya.

Tumeonyesha namna maudhui hayo yanadhihirika katika nchi ya Kenya alikokulia mwendishi na mataifa mengine ya Afrika na kuthibitisha kuwa usasa unaopatikana katika ushairi wa Kithaka wa Mberia ni mambo yanayoshuhudiwa katika nchi ya Kenya, bara la Afrika na kwingine duniani. Kwa kiasi fulani, imebainika kuwa mshairi anachochewa na mfumo mbaya wa siasa, utawala na uongozi duni kutunga mashairi yanayokashifu siasa za unafiki na ukandamizaji zisizoleta maendeleo. Aidha, anachochewa na madhila ya ukoloni kuonyesha namna hali ya sasa ya Kenya na Afrika inatokana na historia.

Hali kadhalika, tumeangazia mtindo alioutumia mshairi kuwasilisha maudhui kwa msomaji kwa kutumia nadharia ya elimumitindo mkabala wa uhakiki mpya. Tumeangazia vipengele vya kimtindo vilivyotumiwa na mshairi anapogusia maudhui mbalimbali hasa vipengele vinavyohusu matumizi ya lugha na mbinu nyingine za kisanaa. Baadhi ya tamathali za lugha zilizochanganuliwa ni sitiari, tashibihi, tashihisi, chuku na maswali ya balagha. Kwa upande mwingine, mbinu za kisanaa zilizoangaziwa ni kama taswira, takriri, usimulizi, nyimbo, mazungumzo, muundo wa tamthilia, shairi-picha na msamiati teule.

SURA YA NNE

UHARIBIFU NA UHIFADHI WA MAZINGIRA

4.1 Utangulizi

Mazingira ni jumla ya vitu vinavyomzunguka kiumbe katika maisha yake. Binadamu hutagusana na mazingira katika shughuli zake za kila siku. Aidha, yeye hutegemea mazingira kujiendeleza kimaisha. Baadhi ya vipengele muhimu vya mazingira ni ardhi, hewa, maji, miti, mimea na wanyama wa aina mbalimbali. Katika harakati za kutumia mazingira, binadamu huharibu mazingira yake. Uharibifu huu huleta madhara makubwa kama vile mmomonyoko wa udongo, kiangazi, njaa, kuongezeka kwa joto, magonjwa na vifo vya watu na wanyama. Kwa jinsi hiyo, binadamu huwa chanzo cha maangamizi yake mwenyewe. Lakini mazingira yanapotunzwa vizuri, yanakuwa na manufaa tele kwa binadamu, miti, wanyama na viumbe wengine. Kwa hivyo, kuna umuhimu wa kuhifadhi na kutunza mazingira kwa kizazi cha sasa na kizazi kijacho. Katika sura hii, tumeangazia uharibifu na uhifadhi wa mazingira pamoja na mtindo uliotumiwa na mshairi kueleza maudhui yanayohusu mazingira.

4.2 Maudhui

Maudhui yanayoangaziwa katika sura hii yamegawanywa katika sehemu mbili: kuna maudhui kuhusu uharibifu wa mazingira na maudhui yanayorejelea umuhimu na manufaa ya kutunza mazingira. Maudhui haya yamechanganuliwa kwa kutumia mihimili ya nadharia ya baadaukoloni. Maudhui haya yanajitokeza katika nchi zilizojikomboa kutoka kwenye minyororo ya ukoloni. Kwa hivyo, athari fulani zilizorithiwa kutoka ukoloni mkongwe zimejitokeza katika maudhui yanayozungumziwa na mshairi.

4.2.1 Uharibifu wa Mazingira

Katika sehemu hii, maudhui tunayoyaangazia kuhusiana na uharibifu wa mazingira ni pamoja na ukataji wa miti, mbinu mbaya za kilimo, uchafuzi wa maji ya mito na mabwawa, uharibifu wa ardhi kupitia uchimbaji wa migodi, uchafuzi wa hewa na uharibifu wa utandu wa ozoni.

4.2.1.1 Ukataji Kiholela wa Miti

Miti ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Miti husaidia katika shughuli ya kujenga nyumba, hutoa na kusafisha hewa, huzaa matunda, hutoa kivuli, hukinga

nyumba na mimea shambani dhidi ya upepo mkali, husaidia kutengeneza dawa, kutengeneza samani za nyumba, kutengeneza karatasi na kupamba mandhari. Lakini ukataji wa miti kiholela huleta hasara kubwa kwa wanadamu na wanyama wengine. Baadhi ya mashairi yanayoelezea maudhui juu ya madhara ya ukataji miti kiholela katika diwani ya *Bara Jingine* ni “Jinamizi” (uk. 55) na “Mikoma” (uk. 66). Katika shairi “Jinamizi”, mshairi anaeleza vile watu wenye tamaa na ubinafsi wanavamia msitu na kukata miti ili wapate mashamba ya kulima na mbao za kujengea. Anaeleza:

Kaumu ya watu
Ikibeba shoka
Panga kali
Na misumeno inayonguruma
Ilikuwa kwa mawimbi
Na bila huruma
Ikachinja miti
Na kunyonga chemchemi
Ikiimba nyimbo
Za mashamba na mbao (uk. 55)

Katika dondoo hili, watu wanapokata miti na kuharibu vyanzo vya maji madhara yake yanakuwa wazi. Ukataji miti unaacha ardhi uchi, ikachomwa na jua kali kisha kunatokea vumbi. Mvua inaponyesha, udongo unasombwa na maji kwa urahisi. Aidha, nyasi hazimeji na mimea haistawi mashambani. Hatimaye kunakuwa na joto kali na ukosefu wa chakula kwa mifugo na binadamu. Ukosefu wa chakula pia unasababisha vifo vya mifugo na binadamu. Kitendo cha ukataji miti na kuharibu chemchemi za maji kwa nia ya kupata mashamba na mbao ni mhimili mmoja wa nadharia ya baadaukoloni unaonyesha upanuzi na ulafi wa kiuchumi katika historia ndefu ya ubeberu na ukoloni. Maudhui ya ukataji miti yamejitokeza tena katika shairi “Wanda” (uk 27) sehemu ya sita katika diwani ya *Rangi ya Anga* ambapo mtunzi anaeleza:

Kama si makali ya panga
Kwa ujeuri na ukatili
Kuhujumu mashina ya miti,
Kingo za mito na vijito
Miinuko ya vilima
Na miteremko ya mabonde
Bado yangekuwa na ngao
Za kulinda afya ya udongo... (uk. 35)

Katika dondoo hili, ukataji wa miti huchangia kingo za mito, vijito, miinuko ya vilima na miteremko ya mabonde kukosa nguvu za kuzuia mmomonyoko wa udongo. Mwandishi anashtumu tabia ya watu kukata miti bila kujali madhara mengi yanayofuatia. Ndio maana anahamasisha watu kuacha tabia ya kutojali katika shairi “Mikoma” (uk. 66) katika diwani ya *Bara Jingine* anaposema:

Hili pambo la ardhi
Hizi nakshi za maumbile
Huu urithi azizi
Leo umesimama ukingoni
Mwa shimo la maangamizi
Na bado hatujazinduka
Kutoka usingizi mnono
Wa kutojali (uk. 66)

Katika kifungu hiki, mshairi anazungumzia tabia ya wagemaji, wasonga mizinga na wakulima ambao wanakata miti ya aina ya mikoma katika maeneo ya Igaironi, Irarani, Kirukuma na Kaguma katika eneo la Meru. Anaonya kuwa ukataji wa mikoma unatishia kuangamiza miti hiyo lakini wenyeji hawajafahamu hatari hiyo.

Kwengineko, nchini Kenya, kumewahi kutokea hali ya ukataji miti kiholela. Kwa mfano, kuna watu waliovamia msitu wa Mau katika eneo la Narok kwa lengo la kutengeneza makao, kupata mashamba ya kulima na kuchoma makaa ya kuuza ili kujipatia riziki. Watu hao walikata miti kiholela katikati ya msitu. Kutokana na kitendo chao, hali ya anga ilianza kubadilika. Kiangazi kilianza kushuhudiwa maeneo hayo. Wakati mvua ya masika iliponyesha, wakaazi wa nyanda za chini waliathirika pakubwa kutokana na mmomonyoko wa udongo. Maji ya mvua yalisomba mimea mashambani na mito ikavunja kingo zake. Ilibidi serikali kuchukua hatua za dharura kufurusha watu waliovamia na kuharibu msitu kwa nia ya kuuhifadhi usiharibiwe zaidi kwa vile ni chanzo cha maji katika eneo la Bonde la Ufa. Ilibidi watu hao watafute makao mbadala. Aidha, kuna watu walionyakua msitu wa Karura uliopo kaskazini mwa jiji la Nairobi kwa sababu ya kutengeneza makao. Watu hao walifurushwa kutoka humo na serikali na miche ikapandwa kama njia ya kuuhifadhi pia.

4.2.1.2 Mbinu Mbaya za Kilimo

Mwandishi vilevile ameangazia namna mbinu mbovu za kilimo zimechangia uharibifu wa mazingira. Ufugaji wa mifugo wengi unaathiri mazingira kwa vile wanyama hao wanakula nyasi na kuacha udongo ukiwa bila kinga. Aidha, kwato za mifugo zinasaga udongo na kuufanya kuwa mwepesi rahisi kusombwa na maji ya mvua. Isitoshe, kulima kandokando ya mito na maeneo yenye miinuko kunachangia mmomonyoko wa udongo. Mshairi anatumia kumbukumbu zake za utotoni kuangazia vile mbinu za kilimo zisizofaa zimeathiri mazingira ambayo yalikuwa yanapendeza lakini leo hii makovu mengi yamejaa kwenye ardhi. Katika shairi “Wanda” (uk. 27) sehemu ya nane katika diwani ya *Rangi ya Anga* anasema:

Ewe Thanantu!
Sahibu wa utotoni!
Nikikumbuka daima
Kwa kumbukumbu pendezi,
Ewe rafiki niliyeamini,
Mikono ya kilimo hasiri
Na kwato za ufugaji shakiri
Zimekugofua, zimekurembua (uk. 41)

Mtunzi anakereka moyoni akiona vile mazingira yaliyokuwa yakivutia wakati mmoja yamehasiriwa na watu waliokata miti, kulima kwenye vilima na kwenye kingo za mito ambapo udongo unasombwa na maji wakati wa mvua na kuacha ardhi ikiwa na makovu ya majabali na mawe tupu. Katika shairi “Wanda” (uk. 27) sehemu ya tisa, katika diwani ya *Rangi ya Anga* anaeleza:

Kibuhuti kinavuma moyoni
Na kuhurumia, ewe Kereka
Mhisani uliyenilea,
Nawasikitikia, enyi Gitugu
Kamwathu
Kaguma ...
Na ahali yenu nzima
Kwa jinsi sura zenu
Zilivyojaa vidonda
Na damu mbichi
Kwenye miinuko ya vilima
Sakafu za mito
Miteremko ya mabonde
Na kandokando mwa njia
Majabali bahili
Na mawe batili
Yameegemeana kwa ndweo ... (uk. 42)

Katika dondoo hili, mshairi ametumia majina ya sehemu halisi mathalani Kereka, Gitugu, Kamwathu, Kaguma, Kamanyaki kudhihirisha sehemu halisi zilizoathirika na mbinu mbovu za kilimo. Japo ametumia majina hayo ya maeneo halisi, maudhui ya uharibifu wa mazingira yanaafiki kokote kunatokea tatizo hili. Kithaka wa Mberia anaonyesha bayana kuwa mbinu mbovu za kilimo zinachangia uharibifu wa mazingira. Aidha, anaonyesha kuwa ufugaji wa kuhamahama hasa katika maeneo kame ambapo wafugaji wanafuga mifugo wengi wanaokula nyasi na majani wakati wa kiangazi unachangia sana uharibifu wa mazingira. Isitoshe, kwato za mifugo hao zinakanyaga na kupondaponda udongo ambao unalegea. Mvua nyingi inaponyesha, huwa hakuna nyasi za kuuzuia udongo. Udongo unasombwa na maji na kuiacha ardhi bila kinga yoyote. Maji yenye udongo huteremshwa kwenye mito na kuijaza udongo. Polepole, chemchemi za maji zinafunikwa na hatimaye mito inakauka. Mshairi anashauri wakulima watumie mbinu bora za kilimo na vilevile wafanye juhudi za kuzuia mmomonyoko wa udongo hasa kwenye milima na mabonde ili wasiharibu mazingira.

4.2.1.3 Uchafuzi wa Maji ya Mito na Mabwawa

Kuna msemo kuwa “maji ni uhai”. Watu huhitaji maji kwa upishi, kufua nguo, kukata kiu, kuoga, kuzalisha umeme, shughuli anuwai za viwandani na unyunyiziaji mimea mashambani. Aidha, wanyama wa ardhini, majini na miti huhitaji maji. Maji haya yanaweza kuwa ya mvua, visima, mito, maziwa na bahari. Licha ya maji kuwa muhimu, watu huchafua maji kwa njia nyingi. Maji yanapochafuliwa, madhara yake huonekana wazi. Kunazuka magonjwa kwa binadamu, wanyama, miti na mimea shambani. Kwa mfano, katika diwani ya *Bara Jingine* mshairi anazungumzia vile wakaazi wa jiji la Nairobi wanachafua maji katika shairi “Mimi, Mto Nairobi” (uk. 63). Anasema:

Wakaazi wa jiji
Wananikaba koo
Wananiziba pumzi
Wananinyonga
Kwa mafuta
Kwa makopo
Kwa tairi
Kwa talimbo
Na takataka bila ukoo (uk. 63)

Katika shairi hili, mwandishi anaonyesha vitendo vya wakaazi wa Nairobi wanaotupa nguo kuukuu, viatu, makopo, tairi, talimbo, mafuta ya magari, vinyesi na plastiki mtoni bila kujali, kiasi kwamba maji yanageuka rangi yake asilia. Isitoshe, majitaka kutoka mitaa mbalimbali na kutoka viwandani yanaelekezwa katika mto huu na mito mingine. Uchafuzi wa mto Nairobi unakuwa mfano tu wa jinsi wakaazi wa miji wanachafua mito iliyoko katika miji husika humu nchini na kwengineko. Lakini si mito ya mijini tu huchafuliwa, mito ya maeneo ya mashambani pia inachafuliwa kupitia vitendo vya watu kuosha nguo na kumwaga maji machafu mtoni, kuogea mtoni, kwenda haja, kuosha magari, kunywesha mifugo ambao husimama majini, kutupa mizoga ya wanyama mitoni na takataka za kila aina. Watu wanapotumia maji haya yaliyochafuliwa kupikia, kunywa au kuoga; wanapata magonjwa kama homa ya matumbo, kuendesha na kujikuna ngozi. Hali kadhalika wanyama wanakufa na mimea kukauka kutokana na sumu iliyomo kwenye maji yenyewe. Maudhui sawa na haya yanapatikana katika diwani ya *Bara Jingine* katika shairi “Bwawa la Ithanje” (uk. 69). Mshairi anadokeza namna wakulima na shughuli za viwanda vya Limuru zinachafua maji katika bwawa la Ithanje:

Wakulima wanyunyiziao maji
Wanakukamulia sumu kinywani
Navyo viwanda vya Limuru
Vinakushambulia mwili
Kama vikosi hatari
Vikishambulia adui
Katika vita vya kikemikali (uk. 69)

Katika dondoo hili, wakulima wanaharibu maji ya bwawa la Ithanje kutokana na sumu wanapofanya shughuli ya kunyunyizia maji mashamba yao. Maji yenye sumu si salama kwa watu wa eneo hilo katika shughuli za upishi, kunywa na kuoga. Aidha, ni hatari kwa mifugo na wanyama wa majini. Fauka ya hayo, kuna kemikali zinazomiminwa ndani ya bwawa hilo kutoka viwanda vya Limuru hasa kiwanda cha kutengeneza viatu vya *bata* maarufu katika mji wa Limuru. Kemikali hizo vilevile zina madhara makubwa kwa binadamu, wanyama na mimea kwa jumla.

4.2.1.4 Uharibifu wa Ardhi Kupitia Uchimbaji wa Migodi

Watu hutafuta madini mbalimbali kwa sababu ya thamani zake ili kutengeneza mapambo, chuma, pesa, chumvi, saruji, mafuta miongoni mwa mahitaji mengine mengi. Machimbo na migodi huchimbwa na kampuni zenye leseni na watu binafsi ili

kutafuta dhahabu, almasi, mawe ya kuchonga vinyago, madini ya kutengeneza chumvi na saruji. Mashine kubwa na hata vifaa duni hutumika kuchimba ardhi ili kutafuta madini hayo. Maeneo yaliyochimbwa yanaachwa wazi. Wakati mwingine watu wanakufa wakati wa shughuli ya uchimbaji ilhali watu, mifugo na wanyama wengine huanguka kwenye mashimo hayo. Isitoshe, wakati wa mvua, machimbo na mashimo hayo hugeuka kuwa vidimbwi vya maji ambapo mbu huzalia humo na kuambukiza watu ugonjwa wa malaria.

Watu wanapasua miamba kwa baruti ili wapate mawe, changarawe na saruji kwa shughuli za ujenzi. Sehemu zilizopasuliwa au kuchimbwa zinaachwa wazi na ni hatari kwa binadamu na wanyama. Maudhui ya uharibifu wa ardhi ndiyo msanii anazungumzia katika diwani ya *Redio na Mwezi* katika shairi “Johari Bamburi” (uk. 8). Anasema:

Trekta, likinguruma kwa nia thabiti
Linateremsha meno jasiri ya chuma
Na kurarua udongo bila tone la huruma
Na kuacha sura kirihi, picha ya utasa
Kero la macho, bughudha ya moyo (uk. 8)

Katika dondoo hili, mtunzi anaonyesha namna watu huichimba ardhi kwa kutumia mashine kubwa katika harakati za kutafuta madini ya kutengeneza saruji (johari) katika eneo la Bamburi. Baada ya uchimbaji huo, ardhi iliyokuwa nzuri awali inabaki kuwa na sura isiyopendeza macho tena.

4.2.1.5 Uchafuzi wa Hewa

Mwandishi amezungumzia pia namna viwanda vinachangia kuchafua hewa safi kwa kutoa gesi zenye sumu ambazo hupaa angani na baadaye kuathiri mimea mashambani na kuharibu udongo. Mchanganyiko huo wa sumu kali unaharibu mapaa ya nyumba. Fauka ya hayo, mchanganyiko huo wa gesi unaathiri ngozi kwa vile watu huanza kujikuna au kuwa na magonjwa ya ngozi yanayotokana na athari za gesi kutoka viwandani. Isitoshe, msanii anaeleza kuwa gesi hatari husababisha shida ya kupumua miongoni mwa watoto. Ingawa shida hii haitokei mara moja ikaonekana, ni tatizo linalonyemelea watu polepole kutokana na mpito wa wakati na kuleta madhara mengi. Katika diwani ya *Redio na Mwezi* kuna shairi “Kiwanda” (uk. 6) ambapo mwandishi anaelezea hali hiyo hivi:

Bughudha nzito ya hudhurungi
Inafuka kutoka dohani jeuri,
Chembe nyeupe za maangamizi
Zinaelea angani zikichunguza
Kabla ya kushuka na sumu ya siri
Kukaba mimea koo mashambani
Na kuhasi udongo, maji na hewa

Ulimi wa sumu kali ya kemikali
Huramba mapaa ya nyumba
Na kutoboa vitundu katika mabati ...
Msimu wa mvua unapowadia
Sakafu hugeuka mabwawa makuu
Kama makazi mwafaka kwa viboko! (uk. 6)

Moshi kutoka viwandani unaharibu mimea mashambani. Fauka ya hayo, sumu kali inaharibu mapaa ya nyumba ambayo huvuja wakati mvua inaponyesha.

4.2.1.6 Uharibifu wa Utandu wa Ozoni

Mshairi anaeleza kuwa utandu wa ozoni ni muhimu katika kukinga binadamu kutokana na miale hatari ya jua ambayo inaathiri afya ya binadamu. Licha ya umuhimu huu, shughuli za binadamu zinachangia kuharibika kwa utandu huu. Kemikali zenye sumu zinaharibu utandu wa ozoni polepole. Kwa hivyo, kumetokea ongezeko kubwa la joto ulimwenguni. Hali hii ni hatari kwa maisha ya binadamu. Mapema mwaka wa 2016, marais kutoka mataifa mbalimbali ya ulimwengu walikongamana mjini New York, Marekani. Ajenda yao kuu ilikuwa ni kuweka mikakati ya kutafuta suluhu kwa ongezeko la joto ulimwenguni linalotokana na uharibifu wa utandu wa ozoni. Mataifa yaliyostawi kiviwanda yanayochangia pakubwa kutoa gesi na kemikali zenye sumu angani yalikusika katika kongamano hilo. Ili kuonyesha madhara ya uharibifu wa utandu wa ozoni katika diwani ya *Bara Jingere* kuna shairi “Ngao” (uk. 59) ambapo mshairi anasema:

Kemikali jeuri
Zinatafuna ozoni
Kama majeshi ya mchwa
Yaliyovamia paa
La kombamoyo...

Ole sisi binadamu!
Kwa teknolojia jeuri
Tunakulegeza afya
Huku adui mauti
Akituangalia
Tayari kutushambulia (kur. 59-60)

Katika shairi hili, mtunzi anaeleza kuwa kuna janga linalotunyemelea utandu wa ozoni unapoendelea kuharibiwa kupitia kemikali hatari. Analaumu binadamu wanaotumia teknolojia kulegeza utendakazi wa ozoni na hivyo hatima ni mauti yanayomnyemelea binadamu.

Kwa misingi ya nadharia ya baadaukoloni, uharibifu wa mazingira ni maudhui yanayoshuhudiwa katika mataifa mbalimbali ulimwenguni baada ya ukoloni mkongwe. Upanuzi na ulafi wa kiuchumi ni baadhi ya mambo yanayochangia uharibifu wa mazingira. Ukataji miti, mbinu mbaya za kulimo, uchafuzi wa maji, uharibifu wa ardhi kupitia uchimbaji wa migodi, uchafuzi wa hewa na uharibifu wa utandu wa ozoni ni matokeo ya vitendo vya mwanadamu katika mataifa huru baada ya kujinyakulia uhuru kutoka kwa wabeberu.

4.2.2 Uhifadhi wa Mazingira

Baada ya kuchanganua namna binadamu anaharibu mazingira, ni muhimu kuangazia vile mwandishi anahamasisha na kuhimiza watu kuhifadhi mazingira. Mazingira yaliyotunzwa vizuri yanapunguza visa vya magonjwa kwa wanadamu, miti na wanyama. Vilevile, mazingira yaliyohifadhiwa vyema yanakuwa mandhari pendezi kwa macho mbali na kuwa kivutio kwa watalii wanaochangia kuimarisha uchumi wa nchi kutokana na biashara, fedha za kigeni na nafasi za kazi. Vyakula na matunda mbalimbali yanatokana na utunzaji wa mazingira. Miti huzuia udongo usibebwe na maji wakati wa mvua. Aidha, miti inazuia nguvu za upepo zisiharibu mimea mashambani, kubomoa mapaa ya nyumba licha ya kutupatia hewa safi ya kupumua na mandhari tulivu ya kupumzikia. Pale mazingira yametunzwa vizuri, mwandishi anasifu hatua hiyo kwa kuonyesha matokeo mazuri yanayotokana na uhifadhi wa mazingira.

Katika diwani ya *Bara Jingine* katika shairi “Nyeri” (uk. 70), mshairi anaeleza juu ya mandhari ya kijani kibichi ya majani-chai, mikahawa, migomba na miti. Anafurahia kuona kampeni ya kupanda miti kwenye milango ya nyumba na vituo vya umma ili kuonyesha mipaka ya mashamba. Anaeleza:

Nimeona mashamba nadhifu
Yakifurika rangi ya kijani;
Nimeona mikahawa na majani-chai
Na migomba na ng’ombe bila pembe...

Lakini pia
Kwenye milango ya nyumba
Kwenye vituo vya umma
Nimeona tangazo
Kwa busara likishawishi
Onyesha mpaka wa shamba
Kwa miti (kur. 70-71)

Tangazo la kupanda miti ni njia moja ya kuhifadhi mazingira. Miti inapopandwa inatoa mandhari ya kuvutia, vivuli, inavutia mvua, kuzuia upepo mkali unaoharibu mimea na mapaa ya nyumba, kuonyesha mipaka ya mashamba na kutoa matunda miongoni mwa manufaa mengi.

Mtunzi anakariri umuhimu wa kukarabati ardhi iliyoharibiwa ikapendeza macho na ikawa kitega uchumi kutokana na shughuli za kitalii. Kwa mfano, katika shairi “Johari Bamburi” (uk. 8) katika diwani ya *Redio na Mwezi*, mshairi anaonyesha mabadiliko makubwa ya kimazingira katika eneo la Bamburi lililoharibiwa wakati mmoja kutokana na uchimbaji wa madini ya kutengeneza saruji. Baada ya miti ya kila aina kupandwa, eneo hilo linavutia wenyeji na wageni, linaletea faida kampuni ya saruji mbali na kuwa kivutio cha watalii. Mshairi anaeleza:

Ardhi ambayo jana, kwa ujeuri
Kwa udongo uchi na vipele kirihi
Iliudhi macho na kuchoma moyo
Sasa ni chemchemi safi ya uhai
Sumaku kwa wenyeji na wageni
Hazina kwa kampuni ya saruji...

Milolongo ya wageni kutoka mbali
Furaha ikiwadundadunda kama muziki
Wanatazama choroa, swara na kuro
Na kuajabia kiboko, mamba na twiga... (kur. 8-9)

Katika dondoo hili, mtunzi anazungumzia ile bustani iliyotengenezwa na kampuni ya saruji ya Bamburi ambapo watu hulipa ada fulani ili kuingia na kujivinjari na kuangalia wanyama wa aina mbalimbali.

Katika shairi “Mkalitusi” (uk. 67) katika diwani ya *Bara Jingine*, msanii anaeleza manufaa ya kupanda miti ya aina ya mikalitusi. Anaonyesha kuwa mikalitusi inapamba mandhari, mizizi inazuia udongo usisombwe na maji ilhali majani

yanasafisha hewa. Aidha, mikalitusi inatumiwa kutengeneza dawa ya kuimarisha afya ya mwanadamu. Isitoshe, mikalitusi inasaidia kuonyesha mipaka ya mashamba mbali na kutoa mbao za ujenzi. Hata hivyo, anaonyesha kuwa licha ya sifa nzuri za mikalitusi, inanyonya maji na kufanya watu wakose maji.

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi “Ol Karia” (uk. 64) linazungumzia umuhimu wa nishati inayotoka udongoni ambayo inasaidia kuzalisha umeme unaosaidia maseremala kutengeneza samani, mafundi kutengeneza milango na madirisha na kuendesha mitambo viwandani. Katika shairi “Mwea” (uk 70), mshairi anaeleza mandhari ya kupendeza ya eneo la Mwea ambako kuna mandhari ya kijani-kibichi na mara rangi ya dhahabu kurejelea shughuli za wakulima wanaopanda mpunga ili kuvuna mchele wa kulisha taifa. Mandhari ya mpunga ya rangi ya kijani-kibichi na mpunga uliokomaa wenye rangi ya dhahabu ni mandhari yanayopendeza macho.

Kwengineko, katika shairi “Ntharene” (uk. 74), mshairi anasifu mandhari ya kituo cha Ntharene cha kuuzia bidhaa kutoka mashambani katika eneo la Meru. Wakulima ambao ni wanakijiji wanauza bidhaa kama mapapai, nyanya, parachichi, viazi vikuu na viazi vitamu pamoja na mikungu ya ndizi. Haya ni mazingira yanayopendeza kutokana na juhudi za kutunza na kuhifadhi mazingira.

4.3 Mtindo Katika Uharibifu na Uhifadhi wa Mazingira

Mtindo ni namna msanii anatumia lugha na mbinu nyingine za kisanaa kujieleza katika kazi ya kifasihi. Katika nadharia ya elimumitindo, kuna dhana kuwa mtindo ni njia ya kujieleza. Katika sehemu hii tumeangazia tamathali za semi na mbinu za kisanii alizotumia mshairi katika kufafanua maudhui kuhusu uharibifu na uhifadhi wa mazingira katika ushairi wake. Baadhi ya tamathali ambazo tumeangazia vile zimetumiwa na mshairi pamoja na umuhimu wake ni kama vile tashibihi, tashihisi, maswali ya balagha, ritifaa na chuku. Mbinu nyingine za kisanaa alizotumia ni pamoja na usambamba, usimulizi, wimbo, takriri, ndoto na msamiati teule.

4.3.1 Tashibihi

Mtunzi anapoeleza athari za ukataji miti anatumia tashibihi katika shairi “Jinamizi” (uk. 55) katika diwani ya *Bara Jingine*. Anaonyesha picha ya namna wanyama

wanataabika kutembea njiani kwa sababu ya kiangazi na ukosefu wa malisho. Anaeleza:

Katika vijiji
Ng’ombe, kondoo na mbuzi
Walibadilika sura
Na kuwa mafupa
Yanayojisukuma njiani
Kama makobe makongwe (uk. 57)

Ili kupata picha halisi ya mwendo wa mifugo waliokonda na kudhoofika sana, mshairi anafananisha mwendo wao wa polepole njiani kama wa kobe wakongwe. Sura ya hali hii inanata vizuri na kuathiri msomaji kuona ukweli halisi wa sura na mwendo unaotisha uliotokana na athari ya kiangazi. Vilevile, katika ubeti mwingine anasema kuwa “**Mazizini na njiani, yaliangukiana magombe kama majani makavu, yakiangushwa na upepo majira ya mpukutiko**” (uk. 57). Analinganisha ng’ombe wanaoanguka njiani sawa na majani makavu yanayoangukushwa na upepo wakati wa kiangazi. Hiyo ni sura ya kutisha inayovuta huruma kwa msomaji.

Mtunzi anatumia tashibihi kueleza mandhari juu ya uharibifu wa utandu wa ozoni kupitia teknolojia. Utandu wa ozoni unamkinga binadamu dhidi ya miale hatari ya jua. Utandu huu unapoharibiwa basi mwanadamu anakuwa katika hatari ya kuangamia kupitia ongezeko la joto na ugonjwa wa saratani ya ngozi. Mshairi katika diwani ya *Bara Jingine* katika shairi “Ngao” (uk. 59) anaeleza:

Kemikali jeuri
Zinatafuna ozoni
Kama majeshi ya mchwa
Yaliyovamia paa
La kombamoyo (uk. 59)

Mwandishi analinganisha kemikali na majeshi ya mchwa ili kuleta ile sura ya kuharibiwa kwa utandu wa ozoni bila tahadhari. Utandu wa ozoni ni ngao inayotulinda dhidi ya miale ya jua yenye sumu kwenye ngozi na mwili. Ulinganishi huu unaonyesha uharibifu wa ozoni kwa kasi kubwa kama vile mchwa wanavyoharibu gogo la mti. Kwa hivyo, maelezo hayo yanamsaidia msomaji kupata taswira ya namna ozoni inaharibiwa.

Kwengineko, mwandishi anafafanua namna bwawa la Ithanje linaharibiwa kutokana na sumu ya wakulima wanyunyiziao maji mashambani ili kukuza vyakula pamoja na kemikali kutoka viwanda katika mji wa Limuru. Anasema katika shairi “Bwawa la Ithanje” (uk. 69) kuwa “**Polepole, afya yako inafifia kama mgonjwa wa kifua kikuu**”. Mshairi anafananisha kuharibiwa kwa bwawa la Ithanje na mgonjwa anayeugua kifua kikuu. Ulinganishi huu unaonyesha bayana vile uzuri wa bwawa la Ithanje unaharibiwa na shughuli za wakulima na wenye viwanda wasiojali huko Limuru. Licha ya kuwa bwawa hilo ni muhimu kwao, wanaliharibu kwa sumu na majitaka. Baadaye wanajuta wenyewe kwa vitendo vyao.

Katika shairi “Thagicu” (uk. 61) katika diwani hii pia, mtunzi anaeleza jinsi eneo la Thagicu lenye mabonde limeharibiwa mpaka likabaki na mchanga mweupe na mawe tupu. Anatumia tashibih hivi:

Thagicu
Ninapona Koonyo na Siili
Mwanianga na Kiujo
Macho ya moyo wangu
Hudondokwa na machozi
Kama ya mtoto... (uk. 61)

Mwandishi analinganisha macho ya moyo wake kudondokwa na machozi sawa na machozi ya mtoto mchanga anayelilia mzazi wake. Ulinganishi huu unaleta taswira fulani na vilevile unaonyesha huzuni nyingi iliyo moyoni mwa mtunzi anapona uharibifu usio na kifani wa ardhi katika eneo la Thagicu.

Katika diwani ya *Redio na Mwezi* kuna tashibih katika shairi “Kiwanda” (uk. 6). Mwandishi anaeleza juu ya madhara ya sumu inayotoka kiwandani. Sumu hiyo inadhuru mimea mashambani, udongo, maji na hewa. Isitoshe, kemikali kutoka kiwandani zinatoboa vitundu katika mabati. Vishimo kwenye mabati vinaingiza maji ndani ya nyumba wakati wa msimu wa mvua. Mshairi anasema:

Msimu wa mvua unapowadia
Sakafu hugeuka mabwawa makuu
Kama makazi mwafaka kwa viboko! (uk. 6)

Mshairi ametumia tashibih hii ili kuonyesha picha ya madhara ya kemikali kutoka kiwandani. Sakafu ya nyumba inajaa maji mengi ya mvua ambayo yanafanana na bwawa la maji wanakopenda kukaa viboko.

Katika shairi jingine “Mombasa Mibuyuni” (uk. 72) katika diwani ya *Bara Jingine*, mwandishi anaeleza juu ya mazingira matulivu ambapo watu wanafurahia kubarizi. Anaeleza namna mibuyu imepamba mandhari hayo yakawa ya kuvutia macho. Mtunzi anasema, “**Mibuyu ambayo imesimama imara kama kazi ya fahari ya msanii mahiri**” (uk. 72). Anafananisha kusimama kwa mibuyu na kazi ya fahari ya msanii mahiri ili kumpatia msomaji picha ya mandhari yanayovutia macho. Kwa hivyo, ufananisho huu unafaa katika kuwasilisha maudhui ya mazingira yanayovutia.

Aidha, katika maelezo ya mazingira pendezi katika shairi “Kambi Malindi” (uk.79) katika diwani hii kuna matumizi ya tashibihii. Mwandishi anasimulia safari ya kwenda kupiga kambi Malindi kwa nia ya kujivinjari na kujionea mandhari ya kuvutia. Anasema kuwa, “**Tulifika alasiri, jua lilikuwa na upole kama mama mzazi.**” (uk.79). Mtunzi analinganisha upole wa jua na upole wa mama mzazi. Maelezo haya yanaonyesha kuwa walifika Malindi wakati wa alasiri jua lilikuwa limetulia wala halikuwachoma miili yao. Vilevile, kupitia ulinganishaji huu, mshairi amewasilisha maana kwa njia inayonata akili ya msomaji na kutia ladha maelezo yake.

Kwengineko, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, katika shairi “Wanda” (uk. 27) sehemu ya tisa, kunajitokeza tashibihii. Mwandishi anaonyesha sura mbaya ya mazingira yaliyokuwa pendezi wakati mmoja kwa sababu ya watu kukata miti, kulima kwenye vilima na kwenye kingo za miti. Udongo unasombwa na maji wakati wa mvua na kuacha ardhi ikiwa na makovu ya majabali na mawe tupu. Mtunzi anasema:

Kwenye miinuko ya vilima
Sakafu za miti
Miteremko ya mabonde
Na kandokando mwa njia
Majabali bahili
Na mawe batili
Yameegemeana kwa ndweo
Kama vikao vya nduli
Vikipanga njama ya mauti (uk. 42)

Mwandishi analinganisha majabali na mawe na vikao vya nduli wanaopanga kusababisha kifo. Hii ni taswira ya athari mbaya za uharibifu wa mazingira. Mwishowe, madhara haya yanampata mwanadamu mwenyewe.

4.3.2 Tashihisi

Tashihisi ni tamathali ya usemi inayohusu uhusisho na ulinganisho pia lakini inakamatana na haja ya mwanadamu kuvihusisha vitu visivyo na uhai na vitu vyenye uhai, hasa binadamu mwenyewe (Mohamed 1995). Kwa hivyo, katika tashihisi, kitu kisicho na uhai au kisicho na sifa za kibinadamu, kinapewa sifa, tabia au matendo ya kiuhai ya kibinadamu. Tashihisi ina umuhimu wa kuvitia nguvu na harakati vitu ambavyo kwa kawaida ni vitulivu. Kwa kuvitia uhai vitu hivyo, mwandishi anavifanya vionekane katika taharuki na mwendo wa picha mbalimbali. Katika hali hiyo, tashihisi inaweka wazi zaidi maana na kuimarisha usanii unaotakikana.

Mwandishi ametumia tashihisi kwingi sana katika mashairi yanayohusu uharibifu na uhifadhi wa mazingira. Kwa mfano, katika diwani ya *Bara Jingere* ambapo anaangazia maudhui ya uharibifu na uhifadhi wa mazingira, tunaweza kuthibitisha matumizi ya tashihisi katika mashairi mbalimbali. Katika shairi “Jinamizi” (uk. 55) mwandishi anaeleza vile watu wengi walikuja na mashoka na mapanga makali kukata miti ili kupata mashamba na mbao. Anatumia tashihisi anaposema, “**Kaumu ya watu ikibeba shoka, panga kali na misumeno inayonguruma**” (uk. 55). Kawaida simba ndiye ananguruma akiwa msituni. Lakini mtunzi anaposema “misumeno inayonguruma” anamaanisha misumeno ya kisasa inayoendeshwa kwa injini na inatoa sauti kali inapowashwa kwa ajili ya kukata miti au kupasua mbao.

Katika shairi “Ngao” (uk. 59) katika diwani hii ya *Bara Jingere*, mshairi anaeleza namna mwanadamu anachangia kuharibu utandu wa ozoni pamoja na athari inayomkodolea macho kutokana na uharibifu huo. Mwandishi anatumia tashihisi kueleza hali hiyo hivi:

Kemikali jeuri
Zinatafuna ozoni
Kama majeshi ya mchwa
Yaliyovamia paa
La kombamoyo...

Ole sisi binadamu!
Kwa teknolojia jeuri
Tunakulegeza afya
Huku adui mauti
Akituangalia
Tayari kutushambulia (kur. 59-60)

Mara nyingi mwanadamu ndiye huwa na ujeuri na uwezo wa kutafuna kwa sababu ya usemi na vitendo vyake. Lakini katika dondoo hili kemikali na teknolojia zimepewa sifa ya ujeuri na uwezo wa kutafuna ili kuweka wazi maana na kuimarisha usanii wa mwandishi. Aidha, ozoni haina afya kama mwanadamu wala mauti hayana uwezo wa kuangalia. Lakini mshairi anavipatia sifa za kibinadamu kuonyesha maana ya ndani na kuongeza ujumi katika shairi lake.

Katika shairi “Mimi, Mto Nairobi” (uk. 63) kuna matumizi ya tashihisi. Msanii anazungumzia namna wakaazi wa jiji la Nairobi wanachafua maji ya mto Nairobi kwa kutupa mafuta, makopo, tairi, karatasi za plastiki na matambara ndani yake. Anasema:

Wakaazi wa Nairobi
Wakanikaba koo
Wananiziba pumzi
Wananinyonga...(uk. 63)

Maneno “Wakanikaba koo, wananiziba pumzi na wananinyonga” yanaonyesha sifa za kiumbe hai. Mto hauna koo, hauna pumzi wala hauwezi kunyongwa kama mtu au kiumbe hai. Lakini kwa kutumia tashihisi hizo, mwandishi anaonyesha wazi jinsi mto huu unachafuliwa na wakaazi ilhali unastahili kutunzwa uwe na maji safi.

Kwengineko, katika shairi “Bwawa la Ithanje” (uk. 69) kuna tashihisi zimetumiwa na msanii. Mwandishi anafafanua jinsi wakulima wanaonyunyizia maji mashamba yao ili kukuza mimea pamoja na wamiliki wa viwanda katika mji wa Limuru wanachafua maji ya bwawa la Ithanje kwa sumu na majitaka. Anatumia tashihisi kurejelea hali hiyo hivi:

Wakulima wanyunyiziao maji
Wanakukamulia sumu kinywani
Navyo viwanda vya Limuru
Vinakushambulia mwili... (uk. 69)

Katika dondoo hili, bwawa la Ithanje limepewa sifa ya kuwa na kinywa ili kuonyesha kuwa sumu inayotoka kwenye unyunyiziaji maji inaingizwa kwenye bwawa hilo. Aidha, viwanda vya Limuru vinapewa sifa ya kushambulia mwili wa bwawa la Ithanje. Bwawa halina mwili. Viwanda vya Limuru vinaelekeza majitaka yenye kemikali na uchafu ndani ya bwawa hilo na kuharibu usafi wa maji katika bwawa hilo. Maji yasipokuwa safi yataletea watu, mifugo na mimea magonjwa.

Anapozungumzia maudhui ya uhifadhi wa mazingira pamoja na mandhari pendezi, mshairi anatumia tashihisi kadha katika diwani ya *Bara Jingine*. Kwa mfano, katika shairi “Mkalitusi” (uk. 67) anaongea kuhusu manufaa yake na mazingira ya kuvutia macho kutokana na upanzi wa mikalitusi. Anaeleza:

Kilele chako
Kinapoongea na anga
Na tanzu zako
Kutuliza hewa hasira,
Shina lako
Linaposimama kwa shani
Na urembo wako
Kupamba mandhari... (uk. 67)

Mwandishi ametumia tashihisi anaposema “kilele chako kinapoongea na anga” kuzungumzia urefu wa mkalitusi. Mkalitusi unapewa sifa ya kuongea kama mwanadamu. Msomaji anapata taswira ya mkalitusi uliochongoka kwenda juu sana kana kwamba unagusa anga. Aidha, anatumia tashihisi anaposema “na tanzu zako kutuliza hewa hasira”. Tanzu za mkalitusi zimepewa sifa ya kutuliza hewa hasira. Isitoshe, hewa kwa kawaida haina hasira kama mtu au kiumbe mwingine hai bali anaonyesha zile nguvu za hewa zinazoweza kuharibu mimea au mapaa ya nyumba. Fauka ya hayo, mwandishi anasema kuwa mikalitusi huonyesha mpita-njia kuwa kilicho shambani si chake na ndiposa anatumia tashihisi kuwa, “**Moyo wangu unakupigia makofi kwa furaha**” (uk. 68). Moyo umepewa sifa ya kupiga makofi ilhali hauna mikono wala viganja vya kupiga makofi. Mwandishi anamaanisha kuwa anafurahi sana moyoni.

Katika shairi “Nyeri” (uk. 70), mtunzi anazungumzia juu ya mandhari ya kupendeza ya majani-chai, kahawa, mahindi na migomba ya ndizi. Anatumia tashihisi anapoongea juu ya rangi ya kupendeza ya kijani-kibichi na kusema, “**Katika mabonde ya miinuko, kijani-kibichi kinatabasamu**” (uk. 70). Kawaida mwanadamu ndiye anatabasamu lakini hapa “kijani-kibichi kinatabasamu” ina maana kuwa rangi ya kijani inapendeza na kuenea kote Nyeri kwa sababu ya kilimo bora na utunzaji wa mazingira.

Mshairi ametumia tashihisi pia katika shairi “Mombasa Mibuyuni” (uk. 72). Anaeleza kuhusu mandhari mazuri ya Mombasa kwa sababu ya miti aina ya mibuyu. Anasema “**Mibuyu ambayo imesahau umri wake imesimama imara**” (uk. 72). Mibuyu imepewa sifa ya kusahau umri kama vile mwanadamu hawezi kukumbuka umri wake. Aidha, katika shairi lili hili la “Mombasa Mibuyuni” mwandishi anaeleza vile ndege wametua juu ya mibuyu wakiimba nyimbo za furaha. Anasema kuwa “**Ndege wakunjufu wanakariri mashairi wakisifia maumbile na rangi nzuri za uhai**”(uk. 72). Kwa hakika ndege hawawezi kukariri mashairi na kusifu maumbile kama mwanadamu. Hii ni sifa tu anawapatia ndege wanaoimba juu ya mibuyu na kuonyesha mandhari yanayovutia.

Kwengineko, katika shairi “Mjakaranda” (uk. 75) tashihisi inajitokeza pia pale ambapo mwandishi anasifu uzuri wa mti wa jakaranda kwa kusema:

Nakumbuka siku ambayo
Macho yetu yalikutana
Nyoyo zetu zikapendana
Mapenzi yakaumana

Nilikuwa Parkview ghorofani
Nawe, katika Jevanje
Ukisimama na wenza
Huku kanzu yako ya urujuani
Ikiimba wimbo mtamu... (uk. 75)

Katika dondoo hili, mti wa jakaranda umepewa sifa ya kuwa na macho, moyo, kusimama na kanzu ya rangi ya urujuani ambayo inaimba. Tashihisi hizi zinatoa mandhari halisi ya kupendeza ya mjakaranda.

Katika shairi “Kambi Malindi” (uk. 79), mtunzi anatumia tashihisi anaposimulia safari yake na wenzake walipoenda kujivinjari katika eneo la Malindi, pwani ya Kenya na kujionea mandhari ya kuvutia anaposema:

Bahari ilitukaribisha
Kwa tabasamu motomoto
Ufukwe ulitupokea
Kwa moyo mkunjufu (uk. 79)

Bahari imepewa sifa ya kukaribisha na kutabasamu kama kwamba ni mwanadamu. Aidha, ufukwe unapewa sifa ya kupokea watu kwa moyo mkunjufu. Sifa hizi zote

anazitoa mwandishi kuonyesha mandhari matulivu walipopiga kambi katika eneo la Malindi.

Kwengineko, katika diwani ya *Redio na Mwezi*, kuna mashairi kadha ambayo yanagusia maudhui ya uharibifu na uhifadhi wa mazingira ambapo tashihisi zimetumika. Kwa mfano, katika shairi “Johari Bamburi” (uk. 8) mwandishi anaeleza vile kampuni ya kutengeneza saruji inaharibu ardhi kwa kutumia trekta ili kutafuta malighafi ya kutengeneza saruji. Anatumia tashihisi kueleza shughuli ya uchimbaji wa ardhi hivi:

Trekta, likinguruma kwa nia thabiti
Linateremsha meno jasiri ya chuma
Na kurarua udongo bila tone la huruma
Na kuacha sura kirihi, picha ya utasa
Kero la macho, bughudha ya moyo (uk. 8)

Mwandishi anasema kuwa “trekta likinguruma” akirejelea ile sauti inayotoka kwa trekta linapolima. Aidha, anaeleza kuwa linateremsha “meno jasiri ya chuma” kurejelea ile sehemu ya trekta ya kutibulia udongo inayofanana na meno ya mwanadamu au wanyama wengine yanayotumika kuuma chakula. Isitoshe, anaonyesha kuwa meno ya trekta “yanararua udongo bila tone la huruma”. Maneno haya ni tashihisi zinazoonyesha namna trekta linachimba kwa nia thabiti bila kujali madhara ya uchimbaji huo.

Fauka ya hayo, katika shairi “Kiwanda” (uk. 6) msanii anaeleza vile sumu ya kemikali kutoka kiwandani inaleta athari mbaya kwa mimea, udongo, maji na hewa. Anasema:

Chembe nyeupe za maangamizi
Zinaelea angani zikichunguza
Kabla ya kushuka na sumu ya siri
Kukaba mimea koo mashambani
Na kuhasi udongo, maji na hewa

Ulimi wa sumu kali ya kemikali
Hurambaramba mapaa ya nyumba
Na kutoboa vitundu katika mabati
Na kuzipa nyota na mwezi nafasi
Kuchungulia shughuli za wazazi... (uk. 6)

Katika dondoo hili, mwandishi amezipatia chembe za sumu sifa za kuchunguza, kukaba mimea koo mashambani, ulimi kuramba mapaa ya nyumba na kuzipa nyota na mwezi nafasi ya kuchungulia shughuli za wazazi usiku. Maelezo haya yote ya tashihisi yanagusa hisia za msomaji mbali na kuchora taswira halisi ya kile anachokizungumzia.

Kwengineko, katika diwani ya *Rangi ya Anga* katika shairi “Wanda” (uk. 27) mwandishi anaeleza jinsi mbinu mbaya za kilimo zinachangia kuharibu mazingira akitumia tashihisi. Kwa mfano, katika shairi hili “Wanda” sehemu ya nane, mshairi anasema, “**Mikono ya kilimo hasiri na kwato za ufugaji shakiri zimekugofua, zimekurembua**” (uk. 41). Kwa kweli kilimo hakina mikono ila anarejelea mikono ya wakulima wenyewe wanaoharibu mazingira. Aidha, kwato za mifugo zimepewa sifa ya kugofua na kurembua kwa maana ya kuharibu.

Katika shairi hili “Wanda” sehemu ya tisa, ametaja sehemu mbalimbali za eneo la Meru, Kenya kama vile Kamwathu, Kaguma, Gaciongo, Ntoroni, Kamajagi na nyinginezo ambazo zimeathiriwa kutokana na ukataji wa miti na ukulima mbaya. Anasema:

...Kamajagi
Ntumira
Na ahali yenu nzima
Kwa jinsi sura zenu
Zilivyojaa vidonda
Na damu mbichi (uk. 42)

Ardhi haiwezi kuwa na vidonda wala damu. Hizi ni sifa za viumbe kama binadamu au wanyama wengine. Sifa hizi zinaonyesha kiwango kikubwa cha uharibifu wa maeneo yote aliyoyataja. Aidha, anatumia tashihisi katika shairi lili hili anaposema kuwa “**Majabali bahili na mawe batili yameegemeana kwa ndweo**” (uk. 42). Majabali yanapewa sifa ya ubahili ilhali mawe yanapewa sifa ya ubatili na majivuno kama kwamba ni binadamu.

4.3.3 Chuku

Mohamed (1995) anafafanua chuku kama mbinu ya kukuza jambo liwe kubwa kuliko ilivyo kikawaida; yaani kinyume na mantiki ilivyo katika uzoefu wetu. Chuku

inatumiwa katika kazi za kifasihi kusesitiza sifa fulani ili kuona uzito wa jambo linalozungumziwa. Maelezo ya Wamitila (2003a) yanaelekea kufanana na Mohamed (khj) anaposema kuwa chuku ni hali ya kuikuza sifa ya kitu fulani kuliko kawaida. Mwandishi ametumia chuku katika shairi “Matone ya Mvua” (uk. 73) katika diwani ya *Bara Jingine* anaposifu uzuri wa mvua. Anaeleza kuwa mvua imekomboa mimea, wanyama, wadudu na ndege kutokana na ukame na njaa. Akizungumzia jinsi kuku wanafurahia kuwa mtama na mawele yatakomaa shambani ili kuku wanufaike anasema:

Katika macho ya kuku
Matumaini yanametameta
Zionyeshavyo dalili
Karibuni
Utanawiri mtama
Yatakomaa mawele... (uk. 73)

Maneno “matumaini yanametameta” ni tamathali ya chuku. Mwandishi anaonyesha kuwa kwa sababu ya mvua kunyesha basi mtama utanawiri na mawele kukomaa ili kuku wapate chakula. Hata hivyo, si dhahiri kuona matumaini yakimetameta katika macho ya kuku lakini msomaji ataona uzito wa ujumbe wa mshairi.

Katika diwani ya *Redio na Mwezi* katika shairi “Kiwanda” (uk. 6) mshairi ametumia chuku anapoeleza vile sakafu za nyumba zinageuka mabwawa makuu kutokana na mashimo kwenye mapaa ya nyumba. Mshairi anasema kuwa, “**Msimu wa mvua unapowadia sakafu hugeuka mabwawa makuu kama makazi mwafaka kwa viboko!**” (uk. 6). Vitundu vilivyosababishwa na sumu kwenye mabati vinaweza kuingiza matone ya mvua ndani ya nyumba. Hata hivyo, kusema kuwa sakafu zinageuka na kuwa mabwawa makuu ni kukuza maji hayo ya mvua kupita kiasi.

4.3.4 Ritifaa

Ritifaa ni tamathali ya kukisemesha kitu ambacho hakina uhai kama kina uhai. Mshairi anatumia ritifaa anapotaka kupitisha hisia zake za moyoni. Kwa mfano, katika mashairi “Bwawa la Ithanje” (uk. 69) na “Matone ya Mvua” (uk. 73) katika *Bara Jingine*, mshairi ametumia ritifaa anapozungumza na bwawa na mvua mtawalia. Katika shairi “Bwawa la Ithanje” mwandishi anazungumza na bwawa anaposema, “**Pole, Bwawa la Ithanje: Polepole, afya yako inafifia**” (uk. 69). Kwa hakika bwawa halina uhai wala uwezo wa kusikiliza usemi wa mwandishi. Kupitia

usemi huu, msomaji anaelewa kuwa mshairi hafurahii namna bwawa la Ithanje linavyochafuliwa na wakulima pamoja na majitaka kutoka viwanda vya Limuru. Anahisi kwamba wanafaa kukoma kutia sumu kwenye maji ya bwawa hilo kwa sababu wanahatarisha maisha ya watu na viumbe wengine.

Katika shairi “Matone ya Mvua” (uk. 73), mtunzi anaongea na mvua moja kwa moja kama kwamba inaweza kusikia maneno yake. Anaisifu mvua kwa kufika wakati mzuri inapohitajika ili kukomboa mimea shambani pamoja na kupatia mifugo nyasi na wanyama wengine wa msituni chakula. Mshairi anasema:

Nyinyi, matone ya mvua
Nyinyi, mashujaa wa uhai
Mmefika wakati mwafaka
Wakati wa mahitaji (uk. 73)

Katika dondoo hili, mwandishi anatumia kiwakilishi “nyinyi” anapoongea na mvua ambayo si kiumbe hai kuonyesha kuwa iko karibu naye na inamsikiliza akiizungumzia. Anaiita mashujaa wa uhai. Anakariri umuhimu wa mvua kwa mimea shambani, binadamu, mifugo, miti na wanyama wengine.

Kwengineko, mtunzi ametumia ritifaa anapozungumza na “Ol Karia”. Ol Karia ni sehemu mojawapo nchini Kenya ambapo nishati fulani inayotoka chini ya ardhi inatumiwa kutoa stima yenye manufaa kwa Wakenya. Mshairi anazungumza na Ol karia kana kwamba ni mtu katika shairi “Ol Karia” (uk. 64) katika diwani ya *Msimu wa Tisa* hivi:

Ol Karia, jirani bila uchoyo
Naelewa maana ya kicheko chako
Unachekelea machozi ya huzuni
Yanayotiririka mashavuni... (uk. 64)

Katika dondoo hili, mtunzi anazungumza na Ol Karia ili kuonyesha manufaa yake kwa Wakenya katika kutoa umeme badala ya kutegemea stima inayotokana na mto Tana. Anaonyesha vile maumbile haya asili ya Ol Karia yanakuwa njia mbadala ya kuzalisha umeme wa kuendesha mitambo ya umeme, kusaidia mafundi wa juakali, taifa ling’ae kwa mwangaza na nchi inawiri kwa uwezo wa kiuchumi.

Ujumbe wa uzuri wa Ekweta una matumizi ya ritifaa katika shairi “Ukarimu wa Ekweta”(uk. 78) katika diwani ya *Msimu wa Tisa*. Mwandishi anaishukuru anga ya Ekweta kwa ukarimu wake. Anaeleza kuwa jua zuri, mvua, udongo mzuri pamoja na hewa vimeshirikiana na kuhakikisha kuna vyakula vya aina mbalimbali kwa wakulima kama vile nanasi, embe, tufaha, pera na plamu. Mshairi anadokeza:

Asanteni jua, mvua, udongo na hewa
Ushirikiano wenu na mkono wa mkulima
Umeifanya meza ya kiamsha-kinywa
Kuwa mwandani wa kutamanika
Katika urafiki wa kuaminika (uk. 78)

Katika shairi “Wanda” (uk. 27) sehemu ya nane, katika diwani ya *Rangi ya Anga* mtunzi ametumia ritifaa. Anazungumza na eneo linaloitwa “Thanantu” kuonyesha vile wakulima wanaotumia mbinu mbaya za ukulima wameliharibu. Anasema:

Ewe Thanantu!
Sahibu wa utotoni!
Nikikukumbuka daima
Kwa kumbukumbu pendezi,
Ewe rafiki niliyeamini,
Mikono ya kilimo hasiri
Na kwato za ufugaji shakiri
Zimekugofua, zimekurembua (uk. 41)

Mwandishi anazungumza na eneo hili linalojulikana kama Thanantu kwa kusema kuwa ni rafiki yake aliyemwamini tangu akiwa mtoto. Anakereka kuwa wakulima wameliharibu kwa kutumia mbinu mbaya za kilimo kiasi kwamba halipendezi tena. Mbali na mshairi kutumia tamathali hii kupitisha dhamira yake kwa msomaji, inadhihirisha uhusiano baina ya ujumbe na namna ya kuusema ujumbe wenyewe. Isitoshe, inaonyesha usasa katika mashairi ya Kithaka wa Mberia kwa sababu haipatikani sana katika mashairi ya washairi wengine wa kisasa.

4.3.5 Maswali ya Balagha

Mwandishi ametumia maswali ya balagha anapozungumzia kuhusu mazingira katika shairi “Wanda” (uk. 27) katika diwani ya *Rangi ya Anga*. Kwa mfano, mwandishi anapozungumza kuhusu ongezeko la joto linalotatiza watu, mimea, udongo na wanyama wengine kutokana na jua kali anauliza maswali ya balagha katika shairi “Wanda” sehemu ya kwanza:

...Mimea na samaki
Ndege na wadudu
Na wanyama na mito
Walikutenda ovu gani
Kukuchochea ulipize kisasi
Kwa ghadhabu pujufu? (uk. 28)

Swali la balagha lililo katika dondoo hili linaamsha tafakari ya msomaji kuona jinsi ongezeko la halijoto linaleta madhara kwa mwanadamu, udongo, mimea, mito na wanyama kwa jumla. Katika kuuliza hivyo, mwandishi anataka msomaji afikirie kuhusu hali hiyo na kutafuta suluhu ikiwezekana dhidi ya ongezeko la halijoto katika mazingira tunamoishi.

Kwengineko, katika shairi “Wanda” sehemu ya saba, mshairi anazungumza kuhusu kiangazi kikali kinachotokea baada ya mvua kupotea. Jua kali linasumbua mimea na viumbe huku vumbi likitatiza macho ya msafiri. Anauliza ni kwa nini mvua ikaondoka haraka:

...Mbona umeondoka haraka
Badala ya kuwa mstahimilivu
Na kukaa nasi kwa miezi kadha
Ukitukirimu kwa utulivu
Na kututilia ndoto rutuba?

Mvua, ewe mvua, mpendwa
Rafiki wa viumbe na mimea
Ungepata hasara ya kimo gani
Ungekaa kwa miezi mingine miwili
Ukaendelea kuhudumia hizi wanda
Kwa dawa yako isiyokadirika thamani? (kur. 36-37)

Katika shairi hili, mwandishi anauliza maswali ya balagha ili msomaji aone hasara iliyotokea baada ya mvua kupotea. Kutokana na mvua kupotea, mimea, nyasi na miti inakauka. Wanyama wanakufa kwa sababu ya ukame. Janga la njaa linavamia watu kwa sababu ya ukosefu wa mvua. Maswali hayo yanaonyesha hali halisi mvua inapokosekana kwa muda mrefu.

Katika shairi “Wanda” sehemu ya kumi na mbili, mwandishi anauliza uhalali wa ufugaji wa kuhamahama badala ya kuzingatia ukulima wa kisasa ambapo wakulima wanastahili kufuga ng’ombe wachache wa gredi wenye manufaa. Mshairi anauliza:

Hii milolongo ya taya
Na pembe na nundu

Inafaidi vipi nyumbani
Zaidi ya viwele vichache
Vya ng'ombe wateule? (uk. 47)

Katika dondoo hili, mwandishi anauliza swali la balagha ili kuwazindua wafugaji wa kuhamahama kuwa hakuna faida ya kufuga ng'ombe wengi wa kienyeji. Ni muhimu kufuga ng'ombe wachache wa gredi wanaotoa maziwa mengi kuliko kuwa na idadi kubwa ya ng'ombe wa kienyeji wasio na faida. Ng'ombe wengi pia wanachangia kuharibu mazingira kupitia kula nyasi zote, kuchafua maji mtoni na kuharibu udongo na hivyo kuchangia mmomonyoko wa udongo wakati wa mvua.

4.3.6 Mbinu Nyingine za Kisanaa

Mbinu nyingine za kisanaa ni vipengele ambavyo si tamathali za usemi lakini mwandishi amevitumia anapozungumzia maudhui yanayogusia mazingira.

4.3.6.1 Taswira

Katika shairi “Jinamizi” (uk. 55) katika diwani ya *Bara Jingine* mshairi anaeleza vile watu wengi waliobeba mashoka, mapanga na misumeno walikata miti wakitafuta mashamba ya kulima pamoja na mbao. Anasema, “**Kaumu ya watu ikibeba shoka, panga kali na misumeno inayonguruma ilikuja kwa mawimbi...**” (uk. 55). Maelezo haya yanachora picha ya namna watu wengi waliobeba vifaa vya kukatia miti waliingia na kuanza kukata miti.

Fauka ya hayo, mshairi anaonyesha taswira ya jinsi wanyama walitaabika wakitembea njiani kwa sababu ya kiangazi na ukosefu wa malisho, hali iliyochangiwa na ukataji miti kiholela. Anasema, “**Ngombe, kondoo na mbuzi walibadilika sura na kuwa mafupa yanayojisukuma njiani kama makobe makongwe**” (uk. 57). Maelezo haya na tashibihi hii inaonyesha picha ya hali mbaya ya wanyama waliokaribia kuangamia.

Kwengineko, katika shairi “Mimi, Mto Nairobi” (uk. 63) kuna taswira ya vile wakaazi wa Nairobi wanachafua maji katika mto Nairobi. Mwandishi anaeleza, “**Wananinyonga kwa mafuta, makopo, tairi, talimbo na takataka bila ukoo**” (uk. 63). Kwa kutumia maelezo hayo, msomaji anapata picha akilini mwake ya namna takataka hizo zimechanganyika au kuelea juu ya maji ya mto Nairobi. Picha hii inamsaidia msomaji kuona wazi namna mto huo unavyoonekana kwa sababu ya uchafu huo wote uliomo majini.

Katika shairi “Nyeri” (uk. 70) mshairi anaeleza juu ya mandhari ya kijani kibichi ya majani-chai, mikahawa na migomba. Maelezo hayo yanachora taswira katika akili ya msomaji jinsi mazingira hayo yanavyopendeza. Anasema:

Nimeona mashamba nadhifu
Yakifurika rangi ya kijani;
Nimeona mikahawa na majani-chai
Na migomba na ng’ombe bila pembe... (uk. 70)

Maelezo haya yanaonyesha jinsi wakulima wamefanya juhudi kukuza majani-chai, kahawa na kufuga ng’ombe wa gredi. Kwa hivyo, mshairi anafurahia na kuhimiza kilimo cha kisasa kinachochangia katika kuboresha na kutunza mazingira.

Fauka ya hayo, katika shairi “Mombasa Mibuyuni” (uk. 72) katika diwani hii ya *Bara Jingine* kuna taswira wakati mwandishi anaeleza juu ya mazingira tulivu huko Mombasa ambapo watu wanafurahia kubarizi. Maelezo yake yanatoa picha ya jinsi mibuyu imepamba mandhari. Anasema, “**Mibuyu ambayo imesimama imara kama kazi ya fahari ya msanii mahiri**” (uk. 72). Msomaji anaona picha ya namna mibuyu imesimama vizuri na hivyo kuelewa kwa rahisi jinsi mandhari hayo yanavyoonekana ingawa hayuko katika mazingira hayo.

Kwengineko, katika diwani ya *Redio na Mwezi*, shairi “Johari Bamburi” (uk. 8) linazungumzia uchimbaji wa madini yanayotumika kutengeneza saruji katika eneo la Bamburi. Kuna taswira ya kimaelezo inayoonyesha namna trekta linainua meno ya chuma na kuchimba ardhi, jambo ambalo linachangia uharibifu wa mazingira. Picha hiyo inajitokeza ifuatavyo:

Trekta, likinguruma kwa nia thabiti
Linateremsha meno jasiri ya chuma
Na kurarua udongo bila tone la huruma
Na kuacha sura kirihi, picha ya utasa... (uk. 8)

Ingawa msomaji hayuko katika eneo la Bamburi, maelezo hayo yanampatia picha kamili vile treka hilo linavyochimba udongo. Aidha, maelezo yanaweza kumpa kumbukumbu vile matingatinga yanararua udongo wakati wa kutengeneza barabara.

Kuna taswira vilevile katika shairi “Kiwanda” (uk. 6) katika diwani hii. Kiwanda ni mahali ambapo bidhaa mahususi hutengenezwa. Kwa mfano, kuna kiwanda cha sukari, majani-chai, mikate, mabati na kadhalika. Wakati wa kutengeneza bidhaa,

kuna uchafu unaotoka kiwandani kwa njia ya majitaka au moshi unaopaa angani. Mwandishi anaeleza vile moshi mzito wa hudhurungi unafuka katika shairi “Kiwanda”. Hii ni picha ya namna moshi huo unaotoka kiwandani unachafua hewa. Anasema, “**Bughudha nzito ya hudhurungi inafuka kutoka dohani jeuri...**” (uk. 6)

Kutokana na madhara ya gesi ya sumu kutoka kiwandani, kwenye mabati ya paa kunakuwa na vitundu ambavyo vinaingiza maji ndani ya nyumba wakati wa msimu wa mvua. Mshairi anatumia tashibihi inayoonyesha picha ya namna sakafu ya nyumba hugeuka kuwa mabwawa makuu. Anasema, “**Msimu wa mvua unapowadia, sakafu hugeuka mabwawa makuu kama makazi mwafaka kwa viboko!**” (uk. 6). Tashibihi hii inatoa taswira ya sakafu ya nyumba iliyojaa maji mengi ya mvua kiasi cha bwawa la maji wanakokaa viboko.

4.3.6.2 Usambamba

Wamitila (2003a) anafafanua usambamba kama “mbinu ambapo msanii anayarudia maneno fulani au maana fulani kwa muundo mwingine tofauti.” Kimsingi, usambamba ni mbinu ya kurudia. Urudiaji huu unaweza kujitokeza katika viwango tofauti kama vipashio vya kisintaksia, virai au sentensi. Mfano mzuri wa usambamba unajitokeza katika shairi “Mimi, Mto Nairobi” (uk. 63) katika diwani ya *Bara Jingine* mshairi anaposema hivi:

Wakaazi wa jiji
Wananikaba koo
Wananiziba pumzi... (uk. 63)

Katika dondoo hili, maneno “wananikaba koo” na “wananiziba pumzi” yana usambamba. Kukaba koo na kuziba pumzi matokeo yake ni mambo japo inarudiwa kwa muundo tofauti. Vipashio hivi vya kisintaksia vimepangwa kwa namna inayoleta maana sawa. Mshairi anasisitiza juu ya uchafuzi wa mto Nairobi kupitia mafuta, makopo, tairi, talimbo na takataka nyingine nyingi.

Kuna usambamba pia katika shairi “Jinamizi” (uk. 55). Mwandishi ametumia wimbo kueleza madhara ya jangwa linalotokana na ukataji wa miti. Msanii anasema:

Ndimi jangwa
Ninyimaye mayai, maziwa na nyama
Ndimi jangwa
Nihiniye mboga, nafaka na matunda... (uk. 58)

Katika dondoo hili, usambamba unajitokeza katika maneno “ninyimaye” na “nihiniye”. Maneno haya tofauti yana ujumbe sawa kwa vile jangwa linafanya watu kukosa mayai, maziwa, nyama, mboga, nafaka na matunda.

Kwengineko, katika shairi “Okidi, Piga Ukelele!” (uk. 64) mwandishi ametumia usambamba ili kutoa hisia za hasira moyoni. Anazungumzia kuhusu uharibifu wa mazingira. Kwa hivyo, ili kusitisha uharibifu zaidi, anasihi Okidi ambalo ni eneo maalumu lisikubali kuharibiwa na badala yake lipige kelele ili lisiharibiwe. Anasema:

La! Okidi-madoa!
Kuangamizwa
Kamwe usikiri....
La! Kuniangamiza
Si halali
Si haki
Ni **maonevu**
Ni **dhuluma**
Ni haramu
Nimekataa! (kur. 64 -65)

Maneno “maonevu”, “dhuluma” japo ni tofauti yana ujumbe sawa kwa sababu yanaonyesha kuharibiwa kwa eneo la Okidi.

4.3.6.3 Usimulizi

Kimsingi usimulizi ni mbinu ya kueleza kisa au tukio fulani. Kuna usimulizi katika wakati uliopo au wakati uliopita. Aidha, kuna usimulizi katika nafsi ya kwanza, pili au nafsi ya tatu. Mwandishi ametumia mbinu ya usimulizi katika baadhi ya mashairi ili kuangazia maudhui kuhusu mazingira. Kwa mfano, katika shairi “Mimi, Mto Nairobi” (uk. 63) katika diwani ya *Bara Jingine*, ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza (mimi) kuzungumzia namna mto Nairobi unavyochafuliwa na wakaazi wa Nairobi. Anatumia mofu “na” na “ni” kurejelea njeo na nafsi mtawalia ili kupunguza umbali kati ya kinachosimuliwa na msomaji. Huu ndio upekee na usasa unaoonekana katika shairi hili. Mshairi anasema:

Wakaazi wa jiji
W**ananik**aba koo
W**ananiz**iba pumzi
W**ananiny**onga... (uk. 63)

Aidha, kuna usimulizi katika shairi “Jinamizi” (uk. 55). Mwandishi anaeleza kuwa halaiki ya watu iliyobeba mashoka, mapanga na misumeno ilikuja ikakata miti ikitafuta mashamba ya kulima na mbao. Anasimulia, “Kaumu ya watu ikibeba shoka, panga kali na misumeno inayonguruma **ilikuja...**” (uk. 55)

Mwandishi vilevile anatumia mofu “na” na “me” katika usimulizi kuonyesha kuwa vitendo vingali vinaendelea au vimefanyika muda mfupi uliopita. Kwa mfano, katika shairi “Mombasa Mibuyuni” (uk. 72) katika diwani ya *Bara Jingine*, mtunzi amechanganya mofu hizi za njeo kusimulia vitendo vyenyewe. Anasimulia hivi:

Upepo laini wa bahari
Unapuliza taratibu...

Mibuyu ambayo
Imesahau umri wake
Imesimama imara...
Nyoyo za wapenzi wapya
Zinavutana kwa nguvu
Kwenye tanzu zake
Ndege wakunjufu
Wanakariri mashairi
Wakisifia maumbile... (uk. 72)

Kwengineko, mshairi anaposifu uzuri wa mti wa jakaranda katika shairi “Mjakaranda” (uk. 75) katika diwani hii pia, anatumia mbinu ya usimulizi kupitia mbinu rejeshi. Anatumia mbinu rejeshi (nakumbuka) na mofu “li” kurejelea wakati uliopita. Anasimulia:

Nakumbuka siku ambayo
Macho yetu yalikutana
Nyoyo zetu zikapendana
Mapenzi yakaumana

Nilikuwa Parkview ghorofani... (uk. 75)

Aidha, mwandishi anaposimulia safari yake na wenzake kwenda Malindi kujivinjari, anasimulia kwa kutumia mofu “li” kuonyesha wakati uliopita. Anasimulia katika shairi “Kambi Malindi” hivi:

Tulifika alasiri
Jua lilikuwa na upole...
Bahari **ilitukaribisha...**
Ufukwe **ulitupokea...** (uk. 79)

Mbinu ya usimulizi hupatikana sana katika hadithi za fasihi simulizi, hadithi fupi na riwaya katika fasihi andishi. Hata hivyo, mshairi anaitumia katika ushairi kama njia ya kusimulia ujumbe wake kwa msomaji ili kuonyesha mpito wa wakati.

4.3.6.4 Nidaa

Nidaa ni mbinu ya kutumia maneno yanayoibua hisia mbalimbali za mwandishi. Hisia zinazoibuliwa zinaweza kuwa za furaha, chuki, kero, huruma, masikitiko na mshangao miongoni mwa zingine. Alama ya kihisishi (!) huwekwa baada ya maneno hayo yaliyokusudiwa kutoa hisia hizo. Kwa mfano, katika diwani ya *Bara Jingine*, shairi “Mimi, Mto Nairobi” (uk. 63) lina nidaa. Nidaa hiyo inaonyesha hisia za hasira za mtunzi kwa wakaazi wa Nairobi wanaochafua maji ya mto Nairobi kwa takataka za kila aina. Anasema, “**Wamenitesa, hawa wajeuri majirani bila shukrani!**” (uk. 63). Anaonyesha hasira kwa wakaazi wa Nairobi ambao wanachafua maji ya mto huu ilhali wanastahili kuulinda kwa sababu wanatumia maji hayo kwa shughuli zao.

Katika shairi “Ngao” (uk. 59) mtunzi anaeleza vile maendeleo ya teknolojia yameharibu utandu wa ozoni. Utandu ambao ndio ngao inayolinda wanadamu dhidi ya miale hatari ya jua. Teknolojia anayozungumzia ni zile kemikali ambazo zinaharibu ozoni na hivyo kumletea mwanadamu madhara ya ugonjwa wa ngozi pamoja na ongezeko la joto duniani. Mwandishi anasema, “**Ole sisi binadamu! Kwa teknolojia jeuri tunakulegeza afya...**” (uk. 60). Mshairi anatumia maneno “Ole sisi binadamu!” kuonyesha hisia za huruma na kujisikitikia kwa sababu ni shughuli hizi za mwanadamu ambazo zinakuwa chanzo cha maangamizi yake mwenyewe.

Fauka ya hayo, mwandishi anashangilia na kuonyesha furaha yake kwa mvua inayonyesha kwa wakati mzuri na kufanya mimea inawiri shambani, kutuliza jua kali pamoja na vumbi katika shairi “Matone ya Mvua” (uk. 73). Mtunzi anaonyesha furaha yake moyoni vile hata wanakondoo wanafurahi wakirukaruka kwa sababu ya joto laini mwilini. Anasema, “**Wana wa Kondoo- Ewee! Watazame uani! Wanaruka na kupinda angani kwani joto laini la furaha limewajaa katika damu**” (uk. 73). Maneno “Ewee! Watazame uani!” yanaonyesha hisia za furaha ndani ya moyo wa mwandishi.

Katika diwani ya *Redio na Mwezi* mwandishi anashangilia mandhari mazuri ya bahari na mwezi katika shairi “Bahari na Mwezi” (uk. 27). Mtunzi anasema:

Bahari, unainua uso wa samawati
Ukitamani kumbusu busu la peponi
Na kumvisha mikufu ya almasi bila mwenza
Na kwa maneno yanayotetema, kumwambia
Mwezi, u lulu ya moyo wangu! (uk. 67)

Mwandishi ametumia nidaa katika diwani ya *Rangi ya Anga* katika shairi “Wanda” (uk. 27). Anavutiwa na hisia za huruma na kilio kuona eneo la Thanantu lililokuwa pendezi limeharibiwa kupitia kilimo hasiri na ufugaji. Mtunzi anasema:

Ewe Thanantu!
Sahibu wa utotoni!
Mikono ya kilimo hasiri
Na kwato za ufugaji shakiri
Zimekugofua, zimekurembua (uk. 41)

Kupitia maneno “Ewe Thanantu! Sahibu wa utotoni!” msomaji anapata hisia za huruma moyoni mwa mwandishi kwamba hafurahii kuona vile sehemu hiyo imeharibiwa na shughuli za ukulima na ufugaji.

4.3.6.5 Ndoto

Ndoto ni maono fulani yatokeayo usingizini mtu anapolala. Katika diwani ya *Bara Jingere*, mwandishi ametumia ndoto katika shairi “Jinamizi” (uk. 55) anapozungumzia juu ya ukataji wa miti. Anaeleza kuwa alipokuwa amelala kitandani, usingizi mnono ulimchukua akaota ndoto ya jinamizi la ukataji wa miti. Katika ndoto hiyo aliona vile kundi la watu lilikuja na mashoka, mapanga na misumeno na likakata miti mingi kwa nia ya kupata mashamba na mbao. Mtunzi ametumia ndoto kama mbinu ya kueleza kero la ukataji miti na madhara yake. Anasema:

Mwili na fahamu
Zilikuwa kitandani
Usingizini mnono

Ghafla, ikaja **ndoto**
Ndoto ya kutisha
Na kubabaisha
Ndoto ya jasho
Na joto kali
Jinamizi! (uk. 55)

Mtunzi ametumia ndoto kama kiunzi cha kuonyesha jinsi watu walivamia miti kwa mashoka, mapanga na misumeno. Bila shaka huu ni uharibifu wa mazingira.

4.3.6.6 Wimbo

Wimbo ni maneno yaliyopangwa kwa muwala fulani na huleta mahadhi ya kimuziki. Wimbo unapotumiwa na msanii huwa na ujumbe wa kukariri katika kazi husika. Kwa mfano, mshairi anatumia wimbo katika shairi “Jinamizi” (uk. 55) katika diwani ya *Bara Jingine* kuisisitiza kuwa hatima ya kukata miti ni kutokea kwa jangwa. Mshairi anadokeza:

Sauti ya kejeli
Iisikika, ikiimba
 Ndimi jangwa
 Niogopwaye na mvua
 Ndimi jangwa
 Ninyongaye mito
 Ndimi jangwa
 Ninyimaye mayai, maziwa na nyama
 Ndimi jangwa
 Nihiniye mboga, nafaka na matunda
 Ndimi jangwa
 Mtawala wenu! (uk. 58)

Katika wimbo huu, mwandishi anaonyesha kuwa jangwa hukausha mito. Aidha, jangwa linasababisha mifugo kukosa kutoa bidhaa muhimu kama vile mayai, maziwa na nyama kwa vile hakuna maji na chakula. Isitoshe, kutokana na jangwa, watu wanakosa mboga, matunda na nafaka. Hatima ya jangwa kwa binadamu na mifugo ni njaa na kifo.

4.3.6.7 Takriri

Kuna takriri kifungu katika shairi “Jinamizi” (uk. 55) katika diwani ya *Bara Jingine*. Mwandishi anarudia maneno “ndimi jangwa” ili kutoa mdundo wa kishairi, uimbikaji wa shairi mbali na kuisisitiza madhara ya jangwa kwa mwanadamu. Anasema:

Ndimi jangwa
 Niogopwaye na mvua
Ndimi jangwa
 Ninyongaye mito
Ndimi jangwa
 Ninyimaye mayai, maziwa na nyama
Ndimi jangwa
 Nihiniye mboga, nafaka na matunda... (uk. 58)

Katika shairi “Mkalitusi” (uk. 67), mshairi anafafanua manufaa ya mti wa mkalitusi. Anasema kuwa mkalitusi huzuia nguvu za upepo mkali, hupamba mandhari,

huonyesha mipaka ya mashamba, huzuia wanyama wasiharibu mimea shambani miongoni mwa mengine. Katika kusesitiza manufaa ya mkalitusi, mwandishi anarudia neno “mnapotusaidia” ifuatavyo:

Wewe na seng’enge’
Mnapotusaidia kuonyesha mipaka
Ili kuepukana na migongano
Mnapotusaidia kuzuia wanyama
Wasiharibu kilicho shambani,
Mnapotusaidia kukumbusha mpita-njia
Kwamba kilicho ndani si chake... (uk. 68)

Kwengineko, katika shairi “Nyeri” (uk. 70) katika diwani ya *Bara Jingine*, mwandishi anarudia neno “nimeona” na “kwenye” anapozungumzia juu ya mashamba nadhifu, mikahawa na majani-chai pamoja na tangazo linalohimiza watu kuonyesha mipaka ya mashamba kwa kupanda miti. Mtunzi anasema:

Nimeona mashamba nadhifu
Yakifurika rangi ya kijani;
Nimeona mikahawa na majani-chai
Na migomba na ng’ombe bila pembe

Kwenye milango ya nyumba
Kwenye vituo vya umma
Nimeona tangazo... (kur. 70-71)

Katika shairi “Mikoma” (uk. 66), mwandishi analaumu wagemaji, wasonga mizinga na wakulima ambao wamekata mikoma katika maeneo ya Igaironi, Irarani, Kirukuma na Kaguma. Anarudia neno “mikono” kuonyesha jinsi shughuli za watu tofauti zimechangia kuharibu mikoma ambayo ni pambo la ardhi na urithi muhimu. Mtunzi anasema:

Kutokana na **mikono**
Mikono ya wagemaji
Mikono ya wasonga mizinga
Mikono ya wakulima
Igaironi na Irarani
Kirukuma na Kaguma
Umejaa makaburi
Ya mikoma (uk. 66)

Kwengineko, katika shairi “Wanda” (uk. 27) katika diwani ya *Rangi ya Anga*, mwandishi anarudia maneno “jua” na “ewe jua” ili kusesitiza juu ya athari za ongezeko la halijoto ya jua. Anasema kuwa joto limeathiri udongo, mimea, samaki, ndege, wadudu, wanyama na miti. Mtunzi anasema:

Jua!
Ewe jua!
Jua la adhuhuri
Mbona kwa ghadhabu
Unaadhibu chembe za udongo
Kwa halijoto kama ya tanuri?

Jua!
Ewe jua!
Jua la wanda za mikwaju... (uk. 28)

4.3.6.8 Msamiati Teule

Jinsi mshairi anavyoteua msamiati wake ni muhimu katika kuwasilisha ujumbe wake pamoja na athari za ujumbe huo kwa msomaji wake. Ingawa Kithaka wa Mberia anatumia lugha ya kawaida kuzungumzia ama uharibifu wa mazingira au utunzaji wa mazingira, anatumia msamiati unaomuathiri na kumuelekeza msomaji. Kwa mfano, anapozungumzia juu ya ukataji miti na madhara yake anatumia neno “jinamizi” na “ikachinja miti” katika shairi “Jinamizi” (uk. 55) na “ngao” anapozungumza kuhusu manufaa ya ozoni kutukinga dhidi ya miale mikali kwenye shairi “Ngao” (uk. 59) katika diwani ya *Bara Jingine*. Vilevile, anatumia majina ya miti kama vile “mikoma”, “mkalitusi” na “mjakaranda” katika diwani hii. Isitoshe, anataja majina ya pekee ya mahali kama vile katika mashairi “Thagicu” (uk. 61), “Mimi, Mto Nairobi” (uk. 63), “Bwawa la Ithanje” (uk. 69), “Nyeri” (uk. 70), “Mombasa Mibuyuni” (uk. 72) na “Kambi Malindi” (uk. 79). Katika diwani ya *Radio na Mwezi* kuna “Johari Bamburi” (uk. 10).

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, kuna mashairi yenye majina kama “Ol Karia” (uk. 64), “Mwea” (uk. 70), “Ntharene” (uk. 75) na “Ukarimu wa Ekweta” (uk. 79). Katika diwani ya *Rangi ya Anga* katika shairi “Wanda” (uk. 27), mtunzi anataja majina ya sehemu zilizoharibiwa kama vile Kereka, Gitugu, Kamwathu, Kaguma, Kanyamaki, Gaciongo, Gakauni, Kamaindi, Mutino, Nkarini, Ntoroni, Kamajagi na Ntumira (kur. 41-42). Lengo kuu la kutaja maeneo haya ni kuonyesha kuwa anaelewa kwa undani anachokisema na hata kutolea msomaji mifano ya sehemu halisi zilizoharibiwa. Aidha, anataja sehemu hizi ili kubuni mandhari mwafaka ya maudhui katika mashairi hayo.

4.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia maudhui juu ya uharibifu na utunzaji wa mazingira kwa kina. Maudhui ya ukataji miti, mbinu mbaya za kilimo zinazochangia kuharibu mazingira, uchafuzi wa maji na uchafuzi wa ardhi kupitia uchimbaji wa migodi yameangaziwa. Aidha, maudhui ya namna hewa huchafuliwa na utandu wa ozoni kuharibiwa yameshughulikiwa. Kwa upande mwingine, umuhimu na utunzaji bora wa mazingira umeangaziwa. Imebainika kuwa mashairi anapenda mazingira yake na anafahamu umuhimu wake na kwa hivyo anachukizwa na vitendo vya watu vya kuharibu mazingira ama kwa kukusudia au kutojua. Kwa hivyo, mazingira ni kichocheo kingine kinachompa mwandishi nafasi ya kutunga mashairi mengi kuhusiana na uharibifu na utunzaji wa mazingira kwa vizazi vya leo na vya kesho.

Katika kuonyesha uhusiano wa maudhui juu ya mazingira na vile anavyoyawasilisha, Kithaka wa Mberia ametumia mbinu kadha za kimtindo ili kuendeleza dhamira yake. Baadhi ya mbinu za kimtindo alizozitumia ni kama vile: tashibihi, tashihisi, chuku, ritifaa, maswali ya balagha na mbinu nyingine za kisanaa mathalani taswira, usambamba, usimulizi, nidaa, ndoto, nyimbo, takriri na msamiati teule. Mbinu hizi zimeongeza ujumi wa kisanaa katika mashairi ya mtunzi mbali na kusaidia maudhui kueleweka.

SURA YA TANO

UTAMADUNI MAHULUTI

5.1 Utangulizi

Kabla ya kuja kwa Waarabu, wamishenari na wakoloni nchini Kenya, Afrika Mashariki na bara la Afrika kwa jumla, wenyeji walikuwa na mila na tamaduni zao. Waarabu, wamishenari na wakoloni walipoingia, tamaduni na mifumo ya maisha ilibadilika. Waarabu walikuja kufanya biashara na kueneza dini ya Kiislamu miongoni mwa wenyeji. Wamishenari vilevile walileta mafunzo mageni kupitia dini ya Kikristo. Baadhi ya wenyeji waliasi tamaduni na mila zao na kupokea mafunzo ya dini ya kigeni. Wakoloni walipokuja, walileta elimu ya kigeni, iliyofundishwa kwa lugha yao; waliendeleza utumwa na kunyakua mashamba licha ya kudhibiti njia kuu za uchumi. Aidha, walileta mifumo mipya ya sheria na kudhihirisha ubaguzi wa rangi kwa sababu ya mila, tamaduni na mienendo yao ya maisha.

Kutokana na ujio na maingiliano ya wageni hawa na wenyeji, athari nyingi za kigeni zilianza kuonekana kama vile unyanyasaji wa kiuchumi, unafiki wa kidini, ukahaba na utumwa. Mambo haya yote yalichangia kuibuka kwa utamaduni mahuluti. Vipengele hivi vya utamaduni wa kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni ndivyo vinaonyesha kuwa utamaduni mahuluti unaweza kuwa mzuri na vilevile mbaya. Katika sura hii, tumedhihirisha athari za utamaduni mahuluti katika ushairi wa Kithaka wa Mberia na namna unavyodhihirika katika jamii ya leo umejadiliwa kwa misingi ya nadharia ya baadaukoloni. Dhana ya utamaduni mahuluti katika nadharia ya baadaukoloni imetumika kuangazia namna utamaduni mgeni wa Waarabu, wamishenari na wakoloni uliathiri mfumo wa maisha ya Waafrika. Baadhi ya vipengele hivyo vya utamaduni mgeni vinaathiri maisha ya Waafrika hata wakati wa sasa kama inavyojadiliwa katika sura hii. Isitoshe, mtindo alioutumia kuangazia utamaduni mahuluti umechanganuliwa kwa kutumia nadharia ya elimumitindo mkabala wa uhakiki mpya.

5.2 Maudhui

Maudhui ambayo tumeyashughulikiwa katika sehemu hii na namna yanavyojitokeza katika ushairi wa Kithaka wa Mberia ni pamoja na ubepari na unyonyaji, ukahaba, uasherati na usenge, vileo na mihadarati, ubaguzi, unafiki wa kidini na elimu ya kigeni.

5.2.1 Ubepari na Unyonyaji

Ubepari ni mfumo wa kiuchumi unaoweza watu wachache kumiliki rasilimali na njia kuu za uchumi wa nchi. Kwa sababu hiyo, watu wengi ambao hawana mali hulazimika kufanya kazi kwa mabwanyenye ili kujimudu kimaisha. Mabwanyenye ambao ndio watu wa tabaka la juu huongozwa na ubinafsi katika kunyonya jasho la wafanyakazi. Mabwanyenye hao wanakosa kuwalipa wafanyakazi ujira unaolingana na kazi wanayoifanya. Kwa sababu hiyo, wafanyakazi wanateseka. Hali hii ni athari moja ya ukoloni. Hivi ndivyo wakoloni waliwanyanya Waafrika kwa kuwafanyisha kazi za sulubu kwa muda mrefu bila kuwapatia malipo yaliyowiana na kazi walizofanya.

Mtunzi anaeleza namna matajiri wanavyojilimbikizia mali na utajiri na kuwakandamiza wanyonge lakini hakuna wa kuwatetea. Kwa mfano, katika shairi “Wimbo wa Mkulima” (uk. 9) katika diwani ya *Mchezo wa Karata* anaonyesha vile wakulima wanajitahidi kufuga mifugo na kukuza mimea mashambani lakini mazao yao yanafaidi wasiofuga na wasiolima na kuwatemea mate wakulima. Hali hii inashuhudiwa wakati wakulima wa majani-chai, kahawa, mahindi pamoja wafugaji wa ng’ombe wa maziwa wanapolalamika kuhusu malipo duni. Wanahisi kuwa serikali haiwajali japo wanafanya kazi muhimu ya kulisha taifa. Vilevile, ujumbe sawa na huu unapatikana katika shairi “Nyuki, Ndege na Nyegere”(uk.10). Nyuki wanasumbuka kutafuta mbelewele ili kutengeneza asali. Lakini wanapotengeza asali hiyo, nyegere na ndege ambao hupenda asali huiba asali yao kutoka mzingani. Hii ni sitiari inayodhihirisha tabia ya mabepari wanaonyonya jasho la wafanyakazi. Hii ni ukandamizaji wa kiuchumi. Isitoshe, dhuluma za unyonyaji zinaonekana katika shairi “Tajiri wa Lulu” (uk. 16). Tajiri wa lulu ambaye hataki ngozi yake iharibike, aogopaye maji ya matope na asiyetaka kuchafua nguo zake ndiye mmiliki wa makasha ya lulu. Mshairi anauliza:

Wewe uogopaye maji ya chumvi
Ngozi yako nyororo isiharibike,
Wewe ukwepaye maji ya matope
Unadhifu wako usipungue
Lulu makasha – makasha
Umekuwaje mmiliki? (uk. 16)

Katika shairi “Mfanyakazi Mahakamani” (uk. 22), mshairi anaeleza juu ya mfanyakazi kiwandani anayefanya kazi ya sulubu. Lakini kinaya ni kwamba ujira anaolipwa haulingani na kazi anayofanya. Mfanyakazi huyu anapelekwa kortini na mwajiri wake wakati anapolalamika alipwe mshahara unaotoshana na kazi aifanyayo. Mfanyakazi huyu anaambiwa kuwa amezua ubishi na hivyo anahukumwa kifungo cha miaka mitatu ili kuwa funzo kwa wengine. Mfanyakazi huyu anawakilisha wafanyakazi wengi ambao wanadhulumwa na waajiri wao. Wananyimwa ujira wao unaofaa kuwiana na kazi wafanyazo kupitia hukumu zisizo za haki mahakamani. Hali kama hii inashuhudiwa katika nchi nyingi, wakati walimu, madaktari na wafanyakazi wa kampuni mbalimbali wanapogoma kudai nyongeza ya mishahara. Mshairi anasema:

Kutoka mvuke wa jasho
Yapanda sauti ya mfanyakazi
Mavune ya mwili
Na machovu ya akili
Yatiwe upande mmoja
Nao upande wa pili
Utiwe ujira wetu
Hadi mikono ya ratili
Ilingane uzani (uk. 22)

Mtunzi pia anatetea usawa na haki katika ugavi wa rasilimali katika shairi-picha liitwalo “Boga” (uk. 2). Ngari (1998) anasema kuwa shairi hili linazungumzia juu ya shamba ambalo lilirithishwa watoto wawili na wazazi wao. Katika shamba hili, kulikuwa na mboga ambao ulizaa boga ambalo kila mtoto anastahili kufaidika kwalo. Kupitia shairi hili, mwandishi anatetea tabaka la wanyonge wapate haki yao. Mshairi anatimiza dhamira yake kwa kusawiri umbo la boga duara ambalo limegawanywa katika sehemu mbili zilizo sawa. Anatumia maneno ishirini na manane katika kila sehemu kuunda umbo hili la boga. Mshairi anasema:

		mboga	si	
		uliozaa	urithi	
		boga	wangu,	
		hili,	ni	
		hukuupanda	urithi	
		sikuupanda;	wetu;	
		tulipozaliwa	boga	
		tuliukuta	hili	
		unastawi	basi,	
		shambani,	si	
		shamba	mali	
		tuliloachiwa	yako,	
		na	si	
		wazazi;	mali	
		maadam	yangu,	
		sisi	ni	
		wawili,	mali	
		tu	yetu;	
		warithi	basi	
		wa	nasisitiza,	
		shamba	tulikate	
		hili,	sehemu	
		utajiri	mbili,	
		uliomo	sehemu	
		shambani,	sawa,	
		si	yako	
		urithi	na	
		wako	yangu.	

Msanii vilevile ametunga shairi-picha jingine liitwalo “Nyumba” (uk. 17) lenye umbo la nyumba. Amelijenga kwa maneno na msisitizo wake ni kuwa wale ambao hawakushiriki kuijenga hawapaswi kuishi mle ndani ila tu wale ambao “misuli yao iliipa uhai” (uk. 17). Anaeleza juhudi za maskini katika kujenga nyumba hiyo ambao ndio wenye haki ya kuishi humo. Kwa hivyo, ni haki ya wanyonge kufaidi juhudi zao bila kunyanyaswa na mabwanyenye. Kwa mujibu wa mshairi, nyumba inarejelea nchi ambayo inajengwa na wananchi wanaojitolea kufanya kazi katika sekta mbalimbali.

	nyumba	
	hii ambayo	
	ilifumwa	kwa
	mawe	yaliyoumbwa
	na	maumbile,
	mawe	ambayo
	yalisongwa	na
	maskini,	nyumba
	hii	ambayo
	ilisimamishwa	kwa
saruji		itokanayo
na		viungo
vya ardhi		vilivyochimbwa na
yahe,		nyumba
hii		iliyoezekwa
vigae		vitokanavyo
na		udongo
kimano		tuliourithi
kutoka		mama,
nyumba		hii

**iliyopambwa kwa vioo vilivyotengenezwa na
matambara, kwa nini wasistarehe katika nyumba
hii wale ambao misuli yao iliipa uhai**

Katika shairi “Kiwambo cha Televisheni” (uk. 37), mwandishi anaonyesha matabaka mawili katika jamii yanayowakilishwa na wahusika wawili ambao ni Sauti 1 na Sauti 2. Mhusika Sauti 1 anawakilisha tabaka la wanyonge wanaodhalilishwa ilhali mhusika Sauti 2 anawakilisha tabaka la matajiri. Tabaka la matajiri linawanyonya watu maskini. Mshairi analalamika:

SAUTI 1: Kwa nini
 Nuru ya miale ya jua
 Ikumulikie maisha pekee
 Wakati nilipo
 Giza larindima ja radi?

SAUTI 2: Ni-ni-no!
Ni-ni-no!

SAUTI 1: Kwa nini
Maji yatokayo angani
Yakufaidi shamba pekee
Wakati nilimapo
Ukame wasongoa ardhi shingo?

III

SAUTI 1: Kugeuzwa yonda
Nimekataa, katakata!

Mali ya mama
Ni haki yangu
Ni haki yako
Basi ya kugawa
Baina yetu (kur. 37-39)

Mhusika wa 1 ambaye anawakilisha watu maskini amejawa na ghadhabu anapomuuliza maswali Mhusika wa 2 ambaye anawakilisha matajiri. Mhusika wa pili naye anajibu maswali hayo kwa kiburi huku amekodoa macho. Kuna ubishi kati ya tajiri na maskini kuhusu umuhimu wa usawa na haki baina yao. Matajiri wanapenda kuwatumia watu maskini wawafanyie kazi. Wafanyakazi wanapohisi kuwa wanadhulumiwa, wanaanza kudai haki ya malipo sawa na mazingira mazuri ya kufanyia kazi jambo ambalo linawakasirisha matajiri. Matajiri hao wanawachukulia hatua za kuwafuta kazi au kuwapeleka kortini ambapo wanahukumiwa hukumu isiyo ya haki.

Kupitia maudhui haya ya ubepari na unyonyaji, ile kanuni ya nadharia ya baadaukoloni kuwa nguvu za upanuzi na ulafi wa kiuchumi zilizoonekana katika historia ya ubeberu na ukoloni inajitokeza bayana. Vitendo vya utumwa, unyanyasaji na uporaji wa mali vinashuhudiwa katika jamii za Kiafrika leo hii. Kithaka wa Mberia anatetea wanyonge kwa kumulika madhila wanayotendewa wafanyakazi wanaofanya kazi katika mazingira mabaya na kulipwa mishahara duni.

5.2.2 Ukahaba, Uasherati na Usenge

Ukahaba ni tabia ya mwanamke kushiriki mapenzi kama njia ya kujiruzuku. Uasherati nao ni kitendo cha kushiriki mapenzi na mtu kwa nia ya kuridhisha hisia za kimwili tu bila nia ya kutafuta pesa. Kwa upande mwingine, usenge ni hali ya mwanamume kufanya mapenzi na mwanamume mwenzake. Maudhui ya ukahaba yanapatikana

katika diwani ya *Bara Jingine* ambapo kuna mashairi kama “Mimi Monika” (uk. 37), “Wanabiashara Barabarani” (uk. 43) na “Mwashi Mahiri” (uk. 45). Maudhui ya uasherati yanajitokeza katika diwani ya *Redio na Mwezi* katika mashairi: “Msimu wa Kaburi!” (uk. 3), “Mgeni Katili” (uk. 4), “Biringanya na Matikiti” (uk. 28), “Vituko Mjini” (uk. 40) na “Matumizi Mengine” (uk. 41). Katika diwani ya *Msimu wa Tisa* kuna mashairi “Miche Pweke I” (uk. 54) na “Micha Pweke II” (uk. 55). Tabia ya usenge inapatikana katika diwani ya *Redio na Mwezi* katika shairi “Dude – Dubwana Mahakamani” (uk. 32).

Mwingiliano na wageni, tamaduni hasa za kimagharibi na mfumo mpya wa maisha umechangia ukahaba, uasherati na usenge kuonekana mambo ya kawaida katika jamii ya leo. Vitendo hivi vinachangia kuvunjika kwa ndoa nyingi, dhuluma za kinyumbani zinazoumiza na kusababisha vifo, kusambaa kwa magonjwa ya zinaa pamoja na ugonjwa hatari wa ukimwi.

Katika diwani ya *Bara Jingine*, shairi “Mimi, Monika” (uk. 37) linagusia maisha ya mwanamke anayeteseka akifanya ukahaba na wanaume wengi kwa kipindi cha miaka kumi ili kujikimu kimaisha. Anajikuta kwenye nyumba za mawe, vyumba vya hoteli na sakafu za polisi. Wakati mwingine halipwi na wateja wake. Athari moja ya kitendo cha ukahaba siku hizi ni vifo vinavyotokana na maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi. Aidha, wanawake wanapata mimba na kuzaa watoto nje ya ndoa. Kwa wanawake, ukahaba ni njia ya kujitafutia riziki lakini kwa wanaume ni njia ya kujistarehesha na kujifurahisha. Hata hivyo, katika shairi hili, mwanamke huyu hafanyi hivyo kwa kupenda bali kwa sababu ya hali ngumu ya kiuchumi na ndio maana amevumilia mateso mengi kwa miaka mingi. Ajabu ni kwamba utamaduni huu mgeni kiwakati unaruhusiwa na kuonekana kama jambo la kawaida katika jamii. Mshairi anasema:

Kwa miaka kumi ya dhiki
Mwongo wenye uzito wa karne
Nimerandaranda kwenye veranda
Na kusimama pembeni
Nikisubiri kunyaka nafasi
Kuhudumia ulimwengu
Kwa tabasamu chungu

Kama mlango wa umma
Nimeguswa na viganja milioni,
Kama jumba la mikutano

Nimetembelewa na halaiki ya watu
Kutoka kila pembe ya ulimwengu (uk. 37)

Katika shairi “Wanabiashara Barabarani” (uk. 43), msanii vilevile anaeleza kinagaubaga chanzo cha ukahaba miongoni mwa kina dada ambao hurandaranda kwenye barabara za miji wakiendeleza biashara haramu hasa nyakati za usiku. Wanatumia njia hatari za mkato kujichumia riziki maishani. Kwa mujibu wa mshairi, uvivu wa kutotia bidii masomoni na kukata tamaa ndiko kunawachochea baadhi yao kushiriki utovu huu wa kimaadili. Hata hivyo, wengine wanajipata wakifanya biashara hii baada ya kudhulumiwa kimapenzi na jamaa zao wa karibu kama vile baba, ami, jirani na wengine ambao si jamaa wa karibu bali wahuni. Mtunzi anaeleza:

Ndio, mhubiri
Hubiri dhidi ya uvivu
Na matarajio hatari
Ya kusafiria njia ya mkato
Katika maisha
Baadhi ya hawa
Ni wajanja ambao
Walitaka kuepuka jasho
Darasani na maktabani,
Ndio, mhubiri
Hubiri dhidi ya kukata tamaa (uk. 44)

Mbali na kumulika ukahaba kama njia ya kujitafutia riziki kwa njia ya mkato, mshairi anaangazia uasherati. Haimaanishi kuwa uovu huu haukuwepo miaka mingi iliyopita lakini ilivyo sasa ni kuwa visa vingi vinaonekana bayana ambapo watu hufumaniwa ndani ya magari, vichakani, ofisini, nyumba za wenyewe na kwenye madanguro wakiendeleza uovu huu si mchana si usiku. Visa hivi vimekuwa ni mambo ya kawaida. Ajabu ni kwamba hata vijana wameshika mkondo huo. Kwa sababu hiyo, mtunzi anaonekana kukerwa na jambo hili kwa vile analaani na kukemea vitendo kama hivi.

Kunayo mashairi kadha katika diwani ya *Redio na Mwezi* yanayogusia maudhui ya uasherati. Kwa mfano, katika shairi “Biringanya na Matikiti” (uk. 28) mshairi anawatahadharisha wanawake na wanaume dhidi ya kushiriki mapenzi nje ya ndoa kiholela kwa sababu kuna hatari ya kuangamia kutokana na ugonjwa wa ukimwi. Wanaume na wanawake walio kwenye ndoa hawafai kushiriki mapenzi nje ya ndoa kwa sababu wanaweza kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi. Wakiambukizwa ugonjwa wa ukimwi wataangamia waache watoto mayatima. Watoto wakibaki mayatima

watapata shida za elimu, chakula, mavazi na mapenzi ya wazazi. Watoto wengine wataishia kuzurura mitaani wakiomba au hata kuwa wezi na majambazi. Mshairi anasema:

Wanawake simile! Dunia imechafuka!
Sumu imemwagikia Bustani ya Edeni
Biring'anya zinazosisimua ndoto
Msizitamani mkazikimbilia kwa pupa:
Mumo humo mna ndwana za mauti!

Wanaume habedari! Kaburi zinanyemelea!
Kutangatanga ovyoovyo katika Bustani
Mkila vipande vitamutamu vya matikiti
Ni kujitia kitanzi cha waya wa chuma:
Matikitini kimejificha chambo cha mauti! (uk. 28)

Ujumbe huu wa uasherati na matokeo yake unapatikana vilevile katika shairi “Msimu wa Kaburi!” (uk. 3). Mshairi anaeleza vile mtu hushawishika kujiingiza katika uasherati, huambukizwa ukimwi, ishara za ugonjwa wenyewe na hatima ya kifo kwa mhasiriwa. Anasema:

Jana, walioteleza, hawakuanguka
Penicillin iliwahimili na kuwainua,
Waliostarehe katika Bustani ya Edeni
Hawakufuatwa na kuangushwa na kaburi,
Leo, maisha yameingiwa na giza katili

Kifo, mbona unajificha katikati ya magoti
Mwanadamu aendaye mandari kiholela
Hushtukia kamba imejipanga shingoni
Punde inaikaza kwa mikono thabiti
Aliyekuwa na afya imara kama kigongo
Unamgeuza mifupa na ngozi yenye vidonda
Kabla ya kumwangusha kaburini kwa shindo? (uk. 3)

Mshairi, vilevile anakerwa moyoni na ugonjwa wa ukimwi unaoenezwa kupitia uasherati. Ugonjwa huu unaathiri watu wote: maskini, wataalamu, mawaziri, wabunge na wanajeshi miongoni mwa wengine wengi. Anatoa ujumbe huu katika shairi “Mgeni Katili” (uk. 4) katika diwani ya *Redio na Mwezi*. Kupitia kwa maelezo ya kuogofya, anaonyesha vile mhasiriwa anakonda na kuwa na sura ya kutisha kabla ya kufa. Mshairi anasema:

Wewe, katili jambazi la kutisha
Mgeni ambaye hakualikwa, hakutarajiwa
Mchinjaji kicheko, mhandisi wa huzuni
Mpenzi wa mifupa ya mavani, izraeli,

Kwa viganja laanifu, kwa furaha tele
Mjanja, unawazuzua wanawake na wanaume
Unawarai kwa asali uliochanganya na sumu
Unawaleweshwa kwa sumaku ya maumbile
Kisha, unawakamua kila tone la uhai
Na kuwatupa kaburini wakavu kama kuni (uk. 4)

Katika shairi “Matunda Haramu” (uk. 39) mshairi anaonyesha bayana udanganyifu wa wanandoa katika kufanya mapenzi nje ya ndoa licha ya kuvishana pete kama ishara ya mapenzi na ndoa thabiti. “Matunda haramu” ni kule kushiriki mapenzi na mtu asiye mke au mume wako kihalali. Anasisitiza kuwa huu ni usaliti mkubwa. Mshairi anafafanua:

Furaha inawayeyusha
Katika pinde za mvua
Katika anga za kigeni
Kinyume na viapo vitamu
Walivyokula hadharani

Wasaliti wa taasisi!
Huchuma raha haramu,
Na kuondoka faraghani
Wakibeba kumbukumbu
Ya karamu marufuku (uk. 39)

Kwa mujibu wa mshairi, visa vya uasherati siku hizi vinatendwa hata mahali ambapo hapastahili ili kutosheleza hisia za kimwili. Kwa mfano, katika shairi “Vituko Mjini” (uk. 40) anakejeli kitendo hiki anaposema kuwa huwa kinafanyika ofisini kwenye mazulia wakati wa jioni na ndani ya magari yaliyoegeshwa kando ya barabara usiku. Vitendo kama hivi havifanyiki kwenye majengo na magari mijini tu bali vinatekelezwa mashambani kwenye misitu, mashamba ya majani-chai, kahawa, miwa na mahindi punde giza linapoingia. Msanii anazungumzia kitendo hiki kwa njia ya kejeli:

Nakuonya, nakukanya
Baada ya watu kuhama
Kutoka mijengo ya jiji
Milango ya ofisi
Usiifungue kwa kasi
Kwani, ewe usiyejua
Utagutushwa na pepo
Wakicheza chakacha
Kwenye mazulia! (uk. 40)

Vitendo vya uasherati vilevile vinazungumziwa na mshairi katika shairi “Matumizi Mengine” (uk. 41). Watu wanazima kiu zao za mapenzi kwenye mazulia ya ofisi, mito ya kukalia viti vya ofisi na viti vya magari ambapo uchafu wa ngono huweza kuonekana. Msanii anaeleza:

Nyakati za nyuma
Mazulia ya ofisi
Kamwe sikuyashuku...

Nyakati za nyuma
Matakia ya ofisi
Abadani sikuyaogopa...

Nyakati za nyuma
Viti vya magari
Havikunighasi moyo ...

Kumbe nilidanganyika
Rangi za chakacha
Zimetambalia huko
Kama mitambazi
Ya matango (uk. 41)

Mbali na uasherati, kitendo kingine kinachokera mshairi ni usenge. Msimamo wa dini ya Kiislamu na Kikristo ni kuwa mwanamume anafaa kujuana kimwili na mtu wa jinsia ya kike. Aidha, mila na tamaduni za Kiafrika hazikuruhusu wala hazijaruhusu kitendo kama hiki miongoni mwa wanaume. Lakini, kitendo hiki kimepuuzwa kwani siku hizi mwanamke kwa mwanamke au mwanamume kwa mwanamume hushiriki mapenzi. Ni jambo ambalo limeanza kuonekana wazi katika jamii za leo kwa sababu ya mwingiliano wa tamaduni za kigeni. Msanii anaeleza kwenye shairi “Dude-dubwana Mahakamani” (uk. 32) katika diwani ya *Radio na Mwezi* namna mwalimu wa dini alivyowalawiti wanafunzi wadogo wa kiume. Kisa hicho kilisababisha mwalimu kufikishwa mahakamani ili kufunguliwa mashtaka. Watu waliofika mahakamani wanashangazwa na maelezo ya watoto kuhusu unyama aliowatendea mwalimu wao wa dini. Mshairi anaeleza:

Wanafunzi wachanga wa kiume
Walinung'unika kwa wazazi
Walitaja yasiyotajika kwa uchungu
Sikio la serikali lilisikia fununu
Mkono wake mrefu ukafikia mtuhumiwa,
Mahakamani, siku ya ukweli kujiri
Watoto walieleza yaliyowakumba
Kinyume cha sheria na haki

Kinyume cha maumbile na miiko,
Walimvua mwalimu kofia na kanzu (uk. 32)

Mtunzi anaeleza kuwa mwalimu huyu ni shetani, nduli, msaliti wa dini na imani licha ya kuwa ni mchafuzi wa maadili na mienendo. Anamlinganisha na kidutu yaani uvimbe mdogo unaotokea kwenye ngozi ya mtu. Kwa hivyo, kitendo cha mwalimu huyu ni cha aibu kulingana na utamaduni wa jamii hasa za Kiafrika.

5.2.3 Vileo na Mihadarati

Katika jamii za Kiafrika, vileo kama “busaa” na chang’aa vilitumiwa na wanaume na wanawake wazee kama njia ya kujiburudisha baada ya kazi au wakati wa sherehe. Kulikuwa na sheria zilizodhibiti matumizi ya vileo dhidi ya makundi fulani kama vijana na wanawake wachanga. Lakini hali sivyo tena katika jamii ya leo. Wanawake, wasichana na wavulana hasa wanafunzi wanashiriki katika ulevi, uvutaji wa bangi na sigara bila kujali. Kulingana na mshairi, baadhi ya wazazi wanashiriki na wana wao katika unywaji wa pombe badala ya kuwashauri na kuwakemea dhidi ya kitendo hicho. Tabia hii ya unywaji pombe ovyo, uvutaji wa bangi na sigara na matumizi ya dawa zingine za kulevya ni tabia ngeni ambayo inaathiri mfumo wa maisha kwa wanawake na wanaume. Suala la vileo na matumizi ya mihadarati linashughulisha serikali ambayo inaunda sheria za kudhibiti utumizi wa vileo na dawa za kulevya.

Katika diwani ya *Bara Jingine* katika shairi “Ni Sumu kwa Watoto (uk. 49), mshairi anaeleza chanzo cha matumizi ya pombe na dawa za kulevya hasa kwa vijana. Kutokana na maelezo ya mshairi ambayo tunakubaliana naye, wazazi wengine wanachangia watoto wao kuvuta sigara na dawa za kulevya. Wanawapatia watoto pesa nyingi kama ishara ya mapenzi kwao. Watoto hao huwa hawana mambo muhimu ya kufanyia pesa hizo ila wanajaribu kuzitumia kwenye sigara na dawa za kulevya za kunusa, kunywa au kujidunga sindano. Uraibu wa matumizi ya dawa za kulevya unasababisha vifo kwa watoto hao. Mshairi anafafanua:

Ni sumu, sumu jeruhi
Unajeruhi watoto
Kwa mapenzi yako hatari
Ya kuliwaza watoto kwa pesa,
Pesa chungu nzima ambazo
Zinawafikisha kwenye sigara na ulevi
Na kisha kwenye dawa za kulevya
Barabara nayofikisha kwenye giza baridi
La kaburi la asubuhi (uk. 50)

Ujumbe wa mtunzi ni kuwa madhara ya pombe pia yanawaathiri hata wasomi. Vijana waliosoma hadi vyo vikiu na wakafuzu badala ya kutafuta kazi ili wapate pesa za kujikimu na kuanzisha familia zao, wanalewa na kuanza kuomba marafiki nauli na malazi. Wanakuwa mzigo na kielelezo kibaya kwa wengine katika jamii. Mshairi katika diwani ya *Redio na Mwezi* anasema kuwa watu hao huwa na upweke na hukosa mwelekeo maishani. Katika shairi “Tembo” (uk. 56) tunasoma:

Atingekuwa mnyonge, mkata, dhalili
Angekuwa anajiweza, anajichumia riziki
Mwavuli wa shahada yake ya chuo kikuu
Ungemkinga ukatili wa jua la ulitima...
Atingekuwa akiomba marafiki nauli daima
Atingekuwa anawasumbua jamaa kupata malazi
Angekuwa na kazi, makazi, labda familia
Lakini tembo lilimtaka urafiki, akakubali
Wakawa masahibu, wakaiga chanda na pete ... (uk. 56)

Isitoshe, katika shairi “Rafiki Katili” (uk. 57) msanii anaeleza bayana matokeo ya kushiriki ulevi miongoni mwa wanaume na wanawake. Kutokana na maelezo ya mshairi katika shairi lenyewe, madhara ya tembo likishaingia mwilini mwa mtu ni wazi, iwe mijini au mashambani. Mtu akishalewa anaanza kuropokwa maneno kiholela. Watu wengine wanadondokwa na mate na hata kulala ndani ya mitaro baada ya kuishiwa na nguvu. Fauka ya hayo, watu wanapigana kwa ngumi, panga na hata bunduki kiasi cha kuuana. Madereva walevi wanasababisha vifo barabarani kwa kuendesha magari kwa kasi bila kuzingatia sheria za barabarani. Wanandoa wanapigana, mbali na kushiriki mapenzi nje ya ndoa kwa sababu ya ulevi ambapo wanaambukizwa ugonjwa wa ukimwi na kisha kufa. Akizungumzia juu ya madhara ya pombe mwilini, msanii anaeleza:

Unawafanya werevu kuwa zumbukuku
Na kuwavuta kwa sumaku ya izraeli
Na kuwaingiza kwenye wingu laanifu,
Virusi vinawafunga minyororo
Na kuwavuruta hadi kaburini,
Tembo, huwezi kukana yaliyo wazi
Unasababisha mieleka nyumbani
Unachoma amani kwa moto wa ugomvi
Na kuifanya nyumba kuwa medani,
Visu vinapasua mapafu na figo
Panga zinashtua mifupa na mishipa
Risasi zinapiga mbizi vifuani
Badala ya ndoa, kunabaki jivu (uk. 59)

Shairi “Evergreen Ltd.” (uk. 49) linazungumzia anasa katika klabu moja. Watu wanatoka sehemu mbalimbali, karibu na hata nje ya nchi ili kujifurahisha. Katika klabu hii ambayo anaiita “Evergreen” kwa maana ya raha na anasa inayodumu, kuna harufu ya pombe, mairungi na pumzi za mioshi mbalimbali. Kuna unywaji wa vileo na mihadarati ya kila aina. Kutokana na nguvu za vileo na mihadarati mwilini, watu wanafanya mambo ya ajabu na pengine kujuta kwa kuambukizana magonjwa ya zinaa. Baadaye ulevi ukiwatoka huogopa gharama za dawa kwa magonjwa walioambukizana katika vituko walivyofanya. Mshairi anasema:

Hii ndiyo Evergreen Ltd
Ambamo, wananchi
Kutoka humu na mbali
Hukutanika kikaoni
Kuvuta na kutafuna
Kunywa na kutazama
Na kwa wasiojali
Kugusa na kuguswa
Na pengine, kesho yake
Minyororo ya tembo
Inapokatika akilini
Kujutia kumbukumbu
Za visa vikuu vya jana
Na kuhofia gharama
Za kulipia penicillin! (uk. 49)

Ingawa biashara ya dawa za kulevya ni chanzo cha kujipatia riziki kwa wanaouza dawa hizo, kero kubwa ni madhara yake hasa kwa watoto. Kuna sheria kali zinazodhibiti ulanguzi wa dawa za kulevya lakini wahusika wakuu hawajali kamwe. Kithaka wa Mberia katika diwani ya *Msimu wa Tisa* anazungumzia juu ya watoto wenye macho mekundu kwa sababu ya kutumia dawa za kulevya. Shairi “Macho Mekundu” (uk. 59) linazungumzia bayana juu ya athari za dawa za kulevya kwa watoto. Watoto hao wachanga wanaenda kunywa pombe na kutumia dawa zingine za kulevya katika vilabu na vituo vingine vya kuuzia dawa hizo. Wanashiriki vitendo hivyo haramu. Shida kuu inatokea wanaporudi nyumbani wakiwa walevi chakari na kudhulumu watu wasio na hatia. Msanii anaeleza kwa uchungu hivi:

Moyo wangu una uchungu mkali
Unateswa na miiba ya hii picha
Unalizwa na majonzi ya watoto,
Ole wao! Kama wanyama wa porini
Watoto wanaishi katika mbuga katili,
Kama nyani, kima na tumbili

Wanajihimili kwa kula matunda-mwitu
Mpaka watakaporejea vijijini walikozaliwa
Kunyang'anya wakaazi vyakula
Wakiwakata koo wazazi na majirani
Na kuwabaka ndugu na binamu wa kike
Thibitisho la ujasiri na utiifu imara
Kwa majemedari waliowateka nyara
Na kuwafanya mtambo wa mauti (uk. 59)

Mshairi anakemea vikali vitendo vya ukatili vya vijana kuibia watu vyakula vijijini, kukata koo wazazi na majirani na vilevile kubaka watoto wa kike kwa sababu ya ulevi na utumizi wa dawa za kulevya. Matumizi ya vileo na dawa za kulevya miongoni mwa vijana ni jambo geni ambalo halikuwepo wala kukubaliwa katika jamii nyingi za Kiafrika miaka ya nyuma. Lakini kwa sababu ya usasa, limekuwa jambo la kawaida na donda sugu licha ya sheria na hatua kali zinazochukuliwa kukomesha tabia hii. Watoto wanapuuza ushauri na maonyo ya wazazi kuhusu ulevi na matumizi ya mihadarati. Watoto hao hufuata shinikizo la marafiki zao na mwishowe hujuta maishani.

5.2.4 Ubaguzi

Ubaguzi ni mfumo wa kijamii wa kutoa huduma kwa upendeleo kwa misingi ya rangi, jinsia, tabaka na kabila. Mfumo wa maisha ya sasa umeibua dhana ya ubaguzi. Hili ni suala ambalo mshairi analiibua katika ushairi wake. Ubaguzi, ambao ni dhana ya “wingine” unachangiwa na elimu, uwezo wa kiuchumi wa mataifa yaliyoendelea, uhaba wa huduma muhimu, ufisadi na rangi ya ngozi. Wamitila (2003a) anaeleza wingine kuwa ni kumbagua mtu, asasi au kundi fulani. Dhana ya wingine katika nadharia ya baadaukoloni inaangazia namna watu wengine wanajiona kuwa bora na tofauti kuliko wenzao kwa sababu ya rangi na uwezo wao wa kiuchumi.

Kithaka wa Mberia anaangazia suala la wingine katika jamii. Kwa mfano, ubaguzi wa rangi unaonekana wazi katika diwani ya *Msimu wa Tisa* katika shairi “Muuaji Mwenye Furaha” (uk. 22). Mshairi anaeleza jinsi mwanajeshi wa kigeni mwenye ngozi nyeupe alimuua mwanamke Mwafrika kwa ncha kali ya chupa na akaachiliwa huru badala ya kuhukumiwa adhabu kali kama wauaji wengine wanavyofanyiwa baada ya kupatikana na hatia. Mwanajeshi huyo anaenda kwao ughaibuni baada ya kuvuka Atlantiki na kupokelewa kwa furaha na watu wao. Kwa familia ya mwanamke

Mwafrika aliyeuawa inakuwa ni kilio cha kutotendewa haki dhidi ya muuaji. Kwa kutumia tashtiti, mshairi anasema:

Kumbe! Sheria za taifa zina macho yasiyohitaji miwani
Zinaona na kutambua vyema ngozi za washtakiwa
Kwa nini mahakama ichanganywe weupe na weusi!! (uk. 22)

Kwingine ubaguzi wa rangi unaonekana katika shairi “Darfur” (uk. 26). Mshairi anazungumzia masaibu ya watu wenye ngozi nyeusi katika nchi ya Sudan. Watu weusi wanawekewa vikwazo wasipate rasilimali ya taifa lao mbali na kunyimwa nafasi ya kuongoza nchi yao. Aidha, watu weusi wanaonewa na kudhulumiwa sana, jambo ambalo linaamsha msukosuko wa kudai wapewe haki, heshima na shibe.

Tunasoma:

Kutemewa mate kwa kuwa na ngozi nyeusi
Na kuwekewa vikwazo wasifikie sinia ya taifa
Kunyimwa kauli kuhusu usukani wa nchi
Na kupagazwa uzito wa maonevu na dhuluma
Kuliwasha nyoyo moto uliowaka bila kuzima
Wa kudai haki, heshima na shibe (uk. 26)

Kithaka wa Mberia anaeleza juu ya mashambulizi ya “wageni” yanayochochewa na wanasiasa katika shairi “Wahalifu Huru” (uk. 30). Wanasiasa wanachochea ghasia za ukabila ili watu wasio wenyeji wafukuzwe kutoka katika nyumba zao. Wageni wanachomewa nyumba zao, maghala ya vyakula na watu wengi wanauawa katika ubaguzi wa kikabila. Kwa mujibu wa mshairi, wanasiasa waliochochea uhasama wa makabila hawachukuliwi hatua yoyote kisheria kwa sababu wao ni wakubwa serikalini. Mshairi anasema:

Bali katika wingu la unafiki wa “amani, upendo na umoja”
Badala ya wahandisi wa jakamoyo kutetemeka mahakamani
Badala ya wenye damu viganjani kutupwa korokoroni
Wanaendesha mashangingi yenye bendera za mamlaka
Wanalipwa mishahara minono wakiitwa “viongozi wa taifa”! (uk. 30)

Watu wenye nyadhifa kuu katika jamii wanapokiuka sheria, hawachukuliwi hatua kali kwa mujibu wa sheria. Lakini mtu wa cheo cha chini akifanya kosa huchukuliwa hatua kali mara moja kwa sababu hana uwezo wa kujitetea au kununua “haki”. Sheria inatumiwa kumbagua mnyonge katika jamii.

Kuna ubaguzi wa uwezo wa kiuchumi na nguvu kati ya mataifa yaliyoendelea dhidi ya mataifa yanayoendelea. Inaaminika kuwa kuna mataifa manane ulimwenguni

yenye usemi mkubwa kiuchumi, kiteknolojia na nguvu za kitororadi. Mataifa hayo ni pamoja na Marekani, Uingereza, Japani, Ujerumani, Urusi, Kanada, Italia na Ufaransa. Akizungumzia jambo hili katika shairi “Mkasa” (uk. 13), mshairi anaeleza namna kitendo cha ugaidi kilitekelezwa dhidi ya ubalozi wa Marekani mjini Nairobi, Kenya mnamo tarehe saba Agosti mwaka 1998. Gari la manjano lililobeba mabomu na vilipuzi lilipuliwa na magaidi. Watu wengi walikufa jijini na wengine wakapata majeraha kwenye miili yao na mali kuharibiwa kutokana na shambulizi hilo. Watoto wengi walibaki mayatima kwa sababu wazazi au walezi wao waliangamia. Hili ni tukio la kihistoria linaloonyesha wazi matokeo ya ubaguzi kutoka kwa mataifa yenye uwezo kwa mataifa yasiyo na uwezo kiuchumi na kiteknolojia. Ndio maana mpaka leo kuna misururu ya mashambulizi kwa vile mataifa yanayoendelea yanahisi kuwa yanabaguliwa na kunyanyaswa. Mataifa yanayobaguliwa kwa kunyimwa uwezo wa kujiendeleza kiuchumi na kiteknolojia hulipiza kisasi kupitia ugaidi ili kuthibitisha uwezo na uwepo wao pia. Mataifa yaliyostawi nayo hulenga kudhibiti nguvu na uwezo wao kwa mataifa machanga kupitia kuyawekea vikwazo vya uchumi, misaada na uwezo wa silaha za maangamizi. Mshairi anasema:

Urafiki wetu na wenye maadui wasioogopa kufa bora waue
Umetugeza nyasi ya kijani katika uwanja wa vita vya fahari (uk. 17)

5.2.5 Unafiki wa Kidini

Dini ni mfumo wa imani ya mtu ambao unamfanya kuamini kuwa Mungu yupo, ndiye muumba na mwenye uwezo wa kutawala maisha yake. Mbali na kumsaidia muumini kuwa karibu na muumba na kujitolea kufanya mambo yanayompendeza Mungu, dini inafaa kukuza maadili miongoni mwa wanadamu. Lakini katika ushairi wa Kithaka wa Mberia, dini inaonekana kuchangia uovu hasa pale wachungaji na waumini wanafanya kinyume na mafunzo ya dini. Dini hasa ya Kikristo ni utamaduni mgeni ulioletwa na wamishenari na kuenezwa katika mataifa ya bara la Afrika.

Kulingana na Kithaka wa Mberia, dini haijawakomboza wanadini na kuwaweka huru dhidi ya ushawishi wa tamaa za mwili. Kwa mfano, katika diwani ya *Redio na Mwezi*, shairi “Muumini” (uk. 29) linazungumzia mwenendo wa mwanamke muumini ambaye anasujudu kanisani na kumwomba Mungu amsamehe kwa kosa alilofanya kwenye klabu usiku uliotangulia. Alikunywa pombe na kushiriki ngono na sasa anaogopa kuwa huenda aliambukizwa virusi vya ukimwi. Ameshika njia panda, anashiriki kanisa na vilevile anapenda “mambo ya ulimwengu”. Mshairi anaeleza:

Muumini anajenga njia ya kuingia mbinguni
Ili siku ya kusafiri, asafiri bila vizuizi
Au jana, Jumamosi, baada ya kikao cha pombe,
Baada ya akili kulemaa, mwili ulimhadaa
Bila tahadhari, kiholela, akapanda angani
Na kukata rumba ukumbini mwa upinde-wa-mvua
Na sasa, akitapatapa katika bwawa la hofu
Anaomba Mola amwepushe na tanzi la virusi
Ili kaburi lisimbusu busu la kumkaribisha
Na kumkumbatia, ili pamoja, wadumu milele (uk. 29)

Katika shairi “Mchungaji na Muumini” (uk. 31) mwandishi anaonyesha unafiki wa hali ya juu pale mchungaji wa kanisa anafanya mapenzi na muumini wake katika lindi la usiku. Ni kinaya kwamba wawili hawa wanafanya kinyume cha mafundisho ya Biblia. Mshairi anaeleza:

Kesho asubuhi, mbele ya waumini, kwenye mimbari
Mchungaji atasimama, vazi lake na darizi azizi
Likiimba wimbo wa imani, likitangaza utakatifu
Likificha jazanda tamu za jana, lugha ya vilua
Likistiri siri ya wawili na ujanja wa kiroho
Likihimili wingu la kutojua miongoni mwa waumini
Maneno yake hayatakuwa ya mnafiki, fasiki mkuu...(uk. 31)

Kwengineko, katika shairi “Mhubiri na Mjinga” (uk. 42) mtunzi anaonyesha ujanja wa mhubiri na mke wa mtu wanapofumaniwa wakifanya mapenzi usiku nyumbani kwa mumewe. Mhubiri anakuwa na urafiki wa kimapenzi na mwanamke ambaye ni mmoja wa waumini wake. Anamtembelea mwanamke huyo nyumbani kwake na mume hamshuku mhubiri akifikiri ni matembezi ya kiroho. Mume anapopanga safari na kwa bahati mbaya anarudi ghafla usiku, anamfumania mhubiri na mkewe wakifanya mapenzi. Mume anakasirika kiasi kwamba anamuua mhubiri. Mshairi anaeleza:

Ujanja wa mwerevu
Na hasira ya mjinga
Ziligongana kama radi
Na kuzaa mkazi mpya
Wa Jamhuri ya wafu

Ilibakia huzuni
Kwa jamaa na marafiki
Za mtumishi wa Mungu
Na vikao mahakamani
Na mshangao kanisani (uk. 43)

5.2.6 Elimu ya Kigeni

Elimu ya kigeni ni kipengele kimojawapo cha utamaduni mahuluti katika jamii ya leo ambayo ililetwa na mkoloni akishirikiana na wamishenari. Elimu ya kigeni hufunzwa katika taasisi za elimu kama vile shule, vyuo na vyuo vikuu. Isitoshe, inasambazwa kupitia vyombo vya habari kama vile televisheni, redio, magazeti na tovuti. Kimsingi, elimu inayofundishwa shuleni hufunzwa kwa kutumia lugha ya mkoloni hasa Kiingereza. Vitabu vya kufundishia, kusomwa na mawasiliano mengi hutekelezwa kwa lugha ya Kiingereza kuliko lugha za wenyeji. Kulingana na mshairi, huu ni ukoloni mamboleo. Ni kwa sababu hii ambapo Ngugi wa Thiong’o katika kitabu chake *Decolonizing the Mind* (1986) alipendekeza kuwa badala ya kutumia lugha ya kigeni, Waafrika waanze kujieleza na kuzungumzia masuala yao kwa kutumia lugha zao za kienyeji.

Kithaka wa Mberia anaonyesha kuwa elimu inachangia kupanua mpaka kati ya wasomi na wasio wasomi na hivyo kuchangia kutokuwepo kwa usawa. Matajiri wanatumia uwezo wao kusomesha watoto wao katika shule nzuri na vyuo vya ughaibuni huku watoto wa maskini wakisomea katika shule duni au kutosoma kabisa. Kwa upande mwingine, hata ingawa watu wengi wamesoma, nafasi za kazi hazitoshi kwa wasomi. Vijana wengi waliosoma hawana kazi. Nafasi chache za kazi zilizopo zinashindaniwa. Hali hii inazua ufisadi kwa vile wasiostahili kupata kazi hupata kazi kwa mlango wa nyuma. Baadhi ya wasomi wanaokosa kazi, wanajiingiza katika uovu kama ukahaba, ujambazi na matumizi ya mihadarati kwa sababu ya kukata tamaa.

Katika suala la elimu, mwandishi anakejeli tabia za wahadhiri wa vyuo vikuu ambao licha ya kupewa taadhima kuwa ni wataalamu wa masuala mengi, baadhi yao hawana maarifa ya kujivunia. Anasema kuwa ukimuuliza mhadhiri maswali yaliyo nje ya yale alifunzwa na walimu wake basi atashindwa kukujibu. Shida ni kuwa amezoea kufunza kile alifunzwa na walimu wake. Hajafanya utafiti zaidi wa kupanua maarifa zaidi ya kile alichofunzwa. Katika diwani ya *Redio na Mwezi* katika shairi “Samaki Nje ya Maji! (uk. 16) mshairi anasema:

Katika anga nyerezi la usomi
Leo nilimkuta mhadhiri
Mwenye shahada ya kilele
Katika taaluma maalumu
Bali, umsukumapo kwa ulimi
Na kumtoa pahali pa mazoea

Alipowekwa na walimu wa jana
Anakwama kama samaki ambaye
Amesukumwa nje ya maji (uk. 17)

Aidha, mwandishi anaonyesha mshangao wake kwa walimu hasa maprofesa ambao licha ya usomi wao na jina lenyewe, wao si weledi kamwe. Kuna baadhi yao ambao uprofesa wao ni wa kutiliwa shaka. Katika shairi “Ugunduzi” (uk. 19), mtunzi anashangaa kuwa maprofesa hawa hawatoshani kielimu katika taaluma zao. Kuna walio na ujuzi mwingi kuliko wengine. Mtunzi anasema:

Profesa
Jina teule
Jina la kilele
Katika mlima wa usomi...

Katika milima maarufu
Kuna miti mitajika
Yenye majina marefu
Mithili miparamuzi

Yenye majina mapana
Mithili mibuyu
Bali:

Baadhi ya hiyo
Si mrefu
Kuliko miviru
Si mikubwa
Kuliko midimu! (uk. 19)

Kithaka wa Mberia akiendelea kumulika matatizo ya elimu katika vyuo vikuu, anaonyesha matatizo na uovu uliokithiri vyuoni. Katika shairi “Wafu Kiwandani” (uk. 20) mshairi analinganisha wahadhiri ambao hawajabobea sawasawa katika taaluma zao na wafu. Anashangaa kuwa si vigumu kukutana na mfu akibeba faili kuukuu, chaki na kifutio akielekea darasani. Anasema kuwa walimu kama hawa walipata nafasi hiyo ya kufundisha kupitia upendeleo na uufisadi. Maadam mtu anamjua mkubwa fulani basi atapata nafasi ya kufunza chuoni hata kama hakuhitimu vizuri. Mshairi anauliza kuwa ikiwa walimu hawa hawana maarifa ya kutosha, watafundishaje? Isitoshe, anaonyesha vile upendeleo na uufisadi umekithiri katika taasisi za elimu ya juu, jambo ambalo halistahili kufanyika kwani mtu anafaa kupewa nafasi humo kutegemea uwezo wake wa kielimu. Tunasoma:

Hawa maiti wanaotembea
Walitolewa makaburini
Na kuingizwa kiwandani
Kupitia mlango mchafu
Wa upendeleo na ufisadi... (uk. 20)

5.3 Mtindo Katika Utamaduni Mahuluti

Vipengele vya mtindo ambavyo tumejadili katika sehemu hii na namna vimesaidia kuendeleza maudhui mbalimbali katika utamaduni mahuluti ni kama vile tashihisi, sitiari, tashibihi, tasifida, maswali ya balagha, takriri, chuku, nidaa, oksimora miongoni mwa vingine vingi.

5.3.1 Tashihisi

Mshairi anapoeleza maudhui mbalimbali kuhusu dhana ya utamaduni mahuluti katika ushairi wake, anatumia tamathali ya tashihisi. Mtunzi ametumia tashihisi anapoeleza juu ya ubepari na unyonyaji. Anaeleza namna wakulima hawafaidiki kutokana na shughuli zao za kilimo lakini wasio wakulima wanafaidi pakubwa katika shairi “Wimbo wa Mkulima” (uk. 9) katika *Mchezo wa Karata*. Anasema:

Inakera sana moyo
Hii anga ambayo
Inawapa
Maziwa ya ng’ombe
Na mayai ya kuku
Wasiofuga
Ng’ombe
Na kuku
Na kutemea mate
Wafugaji! (uk. 9)

Mshairi anaeleza mateso wanayopata wakulima katika shughuli yao ya ukulima akisema kuwa anga inawapa maziwa ya ng’ombe na mayai ya kuku wasiofuga ng’ombe na kuku na kutemea mate wafugaji. Anga imepewa sifa ya kuwapa maziwa na mayai wasiofuga na kutemea mate wakulima halisi. Kutokana na tamathali hii, ni kinaya kuwa mtu asiye mkulima anafurahia jasho la mkulima ilhali mkulima hafaaidiki kwa mazao yake. Wanaofaidika ni serikali na wendakati. Mara nyingi wakulima wa mahindi, majani-chai, miwa na kahawa hulalamika juu ya kulipwa fedha kidogo kwa mazao yao. Huku ndiko kutemewa mate anakozungumzia mtunzi. Ina maana kuwa wakulima wanadharauliwa licha ya kazi nzuri wanayoifanya ili kulisha taifa.

Aidha, katika shairi “Jembe, Surupwenye na Kalamu” (uk. 26) mtunzi anasema:

Jembe limelalamika

Napanda mpunga
Napalilia migomba
Napura mawele
bali
Nasononeka

-Kwa ombwe tumboni (uk. 26)

Jembe ni kifaa cha kulimia au kupalilia shambani. Hakina uwezo wa kulalamika kama mtu. Lakini mshairi anatumia jembe kama taashira ya mkulima anayelalamikia unyanyasaji. Badala ya wakulima kupewa mbolea na mbegu kwa bei nafuu na kulipwa pesa nzuri kwa mazao yao ili kuwapa motisha kuzalisha mazao zaidi, wanadhulumiwa. Isitoshe, katika shairi “Kero” (uk. 28) mtunzi anaeleza:

Inakera moyo
Hii anga ambayo
Huwasonya njiani
Watokao mashambani
Na kusalimu kwa bashasha
Wanaoshinda kivulini
Chini ya mwembe
Wa umma (uk. 28)

Anga imepewa sifa ya binadamu ya kusonya wakulima na kusalimu kwa bashasha wasio wakulima ambao huzembea na kuzurura wakingojea kufaidi jasho la wakulima. Mtunzi anaonyesha kuwa ni kinaya kuwa wakulima hutaabika na kuchafuka mashambani wakulima, wakipanda, wakipalilia na kuvuna lakini watu wazembe wenye unafiki hufaidi mazao yao.

Katika shairi “Kiwambo cha Televisheni” (uk. 37), mshairi ametumia tashihisi pale anaposema, “**Ukame wasongoa ardhi shingo**”. Ukame umepewa sifa ya kusongoa na vilevile kuvunja ardhi shingo. Ardhi haina shingo. Mshairi anauliza:

SAUTI 1 : Kwa nini
Maji yatokayo angani
Yakufaidi shamba pekee
Wakati nilimapo
Ukame wasongoa ardhi shingo? (uk. 38)

Katika diwani ya *Bara Jingine*, katika shairi “Wanabiashara Barabarani” (uk. 43) mshairi anazungumzia maudhui ya ukahaba. Anaeleza namna makahaba

wanavyowashawishi wateja kwa ulaghai ili wapate riziki. Wanatumia macho na mavazi yasiyo na staha kuvutia na kunasa wateja ili wapate pesa. Anasema:

Katika barabara za miji
Husimama pembeni
Macho yao
Yakizungumza kwa ufasaha,
Mavazi yao
Yakitangaza nia imara... (uk. 43)

Mshairi anaposema kuwa “macho yao yakizungumza kwa ufasaha”, anaonyesha mikakati wanayotumia wanawake hao kutongoza wanaume kwa kufumba na kulegeza macho yao ili wawanase kwenye hiyo biashara yao. Aidha, mavazi yamepewa sifa ya kutangaza kama mwanadamu. Wanawake hao hawana budi kubuni mbinu za kuimarisha ufundi wao kibiashara.

Katika diwani ya *Redio na Mwezi* katika shairi “Msimu wa Kaburi” (uk. 3), mwandishi anaeleza vile watu wengi wanakufa kiholela kwa sababu ya ugonjwa wa ukimwi licha ya kampeni kali kuwa ugonjwa huu ni hatari sana. Mshairi anasema:

Kifo, mbona unajificha katikati ya magoti
Mwanadamu aendaye mandari kiholela
Hushtukia kamba imejipanga shingoni
Punde inaikaza kwa mikono thabiti...(uk. 3)

Kifo kimepewa sifa ya kujificha kama mtu pale mwandishi anasema, “Kifo mbona unajificha katikati ya magoti”. Kifo si mwanadamu ambaye anaweza kujificha. Isitoshe, katika shairi hili, kifo kimepewa sifa ya kuwa mjanja na mlaghai bila haya. Sifa hizi zinamsaidia mshairi kueleza juu ya kifo kwa uwazi. Kamba ambayo imepewa sifa za binadamu za kukaza kwa mikono thabiti, inamsaidia mshairi kuonyesha kuwa hatima ya kufanya mapenzi kiholela ni kifo baada ya kuambukizwa ugonjwa hatari wa ukimwi. Kule kukazwa kwa kamba ni dhahirisho la namna mhangana wa ukimwi huanza kuathirika kiafya polepole hadi akafa.

Kwengineko, katika diwani ya *Redio na Mwezi*, mwandishi amezungumzia juu ya maudhui ya ulawiti kati ya mwalimu wa dini na watoto wa kiume katika shairi “Dude-dubwana Mahakamani” (uk.32). Wavulana hao waliripoti kwa wazazi wao ukatili waliofanyiwa na mwalimu, fununu hizo zilifikia serikali ndipo mwalimu akatiwa mbaroni na hatimaye kufikishwa mahakamani. Mtunzi anafafanua:

Wanafunzi wachanga wa kiume
Walinung'unika kwa wazazi
Walitaja yasiyotajika kwa uchungu
Sikio la serikali lilisikia fununu
Mkono wake mrefu ukafikia mtuhumiwa (uk. 32)

Mshairi anahuisha serikali anaposema kuwa “sikio la serikali lilisikia fununu” na “mkono wake mrefu ukafikia” mtuhumiwa. Mtunzi anaonyesha kuwa serikali ina sikio la kusikia kama binadamu na ina mkono mrefu wa kumkamata mhalifu yeyote. Mwandishi anaonyesha kuwa serikali ina mbinu za kupeleleza siri za uhalifu unaofanywa kupitia idara ya upelelezi kisha inatumia askari kumtia mbaroni mshukiwa na kumfikisha mahakamani kama alivyofanyiwa mwalimu huyo.

Mwandishi pia ametumia tashihisi katika shairi “Tembo” (uk. 56). Tembo ni shairi linalozungumzia unywaji wa pombe na madhara yake. Anaeleza namna msomi mmoja anavutiwa na ulevi wa pombe badala ya kutafuta kazi. Hana makazi, familia na upweke unamzidia huku miaka ikisonga mbele. Mshairi anaeleza:

Angekuwa na kazi, makazi, labda familia
Lakini tembo lilimtaka urafiki, akakubali
Wakawa masahibu, wakaiiga chanda na pete (uk. 56)

Tamathali hii inaonyesha vile vijana waliosoma hujiingiza katika uraibu wa unywaji pombe na inakuwa vigumu kuacha tabia hiyo ya ulevi. Mshairi anasema kuwa “tembo lilimtaka urafiki”. Tembo halina kinywa wala maneno ya kumwambia mtu wawe marafiki. Tamathali hii inaonyesha vile mwanamume huyu msomi alijiingiza polepole katika uraibu huu. Matokeo ya uraibu huu ni kuwa anaomba marafiki nauli na kusumbua jamaa kupata mahali pa kulala kwa sababu hana makazi wala familia.

Katika shairi “Muumini” (uk. 29) katika diwani ya *Redio na Mwezi*, mtunzi vilevile anagusia maudhui ya unafiki wa muumini. Muumini anaenda klabu usiku kunywa pombe inayomfanya afanye mapenzi na mwanamume. Siku inayofuata anaenda kanisani akijifanya kutubu kosa lake Mungu amsamehe na amwepushie hatari ya kuambukizwa virusi kwa kitendo alichofanya. Anaogopa asife. Mshairi anaeleza:

Na sasa, akitapatapa katika bwawa la hofu
Anaomba Mola amwepushe na tanzi la virusi
Ili kaburi lisimbusu busu la kumkaribisha
Na kumkumbatia, ili pamoja, wadumu milele (uk. 29)

Katika dondoo hili, kaburi limepewa sifa ya binadamu ya kubusu, kukaribisha na kukumbatia. Sifa hii inaonyesha vile kaburi linaweza kumficha maiti baada ya kufukiwa udongo.

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa* katika shairi “Mkasa” (uk. 13), mwandishi anazungumzia shambulizi la kigaidi lililotekelezwa mjini Nairobi dhidi ya ubalozi wa Marekani mnamo tarehe saba, mwezi Agosti mwaka 1998. Anaeleza kwa masikitiko na majonzi makubwa jinsi watu wasio na hatia waliokuwa kwenye shughuli zao waliumia na wengine wakafa. Ugaidi ni donda sugu katika ulimwengu wa leo. Mtandao wa magaidi umesababisha hasara kubwa. Akizungumzia namna jengo karibu na ubalozi wa Amerika lilianguka baada ya kulipuliwa, mwandishi anasema:

Jengo karibu na ubalozi wa mwewe
Linashindwa kuhimili **hasira kali ya baruti**
Linakata tamaa na kugeuka fusi la takataka (uk. 13)

Kawaida binadamu ndiye huwa na hasira au hukata tamaa anapolemewa na hali au shida maishani mwake. Mshairi anaposema kuwa “jengo linakata tamaa” na kugeuka fusi la takataka anaonyesha nguvu kali za bomu lililolipuliwa siku ya mkasa, nguvu ambazo zilianguka “Ufundi Co-operative House” ikawa vifusi. Mkasa huo ni kumbukumbu ya kihistoria katika nchi ya Kenya. Vilevile, ni kielelezo cha misururu ya visa vya ugaidi vinavyoendelea kushuhudiwa humu nchini na kwengineko, duniani.

Aidha, kuna matumizi ya tashihisi katika shairi “Wahalifu Huru” (uk. 30). Mwandishi anaeleza kuhusu ubaguzi wa kikabila waliofanyiwa watu waliochukuliwa kuwa “wageni” katika makazi yao. Watu hao walichomewa nyumba zao, maghala, pamoja na maduka. Isitoshe, watu hao walichomwa mishale na kukatwa kwa mapanga. Mwandishi anasema kuwa, “**Mishale ilipiga mbizi** katika miili ya wakaazi wa makabila mengine, **panga za ghadhabu zilishuka** baina ya vichwa na viwiliwili...” (uk.30). Katika dondoo hili mishale imepewa sifa ya kupiga mbizi ilhali mapanga yamepewa sifa ya kuwa na ghadhabu. Maelezo haya yote yanaonyesha uhasama wa kikabila waliotendewa watu waliokuwa si wenyeji katika eneo hilo.

5.3.2 Sitiari

Katika diwani ya *Mchezo wa Karata* kuna sitiari zimetumika katika maudhui ya ubepari na unyonyaji. Mashairi “Boga” (uk. 2), “Nyuki, Ndege and Nyegere” (uk.10)

na “Jembe, Surupwenye na Kalamu” (uk. 26) ni sitiari zenye ujumbe fiche. Kwa mfano, katika shairi “Boga” (uk. 2) mwandishi anahimiza umuhimu wa usawa na haki katika ugavi wa rasilimali. Rasilimali inawakilishwa na **boga** lililogawanywa katika sehemu mbili zilizo sawa. Anapigania wanyonge wapate haki yao sawa na wenye uwezo katika jamii. Aidha, shairi “Nyuki, Ndege na Nyegere” (uk. 10) linasimamia makundi mawili katika uzalishaji mali. Mtunzi analinganisha **nyuki** wanaotengeneza asali na wafanyakazi wanaotia bidii kuzalisha mali ilhali **ndege** na **nyegere** ni matajiri au nchi zenye uwezo zinazokandamiza wafanyakazi kwa kunyonya mali yao. Unyanyasaji huu wa kiuchumi ni mfano mzuri wa ukoloni mamboleo.

Mshairi anapozungumzia madhila ya wakulima, wafanyakazi viwandani na walimu katika shairi “Jembe Surupwenye na Kalamu” (uk. 26) anatomia sitiari pia. Neno “**jembe**” linawakilisha wakulima kwa jumla, “**surupwenye**” linawakilisha wanaofanya kazi viwandani ilhali “**kalamu**” linawakilisha walimu. Watu hawa wote wanachapa kazi lakini ujira wanaolipwa haulingani na kiwango cha kazi wanazofanya ili kujikimu maishani mwao.

Katika diwani ya *Bara Jingine*, sitiari imetumika katika shairi “Mwashi Mahiri” (uk. 45). Katika shairi hili mtunzi anawahimiza kina mama kunyonyesha watoto ili wawe na afya njema ili wasipatwe na magonjwa. Anawasuta wanawake ambao siku hizi wanachelea kunyonyesha watoto wao ili wasiharibu urembo na umbo la mwili, bila kujali afya ya mtoto mchanga. Neno “**mwashi**” linarejelea maziwa ya mama. Yana madini na virutubishi ambavyo vinasaidia kujenga afya ya mtoto ili awe na kinga ya kupambana na maradhi. Maziwa ya mama ni muhimu kwa afya ya mtoto kama vile mwashi stadi anavyotumia ujuzi wake na vifaa muhimu kujenga nyumba thabiti inayohimili upepo na tetemeko la ardhi.

Fauka ya hayo, “Mgeni Katili” (uk. 4) na “Biringanya na Matikiti” (uk. 28) ni mashairi yenye sitiari katika diwani ya *Redio na Mwezi*. Biringanya ni aina ya boga ilhali tikiti ni tunda aina ya boga lenye nyama nyekundu ambalo likiiva huwa na maji ndani. Mashairi haya yanagusia maudhui ya uasherati miongoni mwa vijana, wanaume kwa wanawake katika ndoa. Kitendo hiki kinachangia maambukizi ya ugonjwa hatari wa ukimwi. Kwa mfano, mwandishi anaulinganisha ugonjwa wa ukimwi na “**mgeni**” asiye na huruma. Anaeleza vile ukimwi unaua watu wa matabaka

yote na kuacha msururu wa watoto mayatima. Vilevile, maneno “**biringanya**” na “**matikiti**” katika shairi “Biringanya na Matikiti” ni sitiari zinazorejelea viungo vya siri vya wanadamu. Katika shairi hili, msanii anasema pia kuwa “sumu imemwagikia Bustani ya Edeni”. “**Sumu**” ni sitiari ya virusi vya ukimwi. “**Bustani ya Edeni**” ni sitiari ya viungo vya siri vya wanawake na wanaume. Hivi ndivyo mshairi anafanikiwa kutumia sitiari kuwasilisha ujumbe wa kutoa tahadhari kwa wasomaji kuhusu ugonjwa wa ukimwi.

Aidha, katika shairi “Vituko Mjini” (uk. 40), mshairi ametumia sitiari “**pepo**” kurejelea mwanamume na mwanamke wanaoshiriki mapenzi ndani ya ofisi za umma kwenye zulia wakati watu wameenda nyumbani. Tunasoma:

Baada ya watu kuhama
Kutoka mijengo ya ofisi
Milango ya ofisi
Usiifungue kwa kasi
Kwani, ewe usiyejua
Utagutushwa na **pepo**
Wakicheza chakacha
Kwenye mazulia! (uk. 40)

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa* mashairi “Miche Pweke I” (uk. 54) na “Miche Pweke II” (uk.55) ni anwani za kisitiari. Mshairi anazungumzia juu ya athari za ugonjwa wa ukimwi hasa kwa watoto mayatima. Wazazi na walezi waliojiingiza katika mapenzi ya kiholela wameambukizwa ugonjwa wa ukimwi kisha wakafa na kuwaacha watoto mayatima. Katika muktadha huu, “**miche**” ni sitiari inayosimamia watoto wachanga walioachwa bila wazazi wala walezi. Kama kawaida, miche ni miti michanga ambayo inahitaji kutunzwa vizuri ili iwe miti mikubwa yenye manufaa. Kwa hivyo, watoto mayatima katika umri wao mdogo ni miche na wanahitaji malezi bora baada ya wazazi na walezi wao kufariki. Ni shairi linaloangazia changamoto ambazo watoto mayatima hupitia kwa sababu ya athari za ugonjwa wa ukimwi.

Aidha, shairi “Mkasa” (uk. 13) linazungumzia kisa cha ugaidi kilichotokea jijini Nairobi mnamo mwaka 1998 ambapo ubalozi wa Marekani ulishambuliwa na magaidi. Mshairi anatumia sitiari anaposema “jengo karibu na ubalozi wa mwewe” (uk. 13). “**Mwewe**” ni aina ya ndege mwenye mdomo na macho makali ya kuona mbali anapowinda vifaranga wa kuku. Katika muktadha huu, “ubalozi wa mwewe” unarejelea ubalozi wa nchi ya Amerika. Mwewe ni nembo rasmi inayowakilisha nchi

ya Amerika tangu mwaka wa 1782. Kwa hivyo, “mwewe” ni sitiari ya nchi ya Amerika.

Mshairi anaporejelea suala la elimu na walimu wa vyuo vikuu katika diwani ya *Redio na Mwezi*, katika shairi “Ugunduzi” (uk.19) analinganisha kisitiari chuo kikuu na “**mlima**” na wahadhiri wanaofundisha katika vyuo hivyo kama “**miti**”. Mshairi anasema, “Profesa, jina teule, jina la kilele katika **mlima** wa usomi”. Mtu anaposoma hadi chuo kikuu huwa amefika kwenye kilele cha usomi. Kwa hivyo, chuo kikuu ndicho mlima wa usomi. Vilevile, mtunzi anasema kuwa “Katika milima maarufu, kuna **miti** mitajika”. Analinganisha maprofesa maarufu na miti mitajika yenye majina marefu. Ingawa kuna wahadhiri wengi katika vyuo vikuu, umaarufu wao kielimu hautoshani; baadhi ya wahadhiri ni maarufu zaidi kuliko wengine.

5.3.3 Tashibih

Katika kufafanua maudhui mbalimbali katika mashairi yake, mshairi ametumia tashibih pia. Kwa mfano, katika shairi “Mimi, Monika” (uk. 37) katika diwani ya *Bara Jingine*, mshairi anatumia mhusika Monika, kueleza maudhui ya ukahaba. Monika anawakilisha wanawake wengi waliozama katika biashara hii haramu ili kumulika ukosefu wa maadili na changamoto wanazokumbana nazo. Mtunzi anatumia tashibih kusawiri sura kamili ya maisha ya Monika katika ukahaba. Anasema:

Kama mlango wa umma
Nimeguswa na viganja milioni,
Kama jumba la mikutano
Nimetembelewa na halaiki ya watu... (uk. 37)

Mtunzi anatumia neno “kama” kumlinganisha Monika na mlango wa ofisi ya umma unaofunguliwa na kila mtu anayeingia humo. Anarejelea kaumu ya wanaume walioshiriki mapenzi na Monika. Hali ni hiyo hiyo na jumba la mikutano linaloingiliwa na watu wengi kwa shughuli mbalimbali. Tashibih hizi zinaonyesha picha ya namna makahaba huguswa na wanaume wengi katika vilabu na madanguro wakishiriki katika biashara ya ukahaba.

Mwandishi ametumia tashibih pia katika shairi “Mgeni Katili” (uk. 4) katika diwani ya *Redio na Mwezi*. Mshairi anafafanua namna ugonjwa wa ukimwi unamwathiri mtu kiasya kabla ya mauti kumfika. Ugonjwa wa ukimwi ni miongoni mwa magonjwa yanayoua watu wengi hasa katika bara la Afrika. Anasema:

...Mjanja, unawazuzua wanawake na wanaume
Unawarai kwa asali uliochanganya na sumu
Unawaleweshwa kwa sumaku ya maumbile
Kisha, unawakamua kila tone la uhai
Na kuwatupa kaburini wakavu kama kuni (uk. 4)

Katika shairi hili, mwandishi anasema kuwa baada ya virusi vya ukimwi kumsumbua mwathiriwa kwa muda mrefu na afya yake kudhoofika, mwathiriwa anakufa kisha anatupwa kwenye kaburi akiwa amekauka kama kuni. Hii ni taswira ya kutisha kuhusu makali ya ugonjwa wa ukimwi. Kwa kusawiri picha kama hii, mtunzi anawarai vijana kwa wazee wajihadhari sana na vitendo vyovyote vinavyoweza kuchangia maambukizi ya ukimwi.

Kwengineko, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* tashibihi inajitokeza katika shairi “Macho Mekundu” (uk. 60). Macho ya watoto yanakuwa mekundu kutokana na matumizi ya dawa za kulevya. Mwandishi anawaonea huruma watoto wadogo wanaotumia dawa za kulevya. Anawalinganisha watoto hao na “kama wanyama wa porini” na “kama nyani, kima na tumbili” ambao wanakula matunda-mwitu. Hii ina maana kuwa watoto hao wanashiriki kwenye dawa haramu zinazochangia wao kufanya maovu katika jamii. Mshairi anaeleza vituko wanavyofanyia watu vijijini kama vile kuiba vyakula, kuwaua wazazi na majirani na hata kubaka ndugu na binamu wa kike kwa sababu ya uraibu wa mihadarati. Mtunzi anasema:

Moyo wangu una uchungu mkali
Unateswa na miiba ya hii picha
Unalizwa na majonzi ya watoto
Ole wao! **Kama wanyama wa porini**
Watoto wanaishi katika mbuga katili,
Kama nyani, kima na tumbili
Wanajihimili kwa kula matunda-mwitu... (uk. 59)

Akizungumzia suala la ubaguzi wa rangi katika *Msimu wa Tisa*, mtunzi anatumia tashibihi vilevile katika mashairi “Muuaji Mwenye Furaha” (uk. 22) na “Darfur” (uk. 26). Kwa mfano, katika “Muuaji Mwenye Furaha” mshairi anaeleza vile uchunguzi wa mwanajeshi wa kigeni muuaji ulikamilishwa haraka. Kawaida uchunguzi huchukua muda mrefu lakini kwa mwanajeshi Mzungu ulifanywa haraka. Mshairi anatumia maneno “kama kwamba” kuonyesha vile polisi walimaliza uchunguzi haraka sawa na ukanda wa mashine ya umeme. Kwa hivyo, anakuwa muuaji mwenye furaha kwa sababu anaachiliwa huru kuliko vile wanavyopewa adhabu kali watu wengine weusi wanaoshtakiwa kwa kosa la mauaji. Mwandishi anasema:

Kinyume na mwendo wa kesi za uzimaji binadamu uhai
Ambamo uchunguzi hujikokota **kama konokono ukutani**
Kinyume na mazoea, polisi walikamilisha kazi kwa kasi
Kama kwamba harakati zao za kukusanya habari azizi
Ziliendeshwa kwa ukanda wa mashine ya umeme (uk. 22)

Vilevile, akionyesha namna madhila na ubaguzi wa rangi dhidi ya watu weusi umeshamiri nchini Sudan katika shairi “Darfur” anasema, “Wanaochinjwa na kubakwa vijijini Darfur, wasingekuwa na **ngozi nyeusi kama mpingo...**” (uk. 27). Mshairi analinganisha ngozi za Wasudan na weusi wa mpingo ili kusesitiza juu ya rangi yao mbali na kuonyesha ubaguzi wa rangi dhidi ya watu weusi nchini Sudan.

Katika suala la unafiki wa kidini, mshairi anamulika uovu wa mhubiri ambaye anafanya uzinzi na mke wa mtu ambaye ni muumini katika kanisa lake. Mhubiri anamtembelea muumini nyumbani mwake usiku wakati mumewe ameenda safari. Katika harakati ya kushiriki mapenzi, mume wa mke anarudi ghafla usiku huo na kuwafumania. Katika shairi “Mhubiri na Mjinga” (uk. 42) kwenye diwani ya *Redio na Mwezi*, mshairi anataeleza hali ilivyokuwa na yaliyofuatia kupitia matumizi ya tashibihi:

Alikuta mabusu
Yakitoa cheche za moto
Kama makaa ya tanuri
Katika banda la mhunzi

Ujanja wa mwerevu
Na hasira ya mjinga
Ziligongana kama radi
Na kuzaa mkazi mpya
Wa jamhuri ya wafu (kur. 42-43)

Mwandishi ametumia tashibihi anaposema alikuta mabusu yakitoa cheche za moto “kama makaa ya tanuri” kuchora picha ya namna mabusu makali kati ya mhubiri na muumini yaliyamsha hamu ya kushiriki mapenzi. Tashibihi hii inaonyesha wazi unafiki wa watu hawa wawili ambao ni wafuasi wa dini lakini wanazini. Aidha, mtunzi anatomia tashibihi kueleza matokeo ya kitendo chao. Mume ambaye alikuwa kama mjinga asiyejua kilichokuwa kinajiri baina ya mke wake na mhubiri anashikwa na ghadhabu na kumuua mhubiri. Anasema kuwa “**Ujanja wa mwerevu na hasira ya**

mjinga ziligongana kama radi”. Tashibihii hii inaonyesha taswira ya makabiliano makali yaliyotokea baina ya mume na mhubiri.

Isitoshe, mtunzi ametumia tashibihii katika shairi “Samaki Nje ya Maji!” (uk. 16) katika diwani ya *Redio na Mwezi* anapoangazia maarifa duni miongoni mwa wahadhiri katika vyuo vikuu. Anatumia tashibihii “**anakwama kama samaki ambaye amesukumwa nje ya maji**” kurejelea mhadhiri ambaye hawezi kueleza mambo yaliyo nje ya taaluma yake. Hata hivyo, mhadhiri hastahili kujua kila kitu. Mshairi anaeleza:

Leo nilimkuta mhadhiri
Mwenye shahada ya kilele
Katika taaluma maalumu
Bali, umsukumapo kwa ulimi
Na kumtoa pahali pa mazoea
Alipowekwa na walimu wa jana
**Anakwama kama samaki ambaye
Amesukumwa nje ya maji** (uk. 17)

5.3.4 Tasifida

Wakati mwingine msanii huamua kutumia maneno ambayo yanapunguza ukali au kero badala ya maneno yanayoweza kuibua hisia kali kwa msomaji. Maneno hayo hujulikana kama tasifida. Tasifida hutumika ili kudumisha heshima katika mawasiliano. Huonyesha ukomavu wa matumizi ya lugha, hudumisha heshima mbali na kuongeza ladha katika lugha. Kwa mfano, mshairi anapoangazia maudhui ya ukahaba, kwa sababu ya uzito wa vitendo hivi, anatumia tasifida katika shairi “Mimi, Monika” (uk. 37) katika diwani ya *Bara Jingine*. Anaeleza vile ambavyo mhusika Monika ametangamana na wateja wengi katika maisha yake akitafuta riziki. Msanii anasema:

Nimeguswa na viganja milioni,
Kama jumba la mikutano
Nimetembelewa na halaiki ya watu (uk. 37)

Mshairi anarejelea wale wanaume wengi ambao Monika ametangamana nao lakini hataki kusema moja kwa moja. Wanaomgusa na kumtembelea Monika ni wateja wa kiume. Mwandishi anatumia tasifida kueleza halaiki ya wanaume ambao Monika ameshiriki ngono nao akitafuta pesa. Anapotumia maneno “nimetembelewa na halaiki ya watu”, mshairi anahifadhi uso kwa kuzingatia utamaduni katika matumizi ya lugha lakini ujumbe wake unaeleweka.

Aidha, mtunzi anawaonya wanaume na wanawake ambao wanashiriki vitendo vya uasherati kuwa kuna ugonjwa hatari wa ukimwi. Katika diwani ya *Redio na Mwezi* katika shairi “Biringanya na Matikiti” (uk. 28), mshairi anatumia maneno ya kupunguza ukali anaposema kuwa “kutangatanga ovyoovyo katika bustani, mkila vipande vitamutamu vya matikiti”. Kwa hakika anarejelea tabia ya wanaume kufanya mapenzi ovyoovyo, jambo ambalo linawaleta kifo kwa sababu ya ugonjwa wa ukimwi. Mtunzi anatahadharisha:

Wanaume Habedari! Kaburi zinanyemelea!
Kutangatanga ovyoovyo katika Bustani
Mkila vipande vitamutamu vya matikiti
Ni kujitia kitanzi cha waya wa chuma
Matikitini kimejificha chambo cha mauti! (uk. 28)

Kwengineko, katika diwani hii, mwandishi ametumia tasifida vilevile katika shairi “Vituko Mjini” (uk. 40) kuzungumzia tabia ya watu kufanya mapenzi hasa katika ofisi za umma wakati wa jioni baada ya watu kuondoka kwenda nyumbani. Msanii anatumia maneno ya tasifida “wakicheza chakacha kwenye mazulia” kwa maana ya mwanamke na mwanamume kushiriki mapenzi kwenye mazulia wakati wa jioni. Kawaida ni aibu watu kushiriki mapenzi katika ofisi kwenye zulia. Kwa sababu hiyo, mwandishi anatumia tasifida badala ya maneno makali akirejelea kitendo hicho kisichostahili kutendwa ofisini. Kwa ucheshi, mshairi anaonya:

Baada ya watu kuhama
Kutoka mijengo ya jiji
Milango ya ofisi
Usiifungue kwa kasi
Kwani, ewe usiyejua
Utagutushwa na pepo
Wakicheza chakacha
Kwenye mazulia! (uk. 40)

Katika shairi “Dude-dubwana Mahakamani” (uk. 32) katika diwani hii ya *Redio na Mwezi*, mshairi anazungumzia kitendo cha usenge. Anamulika namna mwalimu wa dini alivyowalawiti wanafunzi wachanga wa kiume. Mwandishi anasema “kinyume cha sheria na haki, kinyume na maumbile na miiko” kurejelea kitendo cha mwalimu wa kiume kuingilia watoto wa kiume. Kitendo hiki ni kinyume cha maadili ya mtunzi na jamii kwa jumla. Uzito na aibu inayoandamana na kisa hiki inamfanya mtunzi kutumia tasifida kueleza uchungu alio nao moyoni:

...Mahakamani, siku ya ukweli kujiri
Watoto walieleza yaliyowakumba
Kinyume cha sheria na haki
Kinyume cha maumbile na miiko,
Walimvua mwalimu kofia na kanzu...(uk. 32)

Maneno “watoto walieleza yaliyowakumba kinyume cha sheria na haki, kinyume cha maumbile na miiko” ni tasifida inayorejelea kitendo cha ulawiti alichowafanyia mwalimu wa dini.

Mtunzi anazungumzia matumizi ya pombe na mihadarati ya kila aina katika shairi “Evergreen Ltd” (uk. 49) katika diwani ya *Redio na Mwezi*. Watu wakiwa wamelewa katika klabu hii iitwayo “Evergreen”, wanashiriki katika mambo ya uasherati ambao mtunzi anauzungumzia kwa lugha ya heshima kama “kugusa na kuguswa” ifuatavyo:

Hii ndiyo Evergreen Ltd
Ambamo, wananchi
Kutoka humu na mbali
Hukutanika kikaoni
Kuvuta na kutafuna
Kunywa na kutazama
Na kwa wasiojali
Kugusa na kuguswa... (uk. 49)

Katika shairi “Muumini” (uk. 29) kwenye diwani hii, msanii anaonyesha unafiki wa muumini. Muumini wa kike anaenda kanisani kujenga uhusiano mwema na Mungu wake. Lakini akitoka kanisani, anaenda kunywa pombe na hata kushiriki mapenzi kinyume na imani na mafunzo ya dini. Anasema kuwa “bila tahadhari kiholela, akapanda angani na kukata rumba ukumbini mwa upinde-wa-mvua”. Maneno hayo ni tasifida ya vitendo viovu anavyofanya usiku kwenye klabu kwa kunywa pombe, kucheza densi na kushiriki mapenzi na wanaume. Anaposhiriki mapenzi kiholela kwa sababu ya ulevi anapolevuka, anarudi kanisani kwa wasiwasi mwingi kumuomba Mungu amwepushe na ugonjwa wa ukimwi. Mtunzi anatumia tasifida kueleza hivi:

Au jana, Jumamosi, baaada ya kikao cha pombe,
Baada ya akili kulemaa, mwili ulimhadaa
Bila tahadhari, kiholela, akapanda angani
Na kukata rumba ukumbini mwa upinde-wa-mvua (uk. 29)

5.3.5 Maswali ya Balagha

Mwandishi anapoeleza maudhui ya ubepari na unyonyaji wa kiuchumi anatumia maswali ya balagha. Kwa mfano, katika diwani ya *Mchezo wa Karata*, shairi “Tajiri

wa Lulu” (uk. 16) lina swali la balagha ambapo mshairi anauliza uhalali wa tajiri kumiliki lulu ilhali tajiri huyo hajisumbui na hataabiki kwenye matope kutafuta lulu. Anauliza:

Wewe uogopaye maji ya chumvi
Ngozi yako nyororo isiharibike,
Wewe ukwepaye maji ya matope
Unadhifu wako usipungue,
Lulu makasha – makasha
Umekuwaje mmiliki? (uk. 16)

Katika shairi “Kiwambo cha Televisheni” (uk. 37), mtunzi anaonyesha tofauti za kitabaka kati ya maskini na matajiri zinazochangia ubepari na unyonyaji. Katika shairi hili la aina ya ngonjera, Sauti ya 1 inamwakilisha mtu mnyonge ilhali Sauti ya 2 inamwakilisha tajiri. Mnyonge anamuuliza tajiri maswali ya balagha eti kwa nini anaendelea kuteseka maishani naye tajiri akinawiri. Mshairi anasema:

SAUTI 1: **Kwa nini
Nuru ya miale ya jua
Ikumulikie maisha pekee
Wakati nilipo
Giza larindima ja radi?**

SAUTI 2: Ni-ni-no!
Ni-ni-no!

SAUTI 1: **Kwa nini
Maji yatokayo angani
Yakufaidi shamba pekee
Wakati nilimapo
Ukame wasongoa ardhi shingo?**(kur. 37-38)

Swali la kwanza linauliza ni kwa nini miale ya jua immulike tajiri pekee wakati yeye maskini anakaa gizani? Swali la pili linauliza ni kwa nini mvua inafaidi shamba la tajiri ilhali yeye anapolima ukame unasongoa shingo ardhi yake? Maswali haya hayastahili kujibiwa ila yanahimiza kuchukua hatua fulani ili kuleta usawa wa haki kati ya mnyonge na tajiri.

Shairi “Msimu wa Kaburi!” (uk. 3) katika diwani ya *Redio na Mwezi* lina swali la balagha. Mshairi anaeleza watu wengi wanakufa kwa sababu ya ugonjwa wa ukimwi kwa kujiingiza katika uasherati kiholela. Kwa kutumia swali la balagha anaonyesha

vile kifo kinamdanganya mke au mume akashiriki kitendo ambacho mwisho wake ni kaburi. Anaeleza:

Kifo, mlaghai bila haya, giza bila huruma!
Kwa nini unaturai kwa sauti iliyopakwa asali
Na kutuahidi kimbunga cha furaha faraghani
Na kumbe kiunoni umeficha upanga mkali
Tayari kuchinja wanaoingia mtegoni? (uk. 3)

Kwengineko, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* katika shairi “Muuaji Mwenye Furaha” (uk. 22) kuna swali la balagha. Mwandishi anazungumzia maudhui ya ubaguzi wa rangi mahakamani. Mwanajeshi wa kizungu aliyemuua mwanamke Mwafrika anafikishwa mahakamani. Anakiri kosa la mauaji lakini badala ya kufungwa kama mtu yeyote muuaji, hakimu anamwachilia huru aende kwao. Mshairi anauliza kwa hamaki kuwa ni kwa nini mahakama ichanganywe na weupe na weusi? Kuchanganywa kwa weupe na weusi kunamaanisha ubaguzi wa rangi. Waafrika hupewa adhabu kali ilhali Wazungu huachiliwa huru mahakamani jambo ambalo si haki. Kwa kweli swali hili halistahili kujibiwa. Mwandishi anatuonyesha hali halisi ya ubaguzi wa rangi ili tuchukue hatua kurekebisha hali hii. Anauliza kwa stihizai na ghadhabu:

Kumbe! Sheria za taifa zina macho yasiyohitaji miwani
Zinaona na kutambua vyema ngozi za washtakiwa
Kwa nini mahakama ichanganywe weupe na weusi!! (uk. 22)

5.3.6 Kinaya

Kinaya ni tamathali ya usemi ambapo usemi fulani una maana ya kinyume (Wamitila 2003b). Kinaya kinaweza kuwa cha hali, kitendo au usemi. Katika diwani ya *Radio na Mwezi* kuna matumizi ya kinaya katika shairi “Dude-dubwana Mahakamani” (uk. 32). Mwalimu wa dini anawalawiti wanafunzi wa kiume. Kawaida, mwalimu wa dini anastahili kuwapa mafunzo bora juu ya maadili wanapoendelea kukua. Hata hivyo, kitendo chake ni kinyume na matarajio ya watu kutoka kwa kiongozi wa dini kama yeye. Kwa hivyo, wanafunzi wa kiume wanapomshtaki kwa wazazi wao, inakuwa ni kinaya cha hali na kitendo kwamba mtu anayepewa heshima na kuaminiwa kuwa na maadili anafanya kitendo cha aibu kuwalawiti wanafunzi wake.

Katika diwani ya *Mchezo wa Karata*, kuna kinaya pia katika shairi “Mfanyakazi Mahakamani” (uk. 22). Mfanyakazi ambaye anafanya kazi ngumu analalamika kuwa

mshahara anaolipwa haulingani na kazi anayofanya. Anatarajia kuwa ili kuwe na haki, atapata nyongeza ya mshahara. Kinyume na matarajio yake, mfanyakazi anafikishwa mahakamani na mwajiri wake. Kesi ya mfanyakazi na mwajiri inaposikilizwa mahakamani, mwajiri anashinda kesi ilhali mfanyakazi anahukumiwa miaka mitatu gerehani kwa kisingizio kuwa yeye ni adui wa maendeleo.

Kwengineko, katika diwani ya *Redio na Mwezi*, kinaya kinajitokeza katika shairi “Kisa Chuoni” (uk. 45). Katika shairi hili wanafunzi wa chuo wanapenda kupinga dhuluma na kupendekeza haki itekelezwe kwa watu wote. Lakini licha ya kupinga dhuluma hawafanyi hivyo. Jambo hilo linaonekana wazi pale mwanamke mmoja anatoa huduma za mapenzi kwa wanafunzi wa kiume chuoni akiwa na matarajio kuwa atapata pesa za kutimizia mahitaji ya mtoto wake nyumbani. Baada ya wanafunzi hao kupata huduma za mapenzi kutoka kwa mwanamke huyo, wanaamua kumfurusha kutoka chuoni humo bila kumpa pesa zozote. Kule kumfukuza chuoni bila kumpa pesa ilhali wameshapewa huduma ni kinaya kulingana na msimamo wao kuwa kila mtu anastahili kupewa haki siku zote na kusiwe na dhuluma kwa mtu yeyote.

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, kuna kinaya katika shairi “Muuaji Mwenye Furaha” (uk. 22). Katika shairi hili, mwanajeshi Mzungu anamuua mwanamke Mwafrika rafiki yake karibu na bahari kwa ncha kali ya chupa. Kulingana na sheria, muuaji anastahili kupewa adhabu kali kwa kosa alilotenda. Lakini hali sivyo kwa huyu mwanajeshi. Siku aliyofikishwa mahakamani kuhukumiwa, jaji alitoa hukumu isiyozingatia haki na kumwachilia huru aende kwao. Ni kinaya kuwa badala ya mwanajeshi kufungwa maishani au kunyongwa, anaruhusiwa kwenda nyumbani.

Kinaya pia kinajitokeza katika diwani hii ya *Msimu wa Tisa* katika shairi “Wahalifu Huru” (uk. 30). Katika shairi hili, wanasiasa wenye mamlaka na ushawishi mkuu serikalini wanachochea mapigano ya kikabila. Badala ya viongozi kuhimiza amani, upendo na umoja, wao ndio wanachochea fujo na uhasama miongoni mwa wananchi wanaokaa kwa amani wakiendelea na shughuli za kujenga taifa. Lakini hata baada ya kufitinisha wananchi wa makabila tofauti, wanasiasa hao wanatembea huru wakipeperusha bendera za mamlaka bila kuchukuliwa hatua za kisheria. Kinaya ni kuwa taasisi za kisheria haziwachukulii hatua kwa makosa waliyoyatekeleza.

5.3.7 Chuku

Kithaka wa Mberia anaeleza masuala fulani kwa kutilia chumvi ili ukweli halisi wa maelezo yake ueleweke kwa uwazi zaidi. Matumizi ya chuku vilevile yanaongeza ladha na mvuto kwenye kazi yake. Mfano mzuri wa chuku unapatikana katika shairi “Mfanyakazi Mahakamani” (uk. 22) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Mfanyakazi anayefanya kazi ya sulubu anapelekwa mahakamani na mwajiri wake kwa kutaka apewe mshahara unaolingana na kazi nzito anayoifanya. Mshairi anatomia chuku kuonyesha namna kimya kizito kimetawala mahakamani mpaka mipigo ya moyo inasikika. Anasema:

Sasa, kimya kizito
Kimetanda mahakamani
Hata mipigo ya nyoyo
Inasikika waziwazi! (uk. 22)

Katika hali halisi, hata kukiwa na ukimya wa aina gani huwezi kusikia moyo wa mtu ukipiga. Kwa hivyo, mtunzi anatomia chuku hapa kueleza utulivu wa hali ya juu uliokuwa mahakamani ili kujua hatima ya mfanyakazi kuhusiana na kesi yake. Kinaya ni kuwa mfanyakazi huyo alihukumiwa miaka mitatu gerezani eti alikuwa adui wa maendeleo. Mtunzi anaonyesha bayana kuwa taasisi za sheria zinakosa kuwajibika katika kutoa uamuzi wa haki kwa wanyonge kwa sababu ya ufidadi.

Katika diwani ya *Bara Jingine*, mshairi ametumia chuku katika shairi “Mimi, Monika”(uk. 37). Monika ni mhusika katika biashara ya ukahaba. Biashara ya ukahaba huhusisha wanawake wengi mno. Akimtumia Monika kama mhusika mmoja miongoni mwa wengine, anasema:

Kama mlango wa umma
Nimeguswa na viganja milioni
Kama jumba la mikutano
Nimetembelewa na halaiki ya watu
Kutoka kila pembe ya ulimwengu (uk. 37)

Ni kweli kuwa Monika amekutana na wanaume wengi sana lakini mtunzi anapiga chuku anaposema “nimeguswa na viganja milioni”. Vilevile anatilia chumvi maelezo ya biashara ya ukahaba anaposema kuwa ”nimetembelewa na halaiki ya watu kutoka kila pembe ya ulimwengu”. Haiwezekani kuwa Monika amekutana kimwili na wanaume kutoka pembe zote za ulimwengu. Hata hivyo, kwa kueleza hivyo, tunaelewa waziwazi ujumbe wa mshairi kuhusu wingi wa wanaume aliojikusisha nao kimapenzi Monika katika maisha yake ya taabu akitarazaki.

5.3.8 Ritifaa

Ritifaa ni tamathali ambayo kwayo msanii anawasilisha ujumbe katika kazi ya kifasihi kwa kuzungumza na mfu, vitu visivyoye na uhai au vitu dhahania. Katika ushairi wa Kithaka wa Mberia, mshairi anazungumza na kifo moja kwa moja kwa njia ya balagha katika shairi “Msimu wa Kaburi!” (uk. 3) katika diwani ya *Redio na Mwezi*. Mshairi anahisi uchungu wa kupoteza watu wengi kupitia ugonjwa wa ukimwi. Ndio maana anazungumza na kifo moja kwa moja hivi:

Kifo, mbona unajificha katikati ya magoti
Mwanadamu aendaye mandari kiholela
Hushtukia kamba imejipanga shingoni
Punde inaikaza kwa mikono thabiti...(uk. 3)

Aidha, katika shairi “Mgeni Katili” (uk. 4) katika diwani hii, mwandishi anazungumza na ugonjwa wa ukimwi kana kwamba ni mtu. Anasema, “**Wewe, katili, jambazi la kutisha...**” (uk. 4). Isitoshe, katika shairi “Rafiki Katili” (uk. 57) mshairi anazungumza na tembo pale ambapo anasema, “**Tembo, wewe in sungura mjanja...**” (uk. 57). Anazungumza na tembo na kuonyesha vile linafanya akili za watu kudanganyika, kuropokwa na maneno, kupigana na hata kuuana. Tembo halina uhai lakini anazungumza nalo kwa nia ya kuonyesha madhara ya pombe kwa mtu.

5.3.9 Mbinu Nyingine za Kisanaa

Mbinu nyingine za kisanaa ni vipengele vingine vya kimtindo ambavyo si tamathali za usemi lakini mshairi amevitumia ili kuendeleza maudhui yanayohusiana na utamaduni mahuluti.

5.3.9.1 Takriri

Katika mashairi mengi, mtunzi anarudiarudia maneno au vifungu fulani kwa lengo la kuisitiza ujumbe kwa msomaji. Kwingine anatumia visawe kwenye mshororo mmoja. Msisitizo huu pia unaonyesha hisia za ndani za mshairi kuhusu kile anachokizungumzia. Ni kwa sababu hii ambapo takriri inakuwa kiungo muhimu kati ya kinachosemwa na namna kinavyosemwa. Kwa mfano, katika shairi “Tajiri wa Lulu” (uk. 16) katika *Mchezo wa Karata* mshairi anarudiarudia neno “wewe” akirejelea tajiri mjanja ambaye anamiliki makasha ya lulu ilhali hagusi maji ya chumvi wala matope kutafuta lulu zenyewe. Watu wa chini wanaotafuta lulu kwa hali na mali hawana makasha ya lulu, inakuwaje kwa tajiri wa lulu? Anasisitiza kuwa si

halali kwa tajiri asiyekanyaga maji ya chumvi na kukwepa matope kumiliki makasha ya lulu ilhali wanaotafuta lulu zenyewe hawamiliki makasha ya lulu. Anasema:

Wewe uogopaye maji ya chumvi
Ngozi yako nyororo isiharibike,
Wewe ukwepaye maji ya matope... (uk. 16)

Aidha, katika shairi “Kero” (uk. 28) maneno “inakera moyo” yamerudiwa mara mbili katika shairi sawa na maneno “kwa nini” na “Ni-ni-no!” ambayo yamerudiwa mara kadha katika shairi “Kiwambo cha Televisheni” (kur. 37-38). Maneno hayo yanaonyesha kughadhabishwa kwa maskini kuwa tajiri anawanyanyasa maskini. Maskini hawataki hali hiyo ya kuendelea kudhulumiwa. Kwengineko, katika diwani ya *Redio na Mwezi*, katika shairi “Mgeni Katili” (uk. 4), mtunzi anaangazia kuibuka kwa ugonjwa wa ukimwi kama mgeni ambaye hakutarajiwa. Anatumia takriri wazo ili kurejelea ugonjwa wa ukimwi kwa njia tofauti. Anatumia takriri hivi:

Wewe, katili, jambazi la kutisha
Mgeni ambaye hakualikwa, hakutarajiwa
Mchinjaji kicheko, mhandisi wa huzuni
Mpenzi wa mifupa ya mavani, Izraeli... (uk. 4)

Maneno “katili”, “jambazi la kutisha”, “mchinjaji kicheko” na “mpenzi wa mifupa ya mavani” ni takriri wazo ambalo linarejelea ugonjwa wa ukimwi.

Katika shairi “Matumizi Mengine” (uk. 41), mwandishi anaeleza matumizi mengine ya mazulia, matakia ya ofisi na viti vya magari kwa shughuli za uasherati kuliko alivyodhania. Msanii anaonyesha kuwa tabia ya uzinzi inakera sana. Anarudia maneno “nyakati za nyuma” mara tatu katika beti tatu za kwanza za shairi hili ili kuisitiza kuwa tabia hiyo haikuwepo katika miaka ya nyuma lakini sasa inaonekana wazi kwenye mazulia na matakia ya ofisi na hata kwenye viti vya magari. Uchafu wa kitendo hiki unaonekana wazi. Kwa mshairi, hii ni aibu na ukosefu wa maadili miongoni mwa wanajamii. Anasema:

Nyakati za nyuma
Mazulia ya ofisi
Kamwe sikuyashuku ...

Nyakati za nyuma
Matakia ya ofisi
Abadani sikuyaogopa...

Nyakati za nyuma
Viti vya magari
Havikunighasi moyo...(uk. 41)

Akizungumzia utovu wa maadili kwa mwalimu wa dini aliyewalawiti wanafunzi wa kiume, mshairi anatumia takriri ya neno “kinyume” mara mbili kuonyesha wazi kina cha uozo wa mwalimu kwa wanafunzi wake katika shairi “Dude-dubwana Mahakamani” (uk. 32). Anadokeza:

Mahakamani, siku ya ukweli kujiri
Watoto walieleza yaliyowakumba
Kinyume cha sheria na haki
Kinyume cha maumbile na miiko
Walimvua mwalimu kofia na kanzu...(uk. 32)

Msisitizo wa mtunzi upo kwenye neno “kinyume”. Kitendo cha mwalimu ni kinyume cha sheria, haki, maumbile na miiko ya utamaduni wa Kiafrika. Ni kitendo cha soni ambacho hakielezeki na ndio maana hakimu alimhukumu kifungo kikali korokoroni.

Kwengineko, mwandishi anaonya kuhusu kitendo cha wazazi kuwapa wana wao pesa nyingi kama ishara ya kuwapenda. Watoto wanatumia pesa hizo katika ulevi na dawa nyingine za kulevya. Kwa mfano, katika diwani ya *Bara Jingine*, anaeleza bayana madhara ya pombe na dawa za kulevya hasa kwa watoto katika shairi “Ni Sumu kwa Watoto” (uk. 49) kwa matumizi ya takriri:

Ni sumu, sumu jeruhi
Unajeruhi watoto
Kwa mapenzi yako hatari
Ya kuliwaza kwa **pesa**
Pesa chungu nzima ambazo
Zinawafikisha kwenye sigara na ulevi
Na kisha kwenye dawa za kulevya... (uk. 50)

Katika dondoo hili, mtunzi anarudia maneno “sumu”, “jeruhi” na “pesa” kutilia mkazo ujumbe kwa wazazi kuharibu wana wao kwa mapenzi yanayoishia kuwaingiza katika ulevi na mihadarati. Anazindua wazazi wasiharibu watoto wao kwa kuwapatia pesa nyingi kama ishara ya mapenzi bali wanachangia kuharibu maisha yao. Aidha, katika diwani ya *Redio na Mwezi* kuna takriri ya maneno katika shairi “Tembo”(uk. 56). Mtunzi anatumia visawe vya maneno “mnyonge”, “mkata”, “dhalili” kueleza hali ya mlevi inayotokana na kule kulewa kwake au na ule uraibu wa pombe. Isitoshe, maneno “asingekuwa” na “angekuwa” yanarudiwa kwa lengo la kusisitiza hali ya

msomi mlevi anayesumbua watu kwa sababu ya kuwa mraibu wa tembo. Aidha, maneno hayo yanaonyesha hali angekuwa nazo na zile asingekuwa nazo kama hangekuwa akilewa. Mwandishi anasema:

Asingekuwa mnyonge, mkata, dhalili
Angekuwa anajiweza, anajichumia riziki...
Asingekuwa akiomba marafiki nauli daima
Asingekuwa anawasumbua jamaa kupata malazi
Angekuwa na kazi, makazi, labda familia
Lakini tembo lilimtaka urafiki, akakubali... (uk. 56)

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa* mtunzi anatumia takriri kuonyesha kinyume cha mambo katika shairi “Wahalifu Huru” (uk. 30). Wanasiasa walichochea mapigano ya kikabila ambapo watu wengi waliuawa na mali kuharibiwa. Badala ya viongozi hawa kuhubiri wito wa amani, upendo na umoja, wanachochea vita vya wenyewe kwa wenyewe. Wanasiasa hawa ambao walikuwa waasisi wa uhasama wa kikabila wanatembea huru kwa sababu ya uwezo wao wa pesa na mamlaka katika jamii. Ni kinaya kuwa taasisi za kisheria haziwachukulii hatua kali kwa makosa hayo. Kwa kuonyesha namna taasisi hizo haziwajibiki, anarudia maneno “badala ya” mara mbili kwa kusema:

Bali katika wingu la unafiki wa “amani, upendo na umoja”
Badala ya wahandisi wa jakamoyo kutetemeka mahakamani
Badala ya wenye damu viganjani kutupwa korokoroni
Wanaendesha mashangingi yenye bendera za mamlaka
Wanalipwa mishahara minono wakiitwa “viongozi wa taifa” (uk. 30)

5.3.9.2 Nidaa

Katika diwani ya *Mchezo wa Karata*, mtunzi ametumia nidaa kuonyesha hisia za hasira za mhusika wa Sauti 1 katika shairi “Kiwambo cha Televisheni” (uk. 37). Nidaa inatoa hisia za moyoni za mwandishi mbali na kubainisha toni katika shairi lake. Msanii anasema:

Sauti 1: Kugeuzwa yonda
Nimekataa, katakata! (uk. 39)

Katika dondoo hili, mhusika wa Sauti 1 anaonyesha hisia za hasira na toni ya uchungu anaposema kuwa amekataa kugeuzwa kima. Mhusika Sauti 1 anakataa kunyanyaswa na tajiri.

Kwengineko, ametumia nidaa katika vichwa vya mashairi katika diwani hii kama vile. “Dira Usitupe!” (uk. 24), “Si Maskani Mapya!” (uk. 25), “Dau Haliendi!” (uk. 32) na “Aibu!” (uk. 34). Katika diwani ya *Redio na Mwezi* kuna mashairi kama “Samaki Nje ya Maji!” (uk. 16) na “Mtoto Mchanga!” (uk. 22). Katika *Msimu wa Tisa* kuna shairi “Wasikudanganye Mama!” (uk. 95). Mashairi haya yote yanaonyesha hisia za ndani za mshairi ambazo zinaweza kuwa za chuki, onyo, hasira na dharau juu ya mambo yasiyompendeza.

Katika diwani ya *Redio na Mwezi*, kuna matumizi ya mbinu ya nidaa katika mashairi kadha. Kwa mfano, katika shairi “Biringanya na Matikiti” (uk. 28), mshairi anawatahadharisha wanaume na wanawake dhidi ya kushiriki mapenzi nje ya ndoa kwa sababu ya hatari ya ugonjwa wa ukimwi. Mtunzi anachomwa moyoni anapoona wanaume na wanawake wakichezea maisha yao kwa kushiriki mapenzi kiholela kisha wanakufa kutokana na ugonjwa wa ukimwi. Maneno “wanawake simile!”, “dunia imechafuka!” na mengine yanaonyesha hisia za kukerwa na mshairi kwa wanaume na wanawake wanaoshiriki mapenzi kiholela bila kuchukua tahadhari. Anawaonya:

Wanawake simile! Dunia imechafuka!

Sumu imemwagikia Bustani ya Edeni...

Wanaume habedari! Kaburi zinanyemelea!...

Matikitini kimejificha chambo cha mauti! (uk. 28)

Aidha, mshairi anaonyesha kughadhabishwa kwake na wanandoa waliokula viapo arusini wakivishana pete ilhali ndio wanaoshiriki tena mapenzi nje ya ndoa. Katika shairi “Matunda Haramu” (uk. 39) mtunzi anawataja wanandoa wa aina hiyo kama wasaliti wa taasisi ya ndoa anaposema, “ **Wasaliti wa Taasisi!**” (uk. 39). Mshairi anaonyesha hasira zake kwa wanandoa wanaoshiriki mapenzi nje ya ndoa. Kitendo hiki kinavunja familia nyingi kwani wanandoa hukosa kuaminiana, huachana na pia huchangia kusambaa kwa magonjwa ya zinaa na ukimwi.

Mtunzi anashangaa tabia za wanaume na wanawake kufanya mapenzi kiholela katika shairi “Vituko Mjini” (uk. 40) kwa kutumia nidaa. Anasema, “**Wakicheza chakacha kwenye mazulia!**” (uk. 40). Mshairi anaonyesha hisia za kukerwa kwa wanaume na wanawake wanaoshiriki mapenzi mahali na wakati ambao haustahili. Anaonyesha mshangao wake kuwa kuna ukosefu wa maadili miongoni mwa wanaume na wanawake.

Kwengineko, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, katika shairi “Macho Mekundu” (uk. 59) mwandishi anaeleza jinsi watoto wametumia dawa za kulevya mpaka macho yao yamekuwa mekundu kisha wanaanza kutenda vitendo vya kihayawani kwa wazazi wao, ndugu na binamu wa kike na majirani zao huko vijijini. Mtunzi anaonyesha hisia za huruma kwa watoto hao wachanga anapotumia maneno “Ole wao!” na “watumwa wa majambazi!” Anasema:

Ole wao! Kama wanyama wa porini
Watoto wanaishi katika mbuga katili
Kama nyani, kima na tumbili
Ole wao, watumwa wa majambazi!(uk. 59)

Aidha, katika shairi “Muuaji Mwenye Furaha” (uk. 22) anaonyesha kukerwa kwake kwa jinsi haki haitekelezwi kwa sababu ya misingi ya ubaguzi wa rangi katika kesi ya mauaji. Mwanajeshi wa kizungu alimuua mwanamke Mwafrika lakini hafungwi jela. Mwandishi anaonyesha hisia za mshangao na hasira vilevile kutokana na hukumu isiyo ya haki kwa mwanajeshi aliyewa. Ndio maana mwandishi anasema:

Kumbe! Sheria za taifa zina mambo yasiyohitaji miwani
Zinaona na kutambua vyema ngozi za washtakiwa
Kwa nini mahakama ichanganywe weupe na weusi!! (uk. 22)

Katika diwani ya *Redio na Mwezi* kuna shairi “Ugunduzi” (uk. 19) ambapo mtunzi anaonyesha tofauti za umaarufu wa maprofesa katika vyuo vikuu. Mshairi anaonyesha mshangao kuwa licha ya kupewa jina profesa, bado kuna tofauti za maarifa na umaarufu miongoni mwa wasomi hawa. Mwandishi anaposema kuwa baadhi ya miti si mirefu kuliko miviru au mikubwa kuliko midimu anaonyesha mshangao wa tofauti za maarifa miongoni mwa wasomi ingawa wamepewa jina moja la uprofesa. Anaonyesha kushangaa kwake hivi:

Baadhi ya hiyo
Si mirefu
Kuliko miviru
Si mikubwa
Kuliko midimu! (uk. 19)

5.3.9.3 Oksimora

Oksimora ni aina ya kweli kinzani ambayo ni fupi mno (Wamitila 2003a). Aghalabu oksimora huundwa kwa maneno mawili yaliyowekwa pamoja ambayo hayapatani au hayaingiliani kwa kawaida. Katika baadhi ya mashairi mtunzi ametumia oksimora

kueleza hali fulani ijitokeze wazi. Kwa mfano, katika *Bara Jingine*, shairi “Mimi Monika” (uk. 37) lina Oksimora ambayo inaonyesha jinsi Monika ambaye ni kahaba hutabasamu kwa wanaume kwa tabasamu chungu mradi tu ajichumie riziki. Monika anatabasamu kwa wanaume si kwamba anafurahi kufanya kazi ya ukahaba bali ni kwa sababu ya umaskini na mfumo wa kijamii usiojali maisha ya watu wengine. Mtunzi anatumia maneno “tabasamu chungu” ambayo kwa kawaida yanakinzana kimantiki. Tabasamu huwa tamu bali si chungu Anasema:

Na kusimama pembeni
Nikisubiri kunyaka nafasi
Kuhudumia ulimwengu
Kwa tabasamu chungu (uk. 37)

Shairi “Ni Sumu kwa Watoto” (uk. 49) katika diwani hii pia linajitokeza na oksimora. Mshairi anaonyesha vile mapenzi, pesa na kudekeza kulikopita mipaka kutoka kwa mzazi kunaweza kumharibu mtoto ili aanze kushiriki uvutaji sigara, ulevi na dawa zingine za kulevya. Maneno “giza baridi” kwa mujibu wa matumizi ni oksimora inayoashiria ukosefu wa mwelekeo wa maisha ya usoni kwa watoto wanaotumia dawa za kulevya. Maneno “giza baridi” hayapatani au kuingiliana kwa kawaida. Hata hivyo, mwandishi anayatumia kuonyesha kuwa matumizi ya dawa za kulevya yanaweza kusababisha kifo kwa watoto. Mwandishi anasema:

Kwa mapenzi yako hatari
Ya kuwaliwaza watoto kwa pesa,
Pesa chungu nzima ambazo
Zinawafikisha kwenye sigara na ulevi
Na kisha kwenye dawa za kulevya
Barabara inayofikisha kwenye **giza baridi**... (uk. 50)

5.3.9.4 Uzungumzi Nafsia

Mbinu ya uzungumzi nafsia humsaidia msanii kupitisha ujumbe ulio katika moyo na akili yake kwa njia ya kujizungumzia yeye binafsi bila kumhusisha mhusika au mtu mwingine. Ujumbe unaopatikana katika uzungumzi nafsia ni mzito na unahitaji msomaji kuutafakari kwa makini. Uzungumzi nafsia ni mbinu ambayo humfanya msomaji pia azungumze na nafsi yake. Kwa mfano, katika diwani ya *Bara Jingine*, shairi “Wanabiashara Barabarani” (uk. 43) lina mbinu ya uzungumzi nafsia hivi:

Moyo unaniambia mwambie
Mwambie mhubiri anayehubiri
La, mhubiri
Hubiri bila kutusi

Wale ambao
Katika barabara za miji
Husimama pembeni
Macho yao
Yakizungumza kwa ufasaha,
Yakitangaza nia imara,
Mavazi yao
Yakitangaza nia imara...

**Moyo unaniambia mwambie
Mwambie mhubiri anayehubiri**

Ndio, mhubiri
Hubiri dhidi ya uvivu... (kur. 33-34)

5.3.9.5 Usimulizi wa Nafsi ya Pili

Mshairi ametumia usimulizi wa nafsi ya pili katika baadhi ya mashairi. Matumizi ya nafsi ya pili yanabainika kwa matumizi ya mofu “wewe” na urejelezi wa mofu “u”. Mbinu hii inapotumika huleta ukaribu kati ya msanii na kile anachokisema. Kwa mfano, katika shairi “Mgeni Katili” (uk. 4) katika diwani ya *Redio na Mwezi*, mwandishi anatumia nafsi ya pili kusimulia juu ya ugonjwa mgeni ambao ni ukimwi. Anasema, “**Wewe**, katili, jambazi la kutisha...” (uk. 4). Mwandishi ametumia mofu “wewe” kueleza madhara mbalimbali ya ugonjwa wa ukimwi.

Aidha, katika shairi “Rafiki Katili” (uk. 57) mshairi ametumia nafsi ya pili kusimulia madhara ya pombe kwa walevi. Mtunzi anasema kuwa pombe ni rafiki ya mlevi ambaye humpa mlevi ujasiri bandia, udanganyifu, kuropoka maneno ovyo na kuzua fujo miongoni mwa mengine. Mwandishi anatumia mofu “wewe” na “u” kusimulia juu ya pombe. Kupitia kwa masimulizi haya ya nafsi ya pili, tunaona matokeo ya pombe kwa mlevi na madhara anayofanya kwa watu wengine. Anaeleza:

Tembo, **wewe** ni sungura mjanja
Shujaa wa uzandiki na unafiki
Bingwa wa uwongo na **udanganyifu**
Unachezea akili na kuifanya butu
Unawarairai, unawadanganya
Unawatawala watu kwa mamlaka imara
Unawafanya kuropokwa na maneno... (kur. 57-58)

5.3.9.6 Uchimuzi

Mshairi ametumia mbinu yenye uwezo wa kueleza mawazo yake kwa njia ya maumbo yanayorahisisha maudhui kueleweka katika baadhi ya mashairi yake. Kama anavyoeleza Wamitila (2003a), uchimuzi ni mbinu ya kuyadokeza mambo fulani

katika kazi ya kifasihi kwa namna ya kufanya yajitokeze waziwazi. Mwandishi anayadokeza mambo fulani kwa kutumia maneno kisanaa kuunda michoro au maumbo fulani yanayosaidia kufafanua ujumbe anaokusudia msomaji aupate. Mbinu ya uchimuzi anayoitumia Kithaka wa Mberia katika ushairi wake inaonyesha ubunifu wa maendeleo katika ukuaji wa ushairi wa Kiswahili. Aidha, ni mbinu anayoitumia kuisitizia ujumbe fulani unaonekana kuwa muhimu katika ushairi wake.

Baadhi ya mashairi yanayodhihirisha uchimuzi yanapatikana katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Mashairi hayo ni kama “Boga” (uk. 2), “Nyumba” (uk. 17) na “Dau Haliendi!”(uk. 32). Katika diwani ya *Bara Jingine*, kuna mashairi kama “Mruko wa Nyuki” (uk. 20) na “Mwashi Mahiri” (uk. 45). Jambo muhimu katika mashairi haya yote ni ile picha ya shairi inayojitokeza machoni pa msomaji kuhusiana na kile anachokisema mshairi. Ufundi wake unaonekana kutokana na vile anavyoomba mashairi haya kwa kupanga maneno yachukue sura ya umbo la kitu anachokizungumzia. Mashairi haya ndiyo yanayojulikana kama mashairi-picha. Ingawa ni mashairi ya kimuundo lakini kwa upande mwingine ni mtindo anaoutumia mshairi kuwasilisha maudhui kwa njia rahisi ili yaeleweke.

Shairi “Boga” (uk. 2) kwa mfano linazungumzia kuhusu mboga uliostawi shambani ambao ulizaa boga. Mmoja wa vijana waliorithi shamba hili kutoka kwa wazazi wao anadai wakate boga hilo sehemu mbili zilizo sawa. Mtunzi anazungumzia umuhimu wa kugawa mali miongoni mwa wanajamii kwa usawa bila upendeleo wowote. Kwa kutumia maneno, mshairi anaunda shairi lenye picha ya tunda aina ya boga lililokatwa vipande viwili katikati kuanzia juu hadi chini ambapo kipande cha kushoto kina maneno ishirini na nane na cha kulia vilevile kina maneno ishirini na nane. Msomaji anaposoma na kutafakari anaona kuwa hili ni boga lililokatwa sehemu mbili sawa hivyo kuelewa kwa urahisi ujumbe wa mshairi katika shairi kuliko vile angeeleza bila kuunda umbo hilo la boga. Hivi ndivyo mtindo huu wa ubunifu unavyomwezesha mshairi kuwasilisha maudhui yake.

Katika shairi-picha liitwalo “Nyumba” (uk. 17), mtunzi anatumia maneno kwa usanii mkubwa kuunda shairi linalochukua umbo la nyumba. Kwa kutumia macho, msomaji ataona kuwa ni umbo la nyumba. Mshairi anasisitiza kuwa wale ambao hawakushiriki kuijenga hawapaswi kuishi mle ndani ila tu wale ambao “misuli yao iliipa uhai”.

Maskini waliojenga nyumba hiyo kwa misuli yao ndio wenye haki kuishi humo. Mshairi anaamini kuwa wale watu wanaosaidia kujenga nchi ambayo ndiyo nyumba, wanastahili kufurahia matunda ya juhudi zao. Watu wazembe na wanafiki hawafai kamwe kuishi humo yaani kufurahia jasho la wengine.

Uchimuzi unapatikana pia katika shairi “Mwashi Mahiri” (uk. 45) katika diwani ya *Bara Jingine*. Katika shairi hili mtunzi ametumia maneno kuchora taswira ya ziwa la mwanamke. Maziwa ya mama yana madini na kinga muhimu kwa afya ya mtoto. Mshairi anayalinganisha maziwa ya mama na mwashi stadi anayejenga nyumba imara. Kwa hivyo, mwandishi anahimiza kina mama kunyonyesha watoto wao wachanga ili wawe na afya njema. Watoto wenye siha njema hawatashambuliwa na magonjwa. Anawasuta wale kina mama wanaokosa kunyonyesha watoto wao kwa kuchukulia “titi” kuwa pambo ambalo lapaswa kulindwa “lisitiwe ulegevu na midomo michanga” kwa sababu ya usasa (uk. 46). Anawakemea wanabiashara wanaouza chupa za kunywesha watoto maziwa na uji kuwa wanachangia kuleta magonjwa kwa watoto kwa sababu ya viini vya uchafu vinavyopatikana kwenye chupa hizo kuliko ziwa la mama.

5.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia suala la utamaduni mahuluti katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Utamaduni mahuluti ni hali ya tamaduni mbalimbali kuathiriana. Ubepari na unyonyaji wa kiuchumi ni utamaduni ulioasisiwa na kuja kwa wakoloni na athari zao zinashuhudiwa hadi leo. Kwa sababu ya ulafi na unafiki, mabwanyenye wanakandamiza wanyonge katika harakati za kujilimbikizia mali. Hali hii huendeleza utabaka katika jamii. Wakati mwingine, wanyonge hufanya maandamano na migomo wakipinga dhuluma wanazofanyiwa na mabwanyenye kwa kudai haki na usawa.

Vitendo vya ukahaba, uasherati na usenge ni athari nyingine ya utamaduni mahuluti. Uovu huu haukushuhudiwa katika jamii za Kiafrika kabla ya wageni hao kuingia. Kuja kwa wakoloni, matumizi ya teknolojia kupitia mitandao na filamu yamechangia utamaduni huu mgeni kuenea kwa haraka katika jamii ya leo. Kwa hivyo, utamaduni mahuluti na athari zake katika jamii ni kichocheo kingine kinachompa ari Kithaka wa Mberia kutunga mashairi yake. Vilevile, tumebainisha kuwa suala la vileo na mihadarati miongoni mwa vijana na watu wazima ni athari nyingine ya utamaduni

mahuluti. Ubaguzi wa rangi na hadhi katika jamii ungalipo. Fauka ya hayo, tumeona kuwa unafiki wa kidini na elimu ya kigeni yote haya ni matokeo ya utamaduni mahuluti.

Katika kuangazia suala la utamaduni mahuluti, mshairi ametumia mtindo kwa njia maalumu kuweka wazi ujumbe wake kwa wasomaji. Vipengele vya kimtindo vilivyochanganuliwa na kuonyesha jinsi vimesaidia kuwasilisha maudhui juu ya utamaduni mahuluti ni pamoja na tashihisi, sitiari, tashibihi, tasifida, maswali ya balagha, chuku, kinaya, ritifaa na mbinu nyingine za kisanaa. Usasa wa mtindo unajitokeza pale mshairi anatumia mashairi-picha kama “Boga”, “Nyumba” na “Mwashi Mahiri” kuweka wazi kwa msomaji maudhui mbalimbali. Matumizi haya ya maumbo maalumu ndiyo yanayoonyesha uhusiano kati ya mtindo na maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

SURA YA SITA

DHULUMA NA UKOMBOZI WA WANAWAKE

6.1 Utangulizi

Wanawake wana wajibu muhimu katika masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mchango wao katika maendeleo ya kijamii hauwezi kupuuzwa. Lakini licha ya ukweli huu, wanawake wamewekwa pembeni na kudhulumiwa kwa njia nyingi kutokana na mifumo ya ubabedume inayomweka mwanamume mbele katika masiala mengi hasa katika bara la Afrika kwa mujibu wa mshairi. Kwa mfano, katika ulingo wa siasa, wanawake wanatengwa kwa fikira potovu kuwa siasa ni uwanja wa wanaume. Wanawake wanapoonyesha nia ya kuwania nyadhifa za uongozi, wanapuuzwa kuwa hawana uwezo wa kuongoza. Vilevile, katika uwanja wa elimu, jamii nyingi za Kiafrika huthamini elimu ya mtoto wa kiume kuliko mtoto wa kike kwa imani kuwa ataolewa kwingine na hivyo hatasaidia familia yake. Hata pale msichana anapohimili, yeye hulazimika kukatiza masomo yake lakini mvulana aliyemtunga mimba msichana huendelea na masomo yake hadi akahitimu. Isitoshe, kuna mila potovu zinazokandamiza wasichana na wanawake kwa jumla katika jamii za Kiafrika. Mambo haya na mengine mengi ni dhuluma kwa wasichana na wanawake. Katika sura hii, tumechanganua jinsi wasichana na wanawake wanavyokandamizwa kwa misingi ya ubaguzi na uwingine na kuonyesha hatua zinazofaa kuchukuliwa ili wajikomoe dhidi ya uovu huu. Aidha, tumechanganua mtindo alioutumia mwandishi na kuonyesha jinsi unamsaidia kuwasilisha maudhui yote yanayohusu dhuluma kwa wasichana na wanawake.

6.2 Maudhui

Maudhui yanayoonyesha dhuluma kwa wasichana na wanawake hasa katika jamii za Kiafrika ni: dhuluma za kimapenzi dhidi ya wasichana na wanawake, mila na tamaduni potofu zinazowakandamiza wasichana na wanawake, haki ya urithi wa mali ya familia na ukeketaji wa wasichana. Fauka ya hayo, kuna kutwezewa kwa wanawake wanaojifungua wasichana pekee, dhuluma za kinyumbani dhidi ya wanawake na uozaji wa wasichana wachanga kwa wazee matajiri miongoni mwa mengine.

6.2.1 Dhuluma za Kimapenzi Dhidi ya Wasichana na Wanawake

Kimsingi, suala la mapenzi linastahili kuhusisha hiari ya mwanamume na mwanamke mwenye umri wa miaka kumi na minane ambaye anaweza kufikiria vyema na

kuwajibikia kitendo cha ngono anapojitosa katika mapenzi. Hata hivyo, kutokana na ushawishi wa wavulana, wanaume wa umri wa makamo na hata wazee, wasichana wachanga hujipata wameingizwa katika mtego wa mapenzi ya mapema. Wakati mwingine, wasichana hujihusisha katika mapenzi kwa sababu ya umaskini ili kukidhi mahitaji yao ya kimsingi kama vile mavazi, chakula, makaazi na elimu miongoni mwa mengine mengi. Shida kuu hutokea pale msichana anayesoma huwa mjamzito. Mvulana au mwanamume aliyempachika mimba humtelekeza na mwishowe msichana huacha shule ili kulea mimba na mtoto aliyemzaa. Msichana hutaabika kumlea mtoto kwa sababu hana uwezo kifedha kumkimu mtoto wake kwa vile hakuwa tayari kuwa mzazi katika umri huo mchanga.

Katika diwani ya *Bara Jingine*, shairi “Giza Mbele” (uk. 26) linaeleza namna msichana wa shule anakatiziwa masomo yake na mzee mmoja tajiri akiwa darasa la nane. Mzee tajiri mwenye gari anamnyemelea msichana mchanga akitoka shuleni jioni moja. Anamchukua kwa gari lake na kwenda kusikojulikana. Mzee huyo anamdhulumu msichana huyo kimapenzi. Baadaye, msichana huyo anahimili na anaacha masomo akiwa katika darasa la nane. Maisha yake ya usoni yanaharibiwa na mzee ambaye anafaa kuwa babu yake. Msichana huyo anakosa matumaini katika maisha yake ya usoni. Watu wanapomwona katika hali hiyo wanabaki wakijiuliza ni nani aliyefanya hivyo, ilifanyika lini na kwa nini? Mzee hakukamatwa kwa kumharibia maisha. Mshairi anasema:

Kwa mjamzito-mtoto
Kinachobakia kichwani
Ni kumbukumbu ya maandishi
DARASA LA 8
Kwenye mlango
Wa jengo la jana,
Kinachosalia machoni
Ni giza mbele. (uk. 28)

Mwanamume huyu anayeelewa uchungu wa uzazi ndiye anayemtumia msichana wa shule kuridhisha uchu na tamaa zake za mwili bila kufikiria kuwa anaharibu maisha ya mtoto. Ni kinaya kwamba mtu anayemringa msichana wa shule ni mwanamume mzee tajiri ambaye anaweza kuwa babu yake. Msichana huyu anawakilisha wasichana wengi wanaodhulumiwa kimapenzi kwa sababu ya kutojua na umaskini kama anavyosema mtunzi:

Vitabu mkononi
Kutojua akilini
Umaskini nyumbani
Angojewa kwa hamu
Kama windo, anafika
Katika mtego wa hayawani. (uk. 26)

Ukatili mwingine kwa msichana wa shule unapatikana katika shairi “Pamela” (uk. 29). Msichana kwa jina Pamela alishambuliwa jioni moja akitoka shuleni na kundi la wavulana walevi. Wavulana hawa walimrarulia sare yake, wakatapanya vitabu vyake na hatimaye wakambaka. Mwandishi anatumia neno ‘mkasa’ kama tasifida kurejelea kitendo cha ubakaji alichotendewa Pamela. Mshairi anasema:

Zilianza fujo
Makelele
Mtapanyiko wa vitabu
Mikwaruzano na miguno
Miraruko ya mavazi
Mateke na meno
Mwanguko
Na kisha
Mkasa! (kur. 29-30)

Kitendo hiki kiovu alichofanyiwa msichana huyu kiliathiri maisha yake. Pamela, kwa kuogopa maswali mengi ya fedheha na kuonekana mchafu aliamua kunyamaza na kuweka siri ya tukio hilo baya. Lakini alidhurika akili kwa sababu ya mzongo wa fikira nyingi mpaka akawa kichaa mbali na kutembea uchi barabarani mbele za watu. Mtunzi anasema:

Pamela, mbali na shule
Leo unazurura sokoni
Ukiokota vitakataka
Na kutokwa na maneno
Yanayochoma masikio
Kama cheche za moto
Na mara kwa mara
Uchi wako
Ukitatiza macho ya watu
Kama umeme!(uk. 31)

Watu wengi wanaomwona msichana huyu katika hali hii ya kusikitisha wanasema mengi kumhusu kwa kutojua. Waumini wanasema ni mjeledi wa Muumba kwa wenye dhambi ilhali wazee wa kijiji wanasema ni uchawi mkali wa maziwa ya kinyonga. Wengine wanaona kuwa fahamu ya Pamela inatafunwa na laana ya marehemu mjomba wake. Hii ni dhuluma mbaya aliyofanyiwa na wavulana walevi iliyozima

matumaini na maisha mazuri ya usoni aliyokuwa nayo Pamela. Ajabu ni kuwa wavulana waliomtendea uovu huu wako huru na hawajatiwa mbaroni kwa kitendo cha ukatili walichotekeleza.

Visa vya walimu kuwadhulumu kimapenzi wasichana wa shule vimekithiri katika jamii kwa mtazamo wa mtunzi. Kwa mfano, kuna visa vingi vinatangazwa kwenye runinga na kuandikwa kwenye magazeti vile walimu wa shule za msingi na sekondari wanashiriki mapenzi na wanafunzi wao. Badala ya walimu kuwafunza mienendo mizuri, kuwaelekeza na kuwaandaa wasichana wa shule kwa maisha ya baadaye, wao ndio wanatumia nafasi zao kuwaharibia maisha. Katika shairi “Flora na Wenzake” (uk. 33) mwalimu mkuu anawaambia wanafunzi wa darasa la nane wawe wakifika shuleni alfajiri kwa masomo ya ziada. Mwalimu mkuu anatumia fursa hiyo kuwadhulumu kimapenzi wasichana wachanga. Siku moja alimwambia Flora aingie ofisini mwake kwa kumsingizia kosa ambalo hakuwa amelifanya. Hapo ndipo alipata fursa nzuri ya kushiriki mapenzi naye kisiri bila haya ofisini mwake akiwa amevaa sare za shule. Mshairi anasema:

Vidole bila adabu
Na ngozi changa
Zinakutana ghafla
Na kuchanganyika
Chini ya sare ya shule. (uk. 34)

Athari ya kitendo hiki inaanza kudhihirika pale mimba ya Flora inaanza kuonekana baada ya siku nyingi kupita. Sare ya shule haimtoshi. Habari kwenye gazeti inaeleza kuwa mwalimu mkuu amewafunza utu-uzima nusu ya wasichana wa darasa la nane katika shule ya Fikeni-Alfajiri. Kisa hiki kinagutusha wazazi na walezi wa watoto hao kujua lengo la mwalimu katika mikutano ya shule kwamba watoto wafike mapema kwa vile wana kazi muhimu kila asubuhi. Walimu wenzake wa kiume wanafahamu ni kwa nini alikuwa anajigamba kuwa hawezi kupata ugonjwa wa ukimwi ingawa yeye si malaika kwani alikuwa analala na wasichana wachanga akiamini kuwa wao hawawezi kumwambukiza virusi vya ukimwi. Mke wa mwalimu anabaini ni kwa nini mumewe alikuwa akitoka mapema kila siku asubuhi kwenda shuleni kukutana na wanafunzi.

Kwengineko, katika shairi “Nakumbuka Ulivyokuwa” (uk. 76) mshairi anaeleza yaliyomsibu msichana aliyekuwa akishiriki mapenzi ya kisirisiri na mwanamume

aliyeoa. Ingawa mtunzi hasemi wazi, ukweli ni kuwa majeraha mabaya aliyoyapata msichana huyo mwilini mwake yalitokana na kichapo alichokipata kutoka kwa mke wa mwanamume huyo. Kutokana na majeraha mabaya aliyoyapata, alilazwa hospitalini siku kadha ili kutibiwa. Mtunzi anasema:

Nakumbuka ulivyokuwa
Mwili dhaifu
Hamu hafifu;
Kama maji ya mtungi
Ulikuwa tuli
Katika kitanda,
Kwenye mkono wa kulia
Kwenye mkono wa kushoto
Alama za sindano
Za ulishaji wa mipira
Zikikumbusha wembamba
Ambao ulisimama kati
Baina yako
Na baridi ya kaburi. (uk. 76)

Kutokana na dondoo hili, wote wana hatia. Msichana alishiriki mapenzi na mume wa mtu. Mume naye alimsaliti mkewe kwa kuwa na jicho la nje. Katika kisa hiki haibainiki kama mume aliathirika kama msichana na ndio maana mtunzi anakariri kwa kurudia maneno “nakumbuka ulivyokuwa” ili kuonyesha dhuluma za kimapenzi zilizomkumba msichana pekee. Mara nyingi visa vya mapenzi nje ya ndoa hufanya wanawake na wasichana kuumizwa na wanawake wenzao wanaohisi uchungu kuwa wananyang’anywa waume zao. Wanawake hupigana, hutiana majeraha mwilini kama vile kuumana mashavu, masikio, kufumuana nywele mbali na kutukanana matusi makali.

Katika diwani ya *Redio na Mwezi*, kisa kingine cha dhuluma ya kimapenzi kwa mwanamke kinaonekana bayana katika shairi “Kisa Chuoni” (uk. 45). Katika shairi hili, mwanamke anaenda kutoa huduma za mapenzi chuoni. Anaenda huko akiwa na matumaini kuwa atalipwa pesa na mabarobaro wa chuo. Lakini baada ya kumaliza kutoa huduma kwa wateja wake chuoni, anapodai malipo wanafunzi wanamwita kahaba na kumtimua mbio kutoka chuoni humo bila kumlipa pesa zozote. Mshairi anaeleza:

Aliyehudumu kwa juhudi
Akijiambia kimoyomoyo
Kazi ni kazi

Bora watoto
Wapate maziwa
Akaondoka na machovu
Na mito ya machozi
Bila ndururu
Mfukoni! (uk. 46)

Mtunzi anasema kuwa wanafunzi wa chuo mara nyingi hutetea haki ya kulipwa mshahara mzuri, haki ya kusikilizwa na haki ya kuheshimiwa. Kwa hivyo, wao pia wangezingatia hayo yote baada ya kupewa huduma za mapenzi na mwanamke huyo. Kinaya ni kwamba wanamfurusha chuoni mikono mitupu akaondoka huku akilia kwa uchungu kwa vile watoto wake watakosa chakula. Hii ni dhuluma ya kimapenzi na ubinafsi kutoka kwa wanafunzi. Mtunzi anakemea kutolipwa kwa mwanamke huyu na hata kule kuwa ni wanafunzi wa chuo wanafanya kitendo hicho.

Visa vingine vya dhuluma za kimapenzi vinadhihirika katika mashairi kadha katika diwani ya *Rangi ya Anga*. Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya tisa, mshairi anazungumzia suala la ubakaji wa watoto wachanga, wasichana na wanawake. Wasichana wanadanganywa kwa peremende na mandazi kisha wanadhulumiwa kimapenzi faraghani. Mshairi anaeleza:

Wasichana wanatupiwa vyambo
Wanaraiwa kwa utamu wa peremende
Wanahadaiwa kwa ahadi za mandazi
Na kuvutwa hadi faragha za dhiki

Hata wanaotambaa sakafuni
Au wakembe wanaotembea ndende
Wanalazwa mahututi hospitalini
Baada ya tufani isiyotajika
Kuwasaga kama tamata mbivu
Wasichana na wanawake wazima
Wanaishi katika tanuri ya woga
Baruti za waliojaliwa misuli
Zinawalipua miili na akili. (uk. 12)

Visa vya ubakaji vimekithiri sana katika jamii nyingi siku hizi. Vinaangaziwa katika nchi mbalimbali za Kiafrika kwenye vyombo vya habari kama vile redio, televisheni na magazeti ya nchi husika. Wakati mwingine wahanga huuawa kinyama na wabakaji kwa nia ya kuharibu ushahidi ili wasitiwe mbaroni. Wengine hukatwa sehemu fulani kwa sababu ambazo hazieleweki. Hata kina mama ajuza hawasazwi katika ukatili

huu. Kwa jumla, mwanamke anadhaliwa kimapenzi na wanaume walio na misuli yenye nguvu ambao hutumia nguvu kuzima ashiki zao.

Katika Shairi “Rangi ya Anga”(uk. 1) sehemu ya kumi, mwandishi anaeleza jinsi mapenzi yanavyochipuka miongoni mwa wavulana na wasichana shuleni. Baada ya wote kushiriki mapenzi haramu na kwa bahati mbaya msichana akapachikwa mimba, mvulana huendelea na masomo yake mpaka akahitimu na kupata kazi nzuri kisha akaishi maisha mazuri. Kwa upande mwingine, msichana hutimuliwa shuleni kwa hatia ya ujauzito na hivyo ndoto yake inazimwa. Msichana huyo baadaye huishi maisha ya mateso, njaa, umaskini na kuanza ukahaba kusudi akimu mahitaji ya mtoto wake. Mwandishi anahadithia:

Walikuwa wachanga
Katika kivuli cha shule
Hisia za ujana zilipovutana
Mithili ya sumaku na chuma
Nyoyo zikalainika
Miili ikaitikia mwito mkali
Moto wa maumbile uliwaka...

Mmoja wa wawili washiriki
Aliendelea na mwendo shuleni
Akakusanya vyeti vya maana
Na kupata jina adimu nchini...

Lakini, kichefuchefu maalumu
Kilishambulia wa pili
Asubuhi zikavurugika bila kikomo
Akajipata katika ulimwengu mpya...

Leo, mjini
Akibeba njaa kama saratani ya tumbo
Na kuvaa umaskini kama joho la miba
Pamoja na wenza, anazurura jijini
Akitegea na kuchunguza magari yapitayo... (kur. 13-14)

Kupitia usimulizi huu mshairi anaonekana kusaili uhalali na haki ya mwanafunzi mvulana kuendelea na masomo yake ilhali alimharibia maisha mwanafunzi mwenzake wa kike. Anamulika jamii ambamo mfumo wa ubabedume unathamini masomo ya mvulana na kufumbia jicho elimu ya msichana kutokana na dhuluma za kimapenzi. Msichana au mwanamke kubaguliwa kwa misingi ya jinsia ni suala ambalo wanawake katika nchi zilizotawaliwa na wakoloni wanaliangalia. Wanaangalia hali yao tofauti na wanaume hasa katika zile tamaduni ambapo shinikizo

za kikoloni zikiunganishwa pamoja na misimamo asili ya kiume inawakandamiza maradufu. Wahakiki wa kifeministi katika ulimwengu wa tatu kama vile Spivak (1987) wametumia nadharia ya baadaukoloni kuweka wazi masuala yao. Halmashauri ya shule inamfukuza shuleni kwa sababu ya ujauzito. Hapewi nafasi ya kuendelea na masomo yake baada ya kujifungua. Maisha yake yanakuwa magumu ilhali maisha ya mshirika wake kwenye mapenzi yanawiri. Wasichana wengi wanaodhulumiwa kimapenzi kwa njia hii hukatiza masomo yao wakiwa katika shule ya msingi na sekondari kabla ya kuhitimu. Mfano mzuri wa vile msichana anafukuzwa shuleni baada ya kupachikwa mimba na mvulana mwenzake unapatikana katika tamthilia ya Mwachofi ya *Mama ee* (1987).

Tenge, msichana wa miaka kumi na sita anafukuzwa shuleni kwa sababu amepachikwa mimba na rafiki yake George aliye katika kidato cha sita. Anamlilia mamake amsamehe kwa kosa la kupachikwa mimba na kufukuzwa shuleni. Mwandishi anasema: TENGE: (*kwa kwikwi*) Nime...nimefukuzwa shu...shule nina...nina mi...mba (uk.10). Tenge anapofukuzwa shuleni, mshirika wake George anabaki shuleni akiendelea na masomo yake. Tenge anashangaa ni kwa nini anafukuzwa shuleni pekee ilhali George anaelimika. Tunasoma: TENGE: Lakini mama kwa nini, mimi tu nataabika? Nimefukuzwa shuleni, yeye George anaelimika? (uk. 14).

Wasichana wanaofanya kazi ya uyaya mijini vilevile hudhalilishwa kimapenzi wakati mwingine na wanaume wenye nyumba wanakofanya kazi ya kulea watoto, kazi za jikoni na usafi wa nyumba. Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya kumi na mbili, mshairi anaeleza kisa kilichomkumba yaya aliyekuwa anafanya kazi mjini. Msichana alianza kazi ya uyaya vizuri huku akitii maagizo, matarajio na matakwa ya mama mwajiri. Baada ya muda fulani, mume wa mwajiri wake alianza kumtamani kisiri. Alitafuta mbinu za kumnasa msichana huyo. Alianza kwa kumletea zawadi ndogondogo. Mshairi anasema:

Zilianza chichiri za chini kwa chini
Leo hanchifu kesho chokoleti au keki
Mtondogoo mafuta ya kufurahisha ngozi
Na kisha mavazi yasiyotajwa hadharani. (uk. 18)

Mwanamume huyo alipoona kuwa msichana amezugika akili kwa zawadi zake, siku moja aliondoka kwenda kazini. Mkewe alifuata baadaye. Mwanamume huyo alirudi

ghafla nyumbani akafanya mapenzi na msichana huyo. Baada ya miezi kadha, siri ya ujauzito ilifichuka kwa mama mwenye nyumba. Alianza kumtusi msichana kuwa ni mjanja na kiherehere aliyeleta wanaume nyumbani wakati wao wameenda kazini. Hakujua kuwa mumewe ndiye aliyempachika mimba msichana huyo. Hatimaye alimfukuza nyumbani humo. Mwandishi anaeleza:

Baada ya miezi minne ya machozi
Kiumbe kipya kilifungua mlango
Kikajibwaga kwenye mwanga wa dunia
Mama mkembe na mtoto wa siri
Wakaanza safari ngumu bila ramani
Punde si punde wakaingia kichakani
Wakawa mateka wa michongoma. (kur. 19-20)

Bila shaka shairi hili linazungumzia changamoto ambazo wasichana wanaofanya kazi ya uyaya mijini hukumbana nazo. Wao huamka alfajiri na kuanza kazi za jikoni kama kupika staftahi, kuogesha watoto waende shuleni, kupiga deki, kuosha nguo, kupika chakula cha mchana, kwenda sokoni kununua mboga na kisha kupika chakula cha jioni na kazi nyinginezo. Licha ya majukumu haya, wote hushawishiwa kufanya mapenzi na wavulana, wanaume wa nje na hata wanaume waliowaajiri kazi. Wanapopachikwa mimba, huachwa peke yao wakihangaika kulea mimba na watoto wanaowazaa. Wasichana hawa pamoja na wazazi wao waliowaachilia kwenda kufanya kazi ya uyaya ili wapate pesa za kujikimu nyumbani hujuta na kusunoneka siku zote.

Kwengineko, katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya kumi na nne, mshairi anaeleza kinagaubaga dhuluma za kimapenzi wanazofanyiwa wasichana na wanawake na wanajeshi katika jamii ya Wasamburu nchini Kenya. Wasichana na wanawake hawa wanashambuliwa na wanajeshi wanapokwenda kutafuta kuni kichakani, kwenda kuchota maji mtoni au wanapotumwa kupeleka ujumbe kwa majirani zao kuhusu ukosefu wa utulivu au usalama nyumbani. Wanajeshi hao hutumia hila za zawadi na ahadi na kisha huwabaka kwa kuziba vinywa vyao kwa nguo au vitambara. Mtunzi anasema:

Katika vijiji vya shuka nyekundu
Eneo la shanga shingoni
Hayawani wenye sare za kijeshi
Wakitumia hila za zawadi na ahadi
Huzuzua wenye upeo mdogo wa macho
Wamezewa mate wakoleapo pumbazo

Wamezapo vyambo walivyotupiwa
Huporomoshwa chini kwa dhoruba
Kuzibwa vinywa kwa nguo au vitambara
Na kuwageuza vyombo vya starehe. (uk. 21)

Wasichana na wanawake hawa waliodhulumiwa wanaposhtakia maonevu nyumbani huitwa washenzi, husingiziwa njama za uzinzi, hutukanwa, hupigwa kwa makofi, mateke na mijeledi na hata kupewa talaka ambapo baridi ya upweke na aibu huwatesa bila kikomo. Kwa upande mwingine, badala ya Jeshi la Malkia wa Uingereza kusimama kizimbani kujibu mashtaka ya kunajisi, wao huendelea kuishi kwa faraja na kiburi bila serikali ya nchi kuwachukulia hatua kali. Visa hivi vinaonyesha ukatili, ukosefu wa haki kwa wasichana na wanawake mbali na kutowajibika kwa upande wa serikali kulinda wananchi wake.

Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya kumi na saba, mshairi anaeleza ukosefu wa haki kwa wasichana wa shule wanaoringwa na walimu, jamaa pamoja na majirani. Watu hao wote wanakuwa mahasidi wakuu maishani mwa wasichana wa shule. Wasichana wakishapachikwa mimba na kuacha shule, wazazi, nyanya na babu zao hutafuta njia ya mkato kwa kuitisha rushwa kutoka kwa washukiwa kama fidia ya maonevu kwa mtoto ili haki isitendeke. Mshairi anawasuta kwa toni ya uchungu:

Binti aliyesafiria njia nyoofo na wazi
Anapojipata katika kinamasi cha mianzi
Badala ya wazazi kukang’ata fasiki ajute
Badala ya kung’ang’ania kwamba sheria
Inue mkono wenye mjeledi mkali
Ucharaze vikali mwili na akili ya mshukiwa
Wavyele wanaowazia maslahi ya pesa-nane
Wanajibwagaza katika shimo la ubinafsi:
Watazame wakinyosha mkono mkongwe
Ona wanavyotiririka na ulafi kama udede
Visikize vinywa vyao vikitaja pesa na kondoo
Ati fidia ya maonevu kwa mtoto! (uk. 26)

6.2.2 Mila na Tamaduni Potofu Zinazowakandamiza Wasichana na Wanawake

Tangu zamani, jamii za Kiafrika zina mila na tamaduni ambazo zinatoa mwongozo na taratibu za kuendesha maisha ya wanajamii katika hali na nyakati mbalimbali. Hata hivyo, kutokana na mpito wa wakati, baadhi ya mila hazina manufaa yoyote. Baadhi ya mila zinaonekana kumbagua na kumkandamiza msichana au mwanamke. Ni kwa sababu hii, ndipo kumetokea wanaharakati wa kifeministi, makundi ya kina mama na

sheria kwenye Katiba za kutetea haki za wanawake, kuhamasisha wanawake dhidi ya udhalimu wowote kutoka kwa mifumo mibovu ya unyanyasaji.

6.2.2.1 Haki ya Urithi wa Mali ya Familia

Kwa mujibu wa mila na tamaduni za Kiafrika, mvulana au mwanamume ndiye mwenye haki ya kurithi mali ya wazazi wake na si msichana au mwanamke. Mila na tamaduni kuhusu urithi wa mali zinambagua mwanamke. Mwanamke hapaswi kuhesabiwa katika ugavi wa mali yoyote katika familia yao. Kisa na maana ni kwamba msichana ataolewa kwengine na huko ndiko atachuma mali pamoja na mume wake. Bahati mbaya ni kuwa ndoa yake inapovunjika kwa sababu mbalimbali kisha arudi kwao alikotoka, unapata kuwa yeye hana kitu chochote alichorithishwa ili kimsaidie kujiendeleza kimaisha. Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya tatu, mtunzi anasema kuwa mwanamke anapodai apate sehemu ya mali, ugomvi huzuka hata damu ikamwagika. Mshairi anasema:

Kwamba kuwa navyo mkononi
Ni mpini wa upanga mkali
Mkononi mwa mwanamume
Na kiganja cha mwanamke
Kinaiposhiwa na stahamala
Na kujiinua mapambanoni
Hushika makali ya bapa
Ikatiririka damu bila hatia
Na ndoto ya kufikia usawa
Katika vuta nikuvute ya jinsia
Kuingia baridi. (uk. 3)

Mshairi anakerwa na desturi ya wanawake kutorithishwa mali kama wanaume kwa kuuliza “Ni nani ana haki ya kumiliki shamba, mimea anuwai shambani pamoja na mifugo?” (kur. 3-4). Mbona mwanamke asihesabiwe kama mmoja wa familia na arithishwe sehemu ya urithi? Inabainika kuwa mshairi anawatetea wanawake wanaobaguliwa na mila na tamaduni mbovu katika suala la urithi. Mwandishi anauliza:

Kwa kaida za kitamaduni
Tunatarajia nani, kwa furaha
Atwae tambarare zenye rutuba
Ambamo viazi-vikuu vya thamani
Na mihogo na viazi-vitamu adimu
Na karoti pendezi na wanga changa
Na vitunguu duara na karanga jamala
Zimejificha ndani ya udongo

Kama zana za wazalendo
Zikisubiri zamu iwadie
Zitetee uhai na uhuru? (uk. 4)

6.2.2.2 Ukeketaji wa Wasichana

Suala la kupasha tohara wasichana kwa mujibu wa utamaduni ni kitendo ambacho kinashutumiwa na wanawake wengi hasa wasomi na wakereketwa wengine wa ufeministi. Hata hivyo, licha ya wengi kupinga kitendo cha kukeketa wasichana, baadhi ya wanawake kutoka jamii zinazotekeleza matambiko hayo bado zinaunga mkono ukeketaji. Hawaoni ubaya wowote wa kusitisha ukeketaji wa wasichana. Lakini watu waliosoma na kushika dini wanaonelea kuwa kumkeketa msichana ni kukiuka haki za msichana kwa vile hulazimishwa kukeketwa bila hiari yake. Wanaopinga wanashikilia kuwa msichana hutwiwa uchungu wakati wa kitendo hicho, huvuja damu na huweza kuharibiwa sehemu yake ya uzazi akapata matatizo wakati wa kujifungua akishaolewa. Isitoshe, wasichana wengine hufa katika harakati ya kukeketwa mbali na uwezekano wa kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi. Wasichana wengine huozwa pindi tu wakishapashwa tohara kwani inakuwa ishara ya utu uzima na kibali cha kuolewa.

Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya tatu mshairi anaeleza kuwa wasichana wasiokeketwa wanatengwa na wazazi wao na kuitwa waasi na kusutwa kupitia nyimbo za wasanii waliofungwa pingu za mila. Katika miaka ya nyuma wasichana walikeketwa na hata sasa baadhi ya jamii za Kiafrika bado zinaendeleza mila hii. Hata hivyo, kuna njia murua ya kuvusha wasichana hatua hii muhimu maishani bila kuwakeketa. Isitoshe, sheria imeharamisha kitendo hiki na kutetea haki za wasichana. Msimamo wa mshairi ni kuwa ni dhuluma na aibu kumkeketa msichana kwa kushikilia utamaduni na mila zilizopitwa na wakati. Anasema:

Wasanii waliofungwa pingu za mila
Wametungia nyimbo sumbufu kama mpupu
Wakilalamika kwamba kijana wa kike
Kukataa kukeketwa kunakokeketwa
Ni kinyume na utamaduni wa kabila
Ni kitendo kinachonuka vumba ya aibu! (uk.6)

6.2.2.3 Kutwezwa kwa Wanawake Wanaojifungua Wasichana Pekee

Kulingana na utafiti wa kisayansi, mwanamume ndiye huchangia kuzaliwa kwa mtoto wa kiume wala si mwanamke. Mwanamke anapojaaliwa watoto wa kike tu,

wanaoshikilia taasubi ya kiume humbeza, humdharau, humkemea na kumlaani vikali. Jamii za Kiafrika hushikilia kuwa ndoa haikamiliki bila kuwa na mtoto wa kiume. Dhana hii huelekea kumthamini mtoto wa kiume kuliko mtoto wa kike. Huu ni ubaguzi wa kijinsia dhidi ya mtoto msichana. Watu wengi, wanaume na hata wanawake wenyewe vilevile huamini kuwa mtoto wa kiume ni muhimu katika familia kuliko wa kike. Sababu wanazotoa ni kuwa mtoto wa kiume atawafaa wazazi wake kwa vile msichana ataolewa kwingine akishakuwa mtu mzima, atarithi mali ya familia na vilevile ataendeleza kizazi.

Mshairi anamulika changamoto anazopitia mwanamke anayejaaliwa wasichana pekee kama anavyouliza ifuatavyo katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya nne:

Tueleze, huu ukweli
Au ni mazigazi machoni
Kwamba mamako mzazi
Anaishi katika tufani
Upepo wa masuto ya daima
Na fedheha na vitisho vizito
Ukimviringisha kwenye vumbi
Kwa “kosa lisilostahimilika”
La kuleta duniani watoto wa kike
Badala ya “watoto wastahiki”? (uk. 6)

6.2.2.4 Dhuluma za Kinyumbani Dhidi ya Wanawake

Katika baadhi ya jamii, wanaume huwapiga wake zao kama njia ya kuonyesha upendo kwao, wanapokosea au pengine hata bila makosa. Aidha, wanaume katika jamii kama hizo wanaamini kuwa kumpiga mwanamke ni ishara ya mapenzi. Wanaume hao hushikilia kuwa mwanamke ni kama mtoto na hivyo anafaa kuadhibiwa ili kufuata na kutii maagizo yao siku zote. Isitoshe, wanaume hao wanaoshikilia mfumo wa ubabedume hudai kuwa mume ana haki ya kumwadhibu mkewe kwa sababu alilipa mahari.

Wanawake hao hupigwa kwa fimbo, mijeledi, ngumi, mateke na makofi. Kulingana na maelezo ya mshairi, wanawake hao huachiwa makovu na mikwaruzo usoni, migongoni, mikononi au hata miguuni. Damu huwatoka puani na vinywani na hata meno kung’olewa. Kwa maoni yetu na ya mtunzi pia, huu ni ukatili wa hali ya juu kwa mwanamke. Mambo yanapozidi na mke kurudi kwao, huambiwa na wazazi na ndugu zake arudi kwa mumewe avumilie maisha hayo. Mshairi akizungumzia uovu

huu kwa uchungu na kejeli katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya tano anafafanua:

Mume amemwadhibu mkewe -
Wanawake, ni kama watoto
Usipowarudi, hupoteza njia!

Nyuso zetu zilipoingia kunyanzi
Kwa kutoridhika nyoyo
Sauti “ilifafanua”
Mume ana haki thabiti
Anaruhusiwa kumwadhibu mkewe
Si alilipa mahari! (uk. 7)

6.2.2.5 Uozaji wa Wasichana Wachanga kwa Wazee Matajiri

Kwa mujibu wa Katiba, umri mwafaka wa msichana kuolewa na mvulana kuoia ni miaka kumi na minane. Licha ya ukweli huu, baadhi ya jamii za Kiafrika ambazo hazithamini elimu ya wasichana, zinaoza mabinti zao wenye umri wa miaka chini ya kumi na minane. Jamii hizi huchukulia wasichana kama vitega uchumi vya kujitwalia mali ili kujiondolea umaskini nyumbani. Kwa hivyo, wazazi hupanga kuoza wasichana kwa wazee fulani wenye mali bila hiari yao. Wazazi hawa wanapofanya hivyo, hukiuka haki za kimsingi za wasichana kama vile haki ya elimu, haki ya kujichagulia mume anayempenda na haki ya mapenzi na ulinzi wa wazazi. Hatua hii huwaumiza wasichana wachanga kisaikolojia. Mshairi anawasuta wazee wenye mali wanaoharibu maisha ya wasichana wadogo. Hii ni aibu na ni tabia isiyostahili kuruhusiwa wala kukubaliwa katika jamii ya leo. Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya sita, mtunzi anasema:

Wewe sasa ni mtu mzima
Mshale wa mizani ya miaka
Unaonyesha miaka kumi na minne
Mbona usiolewe na Mzee Malimali
Kusudi mahari ya ng’ombe na mbuzi
Ituzimie moto wa umaskini
Kama wingu kuu la masika
Likizima ukame nyikani? (uk. 8)

Mshairi anakerwa na vilevile kukejeli tabia ya profesa mmoja katika kafeteria, mwenye vyeti vya masomo, pesa, kipara na ndevu akijigamba kwa wahadhiri wenzake kuwa aliposa na kumuoa msichana ambaye umri wake haukuzidi miaka kumi na mitatu. Anashangaa ni kwa nini msomi anajigamba kwa kitendo cha aibu kama hicho. Mshairi anaeleza:

Nilisikia profesa
Vyeti nyumbani
Fedha mifukoni
Kipara utosini
Ndevu kidevuni
Tabasamu midomoni
Na T-bone viganjani
Akijigamba kwa wenza-

Nilipoposa, nikachumbia
Niliyemchumbia, nikamuoa
Hakuzidi kumi na tatu
Kwenye mizani ya miaka! (uk. 9)

6.2.2.6 Dharau ya Mvulana kwa Kigezo cha Tabia ya Mwanamke

Katika jamii za Kiafrika zinazoshikilia mfumo wa ubabedume, mvulana au mwanamume hutarajiwa kuwa na tabia ambayo inamsawiri kuwa tofauti na msichana au mwanamke. Hii ni dhana ya ubaguzi wa jinsia na uwingine katika nadharia ya baadaukoloni. Mwanamume anapotenda jambo linalohusishwa na mwanamke, hukumbushwa kuwa yeye si mwanamke. Kauli ya namna hii humtweza na kumbagua mwanamke. Inaonyesha kuwa mwanamke hana thamani mbele ya mwanamume. Kigezo hiki cha kitamaduni huendeleza ubaguzi wa jinsia ya kike. Kinamweka mwanamume juu ya mwanamke na kumsawiri kuwa tofauti kimaumbile na kwa uwezo dhidi ya mwanamke. Katika shairi “Rangi ya Anga”(uk.1) sehemu ya sita, mshairi anauliza:

Apandapo kwenye akili ya mwanawe
Sio mmea wenye majani ya tiba
Bali wenye matunda ya sumu
Kwa kubeza akisema:
U mwanamume gani
Ushindwaye na madogo
Kama mwanamke? (uk. 9)

Kupitia malezi yao kwa watoto wa kiume kina mama wanaendeleza msimamo hasi kwao wenyewe badala ya kutetea na kuinua hadhi ya mwanamke. Wanaonekana kukubali kuwa mwanamume hafai kushindwa na mambo madogo kama mwanamke. Mwanamke ni kiumbe dhaifu. Hata wanawake wasomi hawapingi nyanyaso hizo bali wanaziunga mkono kwa kukiri kuwa hizo si taasubi, ni mila na kaida za utamaduni. Wanakubali mila na tamaduni zinazomweka mwanamke pembeni siku zote. Ndiposa mtunzi anashangaa:

Profesa wa kike
 Mwenye shahada ya uzamili
 Ateteapo viini vya matende
 Akibeua:
 Hiyo
 Si taasubi
 Ni desturi na mila!
 Hizo
 Si nyanyaso
 Ni kanuni za jadi!
 Hizo
 Si dhuluma
 Ni kawaida za utamaduni! (kur. 9-10)

Katika shairi hili “Rangi ya Anga” (uk. 1), mwandishi anapinga desturi, kanuni na kaida za utamaduni ambazo zinamkanyagia chini mwanamke. Kina mama hawafai kuwakaripia watoto wao wa kiume wasicheke, au kulia kama mwanamke kama anavyoshauri mshairi katika sehemu ya saba:

Usicheke kiholela
 Kama wewe ni mwanamke!
 Nyamaza! Futa machozi!
 Ushindwaye na madogo
 Kama mavazi yako
 Ni kamisi na rinda! (uk. 10)

6.2.2.7 Nyanyaso za Kimapenzi za Wavulana kwa Wasichana Kupitia

Utamaduni Potofu

Katika jamii za ufugaji wa kuhamahama, wavulana wanapobaleghe hutafuta wasichana wa kujiburudisha nao kimapenzi. Barobaro anapokutana na msichana anayempendeza, huenda kwa wazazi wa msichana na kuwaeleza nia yake ili kwa idhini ya kitamaduni ajitafutie faraja. Wazazi wanapokubali ombi lake bila kumuuliza msichana msimamo wake, ghulamu huanza kutafuta pesa za kumnunulia msichana shanga za rangirangi. Mshairi anaeleza katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya kumi na tano hivi:

Ombi linapendeza masikio masikivu
 Bila kujali kama kibali cha wazazi
 Kitaufanya moyo wake kuwaa kwa furaha
 Au kufa ganzi kwa kumbo la majonzi
 Ghulamu huanza mikakati kabambe
 Kutafuta hadi kupata uwezo wa darahima
 Kununulia shanga za rangirangi (uk. 23)

Mvulana anapofaulu kununua shanga, anarudi kwa akina msichana siku iliyopangwa ili kumvisha shanga shingoni kama ishara kuwa yeye ni mchumba wake na ana haki na kibali cha kufanya mapenzi naye wakati wowote akitaka asipende. Ndiposa mshairi anasema:

Kuanzia hii siku tamu kwa mmoja
Siku ya bashasha kwa shababi
Siku ya machozi kwa kimanzi
Kila barobaro ajionapo mhitaji
Kila mwili wake unapootea dhoruba
Ghulamu huacha wenzake mbugani
Na kwa fahari kurejea manyatta
Kusubiri mwangaza kuaga anga
Ndipo atembelee kibanda cha maliwazo
Kwa kanuni zilizoidhinishwa na utamaduni
Kudai na kupata faraja ya usiku kucha
Kidosho asipende ni mamoya (uk. 24)

Kupitia utamaduni katili, wazazi ambao wanafaa kulea na kulinda watoto wao wasichana dhidi ya dhuluma zozote ndio wanatoa mabinti zao kwa wavulana kuwadhulumu kimapenzi. Hawazingatii idhini wala hisia za msichana katika hatua hiyo. Wazazi hao huongozwa na ubinafsi wa zawadi wanazopewa na wavulana na kuruhusu watoto wao kudhalilishwa. Mshairi anaona kuwa tamaduni kama hizi zimepitwa na wakati na zinastahili kuzikwa katika kaburi la saha.

6.2.3 Ukombozi wa Wanawake na Usawa wa Kijinsia

Mwanamke anastahili kujinasua kutokana na udhalimu wa mifumo ya ubabedume, tamaduni na mila potofu zinazombagua, kumuonea mwanamke na kumkweza mwanamume. Hatua hiyo itamfanya mwanamke kuwa huru na mwenye uwezo wa kujisimamia katika mambo mengi. Aidha, elimu kwa wasichana itaondoa mpaka na ukosefu wa usawa wa kijinsia uliopo kati ya wanawake na wanaume. Mshairi anapendekeza kuwa mwanamke anaweza kujikomboa kupitia kumwelimisha mtoto msichana. Elimu kwa mtoto msichana itamhamasisha kuhusu mambo mengi mbali na kumpatia kazi ambazo zinaaminika kuwa ni za wanaume tu. Mwandishi katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya kumi na moja anaonyesha kuwa kuna matumaini mapya katika maisha ya msichana na wanawake kwa ujumla kupitia elimu. Anaeleza:

Upepo wenye manukato ya elimu
Tayari unapulizia mbali mnuko
Kutoka ukumbi wa maisha:
Mijini na mashambani

Shule za upili za wasichana
Zimekuwa barabara adimu
Za kufikisha wasafiri kilimani
Mbali na bonde la unyonge;
Katika shoroba za vyuo vikuu
Katika mihadhara na semina
Minyororo na pingu za jinsia
Zinakerezwa kwa ukakamavu
Mabewa ya kutajika
Yanapamba mandhari
Kwa uhalisi mpya
Unaotumbuiza macho
Na nyoyo za wapenda usawa (uk. 15)

Kwa mujibu wa mshairi, elimu bora kwa wasichana itawasaidia kuwa mahakimu, marubani, madaktari sawa na wanaume madaktari, mameneja kwenye benki, wakubwa jeshini na wakuu wa utawala. Kazi hizi zote na nyinginezo zimechukuliwa kuwa za wanaume. Lakini kupitia elimu, wasichana na wanawake watapewa nguvu na uwezo wa kushindana na wanaume kuimarisha maisha yao. Kwa njia hiyo, mpaka wa kijinsia na ukiritimba wa kitaaluma utakuwa umeondolewa na usawa kudhihirika kama mshairi anavyosema:

Wasioamini waamini
Wakiritimba wa anga
Hawana tena mizungu
Elimu kwa waliopuuzwa
Mwamko imara wa kisiasa
Na mkataba mpya wa fahari
Ni beti adimu
Za shairi la usawa (uk. 17)

6.3 Mtindo Katika Dhuluma na Ukombozi wa Wanawake

Vipengele vya kimtindo ambavyo tumevichanganua hapa ni pamoja na tashibihhi, sitiari, tashihisi, tasifida, kinaya, maswali ya balagha na chuku. Mbinu nyingine za kisanaa tunazoangazia ni pamoja na takriri, nidaa, tanakali za sauti, mgao wa tamthilia, usimulizi, uchimuzi na sajili ya gazeti.

6.3.1 Tashibihhi

Mwandishi ametumia tashibihhi kwingi katika mashairi yanayogusia dhuluma kwa wasichana na wanawake. Analinganisha hali wanazokumbana nazo ili kupata picha nzuri ya kinachosemwa mbali na kuvutia na kunasa makini ya msomaji. Shairi “Giza Mbele” (uk. 26) katika diwani ya *Bara Jingine* linagusia juu ya mzee mmoja tajiri

ambaye anamnyemelea msichana wa darasa la nane jioni moja akitoka shuleni. Mzee anamwingiza katika benzi jekundu na kutoweka naye kisha anamdhulumu kimapenzi. Baadaye, msichana anahimili na kuacha shule akiwa darasa la nane. Maisha na elimu ya msichana huyo inaharibiwa na ndio maana ya “giza mbele” kulingana na mshairi. Mwandishi anapoeleza vile watoto walitawanyika kutoka shuleni jioni hiyo kuelekea nyumbani anasema:

Wanafunzi na walimu
Wanatoleana kwaheri
Uwanja wa shule
Unayeyuka taratibu
Kama barafu ya rangirangi (uk. 26)

Mwandishi anatumia tashibihii “uwanja wa shule unayeyuka taratibu kama barafu ya rangirangi” kutoa picha jinsi watoto waliokuwa wengi walitawanyika kwenda nyumbani mmoja baada ya mwingine mpaka uwanja wa shule ukabaki mtupu sawa na vile barafu iliyoganda inavyoyeyuka na kuwa maji. Mbali na kutoa picha, tashibihii hii inatia ladha lugha ya mwandishi.

Aidha, msanii anaeleza vile benzi jekundu la mzee karibu na lango limetulia akimsubiri msichana atokomee naye kusikojulikana. Anasema, “ Karibu na lango, **benzi jekundu limetulia tuli likisubiri kama chatu**” (uk. 26). Mwandishi analinganisha benzi jekundu na chatu ambaye ni nyoka hatari aogopewaye na binadamu. Mtunzi anaeleza vile mzee tajiri akiwa ndani ya benzi lake jekundu anamsubiri msichana huyo kama vile chatu anavyosubiri kushambulia windo lake lisilojua hatari inayolingojea. Msichana wa shule anatoka shuleni lakini hajui kuwa mzee mwenye benzi anamngojea langoni ili atoroke naye. Mshairi anasema kuwa, “**kama windo**, anafika katika mtego wa hayawani” (uk. 26). Msichana analinganishwa na windo ilhali mzee analinganishwa na mnyama asiye na huruma kama vile simba au chui. Tashibihii hizi zinachora taswira ya namna msichana asiye na habari anaingia katika mtego wa mzee mhuni ambaye hana uadilifu wowote.

Baadaye, mwandishi anaeleza vile mzee alianza kumdhulumu kimapenzi bila aibu wakiwa mafichoni. Anasema kwamba, “**Mkono mkongwe kama karne** ukitetemeshwa na ndoto taratibu unaanza mwendo” (uk. 27). Mtunzi analinganisha uzee wa mkono wa mzee huyo na miaka mia moja. Anaonyesha kuwa licha ya umri wake mpevu, mzee hana aibu bali anaanza kumtomasatomasa ili kumtia nyege

msichana huyo mchanga. Mtunzi akionyesha namna msichana ameharibiwa maisha na mzee huyo baada ya kumdhulumu kimapenzi anasema, “**Awamu ya maisha tayari imeshapita kama maziwa ambayo yamemwagika vumbini**” (uk. 27). Tashibihi hii ina maana kuwa kitendo alichomfanyia msichana huyo kimemharibia maisha yake na ni vigumu kurekebisha hali hiyo. Kwa mfano, ni dhahiri kuwa amevunja ubikira wa msichana huyo mdogo.

Baada ya kitendo hicho cha siri, inabainika kuwa msichana ni mjamzito. Watu wanashangaa kuona msichana mdogo wa darasa la nane akiwa na mimba. Wanabaki kujiuliza maswali ni nani alimringa, ilikuwa lini na kwa nini. Mwandishi akionyesha ukali wa maswali hayo anasema, “Kwa waliolea kwa taabu na kusomesha kwa dhiki, **maswali yanachoma akili kama ukucha wa n’nge** ukichoma mwili” (uk. 27). N’nge ni mdudu ambaye ana sumu. Anapochoma ukucha wake mwilini mwa mwanadamu anamwachia sumu hiyo ambayo inamduru. Kwa hivyo, maswali wanayojiuliza watu kuhusu chanzo cha mimba ya msichana huyo yanawasumbua akili sawa na ukucha wa sumu kali ya n’nge mwilini. Mwandishi anatumia tashibihi hizi kujenga taswira mbalimbali katika akili ya msomaji ili kurahisisha ujumbe wake umfikie msomaji na kuonyesha jinsi wazazi walivyoathirika na wana wao kuharibiwa maisha.

Katika shairi “Pamela” (uk. 29) katika diwani hii ya *Bara Jingine*, mshairi anazungumzia maudhui ya ubakaji. Anaeleza vile wavulana waliokuwa walevi walimshambulia msichana kwa jina Pamela alipokuwa anatoka shuleni jioni kisha wakambaka. Mtunzi anatumia tashibihi kadha kueleza kisa hicho cha unyama alichotendewa Pamela. Kwa mfano, mwandishi anaeleza vile Pamela alikuwa anafuata njia kuelekea nyumbani kwao jioni hiyo akitoka shule. Anasema, “**Taratibu kama mto ambao unakaribia bahari**, Pamela ulifuata mapindo ya njia”(uk.29). Tashibihi hii inatuonyesha picha ya mwendo wa asteaste wa Pamela akitembea polepole njiani akitoka shuleni sawa na mwendo taratibu wa mto unaokaribia bahari bila kasi yoyote.

Pamela hakujua kuwa kuna wavulana waliomwotea njiani wakiwa walevi kwa pombe na moshi leweshi unaotoka kwenye dawa za kulevya za kuvutwa kama hashisha. Msanii akieleza hali yao anatumia tashibihi hivi; “Pombe na **moshi leweshi zikitawala vichwani kama malaria ya ubongo** ikitawala mgonjwa” (uk. 29). “Malaria ya ubongo” ni kulevya kwa vileo mbalimbali na “mgonjwa” ni wavulana

wenyewe ambao walikuwa hawajijui sasa baada ya kutumia vileo. Msanii anatoa picha vile wavulana hao walevi walimshambulia Pamela kwa kusema, “Ulipokanyaga mtego **walikushambulia kama mbwa-mwitu** wakishambulia funo mpweke” (uk. 29). Wavulana wanalinganishwa na mbwa-mwitu naye Pamela akiwa ndiye funo anayetembea peke yake. Ulinganishi huu unaonyesha kuwa Pamela alikuwa peke yake na hangekuwa na nguvu za kujikinga dhidi ya shambulizi la mabarobaro hao walevi. Walitawanya vitabu vyake, wakamkwaruza, wakamrarulia mavazi yake, wakampiga kwa mateke kisha wakamwangusha chini na kumnajisi. Kwa hivyo, wavulana ndio walikuwa mbwa-mwitu naye Pamela akawa ndiye funo mpweke. Wavulana hao wanapomaliza ukatili wao kwa Pamela, wanaondoka wakijifahari kwa kusema kuwa alikuwa bikira.

Baada ya Pamela kubakwa na wavulana hao maisha yake yaliharibika na akabaki kuwa gizani. Mtunzi anasema, “Ulibakia gizani huku **maisha yako yamechafuliwa kama nguo nadhifu iliyovamiwa na mwani ufukweni**” (uk. 30). Mshairi analinganisha maisha ya Pamela baada ya kunajisiwa na nguo safi iliyochafuliwa na mmea wa mwani wenye rangi ya kijani kibichi kwenye maji. Kitendo hiki kilimfanya Pamela kuwa na hofu nyingi asiambie mtu yeyote ili asiulizwe maswali ya aibu au aonekane kuwa mchafu na hivyo alikiweka siri. Mtunzi anasema, “Hofu nyingi **zikakufunga kinywa ukawa kimya kama kaburi**. Siri ikabakia siri **ikakusuka kwa ujeuri kama mawimbi ya bahari** yakisukasuka dau katika dhoruba” (uk. 30). Mwandishi analinganisha unyamavu wa Pamela na namna kaburi linavyokimya baada ya maiti kufukiwa humo. Aidha, analinganisha kitendo cha siri kumsuka Pamela na mawimbi ya bahari yanayorusha dau hapa na pale wakati wa dhoruba.

Kitendo hiki cha kubakwa kiliathiri akili ya Pamela mpaka akawa kichaa kwa sababu ya mzungo wa akili. Aliacha shule akaanza kuzurura sokoni akiokota vitakataka na kuropokwa maneno yenye aibu huku akitembea uchi pia. Mtunzi anasema, “ Na kutokwa na **maneno yanayochoma masikio kama cheche za moto na mara kwa mara uchi wako ukitatiza macho ya watu kama umeme.**” (uk. 31). Maneno makali yanayotoka kinywani mwa Pamela yanalinganishwa na cheche za moto ilhali uchi wake unaosumbua macho ya wapita njia unafananishwa na mweso wa umeme. Ni bayana kuwa Pamela alianza kuropoka maneno ya aibu kwa watu kwa sababu ya kutojijua na watu walibia kumwona akitembea bila nguo. Baadhi ya watu wasiojua

yaliyomfika kabla ya hali hiyo walisema alirogwa kwa maziwa ya kinyonga ilhali wengine walisema ilikuwa laana ya marehemu mjomba wake.

Katika shairi jingine “Flora na Wenzake” (uk. 33), maudhui ya dhuluma za kimapenzi yanaendelezwa na mwalimu mkuu katika shule ya msingi ya Fikeni-Alfajiri. Mwalimu mkuu anawaambia wasichana wa darasa la nane wafike shuleni mapema kwa masomo ya ziada. Mwalimu mkuu anatumia fursa hiyo kuwadhulumu kimapenzi wasichana wengi. Mmoja wa wasichana hao ni Flora. Mtunzi anaeleza vile macho ya mwalimu mkuu yanaangalia katika sebule ya ofisi. Anasema kuwa, “**Macho ya mburukenge yanatupa miali kama ya nyegere mwenye kichaa**” (uk. 34). Macho ya mwalimu yanatoa mwanga unaofananishwa na macho ya nyegegere mwenye kichaa. Isitoshe, mwalimu huyo anamsingizia Flora mashtaka ya uwongo na “**kumziba pumzi kama bahari ikifunika asiyejua kuogelea**” (uk. 34). Mashtaka ya uwongo yanamfanya Flora amuogope mwalimu mkuu na hivyo anashindwa kujitetea kama vile mtu asiyejua kuogelea anafunikwa pumzi na maji ya bahari akabaki akitapatapa majini. Huo ndio ujanja anaoutumia mwalimu na kumshurutisha Flora kuingia ofisini mwake, kumtomatomasa kisha kumdhulumu kimapenzi bila hiari yake.

Kitendo cha mwalimu mkuu kumdhulumu kimapenzi flora kinasababisha Flora kuwa mjamzito. Baada ya miezi kadha, sare za Flora zinaanza kuonyesha hali yake ya ujauzito. Nyanyake Flora anapouliza chanzo cha hali hiyo na kupata jibu, anapatwa na mshangao. Ndipo mwandishi anasema, “**Majibu ya Flora yanachoma na kuzama kama mishale yenye sumu ikizama ndani ya nyama.**” (uk. 35). Majibu ya Flora kwa nyanyake kuwa ujauzito wake umetokana na mwalimu mkuu wa shule ya Fikeni – Alfajiri yanachoma kwenye masikio ya nyanyake sawa na mishale yenye sumu inavyozama ndani ya nyama. Hii ina maana kwamba nyanya haamini majibu ya Flora. Tashibihi hii inaonyesha picha ya mshangao alioupata nyanyake Flora.

Kwengineko, katika shairi “Nakumbuka Ulivyokuwa” (uk. 76) mshairi anaeleza masaibu yaliyomkumba msichana aliyekuwa anashiriki mapenzi na mume wa mtu na mwenye watoto. Mke wa mume huyo alimshambulia msichana huyo na kuumumiza sana. Shambulizi hilo lilimfanya msichana kwenda hospitali kupewa matibabu. Alikuwa na alama za sindano za ulishaji wa mipira kwenye mikono yake. Kwenye

nywele kichwani alikuwa na ukoko mweupe ulioonyesha kuwa alikuwa amepigwa eksirei. Bila shaka hii ni taswira ya kuonyesha jinsi msichana huyo alikuwa amepigwa na mke huyo. Kwa hivyo, mwandishi anatuonyesha picha dhaifu ya msichana akiwa amelala kwenye kitanda hospitalini akiuguzwa majeraha kwa kusema, **“Kama maji ya mtungi ulikuwa tuli katika kitanda”** (uk. 76). Kimya cha msichana kitandani kinafananishwa na maji yaliyotulia ndani ya mtungi. Tashibihii hii inatoa picha vile msichana alikuwa hana nguvu wala uwezo wa kujigeuza, alikuwa ametulia tu akiwa kitandani baada ya kupigwa kiasi kwamba unamwonea huruma kwa hali yake mbaya.

Kuna kisa cha dhuluma za kimapenzi katika diwani ya *Redio na Mwezi* katika shairi “Kisa Chuoni” (uk. 45). Wanafunzi wa chuo kikuu ambao kwa mujibu wa mwandishi wanashiriki kwenye visa vya kuchoma magari ya watu barabarani na kuharibu mali ya wanabiashara kunapotokea fujo, wanapendekeza haki ya kulipwa jasho, ya kusikilizwa na haki kutekelezwa siku zote. Hata hivyo, hawazingatii falsafa hii. Mwanamke mmoja aliyeingia chuoni mwao na kutoa huduma za mapenzi kwa wanafunzi wa kiume alipodai haki ya kulipwa pesa zake, wanafunzi hao waliungana na kumfukuza kutoka chuoni humo bila kumpa pesa zozote. Mwandishi anatumbea picha ya namna mwanamke huyo alivyofukuzwa anaposema kuwa, “Wapinga dhuluma walitoka kwa wingi na **kumkimbiza mchuuzi kama mbwa-mwitu wakimkimbiza swara katika Maasai Mara.**” (uk. 46). Katika kisa hicho, wanafunzi hao wa chuo wanalinganishwa na mbwa-mwitu ilhali mwanamke huyo analinganishwa na swara. Huu ni uhalisia maanake jambo hili linatokea katika mbuga ya Maasai Mara kwani mbwa-mwitu hufukuza swara ili wawaue na wapate kitoweo.

Katika diwani ya *Rangi ya Anga*, katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya tisa, mwandishi anaeleza visa vya ubakaji wa watoto wachanga, wasichana na wanawake. Wanaume wanadanganya wasichana kwa kuwapa peremende na mandazi kisha wanawabaka. Uovu huu unafanywa kwenye kalvati za mabustani, karibu na vituo vya usafiri, katika vichochoro mitaani, ndani ya vichaka vijijini na hata magari ya umma usiku. Mwandishi anaonyesha vile hata watoto wakembe hawasazwi katika dhuluma hiyo kwa kusema, “Hata wanaotambaa sakafuni... wanalazwa hospitalini baada ya **tufani isiyotajika kuwasaga kama tamata mbivu**” (uk. 12). Nguvu kali za wanaume wanaodhulumu watoto wasichana wanaotambaa zinalinganishwa na tufani ilhali watoto hao wanafananishwa na tamata iliyoiva sana. Msomaji anapata

taswira ya watoto wachanga walivyodhulumiwa kama vile nyanya mbivu hupondwapondwa ikikanyagwa. Kupitia ulinganishi huu, mshairi anaibua hisia za uchungu na huruma mtawalia.

Mara nyingi visa vya mapenzi haramu kati ya wavulana na wasichana wanaposoma shuleni hutokea. Mshairi anaeleza vile mapenzi yalichipuka kati ya mvulana na msichana na kuonyesha hatima yake katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya kumi. Anaeleza kuwa “**Hisia za ujana zilipovutana mithili ya sumaku na chuma; nyoyo zililainika... moto wa maumbile uliwaka na kisha kuzimika mithili mwako mbugani**” (uk. 13). Mwandishi analinganisha hisia za mvulana na msichana kuvutana pamoja kama vile sumaku na chuma zinavyovutana na kushikana. Aidha, analinganisha hisia zao za kushiriki mapenzi haramu na moto unaowaka na kuzimika mbugani kwa maana kuwa walikubali kushiriki mapenzi ili kuzima kiu yao ya tamaa. Tashibihi hizi mbili zinatumiwa na mwandishi mtawalia kutoa msisitizo wa ujumbe mbali na kutia ujumi kwenye lugha ya mshairi. Lakini msichana aliishi maisha ya umaskini baada ya kujifungua. Mwandishi anasema, “**Akibeba njaa kama saratani ya tumbo na kuvaa umaskini kama joho la miba**” (uk. 14). Mwandishi anafananisha njaa na saratani ya tumbo inayosumbua mtu na umaskini wa msichana huyu unaomsumbua kama vazi lenye miba linalochoma mwilini. Tashibihi hizi zinaonyesha mateso aliyoyapata msichana huyo baada ya kutelekezwa na mvulana rafikiye baada ya kupata mimba na kujifungua.

Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya kumi na mbili, mwandishi anaeleza changamoto na dhuluma za kimapenzi za yaya fulani. Anasema, “Kwa **ahadi tamu kama halua** wakala alimrairai mama – mzazi akamnyakua binti kutoka shamba” (uk. 17). Ahadi nzuri kwa mama zinafananishwa na halua iliyomfanya mama akubali kumtoa binti yake. Mshairi anakariri kuwa, “**Na baridi ya alfajiri isiyocheka na watu zikawa wandani mithili ya chanda na pete. Amri yenye meno kama ya msumeno ya mama** mwajiri akitangaza majukumu.” (kur. 17-18). Katika tashibihi ya kwanza, mwandishi anafananisha urafiki wa baridi ya alfajiri na msichana ili kutoa picha ya mateso anayopitia anapoamka mapema ili kuanza majukumu ya siku. Yaya anafanya kazi nyingi za nyumba bila muda wa kutosha wa kupumzika. Tashibihi ya pili inaonyesha amri kali ya mama mwajiri akitoa maagizo ya kutekelezwa ili kazi ifanywe anavyotaka.

Mimba ya yaya haingeweza kuzuilika isionekane hadharani. Ndipo mshairi anasema, “Huzuiliwaje **siri ambayo kila uchao huumuka kama unga wa ngano** uliokolezwa hamira ya thamani?” (uk. 19). Mshairi analinganisha mimba na siri. Mimba inaendelea kukua sawa na unga wa ngano uliotiwa hamira. Mimba ya yaya ilianza kukua sawa na unga wa ngano uliokandwa kwa hamira unavyofura. Mama mwajiri alipogundua uja-uzito wa yaya, alimtusi na kumsingizia kuwa alikuwa analeta wanaume nyumbani wakati hayuko. Hakujuu kuwa hiyo mimba ya mjakazi ilikuwa ya mume wake. Alimfukuza nyumbani humo mara moja. Baada ya miezi michache, msichana alijifungua mtoto haramu na wakaanza kuishi maisha ya taabu. Bila shaka hii ni dhuluma ya mwanamume mtu mzima kwa msichana mdogo.

Msanii anaeleza vile walimu, jamaa na majirani huwapachika mimba wasichana wachanga wa shule. Ajabu ni kwamba badala ya wazazi kuwachukulia hatua kali washukiwa, wao huongozwa na tamaa ya kupewa pesa na kondoo kama fidia ya maonevu kwa msichana. Mwandishi katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya kumi na saba anasema, “**Badala ya hamaki yao kufurika kama magma**, wanashuka kwenye mvo mchafu wa utimbakwira” (uk. 26). Mtunzi anamaanisha kuwa badala ya wazazi wa msichana aliyepachikwa mimba kuwa na hasira kama mvuke moto wa magma na kumchukulia hatua za kisheria mshukiwa, wao wanakuwa na tamaa ya pesa na mifugo ili kuficha uovu huo. Wazazi wanaongozwa na ubinafsi kuitisha fidia na kuzuia sheria imwadhibu mshukiwa. Hatua hiyo inamnyima haki msichana aliyeringwa.

Maudhui ya ukeketaji wa wasichana ni suala analogusia mshairi katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya tatu. Ukeketaji wa wasichana ni kitendo kinachopingwa katika jamii za Kiafrika na wanaharakati wengi kutokana na madhara yake kwa mtoto wa kike. Licha ya pingamizi, wazazi wanaoshikilia utamaduni huu huwatenga wasichana wanaokataa kukeketwa kwa kuwachukulia kuwa waasi wa mila. Kwa mujibu wa mwandishi, “Wasanii waliofungwa pingu za mila wametungia **nyimbo sumbufu kama mpupu**” (uk. 6). Nyimbo zinalinganishwa na majani ya mmea fulani unaowasha unapogusa ngozi ili kuonyesha jinsi zinavyoumiza akili na mioyo ya wasichana wanaokataa kupashwa tohara. Wasanii hao wanatunga nyimbo za kukashifu wasichana wanaokataa kukeketwa. Ukeketaji wa wasichana ni dhuluma inayokiuka haki za mtoto wa kike kwa kushikilia mila potovu.

Wanawake wengi walioolewa hukumbana na dhuluma za kinyumbani kutoka kwa waume zao. Baadhi ya wanaume hupiga wake zao kwa madai kuwa wanawake ni kama watoto kwani wasipopigwa watapotea njia. Kwa wengine, mwanamke sharti aadhibiwe kwa sababu walilipa mahari. Wanawake hao hupigwa makofi, ngumi na hata fimbo. Athari za kuadhibiwa huko ni mikwaruzo na makovu kwenye mwili, uvimbe kwenye uso au shingo, matone ya damu puani, kulegezwa kwa meno mdomoni na macho kupasuliwa. Mtunzi akionyesha dhuluma kama hizo kwa mwanamke katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya tano anasema, **Tumeona mikwaruzo na kovu katika mikono na shingo na mashavu na vipaji kama kwamba chui aliyeudhika amepigana vita vya kulipiza dhidi ya binadamu kizimbani**” (uk.7). Majeraha anayopata mwanamke mwilini kutokana na kichapo cha mumewe yanaleta taswira ya chui aliyepigana na binadamu kizimbani akitaka kula mifugo.

Mara kwa mara visa vya wasichana wachanga kuoza kwa wanaume wazee matajiri vinashuhudiwa katika jamii nyingi. Kitendo hiki hunyima wasichana fursa ya kusoma, kukua kimwili, kiakili na uhuru wa kujichagulia wachumba miongoni mwa mengine. Miongoni mwa sababu zinazochangia wazazi kuoza mabinti zao ni ubinafsi na umaskini kama anavyosema mshairi katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya sita, “Mbona usiolewe na Mzee Malimali **kusudi mahari ya ng’ombe na mbuzi ituzimie moto wa umaskini kama wingu kuu la masika likizima ukame nyikani?**” (uk. 8). Mtunzi anasema kuwa mahari ya ng’ombe na mbuzi inaweza kupunguza umaskini wa hali ya juu uliopo kwa kina msichana kama vile mvua ya masika inaweza kupunguza ukame kwenye eneo kame.

6.3.2 Sitiari

Katika diwani ya *Bara Jingine*, kuna shairi “Giza mbele” (uk. 26) linalozungumzia namna mzee tajiri mwenye benzi jekundu anamwotea msichana wa darasa la nane na kumdhulumu kimapenzi. Baada ya kitendo hicho msichana anakuwa mjamzito kama anavyosema mshairi kuwa, **“Katika nyanda za mbali katika udongo mpya, kunachipuka mche...”** (uk. 27). Maneno “nyanda za mbali katika udongo mpya” ni sitiari inayorejelea chupa ya uzazi ya msichana ambamo kijusi kinaendelea kukua. Mshairi analinganisha kijusi kinachokua tumboni mwa msichana mchanga na mche unaomea kwenye udongo ambao haujatumika.

Mwandishi ametumia sitiari nyingine katika shairi “Flora na Wenzake” (uk. 33) katika diwani hii ya *Bara Jingine*. Katika shairi hili, msanii anaeleza juu ya tabia ya mwalimu mkuu wa shule ya msingi kushiriki ngono na wasichana wa darasa la nane. Anawaambia wafike mapema kwa masomo ya asubuhi lakini anatumia wakati huo kuwadhulumu kimapenzi wasichana zaidi ya nusu ya darasa. Anatumia vitisho ili wakubali matakwa yake. Flora, mmoja wa wasichana hao anakuwa mjamzito. Mwandishi anaeleza tabia mbovu ya mwalimu mkuu kwa kusema, “Katika sebule ya ofisi **macho ya mburukenge** yanatupa miali kama ya nyegere mwenye kichaa” (kur. 33-34). Mwandishi anamlinganisha mwalimu na mburukenge yaani mnyama kama mamba mdogo anayeishi kwenye nchi kavu.

Msanii anamwita mwalimu mkuu katika shule ya Fikeni-Alfajiri mbweha. Anasema, “Wenzake **mbweha** sasa wamepata fasiri ya majigambo yake.” (uk. 36). Mbweha ni mnyama anayefanana na mbwa mwitu anayekula kuku. Ulinganishi huu una maana kwamba mwalimu huyo wa kiume alikuwa na tabia ya kuwadanganya au kuwashurutisha wasichana wa darasa la nane ili ashiriki mapenzi nao kama vile mbweha anavyokamata na kuwala kuku. Kwa hivyo, katika muktadha huo mwalimu mkuu ndiye mbweha na wasichana ndio kuku wanaoliwa. Mwalimu mkuu alikuwa anajigamba kuwa hawezi kupata ugonjwa wa ukimwi kwa kufanya mapenzi na wasichana wadogo kuliko wanawake wakubwa ambao kwa maoni yake wangeweza kuwa na ugonjwa huo. Hizi ni fikira potovu na ukosefu wa uadilifu kwa mwalimu mkuu. Heshima aliyopewa na wazazi, walimu na wanafunzi ilitoweka hulka yake ya uozo ilipogunduliwa. Mwalimu mkuu ni mfano wa walimu wengi wanaowanyanyasa kimapenzi wasichana wanaosoma shuleni na wanafaa kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

6.3.3 Tashihisi

Mwandishi ametumia tashihisi katika shairi “Giza Mbele” (uk. 26) katika diwani ya *Bara Jingine*. Katika shairi hili, mzee tajiri mwenye benzi jekundu anamwotea msichana anayesoma katika darasa la nane ili amchukue kwenda kujifurahisha naye. Mtunzi anaeleza ni wakati gani mzee anamnyemelea msichana. Ni bayana kuwa ni wakati wa jioni baada ya masomo ya siku kukamilika kwani wanafunzi na walimu wanaambiana kwaheri. Mshairi anasema, “**Mchana unajiandaa kupasha usiku kigongo katika rilei isiyokoma**” (uk. 26). Katika hali halisi, wanariadha

wanaokimbia uwanjani hupokezana vigongo kwenye mbio za rilei. Mtunzi anaeleza vile mchana unaanza kupisha usiku siku hiyo baada ya shughuli za mchana kutwa shuleni. Maelezo yake yanaonyesha kaida ya kimaumbile mwangaza kupishana na giza daima. Huo ndio ulikuwa wakati mwafaka wa mzee kumnyemelea msichana wa shule ili atoroke naye kwenye benzi lake.

Kuna matumizi ya tashihisi katika shairi “Pamela” (uk. 29). Mshairi anapoeleza vile Pamela aliogopa kuambia watu kitendo cha ubakaji alichotendewa na wavulana walevi njiani akitoka shuleni anasema, “**Hofu nyingi zikakufunga kinywa...**” (uk. 30). Katika dondoo hili, hofu alizokuwa nazo Pamela zimepewa uwezo wa kufunga kinywa chake ili asiseme chochote. Aidha, mwandishi anasema, “**Siri ikabaki siri ikakusuka kwa ujeuri**” (uk. 30). Siri pia inapewa sifa ya kumtikisa Pamela kwa ujeuri kana kwamba ni mwanadamu.

Kwengineko, katika shairi “Flora na Wenzake” (uk. 33) mwandishi anaeleza kisa cha mwalimu mkuu alivyowadhulumu kimapenzi wasichana wa darasa la nane kiasi cha kuwapachika mimba. Mmoja wa wasichana hao ni Flora. Mwalimu mkuu alikuwa anawaambia wanafunzi wafike mapema shuleni kwa masomo ya ziada. Ni wakati huo ambapo alitimiza uchu wake kwa wasichana hao wachanga. Katika kuonyesha ni wakati wa alfajiri mshairi anasema, “Haya ni makutano ya usiku na mchana, katika mashariki **jua lachomoza uso likitabasamu**” (uk. 33). Binadamu ndiye hutabasamu wala si jua. Mwandishi anatumia tashihisi ya jua kuchomoza uso likitabasamu kuchora taswira ya vile jua lilitokea na kutoa miale yake ya mwangaza wakati huo wa macheo wakati wanafunzi walifika shuleni.

Aidha, katika shairi hili “Flora na Wenzake” mwandishi anatumia tashihisi kueleza vile sare ya shule ilianza kumkaza Flora kwa vile mimba yake ilianza kukua kadiri siku zilivyosonga. Mshairi anasema, “**Sare ya Flora polepole, inapanda na kukataa kushuka**” (uk. 35). Sare ya shule ya Flora haikupanda na kukataa kushuka kama mwanadamu bali mshairi anaeleza vile mimba ya Flora ilikua hadi nguo yake ya shule ikawa haimtoshi tena kama hapo awali. Ni taswira inayoonyesha jinsi Flora alivyoonekana ndani ya sare yake na inachangia kumgusa msomaji kwa dhuluma za kimapenzi alizotendewa na mwalimu mkuu.

Katika diwani hii ya *Bara Jingine* katika shairi “Nakumbuka Ulivyokuwa” (uk. 76) mshairi anazungumzia kuhusu matokeo ya mapenzi haramu kati ya mume na msichana mmoja. Mke wa mume alimshambulia msichana na kumjeruhi vibaya hadi akalazwa hospitalini ili kupata matibabu. Mshairi anaeleza:

Katika nywele
Ukoko mweupe
Ulidhihirisha wazi
Kwamba **eksirei**
Ilikutembelea
Ili kukujulia hali (uk. 76)

Mshairi ametumia tashihisi anaposema kuwa “eksirei ilikutembelea ili kukujulia hali”. Tamathali hii inafaa hapa katika kuwasilisha maana aliyokusudia mtunzi kwa sababu inaonyesha kiasi cha majeraha aliyopata msichana huyu ndio maana akapigwa eksirei hospitalini. Anachomaanisha mwandishi ni kuwa msichana alichunguzwa kichwa chake kwa mtambo wa eksirei kubaini ikiwa fuvu la kichwa chake lilikuwa limevunjika.

Katika diwani ya *Rangi ya Anga*, kwenye shairi “Rangi ya Anga”(uk.1) sehemu ya kumi na mbili, mshairi ametumia tashihisi kuzungumzia athari za dhuluma za kimapenzi kwa yaya kutoka kwa mwajiri wake anayemfanyia kazi mjini. Mume wa mke alivutiwa na yaya mpaka akaanza kumletea zawadi bila mke wake kujua. Asubuhi moja mke alipoenda kazini, mume alirudi nyumbani na kushiriki mapenzi na yaya. Mwandishi anasema, “**Mlango wa nyumba ulipomuaga mama**, baba aliyetangulia kuondoka nyumbani hugeuza gari na kulielekeza lilikotoka...” (uk.18). Mlango umepewa sifa ya kibinadamu ya kuaga. Hivyo ndivyo alivyofanya kisirisiri kwa mazoea mpaka akamringa msichana wa kazi. Baada ya kuhimili, matokeo ya kitendo hicho cha siri yalianza kuonekana mpaka mke alipotambua kuwa msichana wa kazi alikuwa mjamzito. Mshairi anaeleza, “Baada ya **rinda la mhudumu mchanga kukataa katakata kuwa mshiriki siri**” (uk.19). Mwandishi ametumia tashihisi hii ya rinda kukataa kuwa mshiriki wa siri kueleza taswira ya msichana na pia kuonyesha kuwa siri ya mimba imefichuka kwani inianza kuonekana bayana kutokana na vile nguo zilivyombana.

Katika sehemu ya kumi na saba katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1), mwandishi anazungumzia ukosefu wa haki kwa wasichana wanaodhulumiwa kimapenzi na wavulana, watu wa ukoo na hata walimu mpaka anahimili. Mara tu msichana

anapokuwa mjamzito, badala ya wazazi, nyanya na babu kutafuta haki kutoka kwa taasisi za sheria dhidi ya washukiwa, wao hupendelea kulipwa fidia ya pesa na kondoo kwa maonevu ya mtoto wao. Anaona kuwa huo ni ubinafsi kwa upande wa wazazi, nyanya na babu na ukosefu wa haki kwa msichana. Mwandishi anatumia tashihisi anapoeleza hali hiyo kuwa, “Badala ya kung’ang’ania kwamba **sheria iinue mkono wenye mjeledi mkali ucharaze vikali mwili na akili ya mshukiwa**, wavyele wanaowazia maslahi ya pesa-nane...” (uk. 26). Kawaida sheria si mtu ambaye anaweza kuinua mkono wenye mjeledi lakini mshairi anamaanisha kuwa mshukiwa anayemdhulumu msichana mdogo anastahili kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria badala ya wazazi, nyanya na babu kuitisha fidia ilhali msichana anasononeka kwa kuachishwa shule, kulea mimba na shughuli ngumu ya kumlea mtoto anayemzaa. Hiyo si haki kamwe kwa msichana bali ni ubinafsi na biashara ya namna fulani kwa mdhulumuwa.

6.3.4 Tasifida

Katika jamii nyingi kuna miko na makatazo ya kutumia lugha ya uwazi, hasa kuhusiana na uchafu wa matusi au karaha ya aina fulani (Mohamed 1995). Kwa sababu jamii imejiwekea ulazima wa kutotumia maneno fulani waziwazi, lazima itafute mbinu ya kuvieleza vitu, dhana au matendo yanayohitaji siri. Njia inayotumika ni kutumia kauli ya mzunguko au mafumbo kutaja hayo. Tasifida hutumiwa na msemaji au mwandishi ili kupunguza makali ya tamko au maandishi fulani. Mara nyingi tasifida huchochewa na utamaduni wa jamii katika matumizi ya lugha ambapo kauli fulani hazifai kutumiwa kiholela ili kudumisha heshima na mahusiano miongoni mwa wanajamii mbali na kuonyesha ukomavu wa kiwango cha lugha cha mtu.

Katika diwani ya *Bara Jingine*, katika shairi “Giza Mbele” (uk. 26) mwandishi anatumia tasifida kueleza vile mzee tajiri mwenye benzi anavyomdhulumu kimapenzi msichana mafichoni. Mshairi anaeleza, “Mkono... taratibu unaanza mwendo kuanzia **miguu ya nje hadi maeneo ya mbali...**” (uk. 27). Mwandishi ametumia maneno “maeneo ya mbali” kurejelea sehemu za siri za msichana ili kudumisha heshima kwa sababu kitendo cha mapenzi na sehemu za siri hazistahili kutajwa wazi kwa sababu ya utamaduni. Aidha, mwandishi anaendelea kusema, “**Tufani inapozima** na fahamu na mwili kutanduka ukungu awamu ya maisha tayari imeshapita” (uk. 27). Mshairi anaposema kuwa “tufani inapozima” anarejelea kitendo cha kufanya ngono baina ya

mzee na msichana huyo mchanga ambaye baadaye anakuwa mjamzito na hivyo maisha yake kuingia gizani.

Kwengineko, katika shairi “Flora na Wenzake” (uk. 33) mwandishi anatumia tasifida kuchora taswira vile mwalimu mkuu alivyomdhulumu Flora ndani ya ofisi yake. Anasema, “Vidole bila adabu na ngozi changa zinakutana ghafla na **kuchanganyika chini ya sare ya shule**” (uk. 34). Maneno haya yanarejelea vile vidole vya mwalimu vilianza kugusa mwili wa msichana baada ya kumvua nguo. Aidha, katika shairi lili hili mshairi anasema kuwa, “Mwalimu-mkuu wa shule ya Fikeni-Alfajiri **ameshawafunza utu-uzima** nusu ya wasichana katika darasa la nane” (uk. 35). Kirai “ameshawafunza utu-uzima” nusu ya wasichana kina maana kuwa mwalimu mkuu amefanya tendo la ngono na nusu ya wasichana katika darasa la nane lakini mwandishi anaamua kutumia “utu-uzima” kwa sababu mapenzi kisheria yanastahili kuhusisha watu wenye umri wa miaka kumi na nane na zaidi. Kulala na wasichana wa shule ni sawa na kuwafunza vitendo vya watu wazima.

Katika diwani ya *Rangi ya Anga* kwenye shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya kumi na mbili, mshairi anaeleza kisa cha dhuluma ya mapenzi kati ya yaya na mwajiri wake mjini. Baada ya mume anakofanya kazi kummezea mate, alianza kumnyemelea na kumshawishi kwa kumnunulia zawadi ndogondogo. Mwandishi anasema, “Zilianza chichiri za chini kwa chini. Leo hanchifu kesho chokoleti au keki, mtondogoo mafuta ya kufurahisha ngozi na kisha **mavazi yasiyotajwa hadharani**”(uk.18). Mshairi anatumia tasifida anaposema “mavazi yasiyotajwa hadharani” kurejelea chupi na sidiria alizonunuliwa yaya na mwajiri wake.

Aidha, katika sehemu ya kumi na nne, mshairi anazungumzia ukatili waliofanyiwa wanawake katika jamii ya Wasamburu. Wanajeshi wa Uingereza walitumia hila, zawadi na ahadi kuwadhulumu wanawake Wasamburu walipokuwa wakienda vichakani kutafuta kuni au kwenda mtoni kuchota maji. Mwandishi anatumia tasifida kueleza vile walibakwa, “Wamezapo vyambo walivyotupiwa, huporomoshwa chini kwa dhoruba, kuzibwa vinywa kwa nguo au vitambara na **kuwageza vyombo vya starehe**” (uk. 21). Kauli “kuwageza vyombo vya starehe” ni tasifida ambayo mshairi anatumia kuonyesha vile wanawake hao walibakwa na wanajeshi wa Uingereza. Chambo ni chakula ambacho mvuvi huweka kwenye ndoana anapovua samaki ili

anapokula amnase kwa urahisi. Kwa hivyo, wanajeshi pia walitumia zawadi za kuwavutia wanawake hao ili waridhie matakwa yao.

6.3.5 Kinaya

Katika diwani ya *Bara Jingine* kwenye shairi “Giza Mbele” (uk. 26) mwandishi anaonyesha vile mzee mmoja tajiri mwenye benzi jekundu anakuja kumnyemelea msichana wa darasa la nane jioni moja na kumpeleka mafichoni. Katika hali ya kawaida, wavulana ndio wanastahili kuwanyemelea wasichana wa shule lakini si wazee. Katika shairi hili, ni kinaya kwamba mzee tajiri ambaye anastahili kuwa babu ya msichana huyu, mzee mwadilifu anayejiheshimu na mshauri mkuu ndiye anamwotea msichana wa shule na kumpeleka mafichoni kumdhulumu kimapenzi. Matokeo ya kitendo hiki ni kuwa msichana huyu wa darasa la nane anakuwa mjamzito. Masomo yake yanakatizwa na mzee na hivyo maisha yake ya mbeleni yanaingia giza. Hili ni jambo la kufedhehesha kwa vile wazee matajiri wanatumia unyonge na umaskini wa wasichana wa shule kuwapatia pesa na zawadi nyinginezo kisha kuwadhulumu na kuwapachika mimba.

Kinaya kingine cha dhuluma za kimapenzi kinapatikana katika diwani ya *Redio na Mwezi* katika shairi “Kisa Chuoni” (uk. 45). Katika shairi hili, mwandishi anasema kuwa wanafunzi wa chuo mara nyingi hutetea haki ya kulipwa mshahara mzuri, haki ya kusikilizwa na haki ya kuheshimiwa. Siku moja mwanamke mmoja alienda chuoni kutoa huduma za mapenzi kwa wanafunzi wa chuo akiwa na matumaini kuwa atalipwa pesa za kutimizia mahitaji ya watoto wake. Baada ya kuwahudumia, alidai malipo lakini wanafunzi hao wa chuo walimwita kahaba na kumtimua mbio kutoka chuoni humo bila kumlipa pesa zozote. Ni kinaya kuwa wanafunzi hao wanaohimiza haki ya kulipwa mshahara mzuri, ya kusikilizwa na haki ya kuheshimiwa ndio wanakosa kumtendea haki mwanamke aliyewapa huduma za mapenzi kwa kutomlipa pesa kulingana na makubaliano kabla ya kutoa huduma hata kama hiyo ni biashara haramu. Ingekuwa vizuri kama wangemfukuza kabla ya kutoa huduma chuoni badala ya kumfukuza baada ya kupewa huduma zenyewe.

Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya kumi na nne katika diwani ya *Rangi ya Anga* mwandishi anaeleza mateso wanawake wa jamii ya Wasamburu wanayopitia mikononi mwa wanajeshi wa Uingereza na waume zao. Wanawake Wasamburu wanabakwa na wanajeshi wanapoenda kutafuta kuni vichakani au kuchota maji mtoni.

Wanawake hao wanaporipoti dhuluma hizi kwa waume zao nyumbani, badala ya waume zao kuwaonea huruma na kushtaki wanajeshi, wanaume hao wanawatukana wake zao, kuwapiga makofi, mateke na mijeledi na mwishowe kuwataliki. Mwandishi anasema, “Waliosagwasagwa katika kinu cha mkasa wanaposhtakia maonevu nyumbani, huitwa washenzi wajionao werevu na husingiziwa njama za uzinzi” (uk. 21). Vitendo hivi vya wanaume Wasamburu kwa wake zao baada ya kudhulumiwa na wanajeshi wa Uingereza vinaonyesha wazi kinaya cha hali kwa sababu wanaume hao wanastahili kuwatetea, kuwalinda na kupigania haki za wake zao dhidi ya dhuluma kutoka kwa wanajeshi hao. Lakini hawafanyi lolote isipokuwa kuwatesa zaidi.

Isitoshe, katika shairi hili “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya kumi na saba, kinaya kinajitokeza vilevile. Mshairi anaeleza vile wasichana wa shule wanapachikwa mimba na walimu, watu wa ukoo pamoja na majirani. Mwandishi anasema kuwa wasichana hawa wakiringwa, wazazi, nyanya na babu zao huitisha malipo kutoka kwa washukiwa kama fidia ya maonevu kwa mtoto. Kitendo hicho cha kudai fidia kinaonyesha kuwa wazazi, nyanya na babu hawako tayari kuruhusu sheria ifuatwe na washukiwa kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria ili msichana apate haki kutoka kwa waliomdhulumu. Kwa hivyo, ni kinaya kuwa wazazi, nyanya na babu hawawalindi watoto wa kike kama inavyotarajiwa na jamii pana dhidi ya wadhalimu lakini wanawasaidia wanaodhulumu msichana kutembea huru. Ikiwa adhabu kali haitatolewa kulingana na sheria, basi visa kama hivyo vitaendelea kushuhudiwa kila kuchao na wasichana wachanga hawataendelea na elimu yao bali watakuwa wazazi wachanga wenye watoto haramu.

6.3.6 Maswali ya Balagha

Mwandishi ametumia maswali ya balagha mahali kwingi katika ushairi wake. Kwa mfano, katika diwani ya *Bara Jingine* katika shairi “Giza mbele” (uk. 26) wazazi waliolea kwa taabu na kusomesha kwa dhiki wanajiuliza maswali ya balagha wanapona msichana mdogo wa darasa la nane akiwa mjamzito. Wanataka kujua ni nani aliyemringa msichana huyo, lini na kwa nini? Mwandishi anasema, “**Jamani ni nani? Ilikuwa lini? Kwa nini?**” (uk. 27). Tunajua kuwa mzee mmoja mwenye benzi ndiye aliyemringa msichana huyo siku moja jioni alipompeleka mafichoni. Alimpachika mimba kwa kumshawishi kwa zawadi na pesa.

Katika shairi “Rangi ya Anga”(uk.1) sehemu ya kumi na mbili kwenye diwani ya *Rangi ya Anga*, mwandishi anatumia swali la balagha anapozungumzia namna mimba ya yaya ilivyojitokeza baada ya kuringwa na mwajiri wake. Ingawa mwajiri alifanya mapenzi kisiri na yaya bila mke wake kujua, matokeo ya kitendo chake hayakufichika. Mshairi anauliza, **“Huzuiliwaje siri ambayo kila uchao huumuka kama unga wa ngano uliokolezwa hamira ya thamani?”** (uk.19). Jibu la swali hili ni kuwa mimba haiwezi kuzuiliwa kuonekana. Kadiri siku zilivyosonga lazima ingeanza kuonekana hadharani.

Kwengineko, katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya pili mwandishi anazungumzia suala tata la urithi wa mali ya familia kwa mujibu wa mila na tamaduni. Mila na tamaduni hupendelea mvulana kurithi shamba, mimea na mifugo kuliko msichana kwa sababu ataolewa kwengine. Kwa kuangazia jinsi mila na tamaduni zinavyombagua mwanamke kuhusu urithi wa mali, mshairi anaeleza hali hiyo kwa kuuliza swali la balagha katika shairi kwenye sehemu ya pili. Mtunzi anauliza:

Kwa mujibu wa ibara za kimila
Ni nani mmliki wa hili bonde
Ambamo tete za mawele
Na za mtama na za wimbi
Zinametameta asubuhi
Kama tembe za dawa-kinga
Ngao imara ya wakaazi
Wasijeruhiwe na michomo
Ya visu vya misimu wa njaa? (uk. 3)

Bila shaka mvulana ndiye hupewa kipaumbele kurithi shamba, mimea pamoja na mifugo kulingana na mila na tamaduni za Kiafrika. Kwa mujibu wa mwandishi msichana hana haki yoyote ya kurithi mali ya familia. Hahesabiwi katika ugavi wa mali ya familia kwa vile ataolewa kwengine. Hata hivyo, hali hii imeanza kubadilika kwa sababu zipo jamii kadha ambazo sasa zinatambua urithi wa wasichana.

Kuhusu suala la thamani ya watoto wa kiume dhidi ya watoto wa kike, mwandishi anatumia swali la balagha kuangazia dharau na maonevu anayopitia mwanamke anayejifungua wasichana pekee ilhali si kosa lake. Jambo hili linapatikana katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya nne. Mshairi anasema:

Upepo wa masuto ya daima
Na fedheha na vitisho vizito
Ukimviringisha kwenye vumbi
Kwa “kosa lisilostahimilika”
La kuleta duniani watoto wa kike
Badala ya “watoto wastahiki”? (uk.6)

Katika shairi “Rangi ya Anga”(uk.1) sehemu ya tano mshairi anazungumzia visa vya dhuluma za kinyumbani dhidi ya wanawake. Anaeleza kuwa wanaume huwachukulia wanawake kama watoto. Kwa hivyo, hawana budi kuwarudi wanapokosea kwa sababu walilipa mahari walipowaoa. Wanaume wanapowapiga wake zao kwa makofi na ngumi, huwaachia majeraha kwenye mikono na shingo, damu hudondoka kutoka puani au kinywani, meno hulegea kwenye taya au macho kuwa na rangi ya damu iliyoivia ndani. Ndiposa mshairi anauliza swali la balagha, **“Au meno yaliyokuwa imara, yaliyolegezwa mizizi na kutoroka taya, au macho yaliyoigiza nyota yakavamiwa na genge la makofi yakawa fumbo la dhiki ya ndoa?”** (uk. 8).

Kwengineko, katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya sita anazungumzia maudhui ya ndoa za mapema miongoni mwa wasichana wa shule kwa wazee wenye mali. Wazazi kutoka jamii maskini wanawalazimisha wasichana wao kuolewa ili kupata mali ya kujinasua kutoka lindi la umaskini. Kwa hivyo, wazazi wanawaona wasichana wao kama vitega uchumi. Mshairi anauliza swali la balagha:

Mbona usiolewe na Mzee Malimali
Kusudi mahari ya ng’ombe na mbuzi
Ituzimie moto wa umaskini
Kama wingu kuu la masika
Likizima ukame nyikani? (uk. 8)

Mshairi anaangazia maudhui ya ubabedume katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya sita. Kulingana na utamaduni, mvulana au mwanamume hapaswi kushindwa na mambo madogo kama mwanamke. Fikiria kama hizi zinaonyesha kuwa wanaume tangu zamani huona kuwa wanawake ni dhaifu katika mambo fulani na hivyo hawapaswi kulinganishwa. Mwandishi anauliza swali la balagha, **“U mwanamume gani ushindwaye na madogo kama mwanamke?”** (uk.9). Ajabu ni kwamba kauli hii inatolewa na mama kwa mwanawe mvulana. Kwa hivyo, inaonekana kuwa hata wanawake wenyewe wamekubali kudharauliwa kuwa wao hawawezi hata mambo madogo.

6.3.7 Chuku

Katika shairi “Flora na Wenzake” (uk. 33) katika diwani ya *Bara Jingine*, mshairi anaeleza vile mwalimu alimwagiza Flora kuingia ofisini mwake asubuhi moja shuleni mwao akiwa na nia ya kumdhulumu kimapenzi. Mwandishi anaeleza, “**Amri nyekundu**: ‘ingia ofisini’ inatupa dhoruba na kumsukuma ofisini” (uk. 34). Maneno “amri nyekundu” ni chuku inayomaanisha amri kali aliyotoa mwalimu mkuu kwa Flora. Katika hali halisi hakuna amri nyekundu lakini haya ni maelezo tu ya mshairi kuonyesha amri nzito “ingia ofisini” iliyotolewa kwa Flora badala ya kutumia lugha ya upole kumwambia aingie ofisini.

Kwengineko, katika shairi “Rangi ya Anga”(uk.1) sehemu ya sita, kuna chuku inayojitokeza. Mwandishi anazungumzia uozaji wa wasichana wachanga kwa sababu ya umaskini. Anaeleza vile Profesa mmoja anajigamba kwa wenzake kuwa msichana aliyemposa na kumuoia hakuzidi miaka kumi na mitatu. Anasema kuwa, “**Kwa masikio matatu**, mawili kichwani na tatu akilini...” (uk. 8). Kwa kawaida, mtu hana masikio matatu. Lakini kupitia chuku hii tunaelewa namna mshairi anatafakari kwa makini katika akili yake vile wasichana wachanga wanaharibiwa maisha yao kupitia tamaduni zilizopitwa na wakati.

Katika shairi ‘Kisa Chuoni’ (uk. 45) katika diwani ya *Redio na Mwezi*, mwandishi anaeleza kisa cha mwanamke mmoja aliyeenda chuoni kutoa huduma za mapenzi kwa wanafunzi wa kiume ili apate kulipwa pesa za kununulia watoto wake chakula. Baada ya kumaliza kutoa huduma alipodai kulipwa pesa na wanafunzi hao, walimfukuza kutoka chuoni humo bila kumpa pesa zozote. Anasema kuwa, “Anaondoka na machovu na **mito ya machozi** bila ndururu mfukoni!” (uk. 46). Maneno “mito ya machozi” ni chuku anayotumia mshairi kuonyesha vile mwanamke huyo alitokwa na machozi mengi ya uchungu alipokosa kupewa pesa zake.

6.3.8 Mbinu Nyingine za Kisanaa

Mbinu nyingine za kisanaa ambazo tumechanganua hapa ni pamoja na takriri, nidaa, majazi, tanakali za sauti, matumizi ya sauti, usimulizi, uchimuzi, sajili ya gazeti na mgao wa kitamthilia.

6.3.8.1 Takriri

Takriri ni muhimu kwa vile hufanya shairi kuwa na mdundo na ridhimu fulani inayosaidia shairi kukaririka au kuimbika. Tumeangalia aina mbili za takriri ambazo mshairi ametumia: takriri neno na takriri konsonanti.

6.3.8.1.1 Takriri-neno

Mwandishi ametumia takriri neno “nakumbuka ulivyokuwa” kwenye shairi “Nakumbuka Ulivyokuwa” (uk.76) katika diwani ya *Bara Jingine*. Anazungumzia namna msichana mmoja alivyoshambuliwa na mwanamke aliyegundua kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na mume wake. Kupitia mbinu ya urudiaji, mshairi anaonyesha kiwango cha majeraha aliyoyapata msichana huyo mwilini mwake mpaka ikabidi alazwe hospitalini. Mshairi anaeleza:

Nakumbuka ulivyokuwa

Mwili dhaifu
Hamu hafifu...

Nakumbuka ulivyokuwa

Kabla ya ugunduzi
Kukukaba koo
Na kukuziba akili...

Nakumbuka ulivyohadithia

Huku matone ya machozi
Yakidondoka ndo! ndo! ndo!

Nakumbuka ulivyokuwa

Katika chumba cha hospitali
Ukirejelea taratibu
Kwenye ukumbi wa maisha... (kur. 76-78)

Mwandishi anarudia maneno “nakumbuka uliyokuwa” mara tatu ili kuisitiza maana mbali na kuonyesha kiwango cha mashambulizi dhidi ya msichana huyo. Aidha, anaonyesha taswira ya msichana akiwa amelazwa hospitalini akiuguza majeraha na hatari iliyoko wasichana wanapojihusisha na mapenzi haramu na wanaume waliooa.

Katika shairi “Kisa Chuoni”(uk.45) katika diwani ya *Redio na Mwezi*, kuna takriri ya maneno “mamlaka”, “haki” na “kahaba”. Msisitizo huu unaonyesha msimamo wa wanafunzi wa chuo kuhusu haki ingawa hawamtendei haki mwanamke aliyewapatia huduma ya ngono chuoni. Katika shairi hili, mwandishi anaeleza namna mwanamke mmoja anafukuzwa kutoka chuoni bila kupewa pesa na wanafunzi wa kiume baada ya

kuwapatia huduma za mapenzi ili wamlipe pesa za kuwanunulia watoto wake chakula. Wanafunzi hao hawamfanyii haki licha ya kupendekeza haki kwa wanyonge katika jamii. Mshairi anasema:

Vinywa vilitangaza:

Mamlaka!
Mamlaka!
Mamlaka...
Mamlaka...
Mamlaka...
Mamlaka na haki!
Mamlaka...

Walipendekeza **haki**

Haki...
Haki...
Haki...
Haki...
Bali mchuuzi
Muuzaji huduma
Alipodai **haki**
Haki ya kulipwa
Kulipwa kandarasi...
Sauti zilipanda angani:
Kahaba!
Kahaba!
Ndugu **kahaba...** (kur. 45-46)

Katika shairi “Rangi ya Anga”(uk.1) sehemu ya kumi na saba mshairi anarudia maneno “hao ndio”. Anaeleza namna walimu, watu wenye ukuruba wa kidamu na majirani wanavyowapachika mimba wasichana wanaosoma shuleni. Anasema:

Hao ndio hasidi wakuu maishani mwao
Hao ndio wawapigao kwa gruneti
Ndio wawatungao jinamizi tumboni (uk. 26)

Mwandishi anarudia maneno “badala ya” katika shairi hili pia anapoeleza vile ni kinyume cha matarajio wazazi wa msichana aliyeringwa wanapokea fidia ya pesa na kondoo kwa maonevu ya mtoto badala ya kuwashtaki washukiwa mahakamani ili haki itekelezwe kwa msichana na mshukiwa. Huu ni msisitizo wa kuonyesha kuwa wazazi wanatarajiwa wafanye au wahisi tofauti na vile wanavyofanya. Mwandishi anaeleza:

Badala ya wazazi kupiga unyende upasua masikio
Badala ya hamaki yao kufurika kama magma
Wanashuka kwenye mvo mchafu wa utimbakwira

Badala ya wazazi kukangata fasiki ajute
Badala ya kung'ang'ania kwamba sheria
Inue mkono wenye mjeledi mkali... (uk. 26)

6.3.8.1.2 Takriri-konsonanti

Katika ushairi, takriri konsonanti ni urudiaji wa sauti ya konsonanti (Wamitila, 2003a). Takriri-konsonanti inatokea mwanzoni mwa maneno ingawa inaweza kupatikana katikati au mwishoni mwa neno. Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya tatu, mshairi anatumia takriri – konsonanti anapozungumzia namna wasichana wasiokeketwa wanatengwa na wanajamii, wanaitwa waasi wa utamaduni na wanatungiwa nyimbo za kuwasuta. Akieleza vile wasichana wasiokeketwa wanasumbuliwa na kudharauliwa anasema:

Wametungiwa nyimbo sumbufu kama mpupu
Wakilalamika kwamba kijana wa kike
Kukataa kukekeketwa kunakokeketwa
Ni kinyume na utamaduni wa kabila (uk. 6)

Katika mfano huu, kuna urudiaji wa konsonanti “k” katika maneno “kukataa kukeketwa kunakokeketwa”. Urudiaji huu unaibua mchezo wa maneno mbali na kuisitiza hali ya kutopashwa tohara kwa wasichana kuwa ni kinyume cha utamaduni katika jamii husika.

Aidha kuna takriri-konsonanti katika shairi “Pamela” (uk. 29) katika diwani ya *Bara Jingine*. Mshairi anaeleza masaibu ya ubakaji yanayomkumba msichana wa shule kwa jina Pamela alipokuwa anatoka shuleni jioni moja. Alikutana na wavulana waliokuwa walevi ambao walitawanya vitabu vyake na kumrarulia mavazi yake kisha wakambaka. Pamela aliogopa kusema kilichomtendelea ili asiulizwe maswali mengi ya fedheha au kuonekana mchafu. Mshairi anasema, “Wasiwasi washiwashi ya kuulizwa maswali fedhehi...” (uk. 30). Kuna takriri-konsonanti “s” na “sh” katika maneno “wasiwasi washiwashi” ambazo zinaibua hali fulani ya kitanza ulimi.

6.3.8.2 Nidaa

Katika shairi “Pamela” (uk.29) katika diwani ya *Bara Jingine* mtunzi anaeleza kwa huzuni na uchungu vile wavulana walevi walimbaka msichana kwa jina Pamela alipokuwa anatoka shuleni jioni. Anasema:

Kwa fahari
Washindi

Walifunua mabawa
Wakaruka
Wakipongezana
Kwamba alikuwa bikira
Sikuwa na shaka! (uk.30)

Kitendo hicho cha ubakaji kilimwathiri Pamela. Aliacha shule kwa sababu ya mzongo wa akili, akawa kichaa. Hali hii ilitokana na kubakwa kwa sababu alikuwa amejitunza. Alianza kuzurura sokoni huku akiokota takataka na kutokwa na maneno makali yasiyostahili kusikika. Isitoshe, alianza kutembea uchi na kutatiza wapita njia. Mshairi kwa huzuni na huruma anasema; “**Na mara kwa mara uchi wako ukitatiza macho ya watu kama umeme!** (uk. 31).

Katika shairi “Flora na Wenzake” (uk.33) katika diwani hii, tunakutana na mwalimu mkuu anayewadhulumu kimapenzi wasichana wa darasa la nane. Kutokana na tabia yake mbovu, mwandishi anaonyesha kukerwa moyoni kwa tabia hiyo anaposema:

Wazazi na wanafunzi
Humwita ‘Mwalimu-Mkuu’
Lakini jina lake halisi
Ni Uoza! (uk.33)

Kwengineko, katika shairi “Kisa Chuoni” (uk. 45) katika diwani ya *Redio na Mwezi*, mwanamke mmoja anaenda chuo kikuu kufanya ngono na wanafunzi wa kiume ili apate pesa za matumizi nyumbani. Baada ya kumaliza shughuli na wanafunzi hao, anatarajia wamlipe pesa. Kinyume na mkataba wao, wanamfukuza bila kumpa pesa. Mshairi anaona kuwa hayo ni maonevu kwa mwanamke huyo. Kwa hisia za huruma na uchungu kwa kuwa mhusika hakutendewa haki mwandishi anasema:

Akaondoka na machovu
Na mito ya machozi
Bila ndururu
Mfukoni! (uk. 46)

Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya tatu katika diwani ya *Rangi ya Anga* mwandishi anaeleza suala la changamoto za wasichana wanaokataa kukeketwa kulingana na mila na tamaduni. Anasema, “Kukataa kukeketwa kunakokeketwa ni kinyume na utamaduni wa kabila, **ni kitendo kinachonuka vumba ya aibu!** (uk.6) Analaani mila na tamaduni zinazolazimisha wasichana kupashwa tohara.

Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya tano, mwandishi anaonyesha hisia kali za moyoni anapoeleza namna wanawake wanadhulumiwa na waume zao. Wanapigwa kwa sababu wanachukuliwa kama watoto na vilevile walilipiwa mahari. Anasema, “Mume amemwadhibu mkewe, **wanawake ni kama watoto, usipowarudi hupoteza njia!** Mume ana haki thabiti, anaruhusiwa kumwadhibu mkewe, **si alilipa mahari!** (uk.7). Kwa kutumia nidaa hii, mwandishi anaonyesha hisia za mwanamke kuwa si chochote na mahari ni kibali cha kumfanyia lolote.

Aidha, katika shairi hili “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya sita mshairi anazungumzia tabia ya wazazi kuwaoza mabinti zao wachanga wanaosoma kwa wazee matajiri. Mwandishi anashangaa ni vipi profesa mmoja mwenye pesa, kipara na ndevu nyeupe anajigamba kwa wenzake kuwa msichana aliyemposa na kumuoa hakuzidi miaka kumi na mitatu. Anashindwa kuelewa ni kwa nini yeye kama msomi anaoa msichana mchanga na basi akawa na mke ambaye hakusoma kama yeye. Anatumia nidaa kuonyesha vile ni msichana mdogo sana. Anasema:

Nilipoposa, nikachumbia
Niliyemchumbia, nikamuoa
Hakuzidi kumi na tatu
Kwenye mizani ya miaka! (uk.9)

Kuna mila na tamaduni zinazomdhalilisha msichana kwa kumwambia mvulana asishindwe na mambo madogo kama msichana. Vilevile, tamaduni hizo zinamkataza mvulana kucheka na kulia kama mwanamke. Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya sita mwandishi anamshangaa profesa wa kike anayetetea kuwepo kwa mila na tamaduni kama hizi. Anashangaa kuwa hata mtu aliyesoma sana bado anashikilia mila dhalilishi. Mwandishi anashangaa:

Hiyo
Si taasubi
Ni desturi na mila!
Hizo
Si nyanyaso
Ni kanuni za jadi!
Hizo
Si dhuluma
Ni kawaida za utamaduni! (uk.10)

Katika sehemu ya saba pia, mama anamkemea na kumkejeli mtoto wake wa kiume asiwe na tabia ya kucheka na kulia kama mwanamke. Mwandishi anashangaa kuwa

mama amekubali kuwa mwanamke ndiye ana tabia ya kucheka na kulia wala si mwanamume:

Usicheke kiholela
Kama wewe ni mwanamke!
Nyamaza! Futa machozi!
Ushindwaye na madogo
Kama mavazi yako
Ni kamisi na rinda! (uk.10)

6.3.8.3 Majazi

Katika kufumbata sifa za mhusika au mahali, mshairi anatumia majazi kuwasilisha ujumbe fulani. Majazi ni mbinu ya kuwapa wahusika majina ambayo yanaakisi tabia zao (Wamitila, 2003b). Hata hivyo, katika ushairi wa Kithaka, mbali na kumpatia mhusika jina la kimajazi, vilevile anatoa jina la kimajazi kwa mahali ili kuweka bayana shughuli zinazofanyika mahali hapo. Matumizi ya majazi katika kazi ya kifasihi yanamsaidia msomaji kuelewa hulka ya mhusika kwa urahisi. Aidha, mwandishi anatumia majazi kubaini mtazamo wake kuhusu mhusika au mahali fulani.

Katika shairi “Flora na Wenzake” (uk.33) katika diwani ya *Bara Jingine*, mshairi ametumia majina ya “**Uoza**” na “**Fikeni-Alfajiri**” kimajazi. Mwandishi anambandika mwalimu mkuu jina “Uoza” ili kuonyesha tabia yake ya ukosefu wa maadili kwani anawaamrisha wanafunzi wa darasa la nane kufika shuleni alfajiri kusoma lakini anatumia fursa hiyo kuwadhulumu kimapenzi wasichana ndani ya ofisi yake. Tabia ya kuwadhulumu kimapenzi inaishia kumpachika mimba mwanafunzi anayeitwa Flora. Badala ya mwalimu mkuu kuwa mfano mwema shuleni, kuwashauri wanafunzi na kuzingatia kanuni za taaluma ya ufundishaji, yeye ndiye mkosa maadili. Kwa hivyo, kutokana na jina hilo “uoza” tunajua kuwa mwalimu mkuu ni mtu mwovu na hastahili kuitwa mwalimu mkuu. Mwandishi anasema, “Wazazi na wanafunzi humuita **‘mwalimu – mkuu’ lakini jina lake halisi ni Uoza!**” (uk. 33).

Aidha, mwandishi anaita shule anakosomea Flora na wenzake kama “Fikeni-Alfajiri.” Anaita hivyo kwa sababu mwalimu mkuu alikuwa anawaambia wanafunzi kupitia idhini ya wazazi kwamba wafike shuleni alfajiri kufanya kazi muhimu. Wazazi pamoja na mke wake waliamini kuwa alikuwa na bidii ya kufundisha ili watie fora masomoni. Lakini alikiuka maadili ya ufundishaji na kufanya mapenzi na hao wasichana wachanga wa shule. Mwandishi anatumia majazi anaposema, “Mwalimu-

Mkuu wa shule ya Fikeni-Alfajiri amewafunza utu-uzima nusu ya wasichana katika darasa la nane...” (uk. 35).

Mbinu ya majazi pia inajitokeza katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1)sehemu ya sita. Mshairi anaangazia suala la ndoa ya msichana mchanga kwa mzee mwenye mali kwa sababu ya umaskini ulioko katika familia yake. Mwandishi anasema:

Wewe sasa ni mtu nzima
Mshale wa mizani ya miaka
Unaonyesha miaka kumi na minne
Mbona usiolewe na **Mzee Malimali**
Kusudi mahari ya ng’ombe na mbuzi
Ituzimie moto wa umaskini... (uk. 8)

Katika shairi hili, mzazi anamuuliza bintiye wa miaka kumi na minne aolewe na Mzee Malimali ili wapate mahari ya kuwaondolea umaskini. Kisheria, msichana mwenye umri wa miaka kumi na minane ndiye anayechukuliwa kuwa mtu mzima aliyekomaa kiasi cha kuolewa. Jina “Mzee Malimali” ni la kimajazi kwa vile linatusaidia kuelewa kuwa mhusika ni mtu mzee mwenye mali lakini aliyeradhi kutumia utajiri wake kumuoa msichana mchanga kutoka familia maskini.

6.3.8.4 Tanakali za Sauti

Tanakali ya sauti ni mbinu ya uigaji wa sauti fulani ya kitu kilivyoanguka, mtu anavyosema, mnyama au kitendo fulani (Wamitila 2003b). Maneno hutumiwa kuonyesha namna sauti fulani inavyosikika. Mwandishi au msemaji anaweza kutumia tanakali ya sauti kwa nia ya kueleza hali au kitendo fulani kikamilifu. Tanakali ya sauti inatoa taswira fulani ya kitendo mbali na kuongeza mnato katika maelezo ya msanii. Kwa mfano, katika shairi “Giza Mbele” (uk. 20) katika diwani ya *Bara Jingine*, mwandishi anaeleza namna gari la mzee limetulia karibu na lango la shule akimsubiri msichana mmoja wa darasa la nane ili amchukue mafichoni kujifurahisha naye. Mshairi anasema, “Karibu na lango, **benzi jekundu limetulia tuli** likisubiri kama chatu” (uk. 26). Maneno “limetulia tuli” ni tanakali ya sauti inayoeleza jinsi gari aina ya benzi limeegeshwa karibu na lango la shule. Tanakali hii inatoa msisitizo na taswira kamili ya vile gari hilo linaonekana.

Kwingine katika shairi “Nakumbuka Ulivyokuwa” (uk. 76), msanii ametumia tanakali ya sauti anapoeleza majeraha ya msichana mmoja aliyeshambuliwa na mwanamke kwa sababu ya kuwa na uhusiano na mume wake. Msichana huyo alilazwa hospitali

kwa siku kadha ili kutibiwa. Msichana alieleza yaliyomsibu siku hiyo huku matone ya machozi yakimdongoka mashavuni. Mshairi anatumia tanakali ya sauti kuonyesha jinsi machozi yalivyomtiririka; “Nakumbuka ulivyohadithia huku **matone ya machozi yakidondoka ndo! ndo! ndo!** (uk. 77). Kwa kweli tanakali hii inatoa taswira jinsi matone ya machozi yalivyomtiririka moja baada ya jingine kama vile maji hudondoka kutoka kwenye mfereji. Matone haya yanadhihirisha uchungu na majuto aliyokuwa nayo baada ya kuumizwa mwili wake.

Aidha, katika shairi “Rangi ya Anga”(uk.1) sehemu ya kumi na mbili, kuna tanakali ya sauti. Msichana mmoja aliyetoka kijijini kwenda kufanya kazi ya uyaya aliringwa kisiri na mume wa mwajiri wake. Mwandishi anasema kuwa mimba ilianza kukua polepole mpaka nguo zake zikakataa kumtoshea na hivyo mama wa nyumba alibaini kuwa yu mjamzito. Mshairi anaeleza kuwa, “Baada ya **rinda la mhudumu mchanga kukataa katakata** kuwa mshiriki siri, uhai wa miezi mitano ya mchachato ulijitangaza...” (uk. 19). Maneno “kukataa katakata” yanasisitiza jinsi nguo hazikumtoshea tena kwa sababu ya mimba iliyoendelea kukua.

6.3.8.5 Matumizi ya Sauti

Sauti ni kipengele cha kimuundo kinachotumika sana katika uigizaji wa tamthilia. Sauti inaweza kuwa ya mhusika fulani, mnyama, kitu kinachopigwa, kelele au kuanguka kwa kitu. Sauti ya mhusika inaweza kuibua woga, kicheko, huzuni, maumivu na kadhalika. Katika ushairi wa Kithaka wa Mberia, mshairi anatumia sauti kama mbinu ya kimtindo kutoa ujumbe au hisia zake za moyoni kwa msomaji. Kupitia sauti, msomaji anaelewa yaliyo moyoni mwake au kwenye fikira zake kuhusu jambo analolizungumzia. Mbinu ya sauti ni ubunifu wa kimtindo anaoutumia kuwasilisha ujumbe katika ushairi wake.

Katika shairi “Kisa Chuoni” (uk. 45) katika diwani ya *Redio na Mwezi* mwandishi anaeleza vile wanafunzi wa kiume walipiga kelele wakimfukuza mwanamke kutoka chuoni wakimwita kahaba:

Sauti zilipanda angani:
Kahaba!
Kahaba!
Ndugu, Kahaba!
Ndugu, chukueni hatua! (uk. 46)

Kupitia sauti za wanafunzi hawa, mwandishi anachukizwa na kitendo cha wanafunzi hawa wanaotetea haki ya mnyonge kulipwa jasho lake na kusikilizwa. Inakuwaje wamwite kahaba na kumfukuza bila kumpa pesa zozote kwa huduma aliyowapa? Sauti za wanafunzi zinaonyesha fujo walizofanya ili kumfukuzilia mbali na ile dhuluma na ukosefu wa haki kwa mwanamke huyo.

Kwengineko, katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya tano, mshairi anaangazia suala la dhuluma za kinyumbani dhidi ya mwanamke. Mara nyingi mzozo wa kinyumbani unapotokea baina ya mume na mke kwa sababu mbalimbali, mwanamke huathirika sana. Mwanamke anapigwa makofi, ngumi, viboko na kukatwa kwa panga au kisu. Katika adhabu kama hii ya kikatili, mwanamke anaweza kufa. Mshairi anasema:

Sauti “ilifafanua”
Mume ana haki thabiti
Anaruhusiwa kumwadhibu mkewe
Si alilipa mahari! (uk. 7)

Katika dondoo hili, mwandishi anatumia sauti ili kuzungumzia mawazo yake ya ndani kuhusu taasubi za kiume na utamaduni unaomchukulia mwanamke kama bidhaa iliyonunuliwa kwa mahari. Kwa hivyo, mume ana haki ya kumpiga mke akoseapo au bila sababu maalumu kwa sababu “alimnunua”. Kupitia sauti hii, mwandishi analaani kitendo cha kumdhulumu mwanamke kwa misingi ya kulipiwa mahari katika jamii ya leo.

Aidha, katika shairi lili hili “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya sita, mwandishi anazungumzia tabia ya kuoza wasichana wachanga kwa wazee wenye mali. Wasichana hawa ni wachanga mno wanaopaswa kupewa elimu, kuonyeshwa mapenzi na kulindwa na wazazi wao hadi wakomae vizuri. Si ajabu wazazi kuwaoza mabinti zao kwa wazee matajiri ili wapate mahari ya kujiondolea umaskini. Ndiposa mshairi anatumia sauti kutoa hisia zake za chuki na kero kwa kitendo kama hicho anaposema:

Sikiza hiyo **sauti**
Ulimi ukitoa kauli
Kama upanga mkali
Ukikata mmea mchanga:
Wewe sasa ni mtu mzima
Mshale wa mizani ya miaka
Unaonyesha miaka kumi na minne,
Mbona usiolewe na Mzee Malimali

Kusudi mahari ya ng'ombe na mbuzi
Ituzimie moto wa umaskini... (uk. 8)

Kuna matumizi ya sauti vilevile katika “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya saba ambapo mzazi anamuonya mtoto wake wa kiume kutocheka kiholela au kushindwa na mambo madogo kama mwanamke:

Sikiza **sauti** ya mzazi
Ambayo inakuja juu
Kama wimbi la sumu
Ikimimina kemikali kali
Katika akili asubuhi:
Usicheke kiholela
Kama wewe ni mwanamke!
Nyamaza! Futa machozi!
Ushindwaye na madogo
Kama mavazi yako
Ni kamisi na rinda! (uk. 10)

Sauti ya mzazi kwa mwanawe inaonyesha vile mwanamke anadharauliwa katika jamii. Mambo mabaya na kutoweza huhusishwa na mwanamke. Kwa maoni ya mtunzi anashangaa ni vigezo gani hutumiwa kupimia uwezo wa mwanamke dhidi ya mwanamume. Mbona mwanamke adhalilishwe siku zote? Huu ni ubaguzi wa kijinsia usio na mashiko yoyote. Mwanamke akiwa shupavu tena na jasiri katika kufanya mambo fulani au kupinga mambo mabaya atachukuliwa kuwa mwenye kiburi. Anastahili kunyenyekea siku zote mbele ya mwanamume.

6.3.8.6 Usimulizi

Usimulizi unahusishwa kwa kiasi kikubwa na tanzu za riwaya, tamthilia na hadithi fupi (Wamitila 2008). Hata hivyo, haina maana kuwa hakuna usimulizi katika ushairi. Ingawa tenzi ndizo zinahusishwa na usimulizi, inawezekana mashairi mafupi yakawa na sifa ya usimulizi kama tunavyoona katika mashairi kadha ya Kithaka wa Mberia. Kuna aina nyingi za usimulizi kama vile usimulizi wa nafsi ya kwanza, nafsi ya pili, nafsi ya tatu na usimulizi maizi. Hata hivyo, tutazungumzia usimulizi wa nafsi ya pili na nafsi ya tatu uliojitokeza katika mashairi ya Kithaka wa Mberia katika sehemu hii.

6.3.8.6.1 Usimulizi wa Nafsi ya Pili

Katika usimulizi wa nafsi ya pili, mshairi anatumia mofu “u” au “wewe” kurejelea mhusika mkuu kuhusu yaliyomtendelea. Usimulizi wa nafsi ya pili una athari kwa hadhira kwa sababu unanuia kumleta karibu msomaji au hadhira kwa kuihusisha na

matukio yanayosimuliwa. Kwa mfano, katika shairi “Pamela” (uk. 29) katika diwani ya *Bara Jingine*, mshairi anatumia mofu “u” kumrejelea Pamela ambaye alinajisiwa na kundi la wavulana walevi alipokuwa akitoka shuleni jioni moja. Mshairi anasimulia:

Taratibu
Kama mto ambao
Unakaribia bahari
Pamela ulifuata mapindo ya njia...

Ulipokanyaga mtego
Walikuhashambulia...

Nawe, Pamela
Ulibakia gizani... (kur. 29-30)

Kwengineko, katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya nne, mwandishi anatumia usimulizi wa nafsi ya pili kueleza mateso anayopitia mwanamke anayezaa watoto wa kike tu. Anatumia mofu “wewe” na “u” kwa kurudiarudia kumrejelea mwanamke huyo. Anasimulia:

Wewe mwenye sauti nyororo
Na maungo mvingo na laini,
Wewe usonywaye maishani
Na wenye taasubi ya jinsia,
Wewe ubezwaye unaposema
Na kutwezwa unapotenda,
Wewe udharauliwaye sokoni
Na kudhalilishwa nyumbani,
Wewe ukemewaye mezani... (uk. 6)

6.3.8.6.2 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu

Mtunzi anatumia vilevile mofu “a” na “wa” kudhihirisha usimulizi wa nafsi ya tatu. Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya kumi, mshairi anaeleza vile mvulana na msichana walianza urafiki wa kimapenzi walipokuwa shuleni. Kwa bahati mbaya msichana alipata mimba na akafukuzwa shuleni ilhali mvulana aliyemringa aliendelea na masomo yake mpaka akahitimu, akapata kazi nzuri na kuishi maisha ya kifahari. Lakini msichana aliyefukuzwa shuleni aliishia kuwa maskini na kahaba mjini ili amkimu mtoto wake. Mwandishi anasimulia hivi:

Walikuwa wachanga
Katika kivuli cha shule
Hisia za ujana zilipovutana...

Mmoja wa wawili washiriki
Aliendelea na mwendo shuleni
Akakusanya vyeti vya maana
Na kupata jina adimu nchini,
Leo, asubuhi, anakula mayai
Na asali na siagi ya thamani,
Anavalia mavazi ya kuteua... (uk.13)

Aidha, katika sehemu ya kumi na mbili ya shairi “Rangi ya Anga”, mshairi anatumia nafsi ya tatu kueleza vile msichana mmoja alichukuliwa na wakala kutoka kijijini kwenda mjini kufanya kazi ya uyaya. Akiwa huko, mwajiri wake wa kiume alifanya mapenzi naye kisha akawa mjazito. Baada ya mke kugundua siri ya ujauzito wake, alimfurusha kutoka nyumbani mwake. Baadaye alijifungua mtoto wakaanza safari ngumu ya maisha ya umaskini. Mwandishi anasimulia:

Kwa ahadi tamu kama halua
Wakala alimrairai mama-mzazi
Akamnyakua binti kutoka shamba
Akambwaga kwenye vimetemete jijini
Kutunza watoto wa watu mtaani
Kupigana mieleka na kazi za jikoni
Na kuipa nyumba sifa kwa unadhifu. (uk.17)

6.3.8.7 Uchimuzi

Uchimuzi ni mbinu ya kutumia maneno kuchora picha ya kile mshairi anaeleza ili kieleweke kwa urahisi kwa msomaji. Uchimuzi kupitia picha ya kuonekana machoni pa msomaji ni mbinu mojawapo bunifu ya Kithaka wa Mberia. Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk.1) sehemu ya kumi, tunaelezwa kuhusu urafiki baina ya mvulana na msichana wanaosoma shuleni pamoja. Urafiki huu unaishia kwenye mapenzi haramu. Msichana anapachikwa mimba ambayo inakuwa chanzo cha yeye kufukuzwa shuleni na halmashauri ya shule. Lakini mvulana anaendelea na masomo yake mpaka anahitimu. Mshairi anasema kuwa msichana alipotimuliwa, alitimuka, akateguka na kuanguka. Anaeleza kwa picha:

Bahati alipotimuliwa, alitimuka
Alipotimuka, aliteguka
Alipotegeuka
a
k
a
a
n
g

u
k
a
! (uk.14)

Neno ‘akaanguka’ limeandikwa kwenda chini kuashiria kwa kina na taswira ya macho shimo alimotumbukia msichana huyo. Kuanguka huku kuna maana ya kufukuzwa shuleni akaacha masomo. Matokeo ya kufukuzwa kwake ni kukosa kusoma, kutopata kazi nzuri, njaa inayomkaba yeye na mtoto wake, kuishi katika umaskini, kulea mtoto peke yake na kufanya kazi ya ukahaba mjini ili kukimu mahitaji ya mtoto wake. Huko ndiko kuanguka kimaisha anakoashiria mshairi.

6.3.8.8 Sajili ya Gazeti

Habwe n.w (2010) wanaeleza sajili kuwa ni mtindo wa lugha ambao hutumika katika muktadha mahsusi. Wanaendelea kufafanua kuwa sajili ni aina maalumu ya lugha ambayo hujipambanua kwa matumizi ya istilahi au msamiati mahsusi ambao huhusishwa na taaluma au kazi ya kundi linalozungumza aina hiyo ya lugha. Kuna sajili mbalimbali kama vile sheria, dini, kilimo, magazeti, hospitali, kandanda na kadhalika.

Katika shairi “Flora na Wenzake” (uk. 33) katika diwani ya *Bara Jingine*, mwandishi anaeleza vile habari za mwalimu mkuu aliyefanya mapenzi na nusu ya wasichana wa darasa la nane zimeandikwa kwenye gazeti. Mwandishi anaeleza:

Leo habari katika gazeti
Zimekuwa kisu kikali
Kinachokata akili zetu
Mwalimu-mkuu
Wa shule ya Fikeni-Alfajiri
Amewafunza utu-uzima
Nusu ya wasichana
Katika Darasa la nane... (uk. 35)

Habari hizi kwenye gazeti zinasaidia wazazi na walezi kuelewa tabia mbovu ya mwalimu mkuu wa shule ya Fikeni-Alfajiri. Mwalimu mkuu hana maadili ya taaluma ya ualimu na hajiheshimu kwani amefanya mapenzi na wasichana wa darasa la nane. Kwa hivyo, hafai kuitwa mwalimu mkuu kwa vile si kielelezo chema shuleni humo.

6.3.8.9 Mgao wa Kitamthilia

Tamthilia huwasilishwa kwa mtindo wa kugawanya vitushi katika maonyesho. Kunakuwa na onyesho la kwanza, la pili, la tatu na kadhalika kulingana na uzito wa mtiririko wa matukio. Kithaka wa Mberia ambaye pia ni mwanatamthilia vilevile anaamua kutumia mtindo huo wa kitamthilia katika baadhi ya mashairi yake. Baadhi ya tamthilia alizotunga ni *Natala* (1997), *Kifo Kisimani* (2002) na *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (2004). Huo ndio ubunifu na usasa wa kimtindo unaonekana katika ushairi wake. Kwa mfano, anaeleza vile msichana wa shule kwa jina Pamela alivyobakwa na vijana walevi akitoka shuleni katika shairi “Pamela” (uk. 29) katika diwani ya *Bara Jingine*. Katika sehemu ya I ya shairi hilo, anaeleza vile aliviziwa na kubakwa. Katika sehemu ya II anaeleza vile Pamela alishikwa na woga akaweka siri kitendo hicho. Katika sehemu ya III, anaeleza vile Pamela aliathirika akili mpaka akaanza kutembea uchi sokoni huku akiokota takataka na katika sehemu ya IV anamulika maoni mbalimbali ya wanajamii wasiojua chanzo cha masaiibu ya Pamela. Kuna wale wanasema ni uchawi alifanyiwa ilhali wengine wanadai ni laana ya marehemu mjomba wake. Mgao kama huu hupatikana katika tamthilia.

Aidha, shairi “Flora na Wenzake” (uk. 33) katika diwani hii limegawanywa mithili ya maonyesho katika tamthilia. Katika sehemu ya I, anaeleza kuwa tabia mbaya ya mwalimu mkuu ilisababisha wazazi na wanafunzi kumbandika jina ‘Uoza’. Sehemu ya II inaonyesha namna mwalimu mkuu anamlazimisha Flora kuingia ofisini mwake. Sehemu ya III inaeleza vile mwalimu anamdhulumu Flora kimapenzi ofisini. Katika sehemu ya IV na V anaeleza vile mimba ya Flora inanza kukua. Sehemu ya VI inaonyesha vile kitendo cha mwalimu kimejulikana kupitia habari kwenye gazeti. Sehemu ya VII inahitimisha vile wazazi, walezi na mke wake wanaelewa sababu ya mwalimu mkuu kuambia wanafunzi wafike shule mapema kila siku.

6.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumeonyesha kuwa wasichana na wanawake wanaonewa na kudhalilishwa mno. Wananyanyaswa kimapenzi na wanaume wenye nguvu kuwashinda. Wasichana na wanawake hao hawana nguvu za kujikinga dhidi ya dhuluma hizo. Fauka ya hayo, mila na tamaduni za jamii mbalimbali zinawakandamiza wasichana na wanawake. Wasichana wanaosoma shuleni wanaozwa bila hiari yao, kukeketwa, kubakwa, kutorithishwa mali ya familia mbali

na kudharauliwa kwa mwanamke anayejifungua watoto wa kike pekee. Mambo haya yote yanafanyika na kushuhudiwa katika jamii mbalimbali tunamoishi leo hii. Hivyo, maudhui haya yanaonyesha kuwa mshairi anatunga kuhusu mambo yanayotendeka katika jamii bali si katika ombwe tupu.

Kwa maoni ya Kithaka wa Mberia ni kuwa ili kupunguza dhuluma dhidi ya wasichana na wanawake, kupewa elimu bora itawanufaisha. Kuelimisha wasichana shuleni na vyuoni kutawasaidia kufahamu haki zao ili wasinyanyaswe na wanaume mbali na kupata uwezo wa kiuchumi ili wajisimamie badala ya kuwategemea wanaume kuwakimu kimaisha. Elimu itaondoa mpaka wa kijinsia kati ya wanaume na wanawake. Wasichana wakipata elimu bora wanaweza kuwa madaktari, marubani, wahandisi; kazi ambazo zinaaminika kuwa za kiume. Hali hii itasaidia kuleta usawa wa kijinsia, kujitegemea kiuchumi na kukomesha ubaguzi wa kijinsia na msimamo hasi wa ubabedume kuwa mwanamke ni raia wa kiwango cha pili siku zote.

Kimtindo, mshairi ametumia tamathali za usemi kama vile tashbihi, sitiari, tashihisi, tasifida, kinaya, chuku na maswali ya balagha. Hata hivyo, ametumia vipengele vingine vya kimtindo visivyozoeleka katika utunzi wa mashairi kama vile sauti, mgao wa kitamthilia wa kugawanya vifungu katika sehemu zinazofanana na maonyesho katika tamthilia, usimulizi, uchimuzi na sajili ya gazeti. Vipengele hivi ndivyo vinavyochangia usasa wa kimtindo katika uwasilishaji wa maudhui. Vipengele vya sauti na ugawanyaji wa mashairi katika sehemu hutumika katika tamthilia ilhali usimulizi hutumika sana katika riwaya na hadithi fupi.

SURA YA SABA

MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

7.1 Utangulizi

Utafiti wetu umehusu uchanganuzi wa usasa katika ushairi wa Kithaka wa Mberia huku msisitizo ukiwa kwenye maudhui anayoyaangazia na mtindo wake wa uwasilishaji wa maudhui hayo. Tumechanganua maudhui yanayojitokeza sana katika mashairi yake na kuonyesha namna yanavyoana na wakati wa sasa katika jamii. Isitoshe, tumebainisha vipengele vya kimtindo, hasa vya kiubunifu na kimajaribio anavyotumia kuwasilisha maudhui na masualaibuka katika ushairi wake. Katika sura hii, tumetoa muhtasari wa matokeo ya utafiti huu, hitimisho na mapendekezo ya utafiti zaidi juu ya ushairi wa Kithaka wa Mberia.

7.2 Muhtasari wa Matokeo

Katika utafiti huu, tumechanganua maudhui katika diwani tano za ushairi wa Kithaka wa Mberia ambazo ni *Mchezo wa Karata, Bara Jingine, Redio na Mwezi, Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Uchanganuzi wetu umebainisha kuwa mashairi yenye maudhui mbalimbali yanadhihirisha ruwaza za kimaudhui. Maudhui hayo yameainishwa katika makundi mahususi yanayounda sura za tasnifu ili kurahisisha shughuli ya uchanganuzi mzuri. Katika kundi la kwanza tuna maudhui anuwai yanayozungumzia juu ya siasa, utawala na mamlaka katika mataifa ya Afrika. Katika kundi la pili, tuna maudhui mbalimbali yanayozungumzia uharibifu na uhifadhi wa mazingira. Ruwaza ya tatu ya kimaudhui ambayo imebainika katika ushairi wa Kithaka wa Mberia inahusu utamaduni mahuluti. Katika kundi hili tumegundua kuwa kuna mambo mazuri na maovu yanayotokana na mtagusano au mwingiliano kati ya wakoloni, wamishenari na wenyeji Waafrika. Fauka ya hayo, kuna tapo la maudhui kuhusu dhuluma na ukombozi wa wanawake. Kwa hivyo, uainishaji huu wa maudhui katika makundi maalumu umejibu swali letu la kwanza tulilouliza ikiwa ushairi wa Kithaka wa Mberia una ruwaza gani za kimaudhui. Kwa kujibu swali hilo, tumeafikia lengo letu la kwanza la uchanganuzi wetu ambalo lilikuwa kuchunguza ruwaza za kimaudhui zinazopatikana katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

Katika uchanganuzi wetu wa mtindo katika ushairi wa Kithaka wa Mberia, tumedhihirisha kuwa kuna vipengele kadha vya mtindo anavyotumia katika ushairi wake ili kuwasilisha maudhui. Baadhi ya vipengele vya kimtindo vilivyotawala

ushairi wake katika diwani zake zote na kuthibitisha dhana kuwa mtindo ni mtu ni kama vile tashibihi, sitiari, tashihisi, takriri, maswali ya balagha, tasifida, chuku, nidaa, ritifaa, msamiati teule, uchimuzi na usimulizi. Mbinu nyingine za kimtindo anazotumia kwa uchache kama kiungo cha kuwasilisha maudhui kwa msomaji ni kejeli, kinaya, wimbo, ndoto, mazungumzo, oksimora, uzungumzi nafsia, majazi, tanakali za sauti, sauti, sajili ya gazeti na mgao wa kitamthilia uliotumika kugawa baadhi ya mashairi.

Imebainika kuwa vipengele hivi vya mtindo ambavyo Kithaka wa Mberia anatumia kutungia ushairi wake vina umuhimu mkubwa. Tumebainisha kuwa vipengele vya mtindo anavyotumia mwandishi kuendeleza maudhui katika mashairi yake vinasaidia kujenga taswira katika akili ya msomaji, kufafanua maana, kukejeli tabia fulani, kutoa mifano mwafaka, kuibua hisia, kuzua ucheshi, kumchochea msomaji kuchukua hatua kuhusu jambo au hali fulani mbali na kuongeza ujumi wa kisanaa ili msomaji aendelee kusoma na kufurahia yaliyomo katika mashairi hayo. Matumizi ya vipengele hivi vya kimtindo yanathibitisha kauli kuwa kinachosemwa na namna ya kukisema ni masuala mawili yanayofungamana pamoja. Kwa kuchanganua sifa hizo zote za kimtindo, tumejibu swali la pili katika utafiti wetu kuwa ni mbinu gani za kimtindo anazitumia kuonyesha usasa wa kimaudhui. Kwa mantiki hiyo, lengo la pili ambalo lilikuwa ni kufafanua mbinu za kimtindo alizozitumia Kithaka wa Mberia na umuhimu wake katika ushairi limefikiwa.

Mbali na ukweli kuwa Kithaka wa Mberia anatunga mashairi huru, imebainika kuwa usasa wa maudhui na mtindo umetokana na msamiati teule anaotumia kutokana na mazingira yake. Anatumia majina ya wadudu, wanyama, miti, matunda, sayari, tabianchi na vifaa vinavyopatikana katika mazingira tofauti. Tumebaini kuwa mwandishi ana uhuru wa kuchagua maneno ya kutumia kusudi awasilishe wazo lake ili kuacha athari aliyonuia. Tumedhihirisha vilevile kuwa mashairi anatumia msamiati unaofungamana na matukio, muktadha na mazingira halisi anamotoka yeye hasa anapozungumzia uharibifu na uhifadhi wa mazingira. Isitoshe, tumedhihirisha kuwa kuna mashairi yenye maumbo ya kipekee kama vile “Boga”, “Nyumba”, “Dau Haliendi!”, “Mruko wa Nyuki”, “Mwashi Mahiri” na yale yenye sura na miundo ya kitamthilia. Kwa hivyo, swali la tatu katika utafiti huu ikiwa kuna mashairi yenye maumbo maalumu katika ushairi wa Kithaka wa Mberia limejibiwa. Aidha, lengo la

tatu kuhusu utathmini wa upekee wa maumbo ya kishairi limefikiwa. Mwandishi anaendelea kubadilisha maumbo ya mashairi yake kutoka diwani za awali hadi zile za hivi karibuni kwa sababu mtindo katika fasihi hubadilika kadiri ya mpito wa wakati.

Katika uchanganuzi wetu, tumetambua kuwa maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia yanadhihirisha namna historia imekuwa nguzo kuu katika kujenga mitazamo na mielekeo katika nyakati za sasa, hasa nchini Kenya na bara la Afrika kwa jumla. Tumeona kuwa mwandishi anadadisi hali za mataifa ya Afrika kabla, wakati na baada ya ukoloni. Anaangazia hali ya siasa, uongozi, mazingira, elimu, mila na tamaduni na mahusiano baina ya nchi baada ya uhuru. Kwa mtazamo wa mshairi, baadhi ya matatizo yanayokumba mataifa ya Afrika hivi leo kama vile ubepari, unyanyasaji wa wafanyakazi, udikteta, ubaguzi wa rangi na hadhi, ufisadi na mengineyo ni athari na matokeo ya ukoloni. Viongozi walioshika hatamu baada ya ukoloni mkongwe bado wanaiga mifumo, sera, kasumba na hila za wakoloni katika utawala wao na hivyo kuendeleza ukoloni mamboleo katika mataifa yao. Masuala haya yanajibu swali letu la nne kuwa ni kwa njia gani Kithaka wa Mberia anasawiri athari na matokeo ya ukoloni. Kutokana na uchunguzi wetu, lengo letu la nne ambalo lilikuwa ni kudadisi athari na matokeo ya ukoloni katika ushairi wa Kithaka wa Mberia limefikiwa pia.

Katika uchanganuzi wetu, tumebainisha kuwa mshairi anachochewa au kusukumwa na mambo mengi ili kutunga mashairi yenye misimamo, mielekeo na maudhui anuwai. Kwanza, tumeona kuwa mtunzi anachochewa na mfumo mbaya wa siasa, utawala na uongozi duni kutunga mashairi yanayokashifu siasa za unafiki na ukandamizaji zisizoleta maendeleo. Aidha, anachochewa na madhila ya ukoloni kuonyesha namna hali ya sasa ya nchi ya Kenya na bara la Afrika inatokana na historia. Pili, mazingira ni kichocheo kingine kinachompa mshairi nafasi ya kutunga mashairi mengi kuhusiana na uharibifu na utunzaji wa mazingira kwa vizazi vya leo na vya kesho. Vilevile, utamaduni mahuluti na athari zake katika jamii ni kichocheo kingine kinachompa ari Kithaka wa Mberia kutunga mashairi yake. Isitoshe, masaibu na nyanyaso za jinsia ya kike zinamsukuma kutetea haki zao.

Tumetambua vilevile kutokana na uchanganuzi wetu kuwa mshairi amejishughulisha sana na masuala hasi kuliko masuala chanya. Tunaamini kuwa amefanya hivyo kwa sababu amelenga kuangazia maovu yote yanayotendeka katika jamii ili kuhamasisha na kumtamamisha msomaji jinsi hali ilivyo ili aweze kuchukua hatua fulani

kurekebisha picha hizo mbovu. Mtunzi anatumia kejeli, tashtiti, kinaya na nidaa kuonyesha msimamo wake juu ya masuala yasiyompendeza kama msanii na mwanajamii. Kwa upande mwingine, pale kuna vitendo na mambo mazuri ameyasawiri kwa njia chanya ili kuwahimiza wasomaji na wanajamii kuyadumisha na kuyaimarisha.

7.3 Hitimisho

Kwa ujumla, Kithaka wa Mberia ametunga mashairi huru ambayo maudhui yaliyomo yanaendana sako kwa bako na wakati uliopo. Mshairi ni mpekuzi wa mambo yanayofanyika katika jamii ya leo. Anazungumzia masuala ambayo tunayashuhudia kila kuchao kwa macho yetu katika jamii, kwenye vyombo vya habari na kusoma katika vitabu na magazeti. Mambo kama vile unafiki wa wanasiasa, uongozi wa kidikteta, ugaidi, ufnisadi, unafiki wa kidini, umaskini, njaa, ukahaba, ugonjwa wa ukimwi, unyanyasaji wa wafanyakazi, uharibifu wa mazingira, dhuluma za kinyumbani dhidi ya wanawake, ubakaji wa wasichana na wanawake, ubaguzi wa rangi na ubaguzi wa wanawake, ukeketaji wa wasichana na mengineyo ni baadhi ya mambo tunayoyashuhudia katika ulimwengu wa leo. Kwa hivyo, ni mambo ya kisasa ambayo hayajapitwa na wakati. Hata pale ambapo anazungumzia masuala ya kihistoria, anayaunda upya na kuonyesha athari za mambo hayo hasa ukoloni mkongwe katika jamii ya leo. Masuala hayo yanatutazamisha jinsi jamii yetu pana ilivyo kwa uzuri au kwa ubaya. Msomaji anaposoma mashairi yake anajitambulisha na mambo hayo na kuona namna anaweza kuchukua hatua au kukabiliana na mambo hayo kama mwanajamii.

Mtindo wa kiubunifu wa Kithaka wa Mberia kama vile mashairi-picha yanayotoa maumbo maalumu kuchimuza maudhui fulani, mbinu ya usimulizi anayotumia na sura za migao ya kitamthilia katika ushairi wake ni mtindo wa kipekee unaoyapa usasa mashairi yake. Kwa hivyo, upo mwoano na mshikamano mkubwa kati ya usasa wa kimaudhui na usasa wa kimtindo katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.

Katika utafiti huu, tumetumia nadharia mbili kuchanganua masuala mawili tofauti lakini yenye uhusiano wa karibu. Nadharia ya baadaukoloni imetufaa katika kuchanganua usasa wa maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Kwa upande mwingine, nadharia ya elimumitindo mkabala wa uhakiki mpya imetusaidia katika kuhakiki mtindo katika ushairi wake.

Kuhusu umuhimu wa utafiti wetu, tumethibitisha kwamba usasa katika ushairi wa Kithaka wa Mberia kimaudhui ni suala ambalo linaonyesha kuwa kazi ya kifasihi huwa na maana zaidi inapogusa maisha ya kila siku ambayo wasomaji au wanajamii wanajitambulisha nayo. Kwa upande wa mtindo, kazi hii ni muhimu kwa kuwa mbali na tamathali za usemi na matumizi ya msamiati teule, mtindo mpya wa maumbo maalumu uliotumiwa na mshairi kutungia baadhi ya mashairi ni dhahirisho kuwa mtindo hubadilika katika uandishi katika kipindi fulani cha kihistoria. Kwa hivyo, utafiti huu umetoa mchango wa kitaaluma kuhusu uhakiki wa mtindo katika utanzu wa ushairi huru kwa vile watafiti wa baadaye watahitajika kurejelea mchango wa kazi hii kimaudhui na kimtindo.

7.4 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Katika utafiti huu, tumejikita katika vipengele viwili ambavyo ni maudhui na mtindo kulingana na malengo ya utafiti wetu. Kuna vipengele vingine vya fani kama vile wahusika na mandhari katika ushairi wa Kithaka wa Mberia ambavyo hatukuvishughulikia kwa sababu ya malengo, muda, upeo na mipaka ya utafiti wetu. Kwa hivyo, kuna haja ya kutafiti vipengele hivyo na kuonyesha ufaafu wake katika ushairi wa mshairi huyu. Aidha, kuna umuhimu wa kuchanganua motifu ya ndoto kama elementi kuu ya kimuundo katika mashairi ya Kithaka wa Mberia na umuhimu wake. Mbali na hayo, suala la toni na aina za toni katika ushairi wake lafaa kuchanganuliwa. Isitoshe, mtafiti anaweza kuangazia matumizi ya maumbo kama ishara kwa kutumia nadharia ya semiotiki. Hatimaye, kuna haja ya kuchunguza ukiushi na aina za ukiushi katika mashairi ya Kithaka wa Mberia.

MAREJELEO

- Abed, K. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.
- Arege, T. (1998). "Ushairi Huru wa Kiswahili: Mchango wa Euphrase Kezilahabi". Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Ashcroft, B. (1989). *The Empire Writes Back: Theory and Practice in Post-Colonial Literatures*. London: Routledge.
- Baldick, C. (2001). *The Concise Oxford Dictionary of Literary Terms*. New York: Oxford University Press.
- Barry, P. (2002). *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory* (Toleo la pili). Manchester: Manchester University Press.
- Bhabha, H. (1990). *Nation and Narration*. London: Routledge.
- Bradford, R. (1997). *Stylistics*. London: Routledge.
- Brooks, C. & Warren, R. (1938). *Understanding Poetry*. New York: Holt, Rinehart and Winston.
- Chacha, N.C. (1992). *Hukumu*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.
- Eagles, M. (2008). *An Introduction to Modern Democratic Government* (Toleo la tatu). Canada: Munroe Eagles.
- Fanon, F. (1967). *The Wretched of the Earth*. Harmondsworth: Penguin.
- Gandhi, L. (1998). *Postcolonial Theory*. New York: Columbia University Press.
- Gicuku, M. (2011). "Usawiri wa Maudhui ya Ndoa katika Ushairi wa Euphrase Kezilahabi na Kithaka wa Mberia". Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Habwe, n.w.(2010). *Darubini ya Isimu Jamii: Kwa Shule na Vyuu*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Hall, D. (2001). *Literary and Cultural Theory: From Basic Principles to Advanced Applications*. New York: Houghton Mifflin Company.
- Harding, J. R. (2017). *Similes, Puns and Counterfactuals in Literary Narrative*. New York: Routledge.
- Hussein, E. N. (1971). *Mashetani*. Nairobi: Oxford University Press.

- Indede, F. (2008). 'Mabadiliko katika Umbo la Ushairi na Athari Zake katika Ushairi wa Kiswahili' katika *Swahili Forum*, Juzuu 15, kur. 73-94.
- _____ (2011). 'Mwanamke Angali Tata katika Ushairi wa Kisasa?' katika *Swahili Forum*, Juzuu 18, kur. 163-197.
- Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinemann.
- _____ (1988). *Karibu Ndani*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- _____ (2008). *Dhifa*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
- Leech, G. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman.
- Leech, G. & Short, M. (1981). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose*. London: Longman.
- Loomba, A. (1998). *Colonialism / Postcolonialism*. London: Routledge.
- Mazrui, A. (1988). *Chembe cha Moyo*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- _____ (2002). *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mulokozi, M. na Kahigi, K. (1976). *Malenga wa Bara*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- _____ (1973). *Mashairi ya Kisasa*. Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.
- _____ (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mvungi, T. (1985). *Chungu Tamu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mwachofi, A. K. (1987). *Mama ee*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mwai, W. (1988). "New Trends in Ushairi" Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Ndung'o, C. na Mwai, W. (1991). *Kiswahili Studies: Misingi ya Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Ngari, A. (1998). "Utetezi wa Haki za Wanyonge katika Diwani ya *Mchezo wa Karata*". Tasnifu ya Elimu Sanaa, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njuguna, H. W. (2015). "Ukiushi katika Ushairi wa Amri Abedi na Kithaka wa Mberia". Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

- Nyambura, J. A. (2014). "Matumizi ya Kinaya katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia". Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Nzuki, P. (2003). "Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia". Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Ongarora, S. O. (2007). "Mtindo katika Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine". Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Padley, S. (2006). *Key Concepts in Contemporary Literature*. New York: Palgrave Macmillan.
- Paxson, J. J. (1994). *The Poetics of Personification*. New York: Cambridge University Press.
- Rodney, W. (2012). *How Europe Underdeveloped Africa*. Nairobi: Pambazuka Press.
- Said, E. (1978). *Orientalism*. London: Routledge.
- _____ (1993). *Culture and Imperialism*. New York: Alfred A. Knopf.
- Sangili, N. K. (2012). "Uchanganuzi wa Mashairi-Picha kama Sitiari katika Baadhi ya Mashairi ya Kithaka wa Mberia". Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Maseno. (Haijachapishwa)
- Spivak, G. (1987). *In Other Worlds: Essays in Cultural Politics*. New York: Methuen.
- _____ (1988). 'Can the Subaltern Speak?' katika C. Nelson and L. Grossberg (wahr)., *Maxism and the Interpretation of Culture*. Basingstoke: Macmillan Education, kur. 271-313.
- Thornborrow, J. & Wareing, S. (1998). *Patterns in Language: An Introduction to Language and Literary Style*. London: Routledge.
- TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Wa Mberia, K. (1990). 'Umbo la Mashairi' katika *Mwamko*, Juzuu 5, kur. 80-111.
- _____ (1997). *Mchezo wa Karata*. Nairobi: Marimba Publications Limited.
- _____ (1997). *Natala*. Nairobi: Marimba Publications Limited.
- _____ (2001). *Bara Jingine*. Nairobi: Marimba Publications Limited.
- _____ (2002). *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publications Limited.
- _____ (2004). *Maua Kwenye Jua la Asubuhi*. Nairobi: Marimba Publications Limited.
- _____ (2005). *Redio na Mwezi*. Nairobi: Marimba Publications Limited.
- _____ (2007). *Msimu wa Tisa*. Nairobi: Marimba Publications Limited.

- _____ (2014). *Rangi ya Anga*. Nairobi: Marimba Publications Limited.
- Wa Mutiso, K. (1986). *Mizani Yangu*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Wa Thiong'o, N. (1986). *Decolonizing the Mind*. Nairobi: Heinemann Educational.
- Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation .
- Wales, K. (2001). *A Dictionary of Stylistics* (Toleo la pili). Harlow: Longman.
- Wamitila, K. (2001). *Kamusi ya Methali*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- _____ (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.
- _____ (2003a). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.
- _____ (2003b). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.
- _____ (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

VIAMBATISHO

Kiambatisho I: Boga (*Mchezo wa Karata*)

mboga
uliozaa
boga
hili,
hukuupanda
sikuupanda;
tulipozaliwa
tuliukuta
unastawi
shambani,
shamba
tuliloachiwa
na
wazazi;
maadam
sisi
wawili,
tu
warithi
wa
shamba
hili,
utajiri
uliomo
shambani,
si
urithi wako

si
urithi wangu,
ni
urithi wetu;
boga
hili
basi,
si
mali
yako,
si
mali
yangu,
ni
mali
yetu;
basi
nasisitiza,
tulikate
sehemu
mbili,
sehemu
sawa,
yako
na
yangu.

Kiambatisho II: Nyumba (*Mchezo wa Karata*)

nyumba
hii ambayo
ilifumwa kwa
mawe yaliyoubwa
na maumbile,
mawe ambayo
yalisongwa na
maskini, nyumba
hii ambayo
ilisimamishwa kwa
saruji itokanayo
na viungo
vya ardhi vilivyochimbwa na
yahe, nyumba
hii iliyoezekwa
vigae vitokanavyo
na udongo
kimano tuliourithi
kutoka mama,
nyumba hii

**iliyopambwa kwa vioo vilivyotengenezwa na
matambara, kwa nini wasistarehe katika nyumba
hii wale ambao misuli yao iliipa uhai**

Kiambatisho III: Dau Haliendi! (*Mchezo wa Karata*)

limo ingawa
mbioni,
hili
dau,
la
kusafiria
mamilioni,
haliendi;
huu
ni
mwendo
duara-
unaduru,
ni
mwendo
mzunguko-
unazunguka.
mwendo
mpeto-
unaopeta,
hauwi
safari,
bali,
hupumbazika
mamilioni,
kwamba
wanasafiri,
katika
bahari ya miaka

Kiambatisho IV: Mruko wa Nyuki (Bara Jingine)

tutasema
lini:
baada
ya
amani
yetu,
kuvurugwa
na
wageni,
sisi
nyuki
wa
afrika,
tulipitia
nyanda
tata,
nyanda
zenye
walembe,
tuliloa
machovu,
machovu
ya
ukusanyaji,
ukusanyaji
wa
mbelewele,
viungo
vya
kutengeneza
asali,

ambayo,
haikutufaidi;
tulichoka
nyoyo,
joto
la
dhiki,
likatukausha
stahamala,
tulikalamua
akili,
zikajiri
ndoto,
ndoto
Jamala,
ndoto
za
tiba;
tulikakamua
mabawa,
mabawa
ya
safari;
safari
ya
tiba;
ulianza
mwendo,
mwendo
wa
mabawa,
na
nyoyo

za
moto,
baada
ya
kitambo,
kitambo
cha
jasho,
kitambo
chekundu-
kitambo
chenye
vimete
vya
umeme,
na
ngurumo
za
radi-
tuliifikia
njia
panda,
panda
tatizi,
ambapo,

njia
moja
iliingia kulia,
nyingine ikapitia
kushoto, baadhi
yetu tulisafiria
kushoto, wengine
walifuata kulia
baada ya
kitambo, ghafla,
njia ya
kushoto
i po
li ro ka
mo
waliokuwemo wakajiunga
na
njia
ya
kulia;
pamoja,
kwa
nguvu
za
akili,
nguvu
za
misuli,
tulijizatiti
na
kuufikia
mti
wa

tiba,
kutoka
tanzu
zake,
tanzu
adhimu,
tukachuna
matunda,
matunda
ya
kutosha,
yakawa
kifariji,
kifariji
cha
umma,
nacho
kivuli,
kivuli
cha
mti,
kivuli
kizito,
kikawa
mwavuli,
ukatukinga
kutokana
na
jua,
jua
ambalo,
siku
za

nyuma,
lilituliza
machozi,
machozi
ya
unyonge

Kiambatisho V: Mwashhi Mahiri (*Bara Jingine*)

Usasa!
Usasa unaodharau uhai?
Usasa unaoua?
Titi, kazi yako
Ni muhimu
Mithili ngome
Chupa ana lipi angavu
Kuliko nuru yako adhimu?
Chupa!
Muuaji vijijini!
Mwenye njama za wivu
Baina yake na uchafu!
Pigana, Titi pigana!
Pigana dhidi ya ulafi
Wa wanabiashara wajanja,
Pigana dhidi ya uchafu
Ndani na nje ya chupa,
Pigania afya ya watoto

Pigana, Titi pigana!
Pigana na wale ambao
Hukuchukulia kuwa pambo
Pambo la kifua ambalo
Lapaswa kulindwa
Lisitiwe ulegevu
Na midomo michanga
Pigana, wewe mwashi mahiri
Ujengaye miili thabiti
Ikawa kama ngome za mawe
Vikosi vya maradhi vinapofika
Na kufanya mashambulizi
Vikarudi makwao
Bila ushindi kujiri.
Pigana, Titi pigana!
Pigana katika vita adhimu
Vya kutetea afya angavu
Ya sasa na siku zijazo.